



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**



ISO 9001:2015 Certified

# **RIPOTI KUU YA MWAKA** **YA UKAGUZI WA UFANISI** **MWAKA WA FEDHA 2022/23**



**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU**  
**WA HESABU ZA SERIKALI**  
**MACHI 2024**





JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Jengo la Ukaguzi, 4 Barabara ya Ukaguzi, S.L.P. 950, Tambukareli, 41104 Dodoma. Simu ya Upepo: "Ukaguzi", Simu: +255(026)2321759, Nukushi: +255(026)2117527, [ocag@nao.go.tz](mailto:ocag@nao.go.tz), [info@nao.go.tz](mailto:info@nao.go.tz) Barua pepe: [ocag@nao.go.tz](mailto:ocag@nao.go.tz), Tovuti: [www.nao.go.tz](http://www.nao.go.tz)

Kumb. Na. CGA.319/421/01B

28 Machi 2024

Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan,  
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,  
Ikulu,  
S.L.P. 1102,  
1 Barabara ya Julius Nyerere,  
Chamwino,  
**40400 DODOMA.**

**YAH: KUWASILISHA RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU  
WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA UFANISI 202223**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 143 (4) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Kifungu cha 28 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418, ninawasilisha kwako Ripoti ya Jumla ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi kwa kipindi kinachoishia tarehe 31 Machi 2024.

Ninawasilisha.


Charles E. Kichere

**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**

# KUHUSU OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

## Mamlaka

Mamlaka ya kisheria na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yanatoka kwenye Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418 [Toleo la 2021].



### Kufanya kazi kwa uhuru na bila upendeleo

Sisi ni taasisi ya umma isiyo na upendeleo, inayotoa huduma za ukaguzi wa hali ya juu kwa wateja wetu kwa njia isiyo na upendeleo.

#### Kufanya kazi kwa ushirikiano

Tunathamini na kufanya kazi kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje.

#### Kufanya kazi kwa kuzingatia matokeo

Tunazingatia katika kufikia malengo muhimu yenye kuaminika kwa wakati, usahihi na utumizi stahiki.



### Kufanya kazi kwa utaalum

Tunatoa huduma za ukaguzi za hali ya juu kwa kuzingatia maarifa ya kitaaluma, ujuzi na mbinu bora.

### Kufanya kazi kwa uadilifu

Tunazingatia na kudumisha viwango vya juu vya maadili na sheria katika utoaji wa huduma za ukaguzi.

### Kufanya kazi kwa ubunifu na uvumbuzi

Tunahimiza, kuvumbua, na kubuni mawazo ya kuongeza thamani kwa ajili ya kuboresha huduma za ukaguzi

# YALIYOMO

ORODHA YA MAJEDWALI .....	vi
ORODHA YA VIELELEZO .....	x
SALAMU KUTOKA KWA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ..	xiii
MUHTASARI .....	xv
SURA YA KWANZA .....	1
UTANGULIZI .....	1
1.1 Usuli wa Ukaguzi wa Ufanisi .....	1
1.2 Mamlaka ya Kufanya Ukaguzi wa Ufanisi.....	2
1.3 Madhumuni ya Ripoti ya Jumla .....	2
1.4 Mtazamo wa Ripoti ya Jumla .....	4
1.5 Umuhimu wa Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu.....	5
1.6 Uhalali wa Ukaguzi.....	6
1.7 Mchakato wa Uthibitisho wa Takwimu na Taarifa Zilizotolewa.....	7
1.8 Muundo wa Ripoti .....	8
SURA YA PILI .....	9
MAELEZO YA MPANGO WA PILI NA WA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO NA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVO .....	9
2.1 Utangulizi .....	9
2.2 Usuli kuhusu Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu.....	9
2.3 Miongozo Muhimu na Mfumo wa Kisheria Unaosimamia Utekelezaji wa Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.....	12
2.4 Watendaji Muhimu katika Utekelezaji wa Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano .....	13
2.5 Mikakati ya Utekelezaji wa Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.....	14

2.6	Ukaguzi wa Ufanisi Uliofanyika na Uhusiano Wake na Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu .....	16
2.7	Ugharamiaji wa Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano.....	19
SURA YA TATU .....		20
UPATIKANAJI WA HUDUMA BORA ZA AFYA .....		20
3.1	Utangulizi .....	20
3.2	Malengo ya Ukaguzi na Mawanda.....	24
3.3	Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Upatikanaji wa Huduma za Afya ya Akili .....	25
3.4	Matokeo ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Vifaatiba katika Vituo vya Afya vya Umma .....	34
3.5	Athari katika kufikia malengo ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Mendeleo Endelevu.	41
SURA YA NNE .....		43
USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA KILIMO.....		43
4.1	Utangulizi .....	43
4.2	Malengo na Mawanda ya Ukaguzi .....	47
4.3	Matokeo ya Ukaguzi Kuhusu Udhhibiti wa Mazao ya Biashara .....	48
4.4	Matokeo ya Ukaguzi wa Udhhibiti wa Usambazaji wa Mbolea .....	57
4.5	Athari katika kufikia malengo ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Mendeleo Endelevu.	62
SURA YA TANO .....		64
MAENDELEO YA RASILIMALI WATU.....		64
5.1	Utangulizi .....	64
5.2	Malengo na Mawanda ya Ukaguzi .....	68
5.3	Matokeo ya Ukaguzi kwenye Udhhibiti wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo .....	70
5.4	Matokeo ya Ukaguzi wa ufanisi Kuhusu ya Uendelezaji, Ufuatiliaji na Tathmini ya Umahiri wa Watumishi katika Sekta za Umma .....	88



5.5	Matokeo ya Ukaguzi katika Usimamizi wa Programu za Urekebu kwa Wafungwa Magerezani.....	98
5.6	Athari katika kufikia malengo ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Mendeleo Endelevu .....	109
SURA YA SITA .....		111
USIMAMIZI WA MIPANGO MIJI .....		111
6.1	Utangulizi .....	111
6.2	Malengo ya Ukaguzi na Mawanda ya Ukaguzi.....	114
6.3	Matokeo ya Ukaguzi juu ya Usimamizi wa Mipango Miji .....	114
6.4	Athari katika kufikia malengo ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Mendeleo Endelevu .....	130
SURA YA SABA .....		132
USIMAMIZI WA HUDUMA ZA BIMA NA UREJESHAJI WA MIKOPO YA WANAFUNZI WA ELIMU YA JUU .....		132
7.1	Utangulizi .....	132
7.2	Malengo na Mawanda ya ukaguzi .....	136
7.3	Matokeo ya Ukaguzi katika Usimamizi na Ufuatiliaji wa Watoa huduma za Bima .....	137
7.4	Matokeo ya Ukaguzi katika Usimamizi wa Urejeshaji wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu .....	149
7.5	Athari katika kufikia malengo ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Mendeleo Endelevu .....	157
SURA YA NANE.....		159
USIMAMIZI WA MALIASILI .....		159
8.1	Utangulizi .....	159
8.2	Malengo na Mawanda ya Ukaguzi .....	163
8.3	Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Usimamizi wa Fukwe .....	165
8.4	Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Uwezeshaji wa Wachimbaji Wadogo wa Madini Nchini.....	173

8.5	Matokeo ya Ukaguzi katika Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi .....	185
8.6	Athari katika kufikia malengo ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Mendeleo Endelevu .....	203
SURA YA TISA .....		204
USIMAMIZI WA UINGIZAJI WA MAFUTA .....		204
9.1	Utangulizi .....	204
9.2	Malengo na Mawanda ya Ukaguzi .....	206
9.3	Matokeo ya Ukaguzi katika Usimamizi wa Uingizaji wa Mafuta nchini .....	208
9.4	Athari katika kufikia malengo ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Mendeleo Endelevu .....	219
SURA YA KUMI .....		221
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....		221
10.1	Utangulizi .....	221
10.2	Hitimisho la Ujumla .....	221
10.3	Hitimisho Mahsusi .....	222
10.4	Mapendekezo ya Ukaguzi .....	227

## ORODHA YA MAJEDWALI

JEDWALI NA. 1: RIPOTI ZA UKAGUZI WA UFANISI NA TAASISI ZILIZOKAGULIWA.....	3
JEDWALI NA. 2: MAENEO YA MKAKATI WA AFYA .....	21
JEDWALI NA. 3: UPATIKANAJI WA VIFAA KATIKA NGAZI ZOTE.....	31
JEDWALI NA. 4: MBOLEA ZA MAJANI ZILIZOSAJILIWA NA ZISIZOSAJILIWA .....	58
JEDWALI NA.5: UHUSIANO KATI YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA UREKEBU WA WAFUNGWA NA MPANGO WA TATU WA TAIFA WA MAENDELEO WA MIAKA MITANO NA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEU .....	67
JEDWALI NA. 6: MIKAKATI NA JUHUDI ZILIZOFANYWA NA SERIKALI KATIKA KUBORESHA RASILIMALIWATU .....	67
JEDWALI NA. 7: MGAWANYO WA SOKO LA AJIRA KWA NGAZI YA MAFUNDI MCHUNDO .....	70
JEDWALI NA. 8:TAFITI ZILIZOFANYWA NA VYUO VYA ELIMU YA UFUNDI NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI KUHUSU UMUHIMU WA UTAFITI WA SOKO LA AJIRA .....	71
JEDWALI NA. 9: MAHITAJI YA SOKO LA AJIRA KATIKA NGAZI YA MAFUNDI MCHUNDO HADI MWAKA 2021 .....	72
JEDWALI NA. 10: UPUNGUFU WA VIFAA VYA KUJIFUNZIA KATIKA VYUO VYA UFUNDI VILIVYOTEMBELEWA .....	74
JEDWALI NA. 11: HALI YA VYUMBA VYA MIHADHARA NA IDADI YA WALIMU NA WANAFUNZI ....	75
JEDWALI NA. 12: USAJILI WA MUDA WA VYUO VYA UFUNDI .....	76
JEDWALI NA. 13: USAJILI WA WALIMU WA UFUNDI NCHINI.....	77
JEDWALI NA. 14: USAJILI WA WALIMU WA UFUNDI KATIKA KANDA ZILIZOTEMBELEWA .....	77
JEDWALI NA. 15: HALI YA UHUISHAJI WA ITHIBATI KWA VYUO VYA UFUNDI .....	80
JEDWALI NA. 16: MATUMIZI YA MITAALA ILIYOPITWA NA WAKATI KATIKA VYUO VYA UFUNDI VILIVYOTEMBELEWA .....	81
JEDWALI NA. 17: ASILIMIA ZA UFUATILAJI WA UTEKELEZAJI KWA KIPINDI CHA (2019/2020- 2022/2023) .....	82
JEDWALI NA. 18: MAKOSA YALIONEKANA KWENYE VYUO VYA UFUNDI .....	84
JEDWALI NA. 19: UPUNGUFU WA WATUMISHI KATIKA BARAZA LA ELIMU YA UFUNDI.....	86
JEDWALI NA. 20: MAKADIRIO NA BJETI HALISI ILIYO POKELEWA NA BARAZA LA ELIMU YA UFUNDI .....	87



JEDWALI NA. 21: MAJUMUISHO YA MAHITAJI YA SHUGHULI ZA UJUZI KATIKA MIPANGO YA TAASISI .....	89
JEDWALI NA. 22: UJUZI MUHIMU ULIOJUMUISHWA KATIKA TATHMINI YA MAHITAJI YA UJUZI WA WATUMISHI KWENYE TAASISI ZA UMMA .....	90
JEDWALI NA. 23: KIWANGO CHA MAARIFA NA UTEKELEZAJI WA MWONGOZO WA UMAHIRI WA UONGOZI KATIKA UTUMISHI WA UMMA .....	94
JEDWALI NA. 24: UTENDAJI KAZI WA UONGOZI KATIKA KIPINDI CHA MPITO .....	95
JEDWALI NA. 25: TATHMINI YA USHAWISHI WA MIFUMO YA MFUMO WA USIMAMIZI WA UTENDAJI KATIKA VIGEZO VINGINE VYA RASILIMALIWATU .....	97
JEDWALI NA. 26: UWEZO WA GEREZA NA WAFUNGWA WALIOPO .....	102
JEDWALI NA. 27: MAUDHUI YA MTAALA WA MAOFISA MAGEREZA WANAOANZA KAZI.....	105
JEDWALI NA. 28: MAOFISA MAGEREZA WALIOHUDHURIA MAFUNZO YA SAYANSI YA UREKEBU KATIKA MAGEREZA YALIYOTEMBELEWA .....	107
JEDWALI NA. 29: UKUBWA WA MAENEO YA VIWANJA USIYOJITOSHELEZA YALIYOTENGWA KWAAJILI YA HUDUMA ZA KIJAMII KATIKA MICHORO YA MIPANGO YA MIJI ILIYOANDALIWA .....	116
JEDWALI NA. 30: KIWANGO CHA UTEKELEZAJI WA MPANGO KABAMBE NA MIPANGO YA MIJI ILIYODHINISHWA KATIKA MAMLAKA YA MIPANGO YA ZIARA .....	120
JEDWALI NA. 31: UZINGATIAJI WA VIWANGO VYA MIPANGO YA UENDELEZAJI WA MIJI KATIKA SKIMU ZA MIPANGO .....	121
JEDWALI NA. 32: IDADI YA WATUMISHI KATIKA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA NA OFISI ZA ARDHI ZA MKOA KWA NCHI NZIMA .....	124
JEDWALI NA. 33: UPUNGUFU WA WAFANYAKAZI KUTOKA MAMLAKA ZA UPANGAJI ZILIZOTEMBELEWA MWAKA 2022/2023 .....	124
JEDWALI NA. 34: UFUATILIAJI WA SHUGHULI ZA MIPANGOMIJI KATIKA MAMLAKA ZA UPANGAJI .....	129
JEDWALI NA. 35: UHUSIANO WA MAENEO YALIYOKAGULIWA NA MPANGO WA PILI NA WA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIKA MITANO .....	134
JEDWALI NA. 36: KIWANGO CHA TATHMINI YA UCHAMBUZI WA KIFEDHA NA UKWASI WA MAKAMPUNI YA BIMA YENYE LESENI ULIOFANYWA NA MAMLAKA YA BIMA KUTOKA 2019 HADI 2023.....	143

JEDWALI NA. 37: HALI YA UTUNZAJI WA AMANA YA CHINI YA DHAMANA KATIKA BENKI KUU YA TANZANIA KWA MAKAMPUNI YA BIMA .....	148
JEDWALI NA. 38: RUZUKU YA SERIKALI KATIKA UTOAJI WA MIKOPO YA WANAFUNZI .....	151
JEDWALI NA. 39: ULINGANISHO WA UKUSANYAJI WA MIKOPO KUTOKA KWA WANUFAIKA WALIOAJIRIWA NA WANUFAIKA BINAFSI .....	153
JEDWALI NA. 40: KIWANGO CHA MUUNGANISHO WA MFUMO WA BODI YA MIKOPO NA MIFUMO YA WADAU WENGINE .....	154
JEDWALI NA. 41: IDADI YA FAINI AMBAZO HAZIKUTOZWA KWA WAAJIRI .....	156
JEDWALI NA. 42: IDADI YA WANUFAIKA WALIO NA MIKOPO INAYODAIWA KWA ZAIDI YA KIPINDI CHA MIAKA KUMI .....	157
JEDWALI NA. 43: UHUSIANO WA USIMAMIZI WA MALIASILI NA MPANGO WA PILI NA WA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO .....	161
JEDWALI NA. 44: SABABU ZA KUTOZINGATIA MAHITAJI YA MAZINGIRA.....	168
JEDWALI NA. 45: MIKAKATI YA BODI YA UTALLII TANZANIA ILIVYO HUSISHA UTANGAZAJI WA FUKWE.....	169
JEDWALI NA. 46: HALI YA UTOAJI WA TAARIFA ZA JIOLOJIA NA UWAPO WA MASHAPO KWA WACHIMBAJI WADOGO NCHINI .....	174
JEDWALI NA. 47: UTAFITI WA KIJIOLOJIA KWA AJILI YA WACHIMBAJI WADOGO .....	175
JEDWALI NA. 48: IDADI YA LESENI ZA UCHIMBAJI MDOGO ZILIZOTOLEWA DHIDI YA ZINAZOFANYA KAZI KUANZIA 2018/19 HADI 2022/2023 .....	179
JEDWALI NA. 49: IDADI YA ZANA ZA UVUVI HARAMU KATIKA MAENEO YALIYOTEMBELEWA WAKATI WA UKAGUZI .....	185
JEDWALI NA. 50: UTOAJI WA TAARIFA ZA UVUVI KATIKA SERIKALI ZA MITAA ZILIZOTEMBELEWA .....	186
JEDWALI NA. 51: UTENDAJI WA USAJILI WA VYOMBO VYA UVUVI .....	187
JEDWALI NA. 52: UTENDAJI WA USAJILI WA KITENGO CHA USIMAMIZI WA FUKWE PAMOJA NA MIALO .....	188
JEDWALI NA. 53: HALI YA UTEKELEZAJI WA MSIMU WA UFUNGAJI WA SHUGHULI ZA UVUVI KATIKA HALMASHAURI ZILIZOTEMBELEWA .....	192
JEDWALI NA. 54: MAJUKUMU YA URATIBU INAYOTAKIWA KUTOLEWA NA WADAU .....	196

JEDWALI NA. 55: USHABILIANO WA UAGIZAJI WA MAFUTA NA MPANGO WA PILI NA WA TATU WA TAIFA WA MAENDELEO WA MIAKA MITANO NA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEU .....	205
JEDWALI NA. 56: ASILIMIA YA MELI KUCHELEWA KUANZA KUPAKUA .....	212
JEDWALI NA. 57: KIWANGO CHA UCHELEWESHAJI .....	212
JEDWALI NA. 58: TOZO KWA KUCHELEWA KUANZA KUPAKUA MAFUTA .....	213
JEDWALI NA. 59: HALI YA TOZO ZA KUCHELEWA KUPAKUA MAFUTA KAMA ILIVYOKUWA TAREHE 22 SEPTEMBER 2023 .....	213

## ORODHA YA VIELELEZO

KIELELEZO NA. 1: KANUNI ZA UKAGUZI WA UFANISI .....	1
KIELELEZO NA. 2: MPANGILIO WA SURA ZILIZOUNDA RIPOTI HII.....	8
KIELELEZO NA. 3: UHUSIANO WA MIKAKATI NA MIPANGO YA KITAIFA .....	10
KIELELEZO NA. 4: MAELEZO KWA UFUPI YA KILA MAUDHUI MAHUSUSI TOKA KWENYE MIPANGO YA MAENDELEO YA TAIFA .....	11
KIELELEZO NA. 5: MIONGOZO MUHIMU NA MFUMO WA KISHERIA KATIKA USIMAMIZI WA UTEKELEZAJI WA MIPANGO YA MAENDELEO YA TAIFA YA MIAKA MITANO .....	13
KIELELEZO NA. 6: WATENDAJI MUHIMU NA MAJUKUMU YAO KATIKA UTEKELEZAJI WA MIPANGO YA MAENDELEO YA TAIFA YA MIAKA MITANO .....	14
KIELELEZO NA. 7: MUHTASARI WA MIKAKATI YA UTEKELEZAJI WA MIPANGO YA MAENDELEO YA MIAKA MITANO .....	15
KIELELEZO NA. 8: KAGUZI ZA UFANISI ZILIZOFANYIKA ZIKIHUSIANISHA NA MAUDHUI YA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEU PAMOJA NA MPANGO WA MAENDELEO WA MIAKA MITANO .....	18
KIELELEZO NA. 9: MIKAKATI NA JITIHADA ZA SERIKALI KATIKA USIMAMIZI WA HUDUMA ZA AFYA .....	23
KIELELEZO NA. 10: MUHTASARI WA SHUGHULI MUHIMU ZINAZOHUSIANA NA MPANGO WA TATU WA TAIFA WA MAENDELEO WA MIAKA MITANO.....	45
KIELELEZO NA. 11: MIKAKATI NA JITIHADA ZA SERIKALI ZILIZOWEKWA ILI KUSIMAMIA SHUGHULI ZA KILIMO .....	47
KIELELEZO NA. 12: THAMANI ZA MAPATO YA MAUZO YA NJE KWA MAZAO YALIYOHAGULIWA .....	50
KIELELEZO NA. 13: TATHMINI YA IDADI YA WAKAGUZI WA MAZAO WALIOPO DHIDIYA WANAOHITAJIKA KUTOA HUDUMA ZA UGANI KATIKA BODI ZA MAZAO .....	53
KIELELEZO NA. 14: MWENENDO WA MABADILIKO YA BEI ZA MAZAO YA BIASHARA KWA MIAKA MITANO ILIYOPITA .....	56
KIELELEZO NA. 15: UTOFAUTI KATI YA MAKISIO YA MAHITAJI NA MATUMIZI HALISI YA MBOLEA .....	60
KIELELEZO NA. 16: ULINGANIFU KATI YA IDADI YA VYUO VYA UFUNDI VILIVYOPATA ITHIBATI NA ZISIZO NA ITHIBATI.....	79

KIELELEZO NA. 17: KIWANGO CHA UFUATILIAJI KATIKA KANDA VILIVYOTEMBELEWA (2019/2020-2022/2023).....	83
KIELELEZO NA. 18: MAWANDA YA UJUZI WA UJUZI KATIKA PROGRAMU ZINAZOTEKELEZWA ZA KUJENGA UWEZO MIONGONI MWA TAASISI ZA UMMA .....	93
KIELELEZO NA. 19: ONGEZECO LA WAFUNGWA WANAORUDIA MAKOSA KUANZIA MWAKA 2019 HADI 2023 .....	99
KIELELEZO NA. 20: ASILIMIA YA WAFUNGWA WALIORUDIA MAKOSA YAKIHUSIANISHWA NA MUDA WAO WA KIFUNGO .....	100
KIELELEZO NA. 21: ASILIMIA YA MAOFISA MAGEREZA WALIOPATA MAFUNZO KATIKA CHUO CHA MAFUNZO YA UREKEBU TANZANIA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19 - 2022/2023 .....	106
KIELELEZO NA. 22: FEDHA ZILIZOPANGWA NA ZILIZOPOKELEWA KWA AJILI YA SHUGHULI ZA MIPANGOMIJI .....	122
KIELELEZO NA. 23: KIWANGO CHA UPIMAJI WA VIWANJA DHIDI YA MALENGO YALIYOWEKWA	126
KIELELEZO NA. 24: MAPATO YALIYOKUSANYWA KUTOKA VYANZO VYA ARDHI.....	127
KIELELEZO NA. 25: MADAI YANAYODAIWA KWA MAKAMPUNI YA BIMA ZA JUMLA NA NA BIMA ZA MAISHA KWA KIPINDI CHA KUANZIA MWAKA 2019 - 2022 .....	138
KIELELEZO NA. 26: UCHAMBUZI WA UCHELEWASHAJI WA ULIPAJI WA MADAI YALIYOIDHINISHWA NA KAMPUNI ZA BIMA KUANZIA 2019-2023 .....	139
KIELELEZO NA. 27: UTENDAJI WA UKAGUZI ULIOFANYWA NA MAMLAKA YA BIMA TANZANIA KWA MAWAKALA WA BIMA 2019/2020 - 2022/2023 .....	141
KIELELEZO NA. 28: ULINGANISHO WA IDADI YA MAAGIZO YALIYOTOLEWA NA RIPOTI ZA UKAGUZI BAADA YA UKIUKWAJI WA SHERIA DHIDI YA IDADI YA MAAGIZO YALIYOAMULIWA NA MIKUTANO YA KAMATI YA UTEKELEZAJI WA SHERIA ...	142
KIELELEZO NA. 29: KIWANGO CHA UTIIFU WA VIWANGO VYA KISHERIA VYA UKWASI KAMPUNI ZA BIMA ZA JUMLA NA BIMA YA MAISHA KUFIKIA TAREHE 30 JUNI 2022 .....	145
KIELELEZO NA. 30: KAMPUNI ZA BIMA ZILIZO NA KIWANGO CHA UKWASI KILICHO JUU YA KIWANGO CHA KISHERIA LAKINI CHINI YA KIWANGO CHA TAHADHARI .....	146
KIELELEZO NA. 31: HALI YA MKOPO YA WANAFUNZI INAYODAIWA .....	149
KIELELEZO NA. 32: MWENENDO WA UKUSANYAJI WA MAREJESHO YA MIKOPO YA WANAFUNZI .....	150

KIELELEZO NA. 33: IDADI YA WANUFAIKA WENYE MIKOPO ILIYOFIKIA MUDA WA MALIPO DHIDI YA WANUFAIKA WALIOLIPA MIKOPO YAO KILA MWAKA.....	151
KIELELEZO NA. 34: HALI YA UTAMBUZI WA WANUFAIKA WA MIKOPO YA ELIMU YA JUU KUWEZESHA UREJESHAJI .....	152
KIELELEZO NA. 35: HALI YA UTAMBUZI WA WANUFAIKA WA MIKOPO YA ELIMU YA JUU ILI KUWEZESHA UREJESHAJI .....	163
KIELELEZO NA. 36: UTEKELEZAJI WA MIKAKATI YA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII KUANZIA MWAKA 2019/2020 HADI 2022/2023 .....	167
KIELELEZO NA. 37: UPATIKANAJI WA TEKNOLOJIA BORA YA UCHIMBAJI NA UCHENJUAJI WA MADINI KWA WACHIMBAJI WADOGO KUPITIA VITUO VYA MFANO .....	177
KIELELEZO NA. 38: UPOTEVU WA MAPATO KUTOKANA NA LESENI YA WAVUVI, KODI, NA ADA ZA SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA KATIKA MIKOA ILIYOTEMBELEWA ..	190
KIELELEZO NA. 39: HALI YA UVUVI WA SAMAKI WASIOFIKIA UKUBWA.....	191
KIELELEZO NA. 40: UTENDAJI WA HALMASHAURI KATIKA UKUSANYAJI WA TAKWIMU ZA UVUVI ZA KILA SIKU .....	195
KIELELEZO NA. 41: HALI YA MATUMIZI YA ZANA HARAMU KATIKA TASNIA YA UVUVI NCHINI .	199
KIELELEZO NA. 42: MAKOSA YA UVUVI HARAMU YALIYOFANYIKA KUANZIA MWAKA 2018/19 HADI 2022/2023 .....	201
KIELELEZO NA. 43: MWENENDO WA UAGIZAJI NA UTUMIAJI WA MAFUTA YA DIZELI KUANZIA MWAKA 2019 HADI 2022 .....	209
KIELELEZO NA. 44: MWENENDO WA UAGIZAJI NA UTUMIAJI WA MAFUTA YA PETROLI KUANZIA MWAKA 2019 HADI 2022 .....	209
KIELELEZO NA. 45: HALI YA MATUMIZI YA NDANI YA MAFUTA YALIYOAGIZWA KWA AJILI YA KUSAFIRISHA NJE ZA NCHI KUANZIA MWAKA 2019 HADI 2022.....	210
KIELELEZO NA. 46: ASILIMIA YA MAKAMPUNI YA MAFUTA YALIYOKIDHI VIGEZO .....	211
KIELELEZO NA. 47: MTIRIRIKO WA JITIHADA KWENYE UANDAaji WA MPANGO MKUU WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU YA MAFUTA.....	217





## SALAMU KUTOKA KWA MKAGUZI NA MDHIBITI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Ninayo furaha kuwasilisha ripoti ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023, ambayo imejumuisha kaguzi za ufanisi. Ninapenda kutambua jitihada za serikali inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za kuhimiza uwajibikaji na uwazi katika usimamizi wa rasilimali za umma. Pia, ninatambua ushirikiano uliokuwapo kati ya taasisi nilizozikagua na Ofisi yangu kwa kutoa taarifa na ufafanuzi wakati wa utayarishaji wa ripoti hii ya ukaguzi.

Matokeo ya ukaguzi yamebainisha masuala muhimu na tathmini inayoonesha uhusiano katika kutoa matokeo yaliyotarajiwa na mchango wake kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21), Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26), na Malengo ya Maendeleo Endelevu. Kwa kuonesha masuala muhimu yaliyobainishwa katika sekta mbalimbali na tathmini ya ufanisi wa taasisi za Serikali, ripoti hii inalenga kuainisha mafanikio na upungufu katika kuyafikia malengo ya mabadiliko ya kiuchumi na maendeleo ya watu yaliyotarajiwa katika mipango ya maendeleo. Ripoti hii inawasilisha matokeo ya tathmini ya kina ya namna usimamizi unaofanyika katika sekta tofauti inavyoathiri malengo makuu ya Mipango ya Maendeleo wa Taifa ya Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu hivyo kutoa mwelekeo wa maboresho.

Matokeo ya ukaguzi yamebainisha mambo mbalimbali yanayoonesha endapo ufanisi katika utekelezaji wa shughuli, mipango, mifumo au miradi ya serikali inayohusisha ukusanyaji au matumizi ya fedha za umma katika wizara, idara, mamlaka za serikali za mitaa, na mashirika ya umma, inafanya kazi kwa kuzingatia kanuni tatu za thamani za fedha yaani, uwekevu, ufanisi na tija. Wakati baadhi ya taasisi zilionesha ufanisi mzuri, tasisi zingine zilikuwa na changamoto katika kufikia thamani ya fedha kwenye rasilimali walizotengewa. Hivyo, ni muhimu kwa serikali kuchukua hatua stahiki ili kuhakikisha kuwa taasisi za serikali zinakuwa na ufanisi na tija katika kutekeleza majuku yao na hatimaye kuchangia kwenye ukuaji wa uchumi na utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Ripoti hii ya jumla inawasilisha matokeo ya ukaguzi, hitimisho, na mapendekezo kwa mujibu wa ripoti 14 za ukaguzi wa ufanisi zilizotekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/24. Ripoti hii imejumisha sura 10, kila moja imejikita katika uwanja

tofauti, ikiwa pamoja na utoaji wa huduma za afya, shughuli za kilimo, maendeleo ya rasilimaliwatu, mipango miji, udhibiti wa huduma za bima, utoaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, usimamizi wa maliasili, na usimamizi wa uingizaji wa mafuta ya petroli na dizeli nchini.

Katika ripoti hii, nimetoa mapendekezo yanayohusu kuboresha upungufu uliobainika katika taasisi zilizokaguliwa ili kuhakikisha kuwa taasisi hizo zinakuwa na ufanisi na tija katika utekelezaji wa shughuli za serikali. Ni matumaini yangu kuwa mapendekezo haya yatakuwa na manufaa kwa serikali na wadau mbalimbali katika kuhakikisha utoaji wa huduma bora.

A handwritten signature in green ink, appearing to read 'Charles E. Kichere', with a large, sweeping flourish extending to the right.

Charles E. Kichere

**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**

## MUHTASARI

Taarifa hii ya jumla ya ukaguzi inaelezea upungufu uliobainika, hitimisho, pamoja na mapendekezo katika ripoti 14 za ukaguzi wa ufanisi zilizofanyika kwa mwaka wa fedha wa 2023/24. Ripoti hizo 14 zilihusu upatikanaji wa huduma za afya ya akili; udhibiti wa vifaatiba katika hospitali na vituo vya afya vya umma; udhibiti wa mazao ya biashara; udhibiti wa usambazaji wa mbolea kwa wakulima; udhibiti wa elimu ya ufundi nchini; uendelezaji, ufuatiliaji, na tathmini ya umahiri wa watumishi katika sekta za umma; utekelezaji wa programu za urekebu kwa wafungwa; usimamizi wa mipango miji; usimamizi na ufuatiliaji wa watoa huduma za bima nchini; usimamizi wa urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu; usimamizi wa fukwe; uwezeshaji wa wachimbaji wadogo wa madini; usimamizi wa rasilimali za uvuvi; na usimamizi wa uingizaji wa mafuta nchini.

Ripoti hii inasisitiza kuwa na mtazamo na tathmini ya kina kutoka kwenye ripoti hizi 14 za ukaguzi kwa kuhusisha matokeo tarajiwa na mchango wake kwenye malengo yaliyowekwa kwenye Mpango wa Pili (2016/17-2020/21) na Tatu (2021/22 - 2025/26) wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano; na ulinganu wake kwenye Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Kwa kuainisha maeneo muhimu ambayo yameonekana katika sekta tofauti, na kutathmini ufanisi wa taasisi za umma, ripoti hii ya jumla inalenga kuleta mafanikio na kutambua umuhimu wa shabaha za mabadiliko ya kiuchumi na maendeleo ya rasilimali watu kwenye mipango ya maendeleo. Vilevile, inatoa mchanganuo wa kina kuhusu namna ambavyo usimamizi wa shuguli za kissekta zinavyochochea ufikiwaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa na Malengo ya Maendeleo Endelevu, hivyo kutoa mwongozo wa maboresho ya kimkakati na utungaji wa sera.

Hata hivyo, ripoti hii haikusudii kuwa mbadala wa ripoti 14 zilizofanyika. Hivyo, kwa taarifa zaidi, msomaji anashauriwa kusoma ripoti za ukaguzi husika kama zilivyoanishwa hapo juu.

## Matokeo ya Ukaguzi

### (a) Upatikanaji wa Huduma Bora za Afya

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi wa hali ya upatikanaji wa huduma za afya ya akili na udhibiti wa vifaatiba katika vituo vya afya vya umma.

#### (i) Upatikanaji wa huduma za afya ya akili

Ukaguzi unatambua jitihada za Serikali za kuunganisha huduma za afya ya akili kwa ufanisi katika ngazi ya taifa. Hata hivyo, maeneo yafuatayo yanahitaji maboresho zaidi:

*Kutofanyika kwa ufanisi utambuzi wa wagonjwa wa afya ya akili katika ngazi ya jamii:* Ukaguzi ulibaini kutokuwapo kwa utambuzi wa watu wenye matatizo ya akili katika ngazi ya jamii. Badala yake, utambuzi ulilenga watumiaji wa dawa za kulevya, wazee, walemavu, watoto walio katika mazingira magumu, na wale waliopata mimba za utotoni. Hali hii lichangiwa na ukosefu wa fedha za kutosha kwa ajili ya huduma za ustawi wa jamii na kukosekana kwa Maofisa ustawi wa jamii katika ngazi za chini, vikiwemo vijiji na mitaa.

*Ukosefu wa huduma za kisaikolojia katika ngazi ya jamii:* Ukaguzi ulibaini kutokuwapo kwa huduma za kisaikolojia katika ngazi ya jamii. Hali hii ilitokana na huduma za matunzo ya kisaikolojia na usaidizi kutokuingizwa kikamilifu katika mipango, bajeti, sera, programu, afua, na mikakati kwa ngazi zote za vituo vya kutolea huduma za afya. Udhaifu huu ulisababisha kutokuwapo kwa huduma kamili kwa makundi mbalimbali, wakiwemo wagonjwa wa akili.

*Rasilimali zisizotosheleza (wataalamu, miundombinu, vifaatiba, na dawa) na kutopatikana kwa huduma za utengamo:* Ukaguzi ulibaini kuwapo kwa upungufu wa wataalamu, miundombinu, vifaatiba, na dawa katika ngazi zote za vituo vya kutolea huduma za afya. Kukosekana kwa wataalamu hao kulichangiwa na Wizara ya Afya kutokuwa na mpango wa kuajiri wataalamu wa afya ya akili na kutokuwapo kwa muundo wa utumishi unaowajumuisha wahitimu wa taaluma ya huduma za afya ya akili. Pia, kulikuwa na ukosefu wa huduma za utengamo kwa ajili ya kuendeleza ujuzi, ushirikiano wa jamii, na misaada inayozingatia urejeshaji, ambapo ilibainika kuwa kati ya mikoa 28, ni mikoa mitano tu ndiyo ilikuwa na vituo vya utengamo kwa ajili ya huduma za afya ya akili ambayo ni Kilimanjaro, Mwanza, Dar es Salaam, Dodoma, na Kigoma.

#### (ii) Udhibiti wa vifaatiba katika vituo vya afya vya umma

Ukaguzi unatambua jitihada za Serikali kupitia Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania kwa kuanzisha idara ya kudhibiti vifaatiba. Pia, Wizara ya Afya imeanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Vifaatiba katika Vituo vya Afya vya Umma. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini maeneo yafuatayo yanayohitaji maboresho zaidi:

*Kuwapo kwa vifaatiba visivyofanya kazi nchini:* Ukaguzi ulibaini kuwapo kwa vifaatiba visivyofanya kazi katika vituo vya afya vya umma 18 vilivyotembelewa sawa na asilimia 27 ya vifaatiba, huku asilimia kubwa ya vifaatiba visivyofaa vikibainika katika kanda ya kati.

*Kutozingatiwa ipasavyo taratibu za usajili wa vifaatiba:* Ukaguzi ulibaini kuwa Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania haikuwa na kumbukumbu za kutosha ya asilimia 56 ya vifaatiba vilivyosajiliwa. Zaidi ya hayo, hakukuwa na uhuishaji wenye ufanisi wa vyeti vya usajili wa vifaatiba unaofanywa na Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania. Pia, asilimia 51 ya wenye usajili wa vifaatiba hawakulipa ada ya mwaka ya kuhifadhi. Kutokana na hali hiyo, Serikali ilipoteza mapato ya shilingi 10,261,473,750 ya ada ya uhuishaji wa usajili wa vyeti vya vifaatiba na kiasi cha shilingi 241,040,000 kwa ajili ya ada ya mwaka ya kuhifadhi vifaatiba vyao vilivyosajiliwa kuanzia mwaka wa fedha 2019/2020 hadi 2022/2023.

Ukaguzi ulibaini kuwa haya ni matokeo ya kutokuwa na ufanisi wa udhibiti wa vifaatiba vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi na vituo vya afya vya umma pamoja ufuatiliaji na usimamizi duni wa Wizara ya Afya.

#### **(b) Usimamizi wa Shughuli za Kilimo**

Ukaguzi wa usimamizi wa shughuli za kilimo ulihusisha udhibiti wa mazao ya biashara na udhibiti wa usambazaji wa mbolea kama inavyofafanuliwa hapa chini.

##### **(i) Udhibiti wa mazao ya biashara**

Ukaguzi unatambua juhudi za Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Bodi za Udhibiti wa Mazao katika kufanikisha uzinduzi wa mnada wa chai wa Dar es Salaam. Lengo la mnada huo lilikuwa kuongeza mapato, kuboresha ubora wa chai, na kulinda uasili wa chai ya Tanzania. Zaidi ya hayo, serikali ilianzisha mfumo wa kidijiti wenye lengo la kufanya mnada kwa njia ya mtandao. Hatua hii itasaidia kupunguza urasimu na kuboresha uwazi. Hata hivyo, maeneo yafuatayo yanahitaji maboresho zaidi:

*Kulikuwa na mabadiliko makubwa ya mchango wa tasnia ya tumbaku na chai kwenye uchangiaji wa pato la taifa:* Ilibainika kuwa chai ilipunguza uchangiaji wake kwa miaka mingi, ambapo katika mwaka wa fedha 2022/23, ilipungua kutoka dola za Marekani 43,213,662 hadi dola za Marekani 32,258,827. Upungufu huo ni wa dola za Marekani 10,954,835 (sawa na asilimia 26). Wakati huohuo, Tumbaku ilikuwa na upungufu wa asilimia 28, ambalo ni anguko la dola za Marekani 81,059,709.01. Tathmini zaidi imeonesha kuwa mchango wa korosho ulishuka kutoka dola za Marekani 209,115,498 hadi dola za Marekani 139,994,994 kuanzia mwaka 2021/22 hadi mwaka 2022/23, ikiwa ni upungufu wa asilimia 33.

Sababu kubwa ilikuwa kutokuwapo kwa Maofisa ugani wa kutosha kwa ajili ya kusimamia uzalishaji wa mazao ya biashara. Hali hiyo ilisababisha kupungua kwa mchango wa kilimo cha mazao hayo ya biashara katika pato la taifa.

*Bodi za mazao zilikuwa na upungufu wa wakaguzi wa mazao kwa wastani wa asilimia 53. Ukaguzi ulibaini kuwa Bodi ya Chai ilikuwa na upungufu wa wakaguzi wa mazao kwa asilimia 89; Bodi ya Tumbaku ilikuwa na upungufu wa wakaguzi wa mazao kwa asilimia 42; Bodi ya Korosho ilikuwa na upungufu wa wakaguzi wa mazao kwa asilimia 75; na Bodi ya Kahawa ilikuwa na upungufu wa wakaguzi wa mazao kwa asilimia 7. Chanzo cha upungufu huo wa wakaguzi wa mazao ni kutoweka kipaumbele kwa shughuli ya ukaguzi wa mazao, hivyo kusababisha kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya biashara.*

## **(ii) Udhhibiti wa usambazaji wa mbolea**

Serikali, kupitia Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea, ilianzisha mpango wa ruzuku ya mbolea kwa lengo la kupunguza gharama za upatikanaji wake kwa wakulima. Matumizi ya mbolea yaliongezeka kutoka tani za ujazo wa metriki 363,599 mwaka 2021/22 hadi kufikia tani za ujazo wa metriki 440,795 mwaka 2022/23. Hata hivyo, maeneo yafuatayo yanahitaji maboresho zaidi:

*Upatikanaji mdogo wa mbolea na virutubisho vya mimea kwa wakulima:* Ilibainika kuwa wafanyabiashara 1,712 kati ya 4,136 wote waliosajiliwa katika mpango wa ruzuku (sawa na asilimia 41) hawakuuza wala kusambaza mbolea za ruzuku kwa wakulima katika maeneo yao. Pia, ilibainika kuwa wakulima 2,551,239 kati ya 3,389,951 waliosajiliwa katika mpango wa ruzuku (sawa na asilimia 75) hawakupata wala kutumia mbolea kupitia mpango wa ruzuku licha ya kuwa na sifa ya kupata mbolea hiyo ya ruzuku. Hali hii ilisababishwa na makisio yasiyojitosheleza ya mahitaji ya mbolea na kutosambaza mbolea kwa wakati, hivyo kuchelewesha mbolea kupatikana kwa wakulima. Hali hii ilisababisha matumizi duni ya mbolea kwa wakulima hivyo kupunguza uzalishaji wa mazao.

*Makisio hafifu ya mahitaji ya mbolea na virutubisho vya mimea:* Ilibainika kuwa Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea haikuwa na utaratibu madhubuti wa makisio ya mahitaji ya mbolea nchini ili kupata mbolea ya kutosha. Ilibainika kuwa Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea haikuwa na utaratibu, mfumo, au programu madhubuti ya kuainisha mahitaji na matumizi ya mbolea ili kupata taarifa sahihi za kiwango na aina ya mbolea inayohitajika. Uhaba wa Maofisa ugani ndio ulisababisha udhaifu katika ukusanyaji wa mahitaji katika ngazi ya kijiji, ambayo yalihatijika ili kupata taarifa sahihi za kiasi cha mbolea kinachoitajika na kinachoendana na aina ya udongo katika vijiji vyao. Kutokana na hali hiyo, takwimu za makisio ya mahitaji ya mbolea yalikuwa makubwa kuliko matumizi halisi ya maeneo husika kwa asilimia kati ya 14 na 48.



### **(c) Maendeleo ya Rasilimali watu**

Ukaguzi wa maendeleo ya rasilimali watu ulibaini udhaifu katika udhibiti wa elimu ya ufundi nchini; uendelezaji, ufuatiliaji, na tathmini ya umahiri wa watumishi katika sekta za umma; na utekelezaji wa mpango wa urekebu kwa wafungwa, kama inavyofafanuliwa hapa chini.

#### **(i) Udhibiti wa elimu ya ufundi nchini**

Ukaguzi huu unatambua jitihada zinazofanywa na Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia katika udhibiti wa elimu ya ufundi kwa kuhakikisha kuwa elimu ya ufundi inayotolewa nchini ni ya viwango vinavyoakisi mahitaji ya soko la ajira. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini udhaifu unaohitaji maboresho zaidi kama inavyoelezwa hapa chini.

*Udhibiti usiotosheleza wa utoaji elimu ya ufundi na mafunzo yenye kuendana na mahitaji ya soko la ajira:* Ukaguzi uligundua kuwa, kulikuwa na kutofautiana kwa ubora wa ujuzi kutoka kwa wahitimu na mahitaji ya mwajiri au mahitaji katika sekta za umma na za binafsi. Hii hii ilichangiwa na upungufu wa tathmini ya mahitaji yanayoendana na mahitaji ya soko la ajira. Hali hii ilihusishwa na idadi ndogo ya mafundi-mchundo waliohitimu kukidhi mahitaji ya soko la ajira na kusababisha ukuaji mdogo wa sekta za kiuchumi.

*Mchakato usioridhisha wa usajili na utoaji wa ithibati kwa taasisi za ufundi na walimu wa ufundi:* Ukaguzi ulibaini upungufu katika mchakato wa usajili na utoaji wa ithibati kwa vyo vya ufundi kutokana na kushindwa kutimiza matakwa ya usajili, kama vile uandikishaji wa wanafunzi wasio na sifa, kuwa na watumishi wachache wa kitaaluma, na kutokuwa na vifaa vya kufundishia. Pia, ukaguzi ulibaini usajili usioridhisha wa wakufunzi wa ufundi, ambapo usajili ulikuwa kwa asilimia 67 kwa mwaka wa fedha 2019/20 na asilimia 56 mwaka wa fedha 2022/23.

#### **(ii) Uendelezaji, ufuatiliaji, na tathmini ya umahiri wa watumishi katika sekta za umma**

Ukaguzi unatambua jitihada zinazofanywa na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika kuboresha uwezo wa watumishi nchini. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini upungufu unaohitaji maboresho zaidi kama ilivyoelezwa hapa chini.

*Kuwapo kwa taasisi za umma zilizokuwa na watumishi wasio na umahiri:* Ukaguzi ulibaini kuwa taasisi za umma hazikufikia ufanisi wa kiwango cha juu katika utendaji wa kitaasisi, kiasi cha kuziwezesha taasisi zinazoingiza mapato kupata faida, na taasisi zinazotoa huduma kuzalisha ziada kutokana na utendaji

madhubuti. Matokeo yake, uwezo duni wa watumishi ulichangia utendaji usio na ufanisi katika taasisi za serikali na kusababisha kushuka kwa tija, kiwango kikubwa cha watumishi kuacha kazi, kushindwa kukua kwenye soko la ushindani, kushuka kwa mauzo na faida na kushuka kwa soka la hisa.

*Utambuzi na uchambuzi usioridhisha wa upungufu wa ujuzi wa watumishi katika taasisi za umma:* Ukaguzi ulibaini kuwapo kwa utambuzi na uchambuzi usioridhisha wa upungufu wa umahiri kwa watumishi katika taasisi za umma zilizotembelewa. Upungufu huo uliathiri uendeshaji wa programu za kujenga uwezo wa watumishi katika taasisi za umma. Ukaguzi ulibaini upungufu kadhaa, ikiwa pamoja na mipango duni ya utambuzi wa ujuzi kwa watumishi wa umma, kushindwa kufanya tathmini ya upungufu wa rasilimali watu, na kushindwa kudumisha orodha ya ujuzi katika taasisi za umma.

Sababu kuu ya kushindwa kufanya uchambuzi wa upungufu wa rasilimali watu ni mkabala finyu wa uandaaji wa tathmini ya mahitaji ya rasilimali watu, ikiwamo kufanya uchambuzi wa mahitaji ya watumishi wanaohitaji kupewa mafunzo ya kawaida kwenye taasisi za umma. Ingawa ni muhimu, tathmini ya mahitaji ya mafunzo kwa watumishi wa umma ina mchango mmoja tu kwenye tathmini ya kina ya kubainisha upungufu wa rasilimali watu.

*Maandalizi yasiyo na ufanisi ya programu za uendelezaji wa ujuzi:* Ukaguzi uligundua kuwapo kwa tofauti kati ya mipango iliyoandaliwa inayolenga kuongeza umahiriwa watumishi na upungufu wa kiutendaji uliobainishwa kutoka kwa watumishi. Hali hii ilisababishwa na kutoshirikisha wadau kwa asilimia 75 kwa taasisi zote isipokuwa Wizara ya Maji ambayo upungufu huu ulikuwa ni kwa asilimia 50.

### **(iii) Utekelezaji wa Mpango wa Urekebu kwa Wafungwa**

Serikali imefanya jitihada mbalimbali za kuboresha programu za urekebishaji wafungwa kwa kuanzisha Kitengo cha Huduma za Urekebu wa Wafungwa chini ya Jeshi la Magereza Tanzania. Pia, Jeshi la Magereza lilianzisha gereza la shule ya ufundi, Ruanda - Mbeya na gereza la vijana, Wami - Morogoro, na kuanzisha Stashahada ya Sayansi ya Urekebu kwa Maofisa wa magereza katika Chuo cha Mafunzo ya Urekebu Tanzania. Hata hivyo, maeneo yafuatayo yanahitaji maboresho zaidi.

*Kuongezeka kwa kiwango cha wafungwa wanaorudia makosa kwa wastani wa asilimia 1.5 kuanzia mwaka 2019 hadi 2023:* Ukaguzi ulibaini ongezeko la wafungwa wanaorudia makosa kwa wastani wa asilimia 1.5 kuanzia mwaka 2019 hadi 2023, licha ya mipango ya urekebu. Hali hii inaonesha kuwa wafungwa zaidi wanarudi kwenye kufanya uhalifu. Kiwango cha kurudia kufanya makosa

kilikuwa hakiendani na muda wa wafungwa gerezani. Wafungwa wengi zaidi walio na hukumu fupi walirudia makosa. Kati ya mwaka 2019 na 2023, hali ya wafungwa waliorudia kufanya makosa ni kama ifuatavyo: asilimia 59.22 walikuwa wafungwa waliohukumiwa kifungo cha chini ya mwaka mmoja (1); asilimia 24.65 walikuwa wafungwa waliohukumiwa kifungo cha kuanzia mwaka mmoja (1) hadi miaka mitatu (3); asilimia 10.14 walikuwa wafungwa waliohukumiwa kifungo cha kuanzia miaka 3 hadi 5; na asilimia 3.09 walikuwa wafungwa waliohukumiwa kifungo cha kuanzia miaka 5 hadi 10. Pia, asilimia 0.37 walikuwa wafungwa waliohukumiwa kifungo cha kuanzia miaka 10 hadi 15; asilimia 2.22 walikuwa wafungwa waliohukumiwa kifungo cha kuanzia miaka 15 hadi 20; asilimia 0.32 walikuwa wafungwa waliohukumiwa kifungo cha kuanzia miaka 20 hadi 30; na asilimia 0.01 walikuwa wafungwa waliohukumiwa kifungo cha zaidi ya miaka 30.

Hali hii ilisababishwa na ukosefu wa mitaala na miongozo ya magereza kwa ajili ya uendelezaji rasmi wa mipango ya urekebu; uainishaji na utengano wa wafungwa kujikita kwenye jinsia na umri pekee; miundombinu isiyotosheleza ya uainishaji; shughuli za msingi za gereza kuamua uainishaji; na ukosefu wa sera na miongozo ya uainishaji wa wafungwa.

*Kukosekana kwa mipango rasmi ya kuunganisha wafungwa wanaotarajia kukamilisha vifungo vyao: Ukaguzi ulibaini kuwa licha kuwapo kwa programu za urekebu, hakukuwa na mpango rasmi wa kuwaanda wafungwa wanaokaribia kukamilisha muda wao wa kifungo ili kuwaandaa kukabiliana na jamii watakayoenda kuishi ikiwemo changamoto kadhaa zinazoweza kuwapata katika kipindi hicho. Kukosekana kwa mfumo huu maalumu wa kuwaandaa wafungwa, kunasababisha wafungwa kuachiwa bila kuandaliwa hivyo kuwapa ugumu wa kupata huduma za jamii na misaada mbalimbali na kuchangia ongezeko la wafungwa wanaorudia makosa.*

#### **(d) Usimamizi wa Mipango Miji**

Kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi, Serikali inaandaa sera mpya ya makazi, na uendeshaji wa shughuli za sekta ya ardhi kupitia Mfumo Jumuishi wa Taarifa za Usimamizi wa Ardhi, ambao umesanikishwa katika mikoa miwili. Aidha, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imefanikiwa kuandaa na kupitisha jumla ya michoro ya mipango miji 8429 kati ya 8000 iliyokuwa imepangwa kutekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2022/23, ambayo inaonesha utendaji wa jumla kwa asilimia 105. Hata hivyo, maeneo yafuatayo yanahitaji maboresho zaidi.

*Usanifu na uendelezaji wa mipango miji usiojitosheleza:* Ukaguzi ulibaini kuwa, Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) hazikuhakikisha kuwa usanifu na uendelezaji wa Mipango miji inajitosheleza. Mipango miji iliyoendelezwa haikuzingatia viwango vinavyotakiwa na utofauti ulikuwa asilimia 2 hadi asilimia 85 katika mamlaka 5 kati ya 11 za upangaji zilizotembelewa. Pia, ilibainika kuwa ni asilimia 61.54 tu ya mipango ya kina 79 iliyopitiwa ilijumuisha maeneo kwa ajili ya maendeleo ya baadaye. Matokeo yake, usanifu na uandaaji wa mipango miji haukufanyika kwa wakati hivyo kuchelewesha ugawaji wa viwanja au utoaji wa hatimiliki kwa wananchi.

*Skimu za mipango miji iliyoandaliwa kutotekelezwa kwa ufanisi:* Ilibainika kuwa miji haikuendelezwa kwa ufanisi kutokana na kutozingatia skimu za mipango miji zilizoidhinishwa wakati wa uandaaji wake. Hali hii ilionekana katika mamlaka 7 kati ya 11 za upangaji zilizotembelewa. Pia, kulikuwa na upungufu wa rasilimali kwa ajili ya kuwezesha shughuli za mipango miji katika Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi na OR - TAMISEMI. Vilevile, Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi na OR - TAMISEMI, kupitia mamlaka ya serikali za mitaa hazikusimamia kikamilifu uhibitaji wa uendelezaji wa miji ili kuhakikisha inalingana na skimu za mipango miji na mipango kabambe ya maeneo husika. Aidha, ukaguzi ulibaini kufanyika kwa tathmini isiyojitosheleza ya utendaji wa mamlaka za upangaji juu ya shughuli za mipango miji. Hali hii ilisababisha kutofikia lengo lililokusudiwa la kupendezesha miji na kuwa na mazingira mazuri ya kuishi, kufanya kazi, na kuburudika.

#### **(e) Usimamizi wa Huduma za Bima na Urejeshaji wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

Sehemu hii inahusu usimamizi na ufuatiliaji wa watoa huduma za bima pamoja na usimamizi wa urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, kama inavyofafanuliwa hapa chini.

#### **(i) Usimamizi na ufuatiliaji wa watoa huduma za bima**

Ninatambua juhudi zilizofanywa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania katika kuwasimamia watoa huduma za bima nchini. Jitihada hizi ni pamoja na kusajili watoa huduma za bima 1,165; kuanzisha Mfumo wa Usajili kwa Njia ya Mtandao kwa ajili ya kusajili watoa huduma za bima; kuidhinisha bidhaa mpya za bima; na kutekeleza programu mbalimbali za uhamasishaji wa bima katika Kanda na Ofisi ya Zanzibar. Hata hivyo, kulibainika maeneo yaliyohitaji maboresho zaidi kama yanavyofafanuliwa hapa chini.

*Usimamizi usioridhisha wa madai ya bima:* Ukaguzi ulibaini kuwa madai ya bima hayakusimamiwa na kufuatiliwa ipasavyo na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania. Hali hii ilithibitishwa na kuwapo kwa ongezeko kubwa la madai ya wateja ambayo yalikuwa hayajalipwa na kampuni za bima kutoka shilingi bilioni 114.532 mwaka 2019 hadi shilingi bilioni 127.253 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 11 kutoka mwaka 2019/20 hadi 2022/23. Ukaguzi ulibaini ongezeko hilo la madai ambayo yalikuwa hayajalipwa lilichangiwa zaidi na kuwapo kwa janga la UVIKO-19 lililosababisha ongezeko la madai ya bima za maisha na ucheleweshaji wa malipo kwa madai yaliyoidhinishwa na kampuni za Bima. Kucheleweshwa kwa malipo ya madai yaliyoidhinishwa kuliathiri vibaya haki ya wateja wa bima ya wanufaika kulipwa kwa wakati na kampuni za bima. Kwa mfano, ripoti za ukaguzi za Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania kuanzia mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2022/23 zilionesha kuwa shilingi milioni 439.15 hazikulipwa kwa wakati na kampuni za bima kwa wateja wao.

## **(ii) Usimamizi wa urejeshaji mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu**

Ninatambua juhudi za Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu katika kusimamia urejeshaji wa mikopo kwa njia ya mapitio ya kina na kuandaa modeli ya kiotomati ya uzalishaji na uzoefu wa wateja kujifunza kupitia mashine na mbinu za kiakili-bandia chini ya Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi. Hata hivyo, maeneo yanayohitaji kuboreshwa zaidi yamebainishwa kama ifuatavyo:

*Ongezeko la mikopo ambayo ilikuwa haijalipwa yenye thamani ya shilingi trilioni 3.15:* Ukaguzi ulibaini kuwa mikopo ambayo ilikuwa haijalipwa iliongezeka kutoka shilingi trilioni 1.25 katika mwaka wa fedha 2015/2016 hadi shilingi trilioni 4.84 kwa mwaka wa fedha 2021/2022, sawa na ukuaji wa wastani wa asilimia 23. Kwa mfano, makusanyo ya ulipaji wa mikopo yalipungua kutoka shilingi bilioni 191 mwaka 2019/20 hadi shilingi bilioni 170 mwaka 2022/23. Hali hii ilitasababishwa na mabadiliko ya sera za utoaji wa mikopo ikiwemo sera ukadiriaji wa uhifadhi wa thamani wa kiwango cha sifuri ya mwezi Julai 2021. Pia, kubadilishwa kwa adhabu na ada za kuhifadhi thamani ya fedha hadi kiwango cha sifuri kulichangia kupungua kwa makusanyo ya mikopo.

Matokeo yake, ufadhili wa Serikali kwa mikopo ya wanafunzi uliongezeka kutoka shilingi bilioni 268.9 mwaka 2018/9 hadi shilingi bilioni 393.8, sawa na ongezeko la shilingi bilioni 124.9 kutokana na ufanisi usioridhisha wa Bodi ya Mikopo Wanafunzi wa Elimu ya Juu katika kukusanya mikopo iliyoiva ya wanafunzi inayothibitishwa na ongezeko la madeni.

Ukaguzi ulibaini pia kuwa marejesho ya mikopo kutoka kwa wanufaika binafsi yalifanywa kwa wastani wa asilimia 11 ikilinganishwa na asilimia 38 kutoka kwa wanufaika walioajiriwa. Aidha, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu

ilikusanya sehemu ndogo ya marejesho ya mikopo kutoka kwa wanufaika binafsi kwa wastani wa shilingi bilioni 38, sawa na asilimia 11 kuanzia mwaka 2014/2015 hadi 2022/23. Hadi mwaka wa fedha 2022/23, Bodi ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 1,181.4 kutoka kwa wanufaika walioajiriwa na shilingi bilioni 104.70 kutoka kwa wanufaika walioajiriwa.

Kukosekana kwa ufanisi wa ukusanyaji wa mikopo kutoka kwa wanufaika walio katika sekta binafsi kulitokana na mikakati isiyoridhisha ya ufuatiliaji ikiwa pamoja na kukosekana kwa mfumo wa TEHAMA unaoweza kusomana na mfumo ya taasisi muhimu kama vile Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii; Wakala wa Usajili, Ufilisi, na Udamini; Tume ya Vyuo Vikuu; Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa; na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni zenye kanzi data nyingi za wanufaika. Hali hii ilisababisha kutokusanywa kwa marejesho ya mikopo, jambo ambalo linaweza kuathiri ustahimilivu wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu katika kuendelea kufadhili wanafunzi.

#### **(f) Usimamizi wa Maliasili**

Katika sehemu hii, ukaguzi ulifanyika katika usimamizi wa fukwe, uwezesaji wa wachimbaji wadogo wa madini; na usimamizi wa rasilimali za uvuvi, na matokeo yake ni kama yanavyofafanuliwa hapa chini.

#### **(i) Usimamizi wa Fukwe**

Jitihada zilizobainishwa katika usimamizi wa fukwe ni pamoja na utambuzi wa baadhi ya fukwe pamoja na uandaaji wa mkakati wa masoko na uendelezaji wa fukwe zilizoko kusini mwa Tanzania. Hata hivyo, yafuatayo yalibainishwa:

*Uendelezaji usiojitosheleza wa fukwe katika uongezaji wa shughuli za utalii katika maeneo ya pwani:* Asilimia 89 ya maeneno ya fukwe yaliyotambuliwa yalikuwa hayajaendelezwa. Hali hi ilitokana na kuwapo kwa hatua zisizoridhisha za uendelezaji wa fukwe, hivyo kuzuia upatikanaji wa manufaa yatokanayo na fukwe hizi, kama vile ukusanyaji wa mapato kutoka kwa watalii wa ndani na wa kigeni.

*Utekelezaji usioridhisha wa masuala ya utunzaji wa mazingira:* Asilimia 82 ya fukwe katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizotembelewa hazikuzingatia masuala ya mazingira kwa sababu ya ukosefu wa kampeni za uelewa wa suala hili. Hali hii ilisababisha uharibifu wa mazingira, kama vile ukataji wa miti ya mikoko katika maeneo ya pwani.

*Uendelezaji na utangazaji usiojitosheleza wa fukwe:* Ukaguzi ulibaini uendelezaji na utangazaji wa fukwe usiojitosheleza kwa ajili ya shughuli za utalii. Hali hii ilisababishwa na mipango isiyojitosheleza ya kuwezesha kukuza



na kuendeleza utalii wa fukwe, hivyo kuzuia upatikanaji wa manufaa yatokanayo na maendeleo ya fukwe hizi, kama vile ukusanyaji wa mapato kutoka kwa watalii wa ndani na wa kigeni.

*Ufuatiliaji na uratibu usio na tija wa shughuli za ufukweni:* Ukaguzi ulibaini kuwa ufuatiliaji na uratibu wa shughuli za ufukweni haukufanyika vizuri. Hali hii ilisababishwa na ukosefu wa takwimu za kuaminika kwa ajili ya kupima utendaji, na hivyo kuathiri utangazaji na ukuzaji wa fukwe nchini.

## **(ii) Uwezeshaji wa Wachimbaji Wadogo wa Madini**

Ili kuwezesha shughuli za uchimbaji mdogo wa madini, Serikali ilianzisha vituo vya mfano, kununua rigi kwa ajili ya wachimbaji wadogo, kufanya utafiti wa kijiolojia, na kuanzisha masoko ya madini katika maeneo mbalimbali nchini. Hata hivyo, upungufu ufuatao ulibainika:

*Wachimbaji wadogo wa madini kutowezeshwa ipasavyo:* Ukaguzi ulibaini kuwa wachimbaji wadogo hawakuwa na taarifa za kutosha za kijiolojia pamoja na mashapo. Vilevile, hawakuwa na teknolojia za uchimbaji na uchenjuaji wa madini. Hali hii ilitokana na ukosefu wa mbinu za kutosha za kuwasaidia, hivyo kuathiri maendeleo kutoka katika uchimbaji mdogo kwenda katika uchimbaji wa kati.

*Utengaji na matumizi ya rasilimali yasiyojitosheleza katika kuwawezesha wachimbaji wadogo wa madini:* Ukaguzi ulibaini changamoto katika kuhakikisha utengaji wa fedha za kutosha na matumizi ya rasilimali zingine katika kuwasaidia wachimbaji wadogo. Hali hii ilitokana na utambuzi mdogo wa mahitaji na vipaumbele wakati wa kupanga na kutumia rasilimali hizo. Vilevile, hakukuwa na njia zilizowekwa ili kutathmini matumizi bora ya rasilimali zilizotengwa kwa ajili ya kuwasaidia wachimbaji wadogo nchini. Changamoto hii ilisababishwa na ukosefu wa taarifa za kutosha kuhusu wachimbaji wadogo, hivyo kukwamisha matumizi sahihi ya rasilimali zilizolenga kuwasaidia wachimbaji wadogo.

## **(iii) Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi**

Wizara ya Mifugo na Uvuvi imechukua hatua mbalimbali za kutokomeza ongezeko la matumizi ya zana haramu za uvuvi na kupata manufaa makubwa yatokanayo na shughuli za uvuvi. Pamoja na jitihada hizo, mambo yafuatayo yalibainika:

*Kuwapo kwa shughuli za uvuvi haramu nchini:* Ukaguzi ulibaini kuwapo kwa uvuvi haramu kutokana na kuwapo kwa zana haramu za uvuvi na wavuvi wasiosajiliwa. Hali hii ilisababishwa na ufuatiliaji na udhibiti usioridhisha.

Upungufu huu ulichangiwa na kuwapo kwa usimamizi na matumizi yasiyojitosheleza ya rasilimali za uvuvi.

*Upungufu katika usimamizi wa kanzidata ya uvuvi:* Ukaguzi ulibaini upungufu kama vile usimamizi usioridhisha wa nyaraka na takwimu za kila siku za uvuvi. Hali hii ilitokana na wizara zinazohusika kutoweka kipaumbele juu ya suala hili. Hali hii ilisababisha kuwapo kwa taarifa zisizo na uhalisia juu ya rasilimali za uvuvi.

*Uratibu usiojitosheleza katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi:* Ukaguzi ulibaini uratibu usijitosheleza baina ya wadau kama ilivyodhihirishwa na kuwapo kwa mawasiliano duni kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mamlaka za Serikali za Mitaa, na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (TAFIRI). Hali hii ilisababishwa na muundo wa kuripoti usiojitosheleza kati ya taasisi hizi tendaji. Matokeo yake, kulikuwa na ushirikiano hafifu katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi nchini.

#### **(g) Usimamizi wa Uingizaji wa Mafuta Nchini**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imechukua hatua mbalimbali za kuhakikisha uhakika wa ugavi wa mafuta nchini. Jitihada zilizochukuliwa ni pamoja na ufungaji wa mfumo wa ufuatiliaji mafuta wakati wa kushusha na kupakia, ujenzi wa Mfumo wa Taifa wa Taarifa za Petroli na Gesi, na ujenzi wa kituo kimoja cha kupokea mafuta bandari. Hatua hizi zinalenga kupunguza upotevu wa mafuta wakati wa kushusha, kufuatilia mafuta yaliyopo nchini kwa watoa huduma mbalimbali, na kushughulikia ucheleweshaji wa ushushaji wa mafuta. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi, upungufu ufuatao ulibainika:

*Mwenendo wa ucheleweshaji wa kuanza kushusha mafuta bandarini umeongezeka kutoka asilimia 66 hadi asilimia 68 kutoka mwaka wa fedha 2020/21 hadi 2022/23.* Kwa upande mwingine, ukaguzi huo umebaini ongezeko la ucheleweshaji kuanza kushusha kutoka asilimia 66 hadi asilimia 68 kati ya mwaka 2020/21 na 2022/23. Meli zilicheleweshwa kuanza kushusha mafuta kwa siku 7-14 na zaidi ya siku 14 katika mwaka wa fedha 2022/23 ukilinganisha na miaka iliyopita. Vikwazo vya miundombinu na kutofuata kwa tarehe iliyopangiwa meli kwa ajili ya ushushaji ilichangia ucheleweshaji huu, na kusababisha serikali kutozwa dola za Marekani 26,934,426.35. Pia, mwenendo wa meli kutoshusha mafuta ndani ya muda uliopangwa uliongezeka kutoka asilimia 27 hadi asilimia 35.

*Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji haikubaini kampuni za uangizaji wa mafuta zilizohifadhi mafuta chini ya siku 15 wakati wote:*

Uchambuzi wa ripoti za mafuta kwa wiki ya 1 na 3 kuanzia mwaka 2020 hadi 2023 zinaonesha kuwa kampuni za uangizaji wa mafuta hazikuhifadhi mafuta ya kuweza kutumika kwa siku 15 wakati wote kati ya asilimia 12 hadi 62, na asilimia 14 hadi 65 kwa petroli na dizeli mtawalia. Hali hii ilitokana na Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kutathmini upatikanaji wa mafuta kwa jumla badala ya hifadhi ya mafuta kwa kila kampuni ya uingizaji wa mafuta, hivyo kupunguza uwezo wa kutambua kampuni ambazo hazikuhifadhi mafuta yanayotakiwa.

Aidha, kukosekana kwa ripoti ya ukubwa wa soko kwa kila kampuni na kwa kila bidhaa kulipunguza uwezo wake wa kubaini hatari kwenye uhakika wa ugavi wa mafuta.

*Wizara ya Nishati kutoandaa mpango kabambe wa uendelezaji wa miundombinu ya mafuta:* Kwa mujibu wa ripoti zake za utendaji kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2022/23, ukaguzi ulibaini kuwa, Wizara ya Nishati haikuandaa mpango kabambe wa uendelezaji wa miundombinu ya mafuta kwa miaka mitano, bali iliandaa andiko la mpango kabambe wa uendelezaji wa miundombinu ya mafuta. Menejimenti ilieleza kuwa Wizara ilikuwa inatafuta rasilimalifedha kwa ajili ya maandalizi ya mpango kabambe huo. Ukosefu wa mpango kabambe unaweza kuzuia uratibu wa shughuli za uendelezaji wa miundombinu ya mafuta hivyo kusababisha kujirudia kwa juhudi za serikali na kusababisha wasiwasi kwa wawekezaji, wadau wa sekta, na washirika wa biashara.

### **Hitimisho la Jumla la Ukaguzi**

Ukaguzi unatambua juhudi zilizofanywa na taasisi zilizokaguliwa katika kuboresha utendaji wao ili kufikia malengo ya Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Mpango wa Maendeleo Endelevu ambao lengo lake kuu lilikuwa kuboresha uchumi na maendeleo ya watu. Jitihada zilizochukuliwa zilibainika wakati wa kutekeleza maeneo mbalimbali ya kipaumbele katika maeneo ya huduma za afya, shughuli za kilimo, maendeleo ya rasilimali watu, mipango miji, bima na mikopo, maliasili na utalii, na uingizaji wa mafuta.

Licha ya jitihada zilizochukuliwa na taasisi zilizokaguliwa katika kuhakikisha kuwa malengo ya Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Mpango wa Maendeleo Endelevu yanatimizwa, ukaguzi ulibaini kuwapo kwa changamoto ambazo zilizoziua kufikia malengo yaliyopangwa.

Upungufu uliobainishwa katika maeneo yaliyotajwa unapaswa kushughulikiwa haraka ili kuhakikisha kuwa malengo ya Serikali ya kukuza ustawi na maendeleo ya watu kama yaliyoainishwa katika Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Mpango wa Maendeleo Endelevu yanafikiwa.

## Mapendekezo ya Ukaguzi

### Wizara, Idara, na Wakala zinatakiwa kufanya yafuatayo:

- (i) Wizara ya Afya inapaswaihakikishe upatikanaji wa huduma za afya ya akili katka ngazi zote za vituo vya afya ili kuhakikisha kuwa wananchi wenye uhitaji wanapata huduma sahihi ya afya ya akili kwa wakati, na kuhakikisha vifaatiba vinasimamiwa ipasavyo ili kuhakikisha kunakuwa na usalama na ubora kwenye huduma za afya zinazotolewa na vituo vya afya nchini;
- (ii) Wizara ya Kilimo inapaswa iteue wakaguzi wa mazao ya biashara sambamba na kuhakikisha wanakuwa na vitendeakazi, ambao watawajibika moja kwa moja kwenye bodi zao za mazao ili kurahisisha ufuatiliaji wao na kuwafanya wawajibike kwenye menejiment za bodi za usimamizi wa mazao;
- (iii) Wizara ya Kilimo inapaswa itathmini ufanisi wa mifumo ya ununuzi wa mbolea kama vile mfumo wa pamoja wa ununuzi wa mbolea na mifumo mingine iliyopo, na kutumia matokeo yake katika kutatua upungufu wote ulioainishwa ili kuwezesha ununuzi na usambazaji wa mbolea kwa wakati ili kukidhi mahitaji ya mbolea;
- (iv) Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi wanatakiwa kufanya tathmini ya kina na endelevu ya uhitaji wa soko la ajira ili kuainisha mahitaji mapya ya ujuzi na kuhakikisha kuwa mitaala inayoandaliwa inazingatia soko la ajira;
- (v) Wizara ya Mambo ya Ndani na Jeshi la Magereza wanatakiwa kuandaa na kutekeleza mitaala ya mafunzo ya urekebu kwa wafungwa ili kurahisisha utekelezaji wa programu za urekebu;
- (vi) Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zinahimizwa kuandaa mikakati madhubuti ya kuwezesha usimamizi mzuri wa utekelezaji wa shughuli za mipango miji nchini. Mikakati hiyo inapaswa kuongeza ufanisi katika usanifu, upangaji, na utekelezaji wa shughuli za mipango miji ili kuwezesha kufikia kwa wakati malengo yaliyokusudiwa;
- (vii) Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Maliasili na Utalii na Kitengo cha Uhifadhi wa Bahari na Maeneo Tengefu

wanatakiwa kuboresha uratibu na ufuatiliaji wa ufanisi wa fukwe ili kuhamasisha uendelevu na kutangaza utalii wa fukwe;

- (viii) Wizara ya Madini ihakikishe inawasaidia wachimbaji wadogo kwa kuwezesha upatikanaji wa taarifa za kijiolojia, teknolojia za uchimbaji na uchenjuaji wa madini, pamoja na utengaji na matumizi ya rasilimali za kutosha kuwasaidia wachimbaji hao;
- (ix) Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wanatakiwa kuhakikisha ufuatiliaji, uhibitaji, na shughuli za uchunguzi ili kukabiliana na uvuvi haramu nchini; na
- (x) Wizara ya Nishati inatakiwa kuweka mkazo uanzishaji wa mpango kabambe wa uendelezaji wa miundombinu ya mafuta na kuratibu uendelezaji wa miundombinu ya kupokelea mafuta kwa pamoja.

# SURA YA KWANZA


## UTANGULIZI



### 1.1 Usuli wa Ukaguzi wa Ufanisi

Ukaguzi wa ufanisi hufanyika ili kubaini iwapo shughuli, mipango, mifumo, au miradi ya Serikali inayohusisha ukusanyaji au matumizi ya fedha za umma katika wizara, idara, mamlaka za serikali za mitaa, na mashirika ya umma inafanya kazi kwa kuzingatia kanuni tatu yaani *uwekevu*, *ufanisi*, na *tija*. Kanuni hizi ni kama zinavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 1**.

#### Kielelezo Na. 1: Kanuni za Ukaguzi wa Ufanisi



*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kwa Taarifa Iliyotolewa kutoka Mwongozo wa Ukaguzi wa Ufanisi wa Mwaka 2021*

Ukaguzi wa ufanisi pia unabainisha iwapo malengo yaliyowekwa mwanzoni mwa shughuli yalifikiwa. Taarifa hizi huwezesha kufahamu iwapo, kwa kiasi kikubwa, uwekevu, ufanisi, na tija ilizingatiwa wakati wa utekelezaji wa shughuli. Mapendekezo ya uboreshaji hutolewa kwenye maeneo yanayodhaniwa kuwa na upungufu.

Ukaguzi wa ufanisi katika sekta ya umma ni muhimu kwa vile hulenga kukuza uwajibikaji, uwazi, na utendaji kazi katika shughuli za Serikali ili wananchi

wake wapate huduma bora na kwa wakati. Ukaguzi wa ufanisi hutumika pia kama msingi wa kujifunza na kufanya maboresho.

Katika ukaguzi wa ufanisi, mambo mbalimbali huzingatiwa katika kuchagua maeneo ya kumakinikia. Mambo haya ni pamoja na kilio cha umma na umuhimu wa eneo kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

## 1.2 Mamlaka ya Kufanya Ukaguzi wa Ufanisi

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepewa mamlaka ya kisheria ya kufanya ukaguzi wa ufanisi na Kifungu cha 28 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2008 kinachosema kuwa:

“Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa madhumuni ya kuzingatia wekevu, ufanisi, na tija ya matumizi yoyote ya rasilimali za taasisi, atahitaji taarifa, kuchunguza, na kutoa taarifa kadiri atakavyoona inafaa juu ya:

- (a) Matumizi ya fedha za umma na matumizi ya rasilimali kwa wizara, idara, wakala, mamlaka za serikali za mitaa, na mashirika na taasisi zingine zote za umma;
- (b) Uendeshaji na ufanisi wa utendaji kazi wa Maofisa masuuli, wakuu wa idara, na watendaji wakuu wa vyombo vyote hivyo; na
- (c) Uzingatiaji wa sheria, kanuni, sera za mazingira, na viwango vya ndani ya nchi”.

## 1.3 Madhumuni ya Ripoti ya Jumla

Ripoti hii ya jumla inalenga kuwapa taarifa muhimu wabunge, Serikali, vyombo vya habari, umma, pamoja na wadau wengine ili waweze kufanya maamuzi yatakayoongeza uwekevu, tija, na ufanisi katika shughuli za serikali.

Ripoti hii inabainisha masuala mbalimbali yaliyobainika katika kaguzi za ufanisi dhidi ya yale yaliyotarajiwa, pamoja na mchango wake katika kutekeleza Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21 na 2021/22 - 2025/26) na kuyafikia Malengo ya Maendeleo Endelevu. Ripoti hii pia inatoa tathmini ya utendaji wa taasisi za serikali katika kutimiza majukumu yao katika Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unaolenga kuleta mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu.

Maeneo yaliyoguswa katika ripoti hii ni pamoja na usimamizi wa huduma za afya; shughuli za kilimo; uendelezaji wa rasilimali watu; na mipango miji. Maeneo mengine yaliyoguswa katika ripoti hii ni usimamizi wa bima na mikopo

kwa wanafunzi wa elimu ya juu, maliasili; pamoja na uingizaji wa mafuta nchini.

Pia, ripoti hii inawasilisha matokeo ya tathmini ya kiwango ambacho shughuli za Serikali zimechangia kufikia malengo ya Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu. **Jedwali Na. 1** linatoa muhtasari wa ripoti za ukaguzi wa ufanisi pamoja na taasisi zilizokaguliwa.

**Jedwali Na. 1: Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi na Taasisi Zilizokaguliwa**

Ripoti ya Ukaguzi	Taasisi Zilizokaguliwa
Upatikanaji wa Huduma za Afya ya Akili Tanzania	Wizara ya Afya; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watu Wenye Mahitaji Maalumu; na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
Udhibiti wa Vifaatiba katika Hospitali na Vituo vya Afya vya Umma	Wizara ya Afya na Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba
Udhibiti wa Mazao ya Biashara	Wizara ya Kilimo na Bodi za Mazao
Udhibiti wa Usambazaji wa Mbolea kwa Wakulima	Wizara ya Kilimo na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea
Udhibiti wa Elimu ya Ufundi Nchini	Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia; na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi
Uendelezaji, Ufuatiliaji, na Tathmini ya Umahiri wa Watumishi katika Sekta za Umma	Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora
Utekelezaji wa Programu za Urekebu kwa Wafungwa	Wizara ya Mambo ya Ndani na Jeshi la Magereza
Usimamizi wa Mipango Miji	Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
Usimamizi na Ufuatiliaji wa Watoa Huduma za Bima Nchini	Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania
Usimamizi wa Urejeshaji wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu	Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu
Usimamizi wa Fukwe	Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Wizara ya Maliasili na Utalii; na Kitengo cha Uhifadhi wa Bahari na Maeneo Tengefu
Uwezeshaji wa Wachimbaji Wadogo wa Madini	Wizara ya Madini
Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi	Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
Usimamizi wa Uingizaji wa Mafuta Nchini	Wizara ya Nishati na Taasisi Zake ambazo ni Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na



Ripoti ya Ukaguzi	Taasisi Zilizokaguliwa
	Maji, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, na Wakala wa Ugazaji Mafuta kwa Pamoja

**Chanzo:** Uchambuzi wa Wakaguzi katika Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi Mwaka 2024

#### 1.4 Mtazamo wa Ripoti ya Jumla

Ripoti hii inalenga kuwasilisha matokeo ya juhudi na shughuli mbalimbali za Serikali katika mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya rasilimaliwatu kama zinavyohusishwa na Malengo ya Maendeleo Endelevu sambamba na utekelezaji wa Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Kwa kutambua umuhimu wa ajenda hii katika kuleta mabadiliko kwenye maisha ya wananchi, Shirika la Kimataifa la Taasisi Kuu za Umma za Ukaguzi lilijumuisha Malengo ya Maendeleo Endelevu kama kipaumbele mtambuka katika Mpango-mkakati wake wa Mwaka 2017 hadi 2022 huku likitoa wito kwa wanachama wake kuchangia katika ufuatiliaji na mapitio ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ndani ya muktadha wa juhudi mahususi za maendeleo endelevu za kitaifa na mamlaka ya taasisi husika za ukaguzi.

Tanzania kama nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa, inashiriki utekelezaji wa Ajenda ya Mwaka 2030. Ajenda hii inasisitiza kuwapo kwa mpango jumuiishi wa hatua za kupata suluhisho la kiuchumi, kimazingira, na kijamii kwa ajili ya kufikia maendeleo endelevu unaojumuisha malengo 17 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu. Malengo ya Maendeleo Endelevu, pamoja na masuala mengine muhimu, yanaweka jitihada katika kukabiliana na umaskini na njaa, kupunguza ukosefu wa usawa, kujenga jamii zenye amani na haki, kukuza usawa wa kijinsia, na kulinda maliasili. Kwa kuwa Malengo ya Maendeleo Endelevu ni kabambe na yanaingiliana, mafanikio na kutumika kwake ni mchakato mgumu na unahitaji ushirikiano wa pamoja.

Kadhalika, kuzinduliwa kwa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 kama nyenzo ya kuelekeza juhudi za kitaifa katika kufanikisha malengo ya kiuchumi na kijamii, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeandaa Mpango wa Muda Mrefu wa Miaka 2011/12-2025/26. Utekelezaji wa Mpango huu umegawanywa katika awamu kuu tatu za mpango wa maendelo wa miaka mitano ambayo inalenga kuelekeza jitihada za kitaifa katika kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo kwa kuzingatia ukuaji wa uchumi ikiwa sambamba na kupunguza umaskini na kuleta maendeleo ya watu.

Mipango ya taifa ya maendeleo ya miaka mitano inaingiliana na inaandaliwa kulingana na maudhui. Maudhui ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa (2016/17-2020/21) ni “Kukuza viwanda kwa mageuzi ya kiuchumi na maendeleo

ya watu”. Maudhui ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa (2021/22-2025/26) ni “Kujenga uchumi shindani wa viwanda kwa maendeleo ya watu”.

Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa unalenga kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, ambayo ina lengo la kuigeuza Tanzania kuwa nchi yenye hadhi ya uchumi wa kipato cha kati na kuendeleza mageuzi ya kuwa nchi ya viwanda kufikia mwaka 2025. Jitihada za kuondoa umaskini na kuboresha hali ya maisha, utawala bora, na uwajibikaji zimejumuishwa kwenye Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa.

Kwa kuzingatia mamlaka na majukumu yao, taasisi za ukaguzi zina wajibu muhimu. Taasisi hizo ndio msingi wa kuwapo kwa taasisi zenye ufanisi, zinazowajibika, na shirikishi kwa maendeleo endelevu na zinazoweza kusaidia utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Hivyo, ripoti hii ya jumla imetokana na uchambuzi uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kutoka kwenye kaguzi 14 za ufanisi zilizotathmini athari za shughuli za Serikali katika kuwezesha kufikiwa kwa Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Malengo ya Afrika ya Mwaka 2063.

### 1.5 Umuhimu wa Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo unalenga kutumia rasilimali ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025. Dira hii inakusudia kuifanya nchi kuwa ya uchumi wa kipato cha kati na kuendeleza mageuzi ya kuwa nchi ya viwanda kufikia mwaka 2025. Ufikiaji wa Dira kutaifanya nchi kuwa na maisha bora na endelevu; kuwa na amani, utulivu na umoja; kuwa na uongozi bora na utawala wa sheria; kuwa na jamii iliyoelimika; na kuwa na uchumi imara na wenye ushindani.

Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo unalenga kutekeleza mipango-mkakati na makubaliano ya kisekta, kikanda, na kimataifa ikiwa pamoja na utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu yaliyopitishwa tarehe 25 Septemba 2015 na nchi wanachama 193 za Umoja wa Mataifa ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya jamii. Mipango hii ya maendeleo inaweka bayana orodha ya maeneo ya vipaumbele na shughuli za kimkakati ambazo ni muhimu ili kuimarisha kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu.

Malengo ya Maendeleo Endelevu yamejumuishwa malengo 17 na shabaha 169 yanayoelekeza hatua za Serikali, mashirika ya kimataifa, asasi za kiraia, na mashirika mengine katika kipindi cha miaka 15 (2016 - 2030).

Ajenda inaweka mkakati wa siku zijazo, ikiongoza ulimwengu kuelekea njia endelevu zaidi na thabiti. Inaelekeza pia mabadiliko ya viwango vya maisha na mapito kwa njia jumuishi zaidi za maendeleo zenye nguvu na endelevu.

Kadhalika, malengo 17 ya malengo tarajiwa ya Malengo ya Maendeleo Endelevu yanalenga kuhakikisha kunakuwa na kazi zenye staha na ukuaji kiuchumi; kunakuwa na viwanda, uvumbuzi, na miundombinu; kupunguza matabaka; kuwa na miji na jamii endelevu; kuwa na matumizi na uzalishaji bora; kuchukua hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; kuhifadhi maisha ya viumbe chini ya maji na juu ya ardhi; kuwa na amani, haki na taasisi imara; na kuwa na ushirika wa malengo.

Malengo haya yote yamehusishwa kwenye maeneo makuu matatu ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ambayo ni malengo ya uchumi, jamii, na mazingira.

## 1.6 Uhalali wa Ukaguzi

Kama moja ya nchi zilizosaini Ajenda ya Mwaka 2030 kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu, Tanzania imechukua hatua za kujumuisha ajenda hii katika muktadha wa kitaifa. Wakati wa uanzishaji wa Ajenda ya Mwaka 2030, Tanzania ilikuwa ikiandaa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano, hivyo sehemu ya malengo ya maendeleo endelevu yaliakisiwa katika mpango huo.

Aidha, kupitia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Tanzania imejiwekea matarajio ya kufanikisha lengo la kuwa na ukuaji wa uchumi kwa angalau asilimia 8 kwa mwaka. Kiwango hicho cha ukuaji kinachukuliwa kuwa muhimu katika kupunguza umaskini na kuisukuma Tanzania kutoka nchi isiyoendelea hadi nchi ya uchumi wa kipato cha kati yenye kiwango cha juu cha maendeleo ya binadamu. Dira ya Taifa ya Maendeleo ina maono ya kubadili uchumi ambao awali ulitegemea uzalishaji wa chini wa kilimo hadi kufikia uchumi wa kilimo wenye tija.

Ili Malengo ya Maendeleo Endelevu yafikiwe, kila mmoja, kama vile Serikali, Bunge, sekta binafsi, asasi za kiraia, na mtu mmojammoja, anapaswa kutimiza wajibu wake.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kama mkaguzi wa nje wa Serikali, ni kiungo muhimu katika kuhakikisha kuwa Serikali inatekeleza wajibu wake wa kutoa huduma zinazohitajika kwa wananchi na kulijulisha Bunge kuhusu utendaji wa serikali na hatua zinazopaswa kuchukuliwa kuhakikisha kuwa Malengo ya Maendeleo Endelevu yanafikiwa.

Hivyo, ili kuitikia wito huo wa kuchangia kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeunganisha ukaguzi wake wa ufanisi na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030. Kadhalika, Ofisi ya Taifa ya

Ukaguzi imeunganisha ukaguzi wake wa ufanisi na maeneo ya vipaumbele na shughuli za kimkakati za Mpango wa Maendeleo wa Taifa ili kutathmini utekelezaji wake na kutoa mapendekezo ya maboresho zaidi. Baadhi ya malengo hayo yameguswa katika kaguzi 14 zilizofanyika.

### 1.7 Mchakato wa Uthibitisho wa Takwimu na Taarifa Zilizotolewa


Ukaguzi wa ufanisi ulifanywa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Taasisi za Ukaguzi kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi. Viwango hivyo vinaitaka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kupanga na kufanya ukaguzi ili kupata ushahidi wa kutosha na unaofaa utakaokuwa msingi mzuri wa matokeo, hitimisho, na mapendekezo kulingana na lengo au malengo ya ukaguzi.

Kwa kuzingatia kanuni za ukaguzi, wakaguliwa wote walipewa fursa ya kujadili na kutoa maoni yao kuhusu matokeo ya ukaguzi na kusahihisha makosa yaliyojitokeza katika rasimu ya ripoti hii. Wakaguliwa hao ni pamoja na Wizara ya Kilimo; Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi; Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Mambo ya Ndani; Wizara ya Afya; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, na Watu Wenye Mahitaji Maalumu; Wizara ya Madini; Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia; Wizara ya Maliasili na Utalii; Wizara ya Nishati na taasisi zake kama vile Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji; Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania na Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja; bodi za mazao; Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania; Jeshi la Magereza; Mamlaka ya Udhubiti wa Mbolea; Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu; Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi; Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba; na Kitengo cha Uhifadhi wa Bahari na Maeneo Tengefu.

## 1.8 Muundo wa Ripoti

Ripoti hii ina sura 10 kama zilivyooneshwa kwenye Kielelezo Na. 2:

**Kielelezo Na. 2: Mpangilio wa Sura Zilizounda Ripoti Hii**



# SURA YA PILI

## MAELEZO YA MPANGO WA PILI NA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO NA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU

### 2.1 Utangulizi


Sura hii inahusu maelezo ya Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu. Masuala muhimu yanayoelezewa ni taasisi muhimu na mfumo wa kisheria unaosimamia utekelezaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano; wahusika wakuu katika utekelezaji wa Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano; na mikakati ya utekelezaji wa Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Masuala mengine yanayoangaziwa ni ukaguzi wa ufanisi uliofanyika kuhusiana na Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu; na mifumo ya ufadhili katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya taifa ya miaka mitano.

### 2.2 Usuli kuhusu Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Mwaka 1999 Tanzania ilizindua Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 ambayo ni nyenzo ya kuunganisha juhudi za taifa katika kufikia malengo ya maendeleo tarajiwa ya kijamii na kiuchumi. Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 unafanyika kupitia Mpango Elekezi wa Muda Mrefu wa Miaka 25 kuanzia mwaka 2011/12 - 2025/26.

Zaidi, mwaka 2015 Tanzania iliingia makubaliano ya Malengo ya Maendeleo Endelevu, ambapo yalijumuishwa kwenye Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, mipango mkakati, na mipango ya mwaka ya taasisi za Serikali. **Kielelezo Na. 3** kinaonesha uhusiano wa mikakati na mipango na mikakati ya kitaifa.

**Kielelezo Na. 3: Uhusiano wa Mikakati na Mipango ya Kitaifa**



Utekelezaji wa Mpango Elekezi wa Muda Mrefu kwa kipindi cha mwaka 2011/12-2025/26 uligawanywa katika mipango ya maendeleo ya miaka mitanomitano, ambapo kila mpango ulikuwa na maudhui mahususi kama inavyofafanuliwa hapa chini.

**Maudhui mahususi ya Mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano**


Mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano ina maudhui mahususi tofauti ambayo inaweka umuhimu kwenye jambo ambalo linatekelezwa na tasisi husika ya Serikali.

Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2011/12-2015/16 uliokuwa na dhima ya “Kufungua Fursa Fiche za Ukuaji wa Uchumi”, uliainisha maeneo ambayo, kama hatua zingechukuliwa, zingefungua fursa za kiuchumi. Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17-2020/21 ulikuwa na dhima ya “Kujenga Uchumi wa Viwanda”. Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26) wenye dhima ya “Kujenga Uchumi Shindani wa Viwanda kwa Maendeleo ya Watu”, una lengo la kuakisi malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya kujenga uchumi shindani ambao ni imara, wa kipato cha kati, wa viwanda, na unaoweza kushindana kikanda na kimataifa bila kupoteza lengo la kuleta maendeleo ya watu.

Mipango hii ya maendeleo inalenga kujenga msingi wa kuibadilisha Tanzania ili kuhakikisha makubaliano ya kimataifa na kikanda (k.m. Ajenda ya Afrika ya Mwaka 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu) yameingizwa katika mipango ya maendeleo ya taifa na mifumo ya utekelezaji wa mipango hiyo.

**Kielelezo Na. 4** hapa chini kinatoa muhtasari wa kila mpango wa maendeleo na maudhui yake mahususi.

**Kielelezo Na. 4: Maelezo kwa Ufupi ya kila Maudhui Mahususi kutoka kwenye Mipango ya Maendeleo ya Taifa**



*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi Mwaka 2024 kutoka kwenye Mikakati ya Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano*



### *Uhusiano wa Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano*

Kama mwanachama wa Umoja wa Mataifa, Tanzania inatakiwa kutekeleza seti 17 za Malengo ya Maendeleo Endelevu ili kufikia maendeleo endelevu ya watu. Malengo ya Maendeleo Endelevu yanashabihiana na ni kabambe, ambayo yanalenga kutatua changamoto za kimaendeleo zinazowakabili Watanzania na dunia kwa ujumla. Changamoto hizo zinataka kuchukuliwa kwa hatua za kutokomeza njaa na kulinda mazingira na tabianchi<sup>1</sup>.

Wizara ya Fedha na Mipango imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kuhakikisha kuwa Malengo ya Maendeleo Endelevu yanajumuishwa katika muktadha wa kitaifa na kutekelezwa ipasavyo. Juhudi zimefanywa ili kuhakikisha kuwa Malengo ya Maendeleo Endelevu yameingizwa katika mipango na mikakati ya kissekta. Hivyo, utekelezaji wa mikakati ya maendeleo ya kitaifa pia utaathiri mafanikio ya Malengo ya Maendeleo Endelevu na malengo ya kitaifa ya maendeleo. Katika kuhakikisha kuwa kuna utekelezaji mzuri wa Malengo ya Maendeleo Endelevu nchini, Kundi la Bunge la Maendeleo Endelevu (PGSD) limepewa jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika ngazi ya mitaa na kutoa maoni na miongozo ya mara kwa mara.

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ina wajibu wa kuhakikisha kuwa malengo haya ya mipango ya maendeleo na Malengo ya Maendeleo Endelevu si tu yanafikiwa bali pia kanuni za tija, ufanisi, na uwekevu zinadumishwa kwa kiwango cha juu na taasisi zinazohusika wakati wa utekelezaji wa programu na shughuli zitakazoweza kufikiwa kwa malengo hayo.

### **2.3 Miongozo Muhimu na Mfumo wa Kisheria Unaosimamia Utekelezaji wa Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano**

Miongozo muhimu na mfumo wa kisheria unaosimamia utekelezaji wa Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unajumuisha sera, mipango-mkakati, na bajeti kwa taasisi zenye dhamana ya utekelezaji. Kadhalika, kila sekta ya uchumi imeendelea kuongozwa na sheria zao. Hivyo, utekelezaji wa Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unaongozwa na sheria ambazo zipo chini ya wizara, idara na wakala husika, tawala za mikoa, mamlaka za serikali za mitaa, mashirika ya umma na bodi mbalimbali, na wadau wengine. Vyombo, mifumo ya kisheria, na wadau


---

<sup>1</sup> <https://sustainabledevelopment.un.org/memberstates/tanzania>, Sustainable Development Goal (SDG) Implementation, Follow-up and review in Tanzania - 2017

muhimu katika utekelezaji wa Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano wamefafanuliwa hapa chini.

**Kielelezo Na. 5** kinaelezea baadhi ya sheria muhimu katika utekelezaji wa Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

**Kielelezo Na. 5: Miongozo Muhimu na Mfumo wa Kisheria katika Usimamizi wa Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano**


	<p>Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sura ya Pili, ya Mwaka 1977</p>	<p>Kwa niaba ya wananchi, kwa lengo la kujenga jamii na kuhakikisha kuwa Tanzania inaongozwa na Serikali ambayo inazingatia misingi ya demokrasia na kuhusisha wananchi kwenye kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo</p>
	<p>Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2004</p>	<p>Sheria ya Fedha inatoa mwongozo wa kiutendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango chini ya usimamizi wa Mhasibu Mkuu wa Serikali na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali</p>

*Chanzo: Uchambuzi wa Ukaguzi Mwaka 2024*

## 2.4 Watendaji Muhimu katika Utekelezaji wa Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

Utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kitaifa ya miaka mitano unagusa wizara, idara, wakala mbalimbali za serikali, tawala za mikoa, mamlaka za serikali za mitaa, mashirika ya umma, bodi mbalimbali, na wadau wengine katika utekelezaji wa shughuli za kila siku zilizopagwa katika mipango yao ya maendeleo ya kila mwaka. Utekelezaji umegawanyika katika ngazi zote zikiwemo uratibu, utekelezaji, na ufuatiliaji na tathmini ya mafanikio ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 6** hapa chini.

## Kielelezo Na. 6: Watendaji Muhimu na Majukumu Yao katika Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano




*Chanzo: Uchambuzi wa Ukaguzi Mwaka 2024*

### 2.5 Mikakati ya Utekelezaji wa Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

Mikakati inayoongoza mageuzi ya kitaasisi na kisera katika utekelezaji wenye tija wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano inajumuisha Mpango wa Utekelezaji - Sehemu ya Kwanza; Mkakati wa Fedha - Sehemu ya Pili; Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini - Sehemu ya Tatu; na Mkakati wa Mawasiliano - Sehemu ya Nne. Mikakati hii imeainisha maeneo muhimu ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Mikakati hii ni kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 7** hapa chini.

**Kielelezo Na. 7: Muhtasari wa Mikakati ya Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano**



*Chanzo: Uchambuzi wa Ukaguzi kutoka kwenye Mikakati ya Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo Mwaka 2024*

**(a) Mpango wa Utekelezaji - Sehemu ya Kwanza**

Mpango huu unaelezea maeneo ya kuzingatia na vipaumbele vya miradi ya kimkakati. Mpango-kazi pia unaonesha maendeleo na hali ya maeneo au miradi, changamoto na fursa, malengo ya utekelezaji, shabaha, shughuli, muda wa utekelezaji, chanzo cha fedha, majukumu, na wadau mbalimbali.

**(b) Mkakati wa Fedha - Sehemu ya Pili**

Mkakati huu unaonesha utekelezaji na makusanyo ya fedha kwa vyanzo vya kawaida na vipya kwa ajili ya kugharamia Mpango. Mkakati pia unajumuisha mafunzo na uzoefu kutoka nchi zilizochaguliwa na hatua zilizopendekezwa kuchukuliwa ili kutambua kiasi kilichokadiriwa cha kugharamia Mpango.

### (c) Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini - Sehemu ya Tatu

Mkakati huu ni chombo cha usimamizi wa matokeo chenye kusisitiza uratibu, uzingatiaji wa muda, viashiria vya utendaji, utoaji wa maoni, na taratibu za usahihishaji wa utekelezaji. Mkakati huu unaonesha ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

### (d) Mkakati wa Mawasiliano - Sehemu ya Nne

Mkakati huu unafafanua mbinu inayopaswa kutumika kuhakikisha kuna mtiririko mzuri wa taarifa na kukuza ushirikiano kwa wadau wote katika kipindi chote cha utekelezaji na baadaye kujadili matokeo yaliyotarajiwa na athari za utekelezaji wake.

## 2.6 Ukaguzi wa Ufanisi Uliofanyika na Uhusiano Wake na Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Kwa mwaka wa fedha 2021/22, nimefanya kaguzi 14 za ufanisi ambazo zinaelezea utekelezaji wa Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Maudhui ambayo yamehusishwa kwenye kaguzi hizi ni yale yanayohusiana na maendeleo ya watu na mageuzi ya kiuchumi kama yalivyoainishwa kwenye Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Mipango yote hii imeweka maeneo ya vipaumbele ambayo ni muhimu katika kuhakikisha utekelezaji wake madhubuti.


Maeneo ya vipaumbele kwa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ni kuimarisha ukuaji wa viwanda kwa mageuzi ya kiuchumi; kuchochea maendeleo ya watu; kuboresha mazingira rafiki ya uendelezaji biashara; na ufanisi wa utekelezaji. Kadhalika, maeneo ya vipaumbele kwa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ni kuchochea uchumi shirikishi na shindani; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; kukuza uwekezaji na biashara; kuchochea maendeleo ya watu; na kuendeleza ujuzi.

Maendeleo ya watu yanalenga kufanikisha kufikiwa kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mipango ya Maendeleo ya Taifa. Dhima ya maendeleo ya watu ni kuboresha hali za watu katika nyanja zote za umma, binafsi, jamii, siasa, na uchumi. Mageuzi ya kiuchumi yanazitaka nchi kufanya maboresho ya sera za kiuchumi kwa kuzingatia ushirikishaji, mageuzi mbalimbali ya ajira za kutosha ambazo zitajumuisha watu wote, kulinda dunia, na kuimarisha misingi ya ekolojia katika nyanja ya uchumi.

Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Pili na wa tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ni nyenzo zilizokubalika katika kutathmini maendeleo ya uchumi na watu kimataifa na kitaifa. Muhtasari wa kaguzi za ufanisi zilizofanywa na maudhui yake kwa kuzingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu zinawasilishwa hapa chini.

**Kielelezo Na. 8** kinaonesha muhtasari wa kaguzi za ufanisi zilizofanyika zikihusianishwa na Malengo ya Maendeleo Endelevu na maeneo ya kipaumbele ya Mpango wa Pili na wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na afua zake kama ilivyowasilishwa hapa chini na maelezo yake katika **Kiambatisho Na. I.**

**Kielelezo Na. 8: Kaguzi za Ufanisi Zilizofanyika Zikihusisha Maudhui ya Malengo ya Maendeleo Endelevu pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano**



Chanzo: Malengo ya Maendeleo Endelevu, Mpango wa Pili na wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano, na Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi

## 2.7 Ugharamiaji wa Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano

Kwa mujibu wa Mkakati wa Fedha wa Mwaka 2018 wa Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka wa Mitano, mafanikio ya mpango ambayo yamejikita katika kuimarisha mabadiliko ya kiuchumi, maendeleo ya watu, maendeleo ya viwanda, na kukuza ufanisi wa utekelezaji yanabebwa na ukusanyaji bora wa rasilimali-fedha na mapato, na utaratibu mzuri wa ugharamiaji.

Ugharamiaji wa utekelezaji unajumuisha vyanzo vya kawaida vya kodi na mapato na vyanzo vipya vya fedha. Chanzo cha kawaida cha fedha kinajumuisha mapato ya kodi, mapato yasiyo ya kodi, ukopaji wa ndani, na fedha za nje. Vyanzo vipya vya fedha pia vimeanzishwa ili kujazia vyanzo vya kawaida. Vyanzo hivi vinajumuisha vyanzo vya fedha vya ndani na nje kupitia fursa zinazohusiana na bidhaa mpya, ambazo zinajumuisha dhamana ya soko la nje; dhamana za mamlaka za serikali za mitaa/dhamana za manispaa; ufadhili wa mabadiliko ya tabianchi; taasisi za fedha za maendeleo; Mfuko wa Usawa wa Pensheni; ubia wa sekta binafsi na umma; na uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje.



# SURA YA TATU



## UPATIKANAJI WA HUDUMA BORA ZA AFYA

### 3.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi yanayotokana na ripoti za ukaguzi wa ufanisi zinazohusiana na upatikanaji wa huduma za afya ya akili pamoja na udhibiti wa vifaatiba katika vituo vya afya vya umma nchini. Sura hii pia inaelezea eneo la ukaguzi, vyombo vya serikali vinavyohusika katika ukaguzi; na uhusiano wa eneo la ukaguzi na Malengo ya Maendeleo Endelevu, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Kaguzi hizi za ufanisi ni Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Upatikanaji wa Huduma za Afya ya Akili; ma Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Udhibiti wa Vifaatiba katika Vituo vya Afya vya Umma.

#### 3.1.1 Usuli Kuhusu Upatikanaji wa Huduma Bora za Afya

Kwa mujibu wa Taarifa ya Utendaji wa Sekta ya Afya ya Wizara ya Afya ya Mwaka 2022, Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili ya Mirembe ilikuwa na ongezeko la wagonjwa waliohudhuria matibabu ya magonjwa ya akili kutoka wagonjwa 3,472 mwaka 2019 hadi wagonjwa 5,060 mwaka 2022, sawa na asilimia 31 ya wagonjwa wa akili. Pia, Muhtasari wa Hali ya Afya ya Akili Tanzania ya Mwaka 2020 inakadiria kuwa mzigo wa magonjwa ya akili umechangia kiwango cha vifo vinavyotokana na kujiua kwa kiwango cha 8.15 kwa kila watu 100,000. Vilevile, Ripoti ya Utendaji wa Sekta ya Afya ya Mwaka 2022 ya Wizara ya Afya inakadiria mzigo wa magonjwa ya akili umeongezeka kutoka wagonjwa 386,358 mwaka 2012 hadi wagonjwa 2,102,726 mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 82.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani wa Vifaatiba: Mwongozo wa Hatua kwa Hatua wa Mwaka 2016, udhibiti wa vifaatiba unajumuisha shughuli za kuhakikisha vifaa ni bora, salama, na vyenye ufanisi. Hujumuisha michakato inayoanzia kwenye utengenezaji, ununuzi, usakinishaji, ufanyaji kazi, udumishaji, na uondoshaji wa vifaatiba ambavyo havifai tena kwa matumizi.

Vilevile, udhibiti sahihi wa vifaatiba husaidia usimamizi wa vituo vya afya kuendeleza na kufuatilia vifaatiba vyao na kuhakikisha usalama na utendaji wake.

Kwa mantiki hiyo, katika mwaka 2020, Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Afya ilitumia kiasi cha shilingi bilioni 68.706 kununua vifaatiba kwa ajili ya vituo vya afya vilivyopo katika mamlaka 22 za serikali za mitaa kote nchini ili kutekeleza Sera ya Taifa ya Afya ya Mwaka 2017. Kwa kuzingatia ukweli huu, ni muhimu kusimamia vizuri vifaatiba ili kupata thamani ya fedha wakati wa kuhakikisha utoaji wa huduma za afya kwa ubora uliokusudiwa.

### 3.1.2 Uhusiano kati ya Huduma za Afya na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano

Lengo la tatu la Malengo ya Maendeleo Endelevu ya kuhakikisha afya na ustawi wa akili ikiwa pamoja na kuzuia kujiua kama ilivyoelezwa katika Lengo la 3.4.2 la Malengo ya Maendeleo Endelevu, linataka, kufikia mwaka 2030, kupunguza kwa theluthi moja vifo vya mapema vinavyosababishwa na magonjwa yasiyo ya kuambukiza kwa kuzuia, kutibu, na kuimarisha afya na ustawi wa akili ikiwa pamoja na kupunguza idadi ya vifo vinavyotokana na kujiua.

Hatua muhimu katika Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano zilikuwa kujenga na kukarabati vituo vya afya jumuishi; kuhakikisha upatikanaji wa dawa, vifaatiba, vitendanishi, chanjo na vifaa vya dawa; kuimarisha huduma maalumu na za kibingwa katika hospitali zote za rufaa za mikoa, hospitali maalumu, na hospitali za kitaifa; na kukuza na kusaidia uanzishaji wa chanjo, dawa, na viwanda vya utengenezaji wa vifaatiba. **Jedwali Na. 2** linatoa muhtasari wa maeneo ya mkakati wa afya na shughuli zake muhimu.

**Jedwali Na. 2: Maeneo ya Mkakati wa Afya na Shughuli Zake**

Maeneo ya Mkakati	Malengo	Programu	Shughuli Muhimu	Matokeo
Kuimarisha huduma maalumu na za kibingwa katika hospitali za kanda, maalumu na taifa	Wagonjwa wanaopewa rufaa kwenda nje ya nchi kwa mwaka kupungua kutoka asilimia 40 hadi asilimia 20 ifikapo mwaka 2025	Kuimarisha huduma maalumu na bobezi	Ununuzi wa vifaatiba vya huduma maalumu na bobezi	Kununuliwa kwa vifaa kwa ajili ya huduma maalumu za kibingwa
	Asilimia 100 ya hospitali za		Kutoa mafunzo kwa watoa huduma 70 wa	

	kitaifa na kanda kutoa huduma za kitaalamu za kibingwa kufikia mwaka 2025		afya waliobobea sana katika maeneo ya moyo, saratani, figo, upasuaji wa neva, mifupa, magonjwa ya tumbo, magonjwa ya mfumo wa neva, radiolojia ya kuingilia kati.	huduma za kibingwa
Kukuza na kuinua uanzishaji wa chanjo, dawa, na viwanda vya vifaatiba	Uingizaji wa chini ya asilimia 50 ya bidhaa za afya kutoka nje ya nchi	Uzalishaji wa ndani wa bidhaa za afya	Kununua, kuhifadhi, na kusambaza dawa, vifaatiba, vitendanishi, na chanjo	Uanzishaji wa kiwanda cha Serikali cha chanjo za binadamu
Kuelimisha jamii kuhusu hatua za tahadhari na utambuzi wa mapema wa magonjwa yasiyoambukiza.	Kutoka asilimia 40 hadi asilimia 60	Udhibiti wa magonjwa yasiyoambukiza	Hazijaainishwa katika Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo.	Utambuzi wa magonjwa, uelimishaji na kukuza uelewa

*Chanzo: Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22- 2025/26)*

### 3.1.3 Mikakati na Jitihada za Serikali katika Usimamizi wa Huduma za Afya

Serikali imeweka mikakati muhimu ya kuboresha sekta ya afya kama inavyoelezwa katika **Kielelezo Na. 9** hapa chini.

**Kielelezo Na. 9: Mikakati na Jitihada za Serikali katika Usimamizi wa Huduma za Afya**

<p><b>Mpango mkakati wa Sekta ya Afya (V) (Julai 2021 - Juni 2026)</b></p>	<p>Mpango-mkakati huu unalenga kupunguza magonjwa na wifo vitokanavyo na magonjwa yasiyoambukiza kwa kutekeleza na kuchochea hatua za kujikinga zinazoshughulikia mambo yanayohusiana na mitindo ya maisha, mazingira, na viashiria hatarishi vya afya ya akili. Mkakati unalenga kuzingatia ubora wa huduma, ambayo itahakikisha upatikanaji wa huduma muhimu za afya na hatua za kibingwa, ambazo zinajumuisha huduma za kutosha za uchunguzi. Mkakati unalenga kuimarisha taratibu za matengenezo na ukarabati wa vifaatiba</p>
<p><b>Mpango mkakati na Utekelezaji wa Mpango wa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza (2016 - 2020)</b></p>	<p>Mkakati huu ulilenga kuboresha huduma za tiba kupitia huduma za uchunguzi na ubora wa huduma za afya katika vituo vyote vya afya. Mkakati huu ulilenga pia kuimarisha usimamizi wa maabara, matengenezo ya vifaatiba katika ngazi zote za vituo vya afya, huduma bora za radiolojia katika ngazi zote, na udumishaji wa vifaatiba katika vituo vyote vya afya.</p>
<p><b>Mpangomkakati na Utekelezaji wa Mpango wa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza Tanzania (2016 - 2020)</b></p>	<p>Mpango huu unaweka mkakati kamili wa kukabiliana na masuala ya afya ya akili na matumizi mabaya ya dawa, kutambua athari zao muhimu kwa ustawi wa umma. Kupitia mchanganyiko wa hatua za kuzuia, taratibu za matibabu, na mipango inayolenga kukua ustawi wa akili, mpango huu unalenga kupunguza athari mbaya za magonjwa yasiyoambukizwa kwenye jamii. Hatua za kimkakati zilizoainishwa katika mpango huu ni kuimarisha upatikanaji wa rasilimali za kutosha kwenye magonjwa hayo ili kupambana na ongezeko lake.</p>

## 3.2 Malengo ya Ukaguzi na Mawanda

### 3.2.1 Malengo ya Ukaguzi

Lengo kuu la ukaguzi huu lilikuwa kutathmini na kubaini iwapo Wizara ya Afya imehakikisha upatikanaji wa huduma za afya ya akili na usimamizi wa vifaatiba ili kuhakikisha utoaji madhubuti wa huduma za afya.

Hususan, ukaguzi ulitathmini iwapo:

- (i) Wizara ya Afya; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, na Makundi Maalumu; na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wamehakikisha upatikanaji wa huduma za afya ya akili ili kuhakikisha watu wenye uhitaji wanapata kwa wakati huduma zinazostahili za afya ya akili; na
- (ii) Wizara ya Afya na Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania wamesimamia ipasavyo vifaatiba ili kuhakikisha usalama na ubora wa huduma za afya zinazotolewa na vituo vya umma vya afya nchini.

### 3.2.2 Mawanda ya Ukaguzi

Taasisi kuu, ambazo ukaguzi huu wa ufanisi ulifanyika kuhusu upatikanaji wa huduma za afya ya akili ni Wizara ya Afya; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, na Makundi Maalumu; na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mtazamo wa ukaguzi ulikuwa kutathmini upatikanaji wa huduma za afya ya akili nchini, hususan njia za utambuzi wa watu wenye changamoto ya afya ya akili; utoaji wa huduma za kisaikolojia katika ngazi ya jamii; upatikanaji wa rasilimali za kutosha (miundombinu, wataalamu, vifaatiba, na dawa); utoaji wa huduma za urekebu; na utoaji wa elimu na uratibu kati ya watendaji kuhusu utoaji wa huduma za afya ya akili na huduma ya kisaikolojia nchini. Mawanda ya ukaguzi yalikuwa miaka mitano (5) ya fedha kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2022/23.

Wakati huohuo, katika ukaguzi wa utendaji wa udhibiti wa vifaatiba katika vituo vya afya ya umma, taasisi zilizokaguliwa ni Wizara ya Afya na Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania (TMDA). Ukaguzi ulitathmini jinsi vifaatiba vinavyodhibitiwa na kusimamiwa wakati wote wa uhai wake, ikijumuisha idhini ya kabla ya uuzaji, wakati wa uuzaji, matengenezo, ufuatiliaji wa utendaji, na uondoshaji wa vifaa vya tiba visivyofanya kazi. Pia, ulitathmini ufanisi wa uratibu kati ya Wizara ya Afya, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania, na watoa huduma za afya katika kudhibiti vifaatiba. Ukaguzi ulihusisha kipindi cha miaka minne ya fedha, kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2022/23.

### 3.3 Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Upatikanaji wa Huduma za Afya ya Akili

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi wa ufanisi kuhusu upatikanaji wa huduma za afya ya akili.

#### 3.3.1 Upatikanaji mdogo wa huduma za afya ya akili kwa ngazi ya msingi ya afya

Ukaguzi ulibaini kuwa huduma za afya ya akili hazikujumuishwa kikamilifu kwenye huduma za afya ya msingi katika mikoa iliyotembelewa. Ukaguzi huu ulibaini kuwa hospitali tano za wilaya zilizotembelewa hazikuwa na kitengo cha afya ya akili ambacho kilipaswa kiwe na Mganga Msaidizi mmoja na wauguzi wawili wa magonjwa ya afya ya akili na Ofisa mmoja wa ustawi wa jamii. Ni hospitali mbili tu kati ya tano za wilaya zilizotembelewa, yaani, Hospitali ya Wilaya ya Igawilo na Hospitali ya Wilaya ya Kivule ndizo zilikuwa na wauguzi wa afya ya akili ambao ni watumishi waliopatiwa mafunzo kwenye eneo hilo.

Pia, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa huduma za afya ya akili zilijumuishwa vizuri katika hospitali za taifa na maalumu, ambapo kati ya hospitali tatu za kanda zilizotembelewa, ni hospitali moja tu ndiyo haikujumuisha huduma za afya ya akili. Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Benjamin Mkapa, Dodoma haikuwa imejumuisha kikamilifu huduma za afya ya akili kutokana na kutokuwapo kwa wataalamu wa eneo hilo na kukosekana kwa miundombinu ya kutoa huduma za afya ya akili kama vile wodi.

Ujumuishaji hafifu wa huduma za afya ya akili katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Benjamin Mkapa kuliathiri wagonjwa ambao walihitaji wataalamu wawili, mmoja akiwa wa huduma za afya ya akili. Wizara ya Afya ilipoulizwa kuhusu kukosekana kwa huduma za afya ya akili katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, ilieleza kuwa wagonjwa waliopelekwa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Benjamin Mkapa walihamishiwa Hospitali ya Taifa ya Akili ya Mirembe kwa sababu hospitali hiyo iko karibu na Hospitali ya Rufaa ya Benjamin Mkapa. Hatu hii ilibainika kuwa kinyume na kiwango cha msingi cha mahitaji ya uanzishaji wa vituo vya afya kwa utoaji wa huduma.

#### 3.3.2 Utambuzi wa watu wenye changamoto ya afya ya akili haukufanyika kwa ufanisi katika ngazi ya jamii

Ukaguzi huu ulibaini ukosefu wa utambuzi wa watu wenye matatizo ya afya ya akili katika ngazi ya jamii. Badala yake, utambuzi ulilenga waathirika wa dawa za kulevya, wazee, walemavu, watoto walio katika mazingira magumu, na wale wanaokabiliwa na mimba za utotoni. Hali hii imechangiwa na ukosefu wa fedha za kutosha kwa ajili ya huduma za ustawi wa jamii na kukosekana kwa Maofisa

ustawi wa jamii katika ngazi za chini, ikiwemo vijiji na mitaa. Kuna asilimia 2.8 tu ya Maofisa ustawi wa jamii kati ya wanaohitajika katika ngazi ya kata na hakuna hata mmoja katika ngazi ya kijiji, hivyo kusababisha kutotambulika kwa watu wenye matatizo ya afya ya akili. Hali hii inazuia uwezo wa Maofisa kutambua watu wenye matatizo ya afya ya akili.

Aidha, licha ya kuwapo kwa watu wenye changamoto ya akili, ambao walishuhudiwa katika mitaa ya majiji ya Dodoma na Dar es Salaam, hawakutambuliwa na kupewa huduma za msaada wa kisaikolojia na rufaa zinazofaa. Ukaguzi haukuona ushahidi wowote wa rufaa za watu wenye matatizo ya afya ya akili katika ngazi za chini zilizotambuliwa hadi ngazi zinazofaa za huduma. Hali hii ni kinyume na Sehemu ya 2.1.4 ya Mwongozo wa Huduma za Msaada wa Kisaikolojia na Jamii katika kiwango cha ngazi za chini zilizotambuliwa ambayo inaelekeza utoaji wa ushauri kuhusu wagonjwa wa rufaa wanaohitaji huduma za kiwango cha juu zaidi za kisaikolojia na msaada au matibabu. Kwa kuongezea, ilibainika kwamba hakukuwa na kumbukumbu au nyaraka zilizohifadhiwa kufuatilia maendeleo ya wagonjwa wa afya ya akili.

Hali hii ilihusishwa na ushirikiano na utaribu hafifu baina ya watoa huduma kutokana na ukosefu wa muundo wa kuripoti na ripoti za utekelezaji wa maelekezo ya wagonjwa kwenda kwenye kiwango cha huduma kinachofuata. Hali hii iliyosababishwa na uhaba wa wataalamu waliopata mafunzo ya afya ya akili katika ngazi za chini, ilizuia mchakato wa rufaa. Wakati vituo vya huduma katika ngazi za vituo vya afya na Maofisa wa ustawi wa jamii wa kata vina usambazaji mdogo wa taarifa, kunaweza kuwa na changamoto za kuhakikisha rufaa zinazofuata zina mtiririko sahihi na kufuatilia maendeleo ya wagonjwa.

### 3.3.3 Ukosefu wa huduma za kisaikolojia na usaidizi katika ngazi ya jamii

Kifungu cha 3.0.5 cha Mwongozo wa Kitaifa wa Huduma na Usaidizi wa Kisaikolojia katika Ngazi ya Kijiji/Mtaa kinaeleza kuwa utoaji na uratibu wa huduma za msaada wa kisaikolojia na jamii hufanyika katika ngazi ya kijiji/mtaa. Maofisa ustawi wa jamii katika ngazi hii wanatoa huduma za msaada wa kisaikolojia na jamii na wana jukumu muhimu katika kuhakikisha kuwa watoa huduma wengine wote wanazingatia Mwongozo wa Kitaifa wa Huduma na Usaidizi wa Kisaikolojia. Pia, wana jukumu muhimu katika kuamua mwitikio wa huduma za msaada wa kisaikolojia na jamii na kujibu hoja maalumu za wanufaika.

Ukaguzi ulibaini kuwa huduma za kisaikolojia na usaidizi hazikupatikana kwa wakati katika sehemu zilizotambulika. Pia, huduma hazikutolewa kwa wakati kwa watu wanaohitaji kutokana na uhaba wa Maofisa ustawi wa jamii na

rasilimali-fedha; na ufuatiliaji duni wa huduma hizi katika mamlaka za serikali za mitaa. Pia, ukaguzi ulibaini kutokuwapo kwa miundombinu kama vile ofisi zinazotoa urahisi wa huduma kwa ajili ya utunzaji wa siri wa masuala yanayojadiliwa na Maofisa ustawi wa jamii wenye jukumu la kutoa huduma za msaada wa kisaikolojia na kamii. Kwa mfano, wakati wa ziara kwenye mamlaka za serikali za mitaa, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa Maofisa ustawi wa jamii waliokuwa wanaotoa huduma za msaada wa kisaikolojia na kijamii walilazimika kuchangia vyumba vya ofisi na Maofisa wengine. Utaratibu huu ulihitaji Maofisa ustawi wengine kuondoka kwenye chumba cha ofisi wakati wowote mteja alipohitaji unasihi ili kuhakikisha faragha na nafasi ya kikao.

Ukosefu wa huduma za kisaikolojia katika ngazi ya jamii ulikuwa na athari pana za kiafya ya jamii, kwani masuala ya afya ya akili yasiyotibiwa yalisababisha kuongezeka kwa matumizi mabaya ya dawa za kulevya na pombe. Ufikiwaji kwa wakati unaofaa wa msaada wa kisaikolojia ni muhimu kwa ajili ya kuzuia mapema matumizi mabaya zaidi ya dawa na pombe.

**(a) *Huduma za kisaikolojia na usaidizi hazikuingizwa kwa ufanisi katika mipango, bajeti, sera, programu, na mikakati katika ngazi zote***

Ukaguzi ulibaini kuwa huduma za kisaikolojia na usaidizi hazikuingizwa kwa ufanisi katika mipango, bajeti, sera, hatua, na mikakati katika ngazi zote. Ukaguzi ulibaini kuwa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa haikujumuisha huduma za kisaikolojia katika mipango yake. Upungufu huu ulisababisha kutofikiwa kwa vikundi maalumu ikiwa pamoja na watu wenye ugonjwa wa akili, na kutojumuisha shughuli za kisaikolojia na vipaumbele vya makundi maalumu. Hali hii imehusishwa na mawasiliano duni na ukosefu wa viashiria muhimu vya utendaji kwa huduma za kisaikolojia na usaidizi hivyo kuathiri maandalizi ya mipango ya kimkakati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake, Jinsia, na Makundi Maalumu.

Pia, ukaguzi ulibaini ukosefu wa ufuatiliaji na tathmini uliofanywa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, na Makundi Maalumu na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa ajili ya huduma za kisaikolojia na usaidizi kwa jamii. Upungufu huu unazuia utambuzi wa changamoto zinazokwamisha utekelezaji mzuri wa huduma za kisaikolojia na usaidizi kwa jamii na maendeleo ya mpango wa utekelezaji unaojibu mkakati.



**(b) Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, na Makundi Maalumu kutohakikisha kuwa utoaji wa huduma za kisaikolojia na usaidizi ulikuwa wa viwango vinavyokubalika kama ilivyoelekezwa na Mwongozo**

Ukaguzi huu ulibaini ukosefu wa usimamizi wa OR - TAMISEMI na Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wanawake, na Makundi Maalumu, kwani walishindwa kuhakikisha uzingatiaji wa malengo yaliyowekwa wakati wa utoaji wa huduma za kisaikolojia na usaidizi. Ukosefu wa usimamizi ulidhihirishwa na Wizara kutokuwa na data kuhusu watumishi wa huduma za kisaikolojia na usaidizi waliofunzwa, ikiwa pamoja na taarifa kuhusu utoaji bora wa huduma hizo; idadi ndogo ya watu wanaohudumiwa na watoa huduma wenye mafunzo, na tathmini ya urekebu kwa watu ambao walipata huduma kutoka kwa watoa huduma.

**(c) Ufuatiliaji hafifu wa wagonjwa wa rufaa ili kuhakikisha walihudumiwa ipasavyo na maoni yalitolewa kwa watoa huduma za kisaikolojia na usaidizi**

Ukaguzi ulibaini kuwa Maofisa ustawi wa jamii katika ngazi za chini hawakutoa rufaa za watu wenye matatizo ya akili kama ilivyoelezwa katika Mwongozo wa Huduma za Kisaikolojia na Usaidizi. Hivyo, hakukuwa na uainisho wa jinsi ya kufanya mrejesho katika miongozo ya huduma za kisaikolojia na usaidizi. Matokeo yake, hakuna mrejesho kwa rufaa zilizotolewa kwa Maofisa wa ustawi wa jamii. Hali hii ilitokana na kutotambuliwa kwa watu wenye matatizo ya afya ya akili katika ngazi ya chini, na hivyo hakuna rufaa iliyofanyika katika ngazi za chini.

Kukosekana kwa mifumo iliyo wazi na iliyopangwa ya kufuatilia na kusimamia rufaa kunaweza kufanya iwe vigumu kuhakikisha kuwa kila mgonjwa anahudumiwa vizuri na kwamba mrejesho unatolewa kwa ufuatiliaji wa mgonjwa unaendelea katika ngazi ya jamii. Ukaguzi huu pia ulibaini kuwa, wagonjwa waliopata rufaa binafsi katika hospitali, bado kulikuwa na mrejesho duni uliotolewa kwa Maofisa ustawi wa jamii kwa ufuatiliaji endelevu wa wagonjwa.

Kushindwa kutoa mrejesho kwa huduma za kisaikolojia na usaidizi humaanisha kuwa ni ngumu kuwatambua wagonjwa waliopo ambao wanahitaji huduma na hawawezi kuunganishwa vizuri katika jamii baada ya matibabu yao.

### 3.3.4 Uhaba wa rasilimali (wataalamu, miundombinu, vifaatiba, na dawa) ili kuwezesha utoaji wa huduma za afya ya akili

Ukaguzi huu ulibaini upatikanaji duni wa wataalamu katika ngazi zote za vituo vya kutolea huduma za afya ambapo, Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais - TAMISEMI hazikuhakikisha upatikanaji na usambazaji wa wataalamu wa kutosha katika ngazi zote kwa ajili ya utoaji wa huduma za afya ya akili katika hospitali za taifa, mikoa, na wilaya.

Kulikuwa na idadi ndogo ya wataalamu katika hospitali za ngazi ya kitaifa kwa ajili ya kutoa huduma za afya ya akili. Hospitali ya Taifa ya Akili ya Mirembe ilikuwa na upungufu mkubwa wa Madaktari bingwa wa magonjwa ya akili, madaktari wa dawa za kulevya, madaktari wa saikolojia ya watoto na vijana, madaktari wa lugha na tiba ya kuongea, na kada ya uchunguzi wa magonjwa ya akili iliyokuwa na upungufu wa asilimia 100. Kwa upande mwingine, kulikuwa na upatikanaji duni wa wataalamu wa magonjwa ya akili, wanasaikolojia, madaktari wa mishipa ya fahamu, na wauguzi wa magonjwa ya akili. Vilevile, Hospitali ya Taifa Muhimbili haikuwa na daktari bingwa wa magonjwa ya mishipa ya fahamu kwa watoto, na kulikuwa na upungufu wa asilimia 95 wa wauguzi wa magonjwa ya akili, na upungufu wa asilimia 21 wa madaktari wa magonjwa ya akili.

Vivyohivyo, kulikuwa na ukosefu wa watumishi wa utoaji wa huduma za afya ya akili katika hospitali za rufaa za kanda. Timu ya ukaguzi ilikagua mahitaji na idadi ya watoahuduma za magonjwa ya akili katika hospitali za kanda na kubaini kuwa hakukuwa na wataalamu katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda Benjamin Mkapa kinyume na Kiwango cha Msingi cha Vituo vya Afya cha Mwaka 2017.

Aidha, kulikuwa na idadi ndogo ya madaktari bingwa wa magonjwa ya akili katika hospitali za rufaa za mikoa kama ilivyobainika katika Hospitali ya Rufaa ya Mikoa Tabora, Dodoma, na Mbeya.

Hata hivyo, kwa wataalamu wa kazi (occupational therapist), hospitali mbili kati ya tano za rufaa za mikoa zilizotembelewa zilibainika kuwa na upungufu wa watumishi ikilinganishwa na idadi inayotakiwa ya wataalamu kwa mujibu wa miongozo hiyo. Mathalani, Hospitali za Mikoa ya Dodoma na Amana, ilikuwa na upungufu kwa asilimia 100. Hali hii imetokana na ukosefu wa mpango wa kuajiri wataalamu wa afya ya akili katika Wizara ya Afya na kukosekana kwa muundo wa utumishi unawatambua wahitimu ambao ni wataalamu wa magonjwa ya akili. Hali hii inasababisha upatikanaji mdogo wa huduma za afya za afya ya akili.

**(a) Miundombinu isiyojitosheleza ya kuwahudumia watu wazima na watoto wakati wa matibabu ya huduma za afya ya akili**

Kwa ujumla, vituo vya afya havikuwa na wodi za kuwalaza watoto na vijana. Vilevile, katika ngazi ya mkoa, Hospitali za Rufaa za Mkoa za Sekou Toure, Mbeya, Dodoma, na Amana hazikuwa na wodi za wanaume, wanawake, Watoto, na vijana. Hali hii ilisababishwa na kutokutengwa kwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa wodi, na ukosefu wa mipango ya ujenzi wa wodi za afya ya akili, hivyo kusababisha changamoto katika utoaji wa huduma hizo.

Kwa hospitali za rufaa za kanda, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Benjamini Mkapa haikuwa na wodi za kulaza wagonjwa wa afya ya akili kwa sababu haikuwa na kitengo cha huduma za afya ya akili.

**(b) Upatikanaji usiotosheleza wa vifaatiba na dawa ili kuwezesha utoaji wa huduma bora za afya ya akili**

Lengo la 3 la Mpango-mkakati wa Wizara ya Afya wa Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza wa Mwaka 2016-2020 unalenga kuhakikisha upatikanaji wa kutosha wa vifaatiba vinavyohusu magonjwa yasiyo ya kuambukiza, ikiwa pamoja na afya ya akili.

Hata hivyo, upatikanaji wa dawa za magonjwa ya afya ya akili ambazo zilitakiwa kutolewa na Bohari Kuu ya Dawa hazikutolewa kwa kiwango kinachotakiwa. Hata hivyo, walifanikiwa kupata vifaatiba kutoka kwa wachuuzi binafsi ili kuziba pengo. Timu ya ukaguzi ilibaini kuwa katika mwaka wa fedha 2021/22, usambazaji mkubwa wa dawa za akili uliofanywa na Wizara ya Afya kupitia Bohari Kuu ya Dawa, ambao ulikuwa asilimia 20 katika Hospitali ya Taifa ya Akili Mirembe. Dawa pekee iliyopatikana ni *haloperido*.

Vilevile, timu ya Ukaguzi ilitembelea hospitali tano katika ngazi ya mkoa na kubaini kuwa thamani kubwa iliyopokelewa ilibainika kuwa ni asilimia tatu ya kiasi cha dawa kilichoagizwa. Timu ya ukaguzi ilibaini kuwa usambazaji mzima wa dawa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Mbeya na Dar es Salaam (Amana) haukutosha.

Uhaba wa dawa umechangiwa na kuweka kipaumbele kidogo katika afya ya akili, hivyo kusababisha kutopatikana kwa dawa na vifaatiba. Hali hii inaweka hatari ya bei za dawa kupandishwa na wauzaji wakuu na kuchelewa kwa usambazaji wa dawa. Ukosefu wa kipaumbele umesababisha uhaba wa mara kwa mara wa dawa muhimu na vifaatiba, na kusababisha hatari kubwa katika kuwahudumia mgonjwa. Ukosefu wa dawa muhimu si tu unahatarisha ufanisi wa

matibabu lakini pia unasababisha hali ngumu inayowakabili watu wenye shida ya afya ya akili.

Aidha, utegemezi wa wachuuzi wakuu kwa ununuzi wa dawa umechangia uhaba huo, kwani mara nyingi dawa zimekuwa zikiuzwa kwa bei ya juu na kuwapo kwa ucheleweshaji wa usambazaji wa dawa.

Pia, ukaguzi ulibaini upatikanaji duni wa vifaatiba vya uchunguzi na matibabu ya huduma za afya ya akili kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 3**. Vifaatiba vinavyohitajika ni pamoja na MRI, EEG, na ECT, ambavyo ni muhimu katika utafiti wa majeraha ya ubongo na unyogovu.

**Jedwali Na. 2.3: Upatikanaji wa Vifaatiba katika Ngazi Zote**

Aina ya Kipimo	Taifa		Kanda		Mkoa	
	Inayohitajika	Inapatikana	Inayohitajika	Inapatikana	Inayohitajika	Inapatikana
ECT	2	0	5	0	31	0
EEG	2	2	5	1	31	0
MRI	2	1	5	3	0	0

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka Mwongozo wa Kitaifa wa Vituo vya Afya na Nyaraka kutoka Wizara ya Afya wa Mwaka 2023*

### 3.3.5 Upatikanaji wa huduma za utengamo kwa maendeleo ya ujuzi, ushirikiano wa jamii, na usaidizi unaoelekezwa kwa urejeshaji

Mpango-mkakati wa Kitaifa wa Urekebu wa Mwaka 2021-2026 unasema kwamba miongozo ya kitaifa ya mazoezi ya kliniki ya kitaifa ni njia muhimu ya kuhakikisha kwamba afua za urekebu zilizotolewa zimethibitishwa kuwa za ufanisi na kusawazisha huduma kote nchini. Hata hivyo, hadi mwaka 2021, hakukuwa na miongozo ya kitaifa ya mazoezi ya kliniki kwa ajili ya utengamo iliyokuwa imetayarishwa.

Ukaguzi umebaini kuwa kati ya mikoa 28, ni mikoa mitano pekee ndio ilikuwa na vituo vya kutolea huduma za afya ya akili ambayo ni Kilimanjaro, Mwanza, Dar es Salaam, Dodoma, na Kigoma. Vituo vitatu tu kati ya vitano ndivyo vinamilikiwa na serikali, na vituo viwili vilivyobaki vinamilikiwa na hisani, hivyo kukwamisha upatikanaji wa huduma kwa wagonjwa wa vijijini. Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa kati ya hospitali hizo tatu za kanda, moja ilikuwa na kituo cha utangamo, yaani Hospitali ya Rufaa ya Kanda, Mbeya. Hospitali ya Rufaa ya Kanda, Benjamin Mkaapa haikuwa na kituo cha kutolea huduma za afya ya akili kwa kuwa ilikuwa ikitegemea Hospitali ya Taifa ya Akili Mirembe kutoa huduma hizo. Katika ngazi ya taifa, Hospitali za Taifa za Akili Mirembe na Muhimbili zilikuwa na huduma za utangamo.

Ukaguzi umebaini kuwa vituo viwili vya wagonjwa wa afya ya akili, Hombolo Dodoma na Vikuruti Dar es Salaam, viko katika hali mbaya kutokana na uchakavu wa majengo, jiko, na vyoo. Kituo cha Utengamo cha Kanda ya Mbeya kimetelekezwa na hakifanyi kazi kiasi cha wananchi wanaoishi karibu na eneo hilo kuvamia na kufanya shughuli za kilimo.

Ukaguzi uligundua ukosefu wa miongozo ya kusanifu na kujenga miundombinu muhimu kwa ajili ya vituo vya utengamo vya huduma za afya ya akili, na kuzuia maendeleo yao kwa ujumla. Ukaguzi ulibaini upungufu wa wataalamu wa huduma ya afya ya akili nchini, huku pengo likionekana kuwa asilimia 72 katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na asilimia 75.8 katika Hospitali ya Taifa ya Akili Mirembe. Hali hii imechangiwa na kukosekana kwa mpango wa kuajiri ili kuwezesha huduma za utengamo, hivyo kusababisha upatikanaji mdogo wa huduma za utengamo.

#### ***(a) Bajeti isiyojitoshleza ya utoaji wa huduma kabambe za utengamo***

Mapitio ya Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Utengamo wa Mwaka 2021-2026 yalifichua kuwa ukarabati haukutengewa bajeti ndani ya muundo wa usimamizi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, hivyo ujumuishaji zaidi katika mifumo ya ufadhili wa afya unahitajika. Utengamo unahitaji rasilimali za kutosha ili kutekeleza na kuendeleza hatua za Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Utengamo.

Aidha, Mfumo wa Matumizi ya Muda wa Kati wa Wizara ya Afya (2018/19 - 2022/23) ulionyesha kuwa hakukuwa na bajeti iliyotengwa kwa ajili ya utengamo. Wakati wa kutembelea vituo vya utengamo, ukaguzi ulibaini kuwa hakukuwa na bajeti iliyotengwa kwa ajili yao. Bado, vituo vya utengamo vilikuwa na shughuli za nyumbani ambazo zilichangia mapato, kama vile ufugaji wa wanyama na kuku. Hata hivyo, mapato hayo yalitoshwa tu kuendesha maisha ya kila siku ya wagonjwa na si kufanya matengenezo makubwa ya vituo.

#### ***(b) Kutokuwapo kwa programu za ufuatiliaji***

Ukaguzi ulibaini kuwa, hakukuwa na mipango ya ufuatiliaji wa kusaidia ujumuishaji wa mipango ya jamii ya utengamo iliyofanyika kutokana na rasilimali chache na ukosefu wa takwimu sahihi. Takwimu za utengamo hazikuunganishwa katika Mfumo wa Taarifa wa Usimamizi wa Afya katika ngazi zote, na hapakuwa na ukusanyaji wa takwimu katika ngazi ya serikali kuu, ukionyesha kutokuwapo kwa viashiria vya kitaifa vilivyojengwa kwenye takwimu za utengamo. Mfumo wa Matumizi ya Muda wa Kati wa Wizara ya Afya unaonesha hakuna vifungu vya bajeti vilivyotengwa kwa ajili ya huduma za urekebu wa afya ya akili, hivyo kusababisha usimamizi hafifu wa huduma za afya.

### 3.3.6 Utekelezaji hafifu wa kampeni za uhamasishaji wa huduma za afya ya akili

Ukaguzi ulibaini uhaba wa mbinu na mikakati ya kampeni za uhamasishaji kuhusu afya ya akili. Wahamasishaji walitumia Siku ya Afya ya Akili Duniani, inayofanyika tarehe 10 Oktoba kila mwaka, na Siku ya Kuzuia Kujiua Duniani, inayoadhimishwa tarehe 10 Septemba kila mwaka kufanya kampeni ya kuongeza uelewa. Kampeni za uhamasishaji zilifanyika katika muda uliotajwa kutokana na kutokuwapo kwa baraza la kitaifa la afya ya akili ambalo lingeandaa, kuhamasisha, na kukuza uelewa na utekelezaji wa taratibu na mikakati ya kukuza uelewa wa huduma za afya ya akili.

Aidha, ukaguzi uligundua kuwa kipaumbele hafifu, ukosefu wa mgao wa bajeti, na kutokuwapo kwa baraza la kitaifa la afya ya akili kumesababisha uelewa mdogo wa jamii na kuongezeka kwa unyanyapaa.

Ukaguzi ulibaini hakuna mipango iliyokuwapo ya Wizara ya Afya; Wizara ya Afya, Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wanawake, na Makundi Maalumu; na Ofisi ya Rais - TAMISEMI ili kuandaa programu za ulimu kuhusu afya ya akili. Katika ngazi ya jamii, hapakuwa na utekelezaji wa programu za uhamasishaji. Mapitio ya Mfumo wa Matumizi ya Muda wa Kati wa Halmashauri zilizotembelewa pia ulibaini kuwa hakukuwa na shughuli za kutoa elimu kuhusu afya ya akili zilizoainishwa kwenye bajeti. Hali hii ilitokana na mipango duni na kutokuwapo kwa kipaumbele kwa ajili ya utoaji wa elimu. Kutokana na hali hiyo, hakukuwa na bajeti iliyotengwa kwa ajili ya kutekeleza programu za uhamasishaji.

### 3.3.7 Uratibu hafifu wa utoaji wa huduma za afya ya akili miongoni mwa taasisi za serikali

Wizara ya Afya, Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wanawake, na Makundi Maalumu na Ofisi ya Rais - TAMISEMI hazikuratibu ipasavyo utoaji wa huduma za afya ya akili miongoni mwa taasisi za Serikali. Hakukuwa na majukumu yaliyoainishwa kati ya wadau ambayo yaliruhusu uratibu unaofaa miongoni mwa wadau. Hali hii ilitokana na kutokuwapo kwa baraza la kitaifa la afya ya akili ambalo lingefafanua majukumu. Kwa mujibu wa Kifungu cha 31, (1), (b) cha Sheria ya Afya ya Akili ya Mwaka 2008, kazi za baraza la taifa la afya ya akili ni kuunda uhusiano wa kiutendaji kati ya sekta na taaluma mbalimbali kwa ajili ya kuratibu na kukuza afya ya akili.

Hata hivyo, hakuna baraza la kitaifa la afya ya akili lililoundwa ili kusimamia, na kuratibu upatikanaji na utoaji wa huduma za afya ya akili. Hali hiyo imechangiwa na Wizara kutofanya juhudi tangu kuanzishwa kwa Sheria ya Afya ya Akili Mwaka 2008 ili kuhakikisha kuwapo kwa baraza linalofanya kazi ya

kusimamia na kuratibu masuala ya afya ya akili nchini. Hata hivyo, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa kulikuwa na rasimu ya Masharti ya Marejeleo ya Kikundikazi cha Kitaalamu baina ya wizara kwa lengo la kukidhi vyema mahitaji ya afya ya akili na kisaikolojia ya watu binafsi, familia na jamii, hasa watoto na watu wanaoishi katika mazingira magumu. Hatu hii ilipaswa kufikiwa kwa kutumia vyema rasilimali zilizopo na kuhakikisha ufanisi na matumizi ya afua kwa mahitaji haya.

### 3.4 Matokeo ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Vifaatiba katika Vituo vya Afya vya Umma

Sehemu hii inawasilisha matokeo makuu ya ukaguzi wa ufanisi wa udhibiti wa vifaatiba katika vituo vya afya vya umma. Masuala yaliyobainika ni kuwapo kwa vifaatiba visivyofanya kazi; uzingatiaji duni wa taratibu za usajili wa vifaatiba; ukusanyaji usiojitosheleza wa sampuli za vifaatiba kwa ajili ya usajili na wakati wa uingizaji nchini; na udhibiti usio na ufanisi juu ya vifaatiba vinavyoagizwa na vituo vya afya vya umma. Masuala mengine ni kutoanzishwa kwa uwekaji wa kumbukumbu za viwango vya vifaatiba kulingana na shirika la viwango vya kimataifa; wizara ya afya haikuhakikisha kuwa vituo vya afya vya umma vinatunza vifaatiba; Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania haikufuatilia utendaji wa vifaatiba katika vituo vya afya vya umma; na uondoshaji usiojitosheleza wa vifaatiba visivyofanya kazi kama inavyofafanuliwa hapa chini.

#### 3.4.1 Kuwapo kwa vifaatiba visivyofanya kazi

Ukaguzi ulibaini kuwapo kwa vifaatiba visivyofanya kazi nchini Tanzania kinyume na malengo yaliyoainishwa kwenye Mpango-mkakati wa Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania wa Mwaka 2016/17-2020/21. Mpango huu uliagiza Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania kuimarisha usimamizi na kuhakikisha ubora, usalama, na ufanisi wa vifaatiba na zana za uchunguzi kupitia hatua zaidi za udhibiti.

Ukaguzi uliofanywa wakati wa ukaguzi katika vituo 18 vya afya vya umma vilivyotembelewa uligundua kuwa, vifaatiba 135 kati ya 492, sawa na asilimia 27, havikuwa vinafanya kazi. Asilimia kubwa zaidi ya vifaatiba visivyofanya kazi vilibainika katika kanda ya kati iliyokuwa na vifaatiba 37 visivyofanya kazi kati ya 115, sawa na asilimia 32. Hata hivyo, rejea ya takwimu zilizokusanywa kwa ajili ya vifaatiba vilivyopatikana kutoka Kurugenzi ya Radiolojia na Huduma za Picha katika Wizara ya Afya ilionesha kuwa Kurugenzi hiyo ilikuwa na takwimu za vifaatiba 9 visivyofanya kazi kati ya 16, sawa na asilimia 14 ya vifaatiba vilivyochaguliwa.

Katika hali nyingine, uchambuzi ulionesha kuwa vifaatiba visivyofanya kazi vilihusishwa na ukosefu wa matengenezo-kinga ya vifaatiba katika vituo vya

afya vya umma. Hata hivyo, mahojiano na Maofisa wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii yalibaini kuwa, vifaatiba visivyofanya kazi vinajumuisha vile vilivyopitwa na wakati ambavyo vimebadilishwa na vifaa vingine vyenye teknolojia ya kisasa. Hali hii inamaanisha kwamba kumekuwa na mabadiliko kutoka analogia kwenda vifaatiba vya dijitali katika vituo vya afya

Kuwapo kwa vifaatiba visivyofanya kazi nchini kulisababisha kushindwa kufikia lengo la kutoa huduma bora za afya na zenye tija kwa wananchi.

### 3.4.2 Uzingatiaji duni wa taratibu za usajili wa vifaatiba

Mamlaka ya Dawu na Vifaatiba Tanzania ilipewa jukumu la kusajili vifaatiba vinavyotengenezwa ndani na nje ya nchi kabla ya kutumika. Katika suala hili, ukaguzi ulibaini upungufu kuhusu taratibu za usajili wa vifaatiba.

Kuanzia mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2022/23, kulikuwa na vifaatiba 150 kati ya 209 vilivyosajiliwa, sawa na asilimia 72, ambavyo havikurekodiwa na Mamlaka ya Dawu na Vifaatiba Tanzania. Kumbukumbu za vifaatiba kuonesha tarehe ya maombi ya usajili au utoaji wa vyeti hazikupatikana katika rejista ya Mamlaka ya Dawu na Vifaatiba. Hali hii ilisababisha kutokuwa na uwezo wa kuamua tarehe ya kumalizika kwa cheti cha usajili wa vifaatiba.

Pia, ukaguzi ulibaini ucheleweshaji wa maombi ya usajili wa vifaatiba kama ilivyobainishwa katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2022/23, ambapo ni vifaatiba 5 tu kati ya 59 ndivyo vilichaguliwa vikiwa na taarifa zote za maombi ya usajili na cheti cha kusajiliwa kutolewa ndani ya siku 90. Vifaatiba 54 vilivyosalia kati ya 59 sawa na asilimia 91 ya vifaatiba vilivyochaguliwa, taratibu zake za usajili zilikamilishwa baada ya zaidi ya siku 45 na 90 za kazi. Vifaa vya tiba 54 vilivyobaki vilikuwa na Vifaatiba vinne ambavyo vilikuwa daraja A ambavyo vinapaswa kuchukua siku 45 za kazi na 50 ambavyo vilianguka katika daraja B na C ambavyo vinahitaji siku 90 za kazi kusajiliwa. Hii ni kinyume na matakwa ya Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa Mamlaka ya Dawu na Vifaatiba Tanzania, 2020 ambao unaonesha kuwa, usajili wa vifaatiba utachukua siku 45 za kazi kwa Daraja A na siku 90 za kazi kwa Daraja B na C. Kwa hiyo, hii inaleta hatari ya kuchelewa kwa huduma za afya zinazokusudiwa kwa kutumia vifaatiba.

### ***Uhuishaji Hafifu wa Vyeti vya Usajili wa Vifaatiba na Mamlaka ya Dawu na Vifaatiba Tanzania***

Uchambuzi wa kanzidata kutoka kwenye dondoo ya Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Udhhibiti wa Mamlaka ya Dawu na Vifaatiba Tanzania ulionesha kuwa, kwa wastani, Mamlaka ya Dawu na Vifaatiba Tanzania haikuhakikisha inahuisa kwa wakati kwa asilimia 53 ya vyeti vilivyoisha muda wake kwa kipindi cha miaka 4 ya fedha yaani kuanzia mwaka 2019/20 mpaka 2022/23.



Ukaguzi ulibaini kuwa, uhuishaji hafifu wa vyeti vya usajili wa vifaatiba kulitokana na Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania kutokuwa na mfumo madhubuti wa udhibiti wa vifaatiba kwa wateja wao kuhusu kumalizika kwa vyeti vya vifaatiba vilivyosajiliwa. Vilevile, Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania haikuwa na utaratibu wa kutekeleza upya wa usajili wa vifaatiba ndani ya siku 90 zilizokubaliwa.

Aidha, Ukaguzi ulibaini kutokuwapo kwa ufanisi wa uhuishaji wa hati za usajili wa vifaatiba na kusababisha Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania kutofanya ufuatiliaji wa vifaatiba vinavyohitajika chini ya Kanuni ya 17(3) ya Kanuni za Chakula, Dawa na Vipodozi (Udhibiti wa Vifaatiba) wa mwaka 2015, ambayo inasema kwamba, waliojiandikisha lazima wawasilishe ripoti za ufuatiliaji baada ya uzaji kila baada ya miaka miwili, ikijumuisha matukio yoyote mabaya yanayotokea baada ya kutumia kifaa tiba husika. Hii ilisababisha upotevu wa ukusanyaji wa mapato kwa kuzingatia kwamba, Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania ingekusanya jumla ya TZS 10,261,473,750 kutokana na kuhuisha Hati ya Usajili kwa mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2022/23. Idadi kubwa ya usajili wa vifaatiba ambavyo havijahuishwa na Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania ilibainika katika mwaka wa fedha 2022/23 ambapo Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania haikukusanya kiasi cha shilingi 9,611,538,750 kutoka vifaatiba 1,538.

### 3.4.3 Ukusanyaji Usiojitosheleza wa Sampuli za Vifaatiba kwa ajili ya Usajili na Wakati wa Uingizaji Nchini

Hata hivyo, kupitia uhakiki wa nyaraka za usajili Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania, ukaguzi ulibaini kuwa Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania ilikuwa haichukui sampuli za vifaatiba kabla na baada ya usajili kabla ya kuruhusu vifaatiba hivyo kusambaa sokoni nchini. Ukweli huu ulithibitishwa wakati wa mahojiano na Maofisa wa Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania, ambao walibaini kuwa Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania haikuhakiki utendaji wa vifaatiba kwa kukusanya sampuli wakati wa usajili na baada ya ufungaji katika vituo vya afya husika. Kutoweza kutimiza matakwa ya kuchukua sampuli za vifaatiba na Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania kulitokana na kutokuweka usimamizi wa kifungu hicho na Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania wakati wa kuandaa kanuni na miongozo mingine ya udhibiti wa vifaatiba.

Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania ililenga tu vifaa vidogo vya tiba kama vile sindano, mashine za upasuaji, glovu za uchunguzi na nyinginezo, kama ilivyoelezwa katika Miaka Kumi ya Mamlaka ya Chakula na Dawaya udhibiti wa chakula, Dawa, vipodozi na vifaatiba. Kwa upande mwingine, ilichangiwa na Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania kutokuwa na nafasi ya kubeba vifaatiba au maabara kubwa kwa ajili ya kupima sampuli za vifaatiba hivyo.

***Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania haikuhakikisha Wasajili wa Vifaatiba Wanalipa Ipasavyo Ada ya Kuhifadhi ya Kila Mwaka kwa Vifaatiba Vyao Vilivyosajiliwa.***

Kanuni ya 17 (2) ya Sheria ya Tanzania, Chakula, Dawa na Vipodozi (Udhibiti wa Vifaatiba), 2015 inaeleza kuwa kila msajili, pamoja na gharama zinazohusiana na usajili wa kila kifaa cha matibabu, kulipa ada ya kuhifadhi kila mwaka kabla ya tarehe 31 Januari ya mwaka wa kalenda.

Mapitio ya malipo ya ada za kuhifadhi, Ukaguzi ulibaini kuwa asilimia 51 ya wasajili wa vifaatiba hawakulipia ada zao za kuhifadhi kila mwaka. Bila kujali waliojiandikisha kutolipa ada zao za kuhifadhi, Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania haikusimamisha wala kufuta usajili wao kwa kipindi cha miaka minne ya fedha, yaani, 2019/20 hadi 2022/23. Hii ni kinyume na Kanuni ya 17(2) & 18(g) ya Tanzania, Chakula, Dawa na Vipodozi (Udhibiti wa Vifaatiba), 2015. Hii ina maana kuwa Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania haikukusanya mapato ya jumla ya shilingi 241,040,000 huku wahusika wengi zaidi waliokosa kulipa kuonekana katika mwaka wa fedha 2022/23 ambapo walikuwa 188 waliosajiliwa na kiasi ambacho kilibainishwa hakijakusanywa ni kiasi cha shilingi 86,977,965.45. Hii ilikuwa kwa sababu Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania haikuhakikisha kama msajili aliyeshindwa kulipa ada ya mwaka ya kuhifadhi vifaatiba vilivyosajiliwa bado anafuata masharti mengine ya usajili ili kulinda afya za watu na umma kwa ujumla wakati wa kutumia vifaatiba hivyo.

#### **3.4.4 Udhibiti usio na Ufanisi juu ya Vifaatiba Vinavyoagizwa na Vituo vya Afya vya Umma**

Ukaguzi ulibaini kuwa, kwa miaka ya fedha 2019/20 hadi 2022/23, ripoti za ukaguzi na vyeti vya uingizaji wa vifaatiba hazikuwa na maelezo ya kina kuhusu ukaguzi uliofanyika kwenye vifaatiba katika bandari ya kuingilia. Hii ni kinyume na matakwa ya Kanuni ya 56 (1) ya Kanuni ya Chakula, Dawa na Vipodozi Tanzania ya Udhibiti wa Vifaatiba ya mwaka 2015. Vilevile vifaatiba katika vituo vya kutolea huduma za afya viliingizwa nchini na kufungwa bila ya kufanyiwa uhakiki wa awali na Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania juu ya usalama, ubora na ufanisi wao.

Hii ilichangiwa na kukosekana kwa rasilimali watu wenye ujuzi unaohitajika ili kuhakiki ubora wa vifaatiba vilivyoagizwa kutoka nje ya nchi. Wakaguzi katika bandari za kuingilia ambao walihusika zaidi na ukaguzi wa vifaatiba walikuwa wengi wafamasia na madaktari wa dawa, wasio na ujuzi wa kutosha wa uhandisi wa vifaatiba (Biomedical Engineers). Kwa upande mwingine, hakukuwa na zana za kutumia kukagua vifaatiba kwenye bandari ya kuingilia, hasa orodha ya vitu vinavyotakiwa kufuatiliwa wakati wa ukaguzi.

### ***Kutotoa kibali cha kuagiza vifaatiba kwa vituo vya afya vya umma***

Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania haikutoa vibali vya kuagiza vifaa vyote vilivyonunuliwa. Hii ilitokana na ukweli kwamba Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania haikuzingatia ipasavyo vigezo vyote vya maombi ya kibali cha kuagiza kama ilivyoielezwa katika Aya ya 1.5.3 (b) ya Mwongozo wa Uagizaji na Usafirishaji wa Vifaatiba, ikijumuisha Uchunguzi wa Vitro (Vitro Diagnostics), 2015. Hii inahitaji maombi ya kibali cha kuagiza bidhaa kutoka nje ya nchi kuwasilishwa pamoja na barua inayoeleza wazi sababu za kuingizwa kwa vifaa hivyo kutoka kwa mwombaji au daktari aliyehitimu kama vile daktari wa meno, daktari wa mifugo au daktari yeyote aliyeidhinishwa. Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania ilitoa vibali kwa kuzingatia ankara ya awali iliyoambatishwa katika Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Pamoja.

#### **3.4.5 Kutoanzishwa kwa Uwekaji wa Kumbukumbu za Viwango vya Vifaatiba kulingana na Shirika la Viwango vya Kimataifa**

Hata hivyo, Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania haikuwa imeanzisha na kudumisha faili za viwango vya kimataifa na mahitaji ya udhibiti kwa ajili ya kumbukumbu ya kila vifaatiba na kundi la vifaatiba (familia) kama matokeo ya malipo ya Shirika la Viwango vya ubora vya kimataifa kwenye usajili wa viwango vyake. Hii ina maana kwamba Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania ililazimika kulipa ada ya usajili kwa ajili ya upatikanaji wa huduma hiyo. Matokeo yake Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania inakosa msimbo kwa ajili ya ufuatiliaji na uwazi katika kufuatilia ufikiwaji wa viwango na kanuni kulingana na viwango husika vya vifaatiba.

Aidha, mapitio ya Mfumo wa Matumizi wa Muda wa Kati kwa mwaka wa fedha 2019/2020 hadi 2022/23 yalibaini kuwa, Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania haikutenga fedha kwa ajili ya kupata msimbo za kumbukumbu za viwango vya Vifaa vya Tiba. Pia, ilikosa taratibu na miongozo ya wazi ya kuweka na kutunza viwango hivyo.

#### ***Utendaji Usiofaa wa Kutokutumia Taratibu za Kawaida za Uendeshaji kwa Vifaatiba katika Vituo vya Afya***

Ukaguzi huo ulibaini kutotumika kwa taratibu za uendeshaji wa vifaatiba katika vituo vya afya. Hii ilibainika katika vituo vya afya vilivyotembelewa ambapo vifaatiba 263 kati ya 426 viliendeshwa bila uwapo wa taratibu za kawaida za Uendeshaji.

Hii ilitokana na ukosefu wa usimamizi wa kutosha kutoka Mamlaka ya Dawu na Vifaatiba Tanzania na Wizara ya Afya kutokana na kutokuwapo kwa ufuatiliaji wa Mamlaka ya Dawu na Vifaatiba Tanzania na kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Wizara ya Afya wakati wa usimamizi. Hii ni pamoja na mipango ya ufahamu ili kuwafahamisha Taratibu za uendeshaji na kuchukua hatua zinazofaa dhidi ya kutofuata. Hii pia ilisababisha kutokufanya kazi kwa baadhi ya vifaatiba kwani vilifanya kazi bila kufuata taratibu zinazohitajika.

### 3.4.6 Wizara ya Afya haikuhakikisha kuwa Vituo vya Afya vya Umma vinatunza Vifaatiba

Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Afya haikuwa na mfumo wa kiutendaji wa kuhakikisha udumishaji wa Vifaatiba katika Vituo vya Afya vya Umma kwa kipindi cha ukaguzi. Hili ni kinyume na matakwa ya aya ya 7.2 ya Miongozo ya Vifaa vya Kupiga Picha (Standard Medical Radiology and Imaging Equipment Guidelines , 2018, ambayo inahitaji matengenezo ya vifaatiba ili kuendelea kufanya kazi inavyokusudiwa. Kutokana na kukosekana kwa mfumo wa utendaji kazi wa matengenezo ya vifaatiba, ukaguzi katika vituo vya afya 17 vilivyotembelewa ulibaini kuwa asilimia 76 ya vituo vya afya vinavifaatiba vinavyofanya kazi vizuri.

#### **(a) Wizara ya Afya haikuhakikisha Matengenezo ya kutosha ya Vifaatiba kwa Vituo vya Afya vya Umma kwa mujibu wa Mwongozo wao wa Uendeshaji na Huduma**

Wakati wa uhakiki wa vituo vya afya vilivyochaguliwa kutoka Kanda 4, ambazo ni Kanda ya Kati, Mashariki, Kaskazini na Kanda ya Ziwa Magharibi, timu ya ukaguzi ilibaini uwapo wa vifaatiba ambavyo havijafanyiwa matengenezo katika vituo vya afya vinavyohusika. Ilibainika kuwa kila kifaa cha matibabu kina ratiba yake ya matengenezo. Kwa hivyo, wahandisi wa vifaatiba hupanga vipindi vya matengenezo kulingana na taratibu za uendeshaji na Mwongozo wa Uendeshaji wa Kifaa. Katika suala hili, matengenezo ya Vifaatiba mara nyingi huchelewa kwa kipindi cha mwaka 1 hadi 3, wakati mpango unaonesha matengenezo yanapaswa kufanywa kwa muda wa miezi 1, 3, 6 au 12, kulingana na aina ya vifaatiba. Hii ina maana kwamba vifaatiba katika vituo vingi vya afya havifanyiwi matengenezo na vinapofanyiwa matengenezo, matengenezo hayo hayafanyiki kwa mujibu wa ratiba ya matengenezo inayohitajika.

**(b) Utekelezaji wa Usawazishaji Upya na wa Kuendelea wa Vifaatiba katika Vituo vya Afya.**

Kupitia ziara za ukaguzi katika vituo vya afya vya umma, ilibainika kuwa urekebishaji wa vifaatiba ulifanyika kwa mashine za ‘centrifuge’ pekee. Vifaa vingine havikufanyiwa urekebishaji. Hali hii ilibainishwa katika vituo vyote 18 vya afya vilivyotembelewa katika ukaguzi huu, vitatu katika Ngazi ya Taifa na Mkoa, Ngazi ya Wilaya, na vituo vya Afya viwili vya Ngazi ya Kanda na Hospitali Maalumu za Juu mtawalia.

Ikumbukwe zaidi kuwa vifaatiba ambavyo havikutengenezwa vilihusishwa na vituo vya Afya kutotenga bajeti ya usawazishaji wa vifaatiba ili kuhakikisha matokeo yanayotokana na matumizi ya vifaatiba katika matibabu yanakuwa ya kuaminika na yanakidhi kiwango na lengo lililokusudiwa. Katika suala hili, upungufu wa vifaatiba ulisababisha vituo vya afya kutokuwa na uhakika kwa kuzingatia ufanisi wao katika uchunguzi na matibabu hivyo, kuathiri afya na usalama wa wagonjwa.

**3.4.7 Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania haikufuatilia Utendaji wa Vifaatiba katika Vituo vya Afya vya Umma**

Ukaguzi huo ulibaini kuwa, Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania haikupanga kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa Vifaatiba katika Vituo vya Afya. Hayo yamebainishwa kupitia mapitio ya Mipango ya Mwaka ya Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania kwa miaka ya fedha 2019/20 hadi 2022/23, ambapo mipango ya ukaguzi wa Vifaatiba katika Vituo vya Afya haikuzingatiwa katika mpango wa mwaka.

Vilevile, ilibainika kuwa mpango ulioandaliwa kwa ajili ya ufuatiliaji baada ya ununuzi wa mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2020/21 na 2020/21 hadi 2022/23 haukuwa na masharti ya ukaguzi wa mara kwa mara wa vifaatiba katika vituo vya afya. Badala yake, mpango huo ulilenga ukaguzi wa ufuatiliaji wa baada ya ununuzi wa Vifaatiba.

Hata hivyo, Ukaguzi ulibaini kuwa Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania haikuwa na mpango wa kukagua vifaatiba katika Vituo vya Afya vya Umma. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kulikuwa na pengo la rasilimali watu kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao kwa vile wahandisi wa vifaatiba (biomedical engineers) na wateknolojia wa biomedical’ hawakupatikana. Katika suala hili, Maofisa waliopewa kazi ya kukagua vifaatiba walikuwa Wakaguzi wa Dawa ambao walikuwa wataalamu wa dawa na maduka ya dawa tu, hivyo, ukaguzi huo haukufanyika.

Kutokana na hali hiyo, kukosekana kwa mpango wa ukaguzi wa mara kwa mara wa vifaatiba katika vituo vya afya kulisababisha vifaatiba katika vituo vya afya kubaki na utendaji usiojulikana au usiofuatiliwa, jambo ambalo halikuweza kuwahakikishia watumiaji na waendeshaji ubora, usalama na ufanisi.

### 3.4.8 Uondoshaji Usiojitosheleza wa Vifaatiba Visivyofanya Kazi<sup>2</sup>

Mapitio ya ripoti za uondoshaji wa Vifaatiba katika Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania kwa mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2022/23 yamebaini kuwa, Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania haikuanzisha wala kupokea maombi ya kuidhinisha uondoshaji wa vifaatiba kwa miaka minne ya fedha 2019/20 hadi 2022/23. Badala yake, ilipokea ripoti tu ya uondoshaji wa bidhaa zingine zilizodhibitiwa kama sindano na glavu. Ukaguzi huo umebaini kuwa, uwapo wa vifaatiba ambavyo havijatolewa nchini ni kutokana na Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania kutokuwa na miongozo ya uondoshaji wa vifaatiba. Hii inaweza kuwa chombo muhimu cha kuwezesha Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania kuanzisha na kuongoza utupaji wa vifaatiba na kuwezesha vituo vya afya vya umma kuomba kibali na ushauri kutoka Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania juu ya njia sahihi ya kuondoa vifaa hivyo kwani ni mazoea ya bidhaa nyingine zilizodhibitiwa.

Vilevile, kanuni ya 60 ya Sheria ya Tanzania, Chakula, Dawa na Vipodozi (Udhibiti wa Vifaatiba), ya mwaka 2015 haikufafanua waziwazi ni katika hali gani Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania itaanzisha uteketezaji na uondoshaji wa Vifaatiba. Kwa kuzingatia hili, Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania haikuanzisha mchakato wa uondoshaji wa vifaatiba.

Hivyo basi, kukosekana kwa mwongozo wa uondoshaji wa vifaatiba visivyofanya kazi kulisababisha vituo 6 kati ya 18 vilivyotembelewa kuwa na mlundikano wa vifaatiba visivyofanya kazi ambavyo havikuondolewa.

### 3.5 Athari katika kufikia malengo ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Mendeleo Endelevu

Upungufu wa utoaji wa huduma za afya ya akili na uchunguzi kutokana na kutodhibitiwa kwa vifaatiba kutazuia kufikiwa kwa afua muhimu katika Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambayo ilikuwa kujenga na kukarabati vituo vya afya jumuishi ambavyo vitahakikisha upatikanaji wa kutosha wa huduma zote zinazohitajika ikiwa pamoja na afya ya akili.

Pia, upatikanaji duni na utoaji wa dawa za afya ya akili na upatikanaji duni wa vifaatiba vinavyodhibitiwa kutaathiri kufikiwa kwa malengo ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, ambayo ulilenga kuhakikisha upatikanaji wa dawa, vifaatiba, vitendanishi, chanjo na vifaa vya dawa.

Zaidi ya hayo, Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ulilenga kuimarisha huduma maalumu na bobezi katika hospitali zote za rufaa za kanda,

<sup>2</sup> Vifaa vya tiba visivyofaa vinavyotajwa kwa utupaji ni vile ambavyo vina upungufu katika ubora; Ukosefu wa usalama; na Upungufu katika utendaji (Para 7 & 14 ya Mwongozo wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania wa Kushughulikia Vifaatiba na Uchunguzi visivyofaa, 2023).

maalumu na za kitaifa hii inaleta hatari ya kutofikia lengo lililowekwa kwani kulikuwa na utekelezaji duni wa mafunzo kwa madaktari wa magonjwa ya akili kwa watoto, madaktari wa neva na upasuaji wa neva ambao ni muhimu katika utoaji wa huduma maalumu na za juu za huduma za afya ya akili. Utoaji usiotosheleza wa vifaatiba vilivyodhibitiwa hautasaidia upatikanaji wa huduma za uchunguzi wa hali ya juu ili kuimarisha huduma maalumu katika Hospitali za Kitaifa, Maalumu na za Kanda.

Zaidi ya hayo, Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ulilenga kuimarisha huduma maalumu na bobebi zaidi katika hospitali zote za rufaa za kanda, maalumu na za kitaifa. Hii inaleta hatari ya kutofikia lengo lililowekwa kwa kuwa hakukuwa na utekelezaji wa kutosha wa kutoa mafunzo kwa madaktari wa magonjwa ya mishipa ya fahamu, wataalamu wa mishipa ya fahamu na upasuaji wa mishipa ya fahamu ambao ni muhimu katika kutoa huduma za afya ya akili iliyobobea. Utoaji duni wa vifaa vya tiba vilivyodhibitiwa hautasaidia upatikanaji wa huduma bora za uchunguzi ili kuimarisha huduma maalumu na za utaalim katika Hospitali za Kitaifa, hospitali Maalumu na hospitali za Kanda.

Lengo la tatu la Malengo ya Maendeleo Endelevu la kuhakikisha Afya ya Akili na Ustawi Imara, ikijumuisha kuzuia kujiuu, kama ilivyoielezwa katika Lengo la 3.4.2 la Malengo ya Maendeleo Endelevu, ifikapo 2030, inakusudia kupunguza kwa theluthi moja vifo vya mapema kutokana na magonjwa yasiyoambukiza kupitia kinga na matibabu na kukuza afya ya akili na ustawi ikiwa pamoja na kupunguza kiwango cha vifo vya kujitoa mhanga. Kutofikiwa kwa Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambayo umehuisa Malengo ya Maendeleo Endelevu kunaweza kuzuia ufanisi katika kufikia lengo hili ambalo linaweza kupimwa kwa kuzingatia utoaji endelevu wa Huduma ya Afya ya Akili na huduma za uchunguzi nchini.



## USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA KILIMO

### 4.1 Utangulizi

Sura hii inatoa matokeo ya ukaguzi yaliyotokana na ripoti za ukaguzi wa ufanisi katika udhibiti wa mazao ya biashara na udhibiti wa usambazaji wa mbolea simamizi. Vilevile sura hii inatoa maelezo juu ya maeneo yaliyokaguliwa, taasisi za Serikali zilizohusika, uhusiano wa kaguzi hizi na athari za matokeo yake katika Malengo ya Maendeleo Endelevu pamoja na Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano:

Kaguzi hizi za ufanisi ni pamoja na:

- (a) Ukaguzi wa Ufanisi katika Udhibiti wa Mazao ya Biashara; na
- (b) Ukaguzi wa Ufanisi katika Udhibiti wa usambazaji wa mbolea kwa wakulima; na

#### 4.1.1 Usuli kuhusu usimamizi wa shughuli za kilimo

Maendeleo ya Tanzania, kwa kiasi kikubwa yanategemea matumizi ya maliasili yake na mfumo ikolojia wake uliopo, kwa mfano, asilimia 80 ya hali ya maisha ya wakazi wa vijijini, yanategemea ardhi ya kilimo na ufugaji. Uchumi wa nchi unategemea zaidi kilimo, ambacho kinachangia takribani asilimia 24.1 ya Pato la Taifa la Tanzania, na huchangia asilimia 30 ya mapato ya nje na kutoa ajira kwa takribani asilimia 77.5 ya nguvu kazi yote (Sera ya Kilimo ya Kitaifa, 2013).

Shughuli za kilimo zina jukumu muhimu kama kichocheo cha uchumi na kuboresha usalama wa chakula wa kitaifa. Utumiaji wa mbolea kwa wakati kipindi cha kilimo una athari ya moja kwa moja katika kuboresha kilimo katika mazao ya chakula na biashara.



Maendeleo ya Tanzania yanategemea sana kilimo. Hata hivyo, nchi inakabiliwa na tishio la kuongezeka kwa kiwango cha matumizi ya mbolea ambazo hazijasajiliwa na zisizo na ubora. Zaidi ya hayo, kuna kupungua kwa kasi ya uzalishaji wa mazao ya biashara nchini ambayo imesababisha kupungua kwa mapato yatokanayo na mazao ya biashara.


#### 4.1.2 Ushabihiano wa Shughuli za Kilimo na Mpango wa Maendeleo Endelevu na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano

Sehemu hii inaelezea jinsi shughuli za kilimo zinavyohusiana na ukaguzi wa ufanisi kwenye maeneo ya udhibiti wa mazao ya biashara na udhibiti wa usambazaji wa mbolea, na jinsi maeneo hayo yanavyo husiana na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu. Maelezo ya kina ni kama yalivyo tolewa hapa chini:

##### (a) Shughuli za Kilimo kama zilivyo akisiwa kwenye Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano

Udhibiti wa mazao ya biashara na udhibiti wa usambazaji wa mbolea umeakisiwa katika Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Kifungu cha 5.3.1 cha mpango huo kinaonesha kusudio la kujenga uhusiano kati ya sekta ya kilimo na sekta nyingine za kiuchumi; kuweka mazingira mazuri kwa sekta binafsi ili kuleta manufaa katika uzalishaji na usafirishaji wa malighafi za kilimo nje ya nchi; na kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya kimkakati kwa kutumia mbolea. **Kielelezo Na. 10** hapa chini kinatoa muhtasari wa uhusiano ulioelezwa wa maeneo yaliyo akisiwa na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

**Kielelezo Na. 10: Muhtasari wa Shughuli Muhimu zinazohusiana na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano**



*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa taarifa kutoka Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2024*

**(b) Shughuli za Kilimo kama zilivyoakisiwa kwenye Mpango wa Maendeleo Endelevu**

Ili kukabiliana na changamoto katika shughuli za kilimo, kaguzi mbili zilifanyika. Ukaguzi wa kwanza ulihusiana na udhibiti wa mazao ya biashara na ukaguzi wa pili ulihusiana na udhibiti wa usambazaji wa mbolea nchini.

Kwa upande wa ukaguzi wa ufanisi kwenye eneo la udhibiti wa mazao ya biashara nchini umeakisiwa kwenye lengo namba 8 na lengo namba 2 la Malengo ya Maendeleo Endelevu. Lengo Namba 8 linalenga kushughulikia ukuzaji, endelevu, ushirikishwaji na ukuaji endelevu wa uchumi, ajira kamili na zenye tija. Shabaha 8.2 ya lengo hilo inalenga kuhakikisha viwango vya juu vya

uzalishaji wenye tija ya kiuchumi kupitia mseto na kwa kuzingatia uongezaji wa thamani.

Zaidi ya hayo, ukaguzi unashughulikiwa katika lengo namba 2 la Malengo ya Maendeleo Endelevu ambalo linakusudia kumaliza njaa. Utekelezaji wa udhibiti wa mazao ya biashara na udhibiti wa usambazaji wa mbolea umeangaziwa mahsusi katika lengo la 2.4 ambalo linakusudia kuhakikisha mifumo endelevu ya uzalishaji wa chakula na kutekeleza mazoea ya kilimo ambayo huongeza tija na uzalishaji, ambayo itasaidia kudumisha mifumo ya ikolojia ambayo ingeweza kuboresha ardhi na ubora wa udongo hatua kwa hatua.


Pamoja na hayo, Kaguzi hizi mbili za udhibiti wa mazao ya biashara na udhibiti wa usambazaji wa mbolea zimeainishwa zaidi katika lengo namba 12 ambalo linalenga kuhakikisha matumizi endelevu ya mifumo ya uzalishaji. Kupitia shabaha Na.12.4, inakusudiwa kufikia usimamizi mzuri wa hali ya maji na udongo ili kupunguza athari zake kwa afya ya binadamu na mazingira.

Mbolea ni kemikali ambazo huacha mabaki kwenye udongo ambayo ni hatari inapozidi kiwango kinachokubalika. Udhibiti wa mazao ya biashara na udhibiti wa usambazaji wa mbolea utasababisha utekelezaji wa lengo namba 2, 8 na 12 la Malengo ya Maendeleo Endelevu.

#### 4.1.3 Mikakati na Juhudi za Serikali katika Usimamizi wa Shughuli za Kilimo

Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Kilimo na Bodi za Udhibiti wa Mazao imeonesha jitihada zilizoweza usimamizi wa shughuli za kilimo hasa katika udhibiti wa mazao ya biashara na usambazaji wa mbolea. **Kielelezo Na. 11** kinaonesha mikakati na juhudi za serikali zilizowekwa.

### Kielelezo Na. 11: Mikakati na Jitihada za Serikali zilizowekwa ili Kusimamia Shughuli za Kilimo



Chanzo: Uchambuzi wa Wakaazi, 2024

## 4.2 Malengo na Mawanda ya Ukaguzi

### 4.2.1 Malengo ya Ukaguzi

Lengo kuu la ukaguzi huu lilikuwa kutathmini kama Wizara ya kilimo kupitia Bodi za Udhibiti wa Mazao pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea zimesimamia ipasavyo shughuli za kilimo ili kuongeza uzalishaji wa mazao na kuongeza mapato nchini.

Malengo mahususi ya ukaguzi yalikuwa ni:

- Kutathmini iwapo Wizara ya Kilimo, kupitia Bodi za Mazao, imedhibiti vya kutosha uzalishaji, ubora na bei za mazao ili kuhakikisha mapato yanaongezeka na kuinua kipato cha wakulima.

- b) Kutathmini iwapo Wizara ya Kilimo kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania, imesimamia ipasavyo usambazaji wa mbolea na virutubisho vya mimea ili kuhakikisha urahisi wa upatikanaji wa mbolea bora na virutubisho vya mimea kwa wakulima na kwa wakati.

#### 4.2.2 Mawanda ya Ukaguzi

Kwa ukaguzi wa udhibiti wa mazao ya biashara, taasisi kuu zilizokaguliwa ni Wizara ya Kilimo kupitia Bodi za Udhibiti wa Mazao. Ukaguzi huu umezingatia zaidi ufanisi katika kutunza taarifa za wakulima; udhibiti wa ubora wa mazao ya biashara; udhibiti wa bei; uhamasishaji na utafutaji wa masoko ya mazao ya biashara na uratibu wa shughuli za udhibiti wa mazao hayo. Mazao ya biashara yaliyoangaliwa ni korosho, chai, tumbaku na kahawa huku maeneo yaliyotembelewa ni Mtwara, Dar es Salaam, Morogoro na Kilimanjaro. Ukaguzi ulihusisha miaka mitano ya fedha kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2022/23.

Wakati huohuo, katika ukaguzi wa udhibiti wa usambazaji wa mbolea, taasisi kuu zilizokaguliwa ni Wizara ya Kilimo na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania. Ukaguzi ulijikita zaidi kwenye kudhibiti usambazaji wa mbolea na virutubisho vya mimea kwa wakulima. Hasa, ukaguzi ulilenga makisio ya mahitaji, usambazaji, udhibiti wa bei na ukaguzi wa mbolea na virutubisho vya mimea. Ukaguzi ulihusisha miaka mitatu kuanzia mwaka 2020/21 hadi 2022/23.

#### 4.3 Matokeo ya Ukaguzi Kuhusu Udhibiti wa Mazao ya Biashara

Sehemu hii inatoa muhtasari wa matokeo ya udhibiti wa mazao ya biashara. uchambuzi wa kina wa mambo yaliyozingatiwa ni kama yalivyowasilishwa hapa chini:

##### 4.3.1 Kiwango cha Udhibiti wa mazao ya biashara hakikutotosheleza

Udhibiti wa mazao ya biashara nchini Tanzania haukuwa wa kutosha kwani hakukuwa na ongezeko kubwa la uzalishaji wa mazao ya biashara kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2022/23 kama ilivyoainishwa katika ukaguzi huu. Ilibainika kuwa Bodi za Mazao hazikutekeleza ipasavyo mikakati ya uzalishaji na uuzaji kwa vile haikuwa imeidhinishwa. Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na mabadiliko ya mapato yatokanayo na mazao ya biashara. Tathmini ya kina ni kama inavyooneshwa hapa chini:

**(a) Bodi tatu kati ya nne za Udhhibiti wa Mazao hazikuwa na Mikakati iliyoidhinishwa ya Uzalishaji, uuzaji na uendelezaji wa mazao ya biashara**

Ilibainika kuwa Bodi za Mazao zilizotembelewa, isipokuwa Bodi ya Kahawa, hazikuwa na Mpango-mkakati wa Miaka Mitano uliyoidhinishwa ili kutohoa malengo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mita, Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Kilimo na mipango mingine ya Kitaifa na Kimataifa. Bodi hizi za Mazao zilikuwa bodi ya korosho, chai na tumbaku. Ukaguzi pia ulibaini kuwa, Bodi ya Kahawa ambayo iliidhinisha mkakati nao ulibainika kukosa vipengele muhimu vya utendaji kama vile masoko, kiasi kilicho pangwa kuzalishwa na ubora ulio kusudiwa.

Uwapo wa mikakati duni, umepelekea uzalishaji wa mazao hayo kudorora kwa kipindi chote cha miaka mitano ambapo Mwaka wa Fedha wa 2018/19 ulichukuliwa kama kigezo cha ulinganifu.

**(b) Kulikuwa na mabadiliko makubwa katika Mchango wa mapato katika Pato la Taifa linalotokana nazao la Tumbaku na Chai**


Tathmini ya mapato yanayotokana na mazao ya biashara yanayouzwa nje ya nchi iliashiria kubadilika-badilika kwa zao la chai na tumbaku. Ilibainika kuwa chai imepungua kwa miaka mingi ambapo mwaka wa fedha 2022/23 ilipungua hadi dola za Marekani 10,954,835, mwaka 2018/19 ukiwa kama kipimo cha ulinganifu. Kupungua huku ni sawa na upungufu wa asilimia 26. Wakati huohuo Tumbaku ilishuka kwa asilimia asilimia 28, na upungufu huo ni sawa na anguko la dola za Marekani 81,059,709.01 katika Mwaka wa Fedha wa 2020/21, na ilianza kuongezeka tena hadi kufikia ongezeko la asilimia 25 kwa Mwaka wa Fedha 2022/23. Ongezeko hili la mapato lilitokana na masoko mapya ya tumbaku yaliyotafutwa na Bodi ya Tumbaku katika kipindi hiki.

Tathmini zaidi zimeonesha kuwa mchango wa mapato ya korosho ulibainika kuwa na ongezeko la kutosha kwa miaka minne ya fedha kutoka 2018/19 hadi 2021/22. Kisha, ulishuka kutoka dola za Marekani 209,115,498 hadi dola 139,994,994, kiwango kilicho shuka ni sawa na asilimia 33 kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/23.

Kwa upande wa Korosho, ilibainika kuwa pamoja na juhudi zilizofanywa na Serikali, bado mapungufu yalibainika. Kwa mfano, ilielezwa kuwa zaidi ya asilimia 90 ya korosho zinazozalishwa nchini ziliuzwa nje ya nchi kama korosho ghafi, hali inayo changia upotevu zaidi wa mapato.

Uchambuzi wa kina wa mabadiliko ya mapato kwa mazao ya biashara yaliyo kaguliwa umeoneshwa kwenye Kielelezo Na. 12.

**Kielelezo Na. 12: Thamani za Mapato ya Mauzo ya Nje kwa Mazao yaliyochaguliwa**



*Chanzo: Mchanganuo wa Wakaguzi kutoka kwenye mapato Yaliyo kusanywa kutokana na Mauzo ya Mazao ya Biashara, 2023*

**Kielelezo Na. 12** kinaonesha kahawa ilikuwa na ongezeko chanya la mapato, wakati chai ilikuwa na ongezeko hasi katika uzalishaji wa mapato. Pia, ilibainika kuwa Bodi ya Chai ilikuwa imeweka juhudi kidogo katika kutafuta masoko mapya, kudhibiti bei, na kuimarisha uzalishaji.

Sababu za mabadiliko ya mapato zilibainishwa kusababishwa na uuzaji wa mazao ya biashara yakiwa ghafi bila kuongezwa thamani kupitia usindikaji, kutokuwapo kwa Maofisa ugani wa kilimo katika ngazi za Vyama vya Msingiambavyo vingedhibiti ubora. Aidha, mabadiliko hayo ya mapato yamesababishwa na kupungua kwa uzalishaji kulikochangiwa na upungufu wa huduma za ugani wa Kanuni Bora za Kilimo.

Hivyo basi, kushuka kwa mapato kumesababisha kutofikiwa kwa mchango wa kilimo katika Pato la Taifa. Hii inaweza kusababisha serikali kushindwa kutoa huduma nyingine za msingi, kama vile afya na elimu, kutokana na uhaba wa mapato.

Ukaguzi ulibaini kuwa, kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya biashara kwa kiasi fulani kulisababishwa na kukosekana kwa mikakati ya miaka mitano ya kuongeza

uzalishaji yenye viashiria muhimu vya utendaji kazi kama vile wingi wa uzalishaji, ubora uliokusudiwa na masoko haukuwapo.

#### 4.3.2 Kanzidata ya Wakulima wa Mazao ya Biashara haikuwa na taarifa za kina kukidhi shughuli za utendaji wa Bodi za Mazao

Ukaguzi ulibaini kuwa kanzidata ya wakulima wa mazao ya biashara haikuwa na taarifa za kutosha kukidhi shughuli za utendaji wa Bodi za Mazao. Hii inathibitishwa na ukweli kwamba, tathmini ya Mfumo wa Usajili wa Wakulima ilionesha kuwa bodi tofauti za udhibiti wa mazao hazikutumia mfumo ulioandaliwa. Ilibainika kuwa, mfumo huo ulikuwa haujahuishwa tangu mwaka 2019.

Ukaguzi pia umebaini kuwa, mfumo haukutengenezwa kukidhi shughuli za utendaji wa Bodi za Udhibiti wa Mazao. Wakati wa maandalizi yake, mfumo haukujumuisha taarifa kutoka kwa watumiaji; kwa mfano, mfumo haukuwa umejumuisha vipengele muhimu kama vile mahali shamba lilipo, historia ya shamba, pembejeo za kilimo zinazohitajika kwa mkulima na vyama vya msingi na masoko.

Pia ilibainika kuwa, Mfumo wa Usajili wa Wakulima uliyotengenezwa ulikosa vipengele 13 ambavyo, kama vingeboreshwa vingeweza kukidhi mahitaji ya utendaji kazi wa bodi zote. Vipengele hivyo ni pamoja kipengele cha kuwezesha mfumo kuhuisha taarifa za wakulima mwanzoni mwa kila msimu wa mazao; kubaini mazao yanayouzwa kwa kulinganisha ukubwa wa shamba pamoja na mamavuno yanayotarajiwa; matumizi ya geotags na GPS ili kuwa na ramani sahihi ya mahali shamba lilipo; uwapo wa taarifa sahihi za shamba ikiwa pamoja na eneo, ukubwa; kufuatilia shughuli za kilimo; na uwezo wa kufanya makadirio ya uzalishaji kwa mkulima mmoja mmoja katika ngazi ya usajili wa wakulima. Pia vipengele vingine vina jumuisha uwezo wa usambazaji wa pembejeo katika mnyororo wote; usambazaji wa pembejeo katika mlolongo wote hadi kwa wakulima; pamoja na takwimu za kiasi cha pembejeo.

Vipengele vingine ni vile vya kuweka makisio ya mahitaji ya kiasi cha pembejeo; kutoa taarifa mwishoni mwa kila msimu wa kilimo huku zikionesha kiasi cha pembejeo zilizopokelewa, kiasi cha mazao ya biashara kinachozalishwa, na salio la pembejeo kwa kila mkulima; na, mfumo hauna kipengele cha kutoa ripoti za usajili wa wakulima kwa mkulima mmoja mmoja katika ngazi ya vyama vya msingi.

Kwa sababu ya kutokuwapo kwa vipengele 13 katika mfumo wa usajili wa wakulima, hali hii iliufanya mfumo kutokukamilika. Hali hiyo iliifanya Bodi ya Mazao kuwa na ugumu kupanga uzalishaji kwa sababu mfumo huo haukuwa na kipengele cha uzalishaji. Kwa hivyo, mfumo hauwezi kutoa taarifa ya mauzo ya kila msimu wa kilimo.



Zaidi ya hayo, kutokuwapo kwa vipengele vyote vilivyoorodheshwa katika mfumo wa usajili wa wakulima kulizifanya bodi za mazao kufanya shughuli hizo bila kutumia mfumo.

Kwa upande mwingine, Timu ya Ukaguzi ilifanya uchambuzi zaidi wa ukamilifu wa mfumo unaotumiwa na Bodi ya Korosho Tanzania na kubaini kuwa Bodi ya Korosho Tanzania iliboresha mfumo huo kutoka Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea Tanzania. Licha ya kutumia Mfumo huo, ilibainika kuwa mfumo huo haukuwa umekamilika kwani ulikuwa na upungufu wa mambo yafuatayo:

- (a) Mfumo huu ulihusisha Manispaa ya Mtwara, Halmashauri za Miji ya Nanyamba, na Tandahimba pekee, na kuacha mikoa mingine 12 inayolima korosho nchini Tanzania;
- (b) Mfumo hausaidii kuonesha wingi wa korosho inayotarajiwa kuzalishwa; badala yake, unaonesha idadi ya miti ya mikorosho kwa kila shamba;
- (c) Mfumo hauoneshi wingi wa pembejeo za kilimo zinazotolewa na kiasi cha pembejeo kwa mkulima mmoja mmoja; na
- (d) Mfumo hauoneshi muda wa Bodi ya Korosho kupokea pembejeo na muda pembejeo zilipotolewa kwa wakulima ili kuweza kupima ufanisi.

Matumizi ya mfumo wenye vipengele vichache ili kusajili wakulima ulisababishwa na uamuzi wa Wizara ya Kilimo kutengeneza mfumo huo bila kushauriana na bodi za mazao ili uendane na shughuli za bodi husika. Zaidi ya hayo, bodi zilikuwa na upungufu wa Maofisa ugani ambao wangwezesha kutoa taarifa za kuhuisha mfumo katika kila msimu wa kilimo.

Hii imesababisha bodi za mazao kuanzisha mifumo mbalimbali jambo ambalo linapelekea kutokuwapo kwa thamani ya fedha. Pia uwapo wa mifumo mingi inayofanya shughuli zinazofanana ni kinyume na sheria ya Mamlaka ya Serikali Mtandao.

#### 4.3.3 Utoaji Usiojitosheleza wa Huduma za Ugani ili Kuhamasisha Uzalishaji Endelevu wa Mazao ya Biashara


Kutokana na Sheria za uanzishwaji wa Bodi za mazao ya biashara na Kanuni zake, Bodi za Mazao zinatakiwa kutoa huduma za ugani kwa wakulima wa mazao ya biashara ili kuhakikisha ongezeko la uzalishaji na ubora wa mazao. Ili kuhakikisha utoaji wa huduma za ugani, Bodi za Mazao zinapaswa kuteua Wakaguzi wenye jukumu la kuhakikisha kunakuwa na utoaji wa huduma za ugani kwa wakati.

Licha ya mahitaji hayo, ukaguzi ulibaini kuwapo kwa mashamba ya wakulima ambayo hayakuhudumiwa ipasavyo huku Uwiano wa Wakaguzi na wakulima ukiwa mkubwa. Ilibainika kuwa uwiano wa huduma ya mkaguzi na wakulima ulianzia 1,680 hadi 23,069, licha ya mtawanyiko mkubwa wa kijiografia. Kwa sababu hiyo, shughuli za kilimo hazikusimamiwa ipasavyo. Muhtasari wa Mikutano ya Bodi iliyopitiwa na mahojiano yaliyofanywa na Maofisa mbalimbali wa Bodi yalibaini mambo yafuatayo:

**(a) Bodi za Mazao zilikuwa na upungufu wa Wakaguzi kwa Wastani wa asilimia 53**

Bodi za mazao zilikuwa na upungufu wa wakaguzi kwa wastani wa asilimia 53. Mapitio ya majalada ya mawasiliano kutoka Bodi za Mazao zilizotembelewa yalibaini kuwa Bodi ya Chai ilikuwa na uhaba wa wakaguzi kwa wastani wa asilimia 89, Bodi ya Tumbaku ilikuwa na uhaba wa wakaguzi kwa asilimia 42, bodi ya korosho ilikuwa na uhaba wa wakaguzi kwa asilimia 75 na bodi ya kahawa ilikuwa na uhaba wa wakaguzi kwa asilimia 7 pekee. Licha ya Bodi ya kahawa kuwasilisha majina na barua za uteuzi wa wakaguzi, na ingawa bodi ya kahawa ilidai kutokuwa na uhaba wa wakaguzi, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa bodi hiyo haikuwa imejumuishwa taarifa za maeneo mengine yanayolima kahawa. Maeneo ambayo hayakujumuishwa katika orodha hiyo ni Ukerewe, Geita, Mara na Tanga. Uchambuzi wa kina ni kama unavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 13**.

**Kielelezo Na. 13: Tathmini ya Idadi ya Wakaguzi wa Mazao Waliopo Dhidi ya Wanaohitajika kutoa Huduma za Ugani katika Bodi za Mazao**



**Chanzo:** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Mazao katika Bodi za Mazao, 2023

Kulingana na matokeo ya ukaguzi, **Kielelezo Na. 13** kinaonesha kuwa idadi ya Wakaguzi wa mazao inayohitajika ilitofautiana kulingana na ukubwa wa shughuli za bodi husika. Bodi ya Chai ilikuwa na uhaba mkubwa wa wakaguzi wanaohitajika kwani ilikuwa na upungufu wa asilimia 89, wakati Bodi ya Kahawa ilikuwa na upungufu mdogo wa wakaguzi sawa na asilimia 7 pekee. Zaidi ya hayo, ilibainika kuwa Bodi ya Kahawa iliteua wakaguzi kutoka Serikali za Mitaa ambako kahawa inakuzwa kuchukua majukumu ya udhibiti katika ngazi ya serikali za mitaa. Licha ya hayo, Maofisa waliohojiwa kutoka Bodi ya Kahawa walionesha kuwa wakaguzi walioteuliwa hawakutekeleza majukumu waliyopaswa kutekeleza kwa sababu ya kuwa na majukumu mengine kutoka kwa mwajiri wao.

Sababu ya uhaba wa wakaguzi wa kusaidia katika majukumu ya usimamizi ulisababishwa na kutokuwapo kwa kipaumbele kwani shughuli hizi ilibidi ziwe jumuishi.

#### **(b) Upungufu wa Huduma za Ugani katika Ngazi ya Vyama vya Msingi kwa asilimia 98**

Ukaguzi pia ulibaini upungufu wa Maofisa Ugani katika ngazi ya vyama vya msingi ambapo shughuli za uzalishaji zinafanyika. Vyama vya msingi havikuwa na uwezo wa kuajiri Maofisa Ugani, na baadala yake walitegemea Maofisa Ugani kutoka Serikali za Mitaa, ambao walikuwa hawatosheshezi. Ilibainika kuwa, vyama vya msingi vilikuwa na wastani wa uhaba wa Maofisa Ugani kwa asilimia 98.6. Tasnia ya Korosho ilikuwa na upungufu mkubwa la Maofisa Ugani kwani ilikosa Maofisa Ugani 734, sawa na asilimia 100, ikifuatiwa na Tumbaku ambayo ilikuwa na upungufu wa asilimia 97.

Aidha, ili kuondokana na tatizo la upungufu wa idadi ya Maofisa Ugani, Wizara ya Kilimo ilianzisha huduma za ugani za kielektroniki kama vile M-Kilimo na kituo cha simu za miito ambapo wakulima hutuma jumbe fupi za bure kuomba huduma za ushauri; Pia Wizara imekuwa na utoaji wa vyombo vya usafiri kwa Maofisa Ugani ili kuwafikia wakulima wengi zaidi katika muda mfupi.

Kwa upande mwingine, viongozi wa vyama vya msingi walikiri kuwa vyama hivyo haviwezi kuajiri Maofisa Ugani kutokana na uhaba wa fedha. Badala yake, walitegemea Maofisa Ugani wa Serikali, ambao walipatikana mara chache kwani Maofisa hao walipangiwa shughuli nyingine na waajiri wao, na kusababisha kutokupatikana pindi wanapohitajika. Hali hiyo hiyo ilibainika kupitia mapitio ya Ripoti ya Ukaguzi wa Ndani ya Bodi ya Tumbaku ya mwaka wa fedha 2022/23.

#### 4.3.4 Mipango duni ya Udhibiti wa Ubora wa Mazao ya Biashara

Mapitio ya Mipango Mikakati ya Bodi ya Tumbaku Tanzania, Bodi ya Chai Tanzania, na Bodi ya Korosho Tanzania ilionesha kuwa Bodi hazikuwa na mpango wa kutosha wa kudhibiti ubora wa mazao ya biashara. Hii ni kwa sababu, vipengele vya udhibiti wa ubora havikuingizwa kwenye Mipango Mkakati ya Bodi za Mazao kwa vile hakukuwa na mipango hiyo.

Kwa upande mwingine, Timu ya Ukaguzi iligundua kuwa Bodi za Mazao hazizingatii masuala ya udhibiti wa ubora kama vile kuanzisha maabara za udhibiti wa ubora, uwapo wa mipango yao ya mwaka. Ukosekanaji wa mipango imepelekea kuwapo kwa mapungufu ya ubora.

Kwa mfano, katika zao la tumbaku, ilionyeshwa kuwa madaraja ya juu katika tumbaku iliyosafishwa na moshi yameshuka kwa asilimia 10 kutoka asilimia 68 mwaka 2014/15 hadi asilimia 58 mwaka 2018/19. Wakati huohuo, madaraja ya kati yaliongezeka kwa asilimia 10 kutoka asilimia 13 hadi asilimia 23, na madaraja ya chini hayakuongezeka kwani yalibaki kuwa na asilimia 19.

Aidha uchambuzi uliofanywa kwenye eneo la usimamizi wa ubora wa korosho ulibaini taarifa za ubora kuwa mdogo kwa sababu bodi ya korosho haikuwa ikitunza kumbukumbu za ubora wa korosho zinazozalishwa katika kumbukumbu zake za mwaka. Kutokana na hali hiyo, hakukuwa na kumbukumbu za ubora wa korosho kwa mwaka 2018/19 hadi 2022/23. Hii ilitokana na ukosefu wa mifumo ya uhifadhi wa kumbukumbu za uzalishaji, ubora, viwango au madaraja.

Chanzo kikubwa kilibainika kuwa ni uelewa mdogo wa Kanuni za Kilimo Bora kwa wakulima na Maofisa ugani, matumizi ya pembejeo yasiojitosheleza mathalani kwa wakulima wa zao la korosho. Aidha, kumekuwa na ongezeko la miti ya korosho iliyozeeka na mikorosho ya kienyeji ambayo uzalishaji wake una tija kidogo. Sababu nyingine muhimu ni pamoja na kukosekana kwa upimaji wa ubora wa kisayansi wa korosho na upangaji madaraja katika ngazi ya msingi. Hii ilisababisha ubora usioendeleu kwenye mazao ya biashara yanayozalishwa.

Kutokana na kwamba ubora wa mazao unaanzia shambani hali hiyo imechangia kupunguza kwa uzalishaji wa mazao ya biashara.

#### 4.3.5 Kutokuzingatia Upangaji wa Gharama za Uzalishaji, Masoko na ushiriki wa wakulima wakati wa Kupanga Bei za Mazao

Mapitio ya Mipango Mkakati ya Bodi za Mazao na mipango ya kila mwaka ya kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2022/23 ilionesha kuwa, Bodi za Mazao

hazikuwa na miongozo au mifumo ya kupanga bei elekezi za mazao ya biashara. njia inayotumika na bodi za mazao wakati wa kupanga bei haifanyi kazi vizuri kwa sababu haitokani na mikakati au mwongozo uliowekwa.


Kwa mujibu wa Maofisa wa Bodi za Mazao ya Tumbaku na Chai ilibainika kuwa, mbinu iliyokuwa ikitumika kupanga bei za mazao ilihusisha mapitio ya bei za miaka ya nyuma kwa miaka mitatu ili kupata bei elekezi. Hata hivyo, Ukaguzi haukubaini uwapo wa nyenzo yoyote yenye kuonesha utaratibu wa upangaji wa bei elekezi.

Zaidi ya hayo, ilibainika kuwa Bodi ya Korosho na Bodi ya Tumbaku zilitegemea tu bei zilizokubaliwa wakati wa mikutano ya mwaka ya wadau, na wakati huohuo bodi ya chai ilitumia bei zilizopangwa wakati wa mkutano wa wadau.

Kati ya Bodi nne za Mazao, ni bodi ya Kahawa pekee iliyokuwa na mbinu bora zaidi, kwani bei elekezi zilizotolewa na bodi ya kahawa zilitegemea kanuni za kimataifa kwa kurejea soko kuu la kahawa. Kwa kahawa aina ya Robusta, soko kuu liko London nchini Uingereza(LIFE Market), na kahawa aina ya Arabika soko lake liko katika jiji la New York nchini Marekani.

Mchakato usioridhisha wa upangaji bei elekezi za mazao ya biashara umesababisha kushuka kwa bei inayoletwa na wakulima. Kwa mfano, bei ya korosho ilikuwa shilingi 2,997 mwaka 2018/19 na imeshuka hadi shilingi 1,810 mwaka 2022/23. Hii ni sawa na kushuka kwa asilimia 40. **Kielelezo Na. 14** kinaonesha mwenendo wa mabadiliko ya bei elekezi ya korosho.

**Kielelezo Na. 14: Mwenendo wa Mabadiliko ya Bei za Mazao ya Biashara kwa Miaka Mitano Iliyopita**



*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Bei za wastani zilizopatikana, 2023*

**Kielelezo Na. 14** unaonesha kupungua kwa bei iliyopatikana baada ya mauzo ya korosho. Bei ya Korosho ilianza kwa bei ya juu zaidi ya shilingi 2,997 mwaka 2018/19 hadi shilingi 1,810 mwaka 2022/23, kushuka kwa shilingi 1,187 kwa miaka mitano.

Zaidi ya hayo, mapitio ya mfumo wa upangaji bei yalionesha kuwa Bodi za Mazao hazikuwa na utaratibu wa kisasa wa kupata bei elekezi za mnada wa dunia wa mazao maalumu ya biashara. Ilielezwa kuwa Bodi ya Korosho ilikuwa na utaratibu wake shirikishi kupitia Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wadau kwa ajili ya kupanga bei elekezi kabla ya 2018/19 kabla Serikali hijasitisha upangaji bei. Hivyo, Bodi ya Korosho haikuwa na bei elekezi kuanzia mwaka wa fedha wa 2019/20 hadi misimu ya mazao 2022/23. Wakulima waliuza mazao yao chini ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani kupitia minada na Soko la Msingi.

#### 4.4 Matokeo ya Ukaguzi wa Udhhibiti wa Usambazaji wa Mbolea

##### 4.4.1 Uwapo wa Mbolea yenye Ubora Unaotia Shaka Sokoni

Mapitio ya Ripoti za Ukaguzi kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Mbolea, na mapitio ya Ripoti za Ukaguzi wa Ndani za kipindi cha kuanzia 2020/21 hadi 2022/23 zilionyesha uwapo wa mbolea zenye sifa zinazo tia shaka.

Ukaguzi ulibaini uwapo wa mbolea za majani ambazo hazikusajiliwa, uwapo wa mbolea na virutubisho ambavyo havikuweza kufanyiwa majaribio na uwapo wa mbolea iliyoisha muda wake sokoni. Maelezo ya kina ni kama yalivyo fafanuliwa hapa chini:

##### (a) Asilimia 2.5 ya Mbolea za Majani zilizokaguliwa hazikuwa zimesajiliwa

Mapitio ya Ripoti ya Ukaguzi ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea ya mwaka 2020/21 hadi 2022/23 na Ripoti ya Ukaguzi wa Ndani ya Julai hadi Septemba 2020 ilibaini kuwa, aina 28 za mbolea za majani ambazo hazikuwa zimesajiliwa zilisambazwa sokoni na kuuzwa kwa wakulima. Hii inakinzana na kifungu namba 1.4 cha Muundo wa Taasisi ulioidhinishwa wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea Tanzania wa mwaka 2019, inayoitaka Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea kusajili na kutunza daftari la kumbukumbu la mbolea kabla ya kupelekwa sokoni.

Usajili huo pamoja na mambo mengine unalengo la kuhakikisha mbolea na virutubisho vinavyosambazwa sokoni vinakidhi viwango vya ubora vinavyotakiwa. Uwapo wa mbolea ambazo hazijasajiliwa sokoni ni ishara ya kuwapo kwa mbolea za majani ambazo hazikuwa zimejaribiwa ili kuthibitisha

ubora wake. **Jedwali Na. 4** linatoa mchanganuo wa idadi za mbolea ambazo hazijasajiliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea.

**Jedwali Na. 4: Mbolea za Majani Zilizosajiliwa na Zisizosajiliwa**

Mwaka wa Fedha	Mbolea za Majani ziliyosajiliwa	Mbolea za Majani zisizosajiliwa zinapatikana Sokoni	Asilimia ya Mbolea za Majani ambazo hazijasajiliwa
2020/21	282	7	2.48
2021/22	360	9	2.50
2022/23	470	12	2.55

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka Ripoti ya Ukaguzi wa Ndani, Ripoti ya Ukaguzi wa Kanda (2023)*

**Jedwali Na. 4** linaonesha ongezeko la idadi ya mbolea na virutubishi vilivyosajiliwa kutoka 282 mwaka wa fedha 2020/21 hadi 470 mwaka wa fedha 2022/23. Kwa upande mwingine, kupitia ukaguzi uliofanywa na Mamlaka ya Usimamizi wa Mbolea kulikuwa na ongezeko la mbolea za majani ambazo hazijasajiliwa zilizopatikana sokoni kwa kipindi hicho. Asilimia ya mbolea za majani ambazo hazijasajiliwa iliongezeka kutoka asilimia 2.48 kwa mwaka wa fedha 2020/21 hadi asilimia 2.55 kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Hii ilisadifu ongezeko la kiasi cha mbolea iliyoagizwa kutoka nje ambayo haikuzingatia taratibu za usajili zilizowekwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea, ingawa ilisambazwa kwa wakulima. Mbolea na virutubisho ambavyo havijasajiliwa vinatokana na kutofanyiwa ukaguzi wa kutosha mipakani, ukaguzi wa wauzaji wa pembejeo za kilimo na ukaguzi wa watengenezaji wa mbolea na virutubisho.

**(b) Asilimia 14 ya Mbolea na Virutubisho vya Mimea vilivyokuwa Sokoni havikua vimefaulu majaribio ya Ubora**

Ukaguzi ulibaini kuwa Idadi 3 kati ya 21 ya Mbolea ambayo ni sawa na Asilimia 14 ya mbolea zilizo sajiliwa kati ya mwezi Januari na Machi 2021 zilisajiliwa ingawa hazikuwa zimekidhi viwango baada ya majaribio ya maabara.

Ilibainika kuwa, mbolea zilisajiliwa kabla ya kupokea majibu ya vipimo vya maabara. Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea ilikuwa bado haijajumuisha hatua ya kupitia na kutafsiri taarifa za vipimo vya maabara, kabla ya mbolea haijasambazwa kwa wafanyabiashara wa pembejeo za kilimo na wakulima. Usajili wa Mbolea na Virutubisho ambavyo havijakidhi vipimo vya ubora unaweza kuathiri dhana ya kiasi cha mbolea kinacho hitajika kwa kila eneo, hii inaweza kusababisha kutokufikiwa kwa kiasi cha mbolea kinacholengwa kutumika mashambani na hali hii inaweza kuathiri uzalishaji wa wakulima na uchumi.

#### 4.4.2 Upatikanaji Mdogo wa Mbolea na Virutubisho vya Mimea kwa Wakulima

Upatikanaji wa mbolea zenye ubora unaathiriwa moja kwa moja na uwapo wa wa vituo vya usambazaji na wauzaji wa pembejeo za kilimo ambapo wakulima wanaweza kupata mbolea kwa urahisi kulingana na mahitaji yao na kwa bei nafuu.

Mapitio ya Daftari la Wauza wa pembejeo za Kilimo na Ripoti ya Utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku kwa mwaka 2022/23, ukaguzi ulibaini kuwa wafanyabiashara 1,712 kati ya 4,346 waliosajiliwa (sawa na asilimia 39) katika programu ya ruzuku hawakuwa wakiuza wala kusambaza mbolea za ruzuku. Vilevile, katika mikoa mitano iliyo kaguliwa, ni asilimia 58 hadi 75 ya wafanyabiashara wa pembejeo za kilimo hawakuuza mbolea ya ruzuku.

Aidha, Halmashauri 41 kati ya 185 ambapo ni sawa na asilimia 22 hazikupata mbolea chini ya mpango wa ruzuku. Halmashauri nane(8) kati ya 39 ambazo ni sawa na asilimia 21 hazikuwa na wafanyabiashara wa pembejeo za kilimo waliosajiliwa katika mpango wa ruzuku katika mikoa mitano iliyotembelewa. Kutokana na kutokuwapo kwa wafanyabiashara wa pembejeo za kilimo katika Halmashauri husika, wakulima walilazimika kusafiri kwenda kwenye Halmashauri nyingine kutafuta mbolea ya ruzuku.

Pia ilibainika kuwa wakulima 2,551,239 kati ya 3,389,951 waliojiandikisha katika mpango wa ruzuku sawa na asilimia 75 hawakupata na kutumia mbolea kupitia mpango wa ruzuku licha ya kuwa na sifa ya kupata mbolea ya ruzuku. Ukaguzi ulibaini kuwa, hii ilitokana na sababu mbalimbali kama vile:

- Kutokuwa na ufanisi katika kufanya makisio ya mahitaji ya mbolea na virutubisho vy mimea;
- Ucheleweshaji wa usambazaji wa mbolea, hivyo kuchelewesha upatikanaji wa mbolea kwa wakulima;
- Udhhibiti usiojitosheleza wa bei za mbolea na virutubisho vy mimea;
- Ukaguzi usio na tija wa wasambazaji na wauzaji wa pembejeo za kilimo; na
- Tathmini isiyojitosheleza ya utendaji wa mamlaka ya udhibiti wa mbolea, Pamoja na wafanyabiashara wa pembejeo za kilimo.

Upatikanaji mdogo wa mbolea ulichangia utumiaji mdogo wa mbolea, ambao ulikuwa Kilo 19 kwa hekta. Kiwango hiki kilikuwa chini ya kilo 50 ya malengo ya Mkataba wa Abuja wa 2006, ambao unataka matumizi yawe kilo 31 kwa hekta sawa na asilimia 62 ambayo ni shabaha iliyopangwa kufikiwa na nchi.



### 4.4.3 Makisio Hafifu ya Mahitaji ya Mbolea na Virutubisho vya Mimea


Ukaguzi ulibaini kuwa Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea haikuwa na utaratibu madhubuti wa kufanya makisio ya mahitaji ya mbolea na virutubisho vy mimea ili kupata mahitaji halisi yanayo hitajika nchini. Ilibainika kuwa Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea haikuwa na utaratibu, mfumo au programu madhubuti ya kuainisha aina ya mbolea pamoja na mahitaji sahihi yanayo hitajika.

Badala yake, Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea ilikusanya takwimu na taarifa za mahitaji kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuzitumia kufanya makisio ya mahitaji, jambo ambalo halikuweza kutoa taarifa sahihi zinazohitajika. Kulikuwa na utofauti wa takwimu za makisio ya mahitaji ya wa mbolea na virutubisho vya mimea ambayo ilikuwa kati ya asilimia 14 hadi asilimia 18.

Pia, uchambuzi wa wakaguzi juu ya michakato ya makisio ya mbolea inayohitajika ulibaini kuwa haukuzingatia ukubwa wa shamba, kiasi cha mbolea kinachohitajika na aina ya mazao yatakayolimwa. Mambo yaliyozingatiwa hayakuwa na ufanisi katika kutoa taarifa za kuaminika.

Uchambuzi wa Wakaguzi juu ya takwimu halisi ya mahitaji ya mbolea ulibaini kuwa mahitaji ya makisio ya mbolea ulikuwa mkubwa kuliko takwimu halisi za matumizi. **Kielelezo Na. 15** kinaonesha tofauti kati ya makisio ya mahitaji na matumizi halisi ya mbolea.

**Kielelezo Na. 15: Utofauti kati ya Makisio ya mahitaji na matumizi Halisi ya Mbolea**



*Chanzo: Mchanganuo wa wakaguzi kutokana na Taarifa za Mahitaji na Matumizi kutoka Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea(2023)*

**Kielelezo Na. 15** kinaonesha kuwa kwa miaka yote mitatu, makisio ya mahitaji yalikuwa juu kuliko kiwango cha matumizi ya miaka husika. Pia inaonesha kuwa tofauti ya asilimia ya makisio na uhalisia ilikuwa kati ya asilimia 14 hadi asilimia 48, na asilimia kubwa zaidi ilionekana mwaka 2021/22. Utofauti mkubwa kati ya makisio ya mahitaji na mahitaji halisi ulisababishwa na utumiaji mdogo wa taarifa wakati wa ufanyaji wa makisio.

Aidha, uchambuzi uliofanywa na timu ya ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea haikuzingatia vya kutosha kiasi, aina, na kiwango cha maombi kwa misimu ya kilimo ili kutoa taarifa za uhakika. Vilevile, Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea haikuratibu ipasavyo na Mamlaka za Serikali za Mitaa, wakati wa makisio ya mahitaji.

Udhaifu katika ukusanyaji wa makisio ya mahitaji ya mbolea ulisababishwa na uhaba wa Maofisa kilimo katika ngazi ya kijiji ambao ulihitajika ili kupata taarifa ya aina ya mbolea inayohitajika kulingana na udongo katika vijiji vyao.

Kutokana na hali hiyo, uchambuzi wa takwimu za mahitaji na matumizi halisi ya mbolea umebaini kuwa kwa miaka mitatu ambayo ukaguzi huu ulijikita, takwimu za makisio ya mahitaji ya mbolea zilikuwa kubwa kuliko matumizi halisi ya maeneo husika kwa asilimia 14 hadi asilimia 48.

#### 4.4.4 Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea Haikuhakikisha Usambazaji wa Mbolea na Virutubisho vya Mimea Unafanyika kwa Wakati kwa Wakulima

Ukaguzi ulibaini uratibu mdogo wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea na Mamlaka ya Bandari Tanzania ili kuhakikisha usambazaji wa Mbolea yenye bora kwa wakulima unafanyika kwa wakati. Kwa mfano, kutokuwapo kwa uratibu wa kutosha kati ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ulishindwa kusimamia uingiaji wa shehena ya mbolea nchini, ambayo ilitarajiwa kuwasili tarehe 22 Agosti, 2022, badala yake ilichelewa na kufika tarehe 2 Septemba, 2022. Hii ilisababisha ongezeko la gharama la shilingi 1,086 kwa mfuko mmoja wa kilo 50 ya mbolea aina ya NPK iliyosambazwa wakati wa msimu wa kilimo wa mwaka 2022/23.

Aidha, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea haikusimamia udhibiti wa uagizaji wa mbolea na virutubisho vya mimea kupitia Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21 hadi 2022/23, Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea ilitangaza zabuni nne zinazowahitaji waagizaji kuagiza kutoka nje kupitia Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja, lakini ilibainika kuwa zabuni mbili kati ya nne zilizotangawa wazabuni hawakuonesha nia ya kushiriki.

Aidha ilibainika kuwa hata zabuni mbili (2) zilizofanikiwa baada ya kutangazwana Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea hazikuzingatia uingizaji wa mbolea na virutubisho vya mimea vilivyoidhinishwa ambavyo ni UREA, DAP, SA, CAN na NPK, kwa mujibu wa jedwali la kwanza la kanuni ya Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja, ya mwaka 2017. Badala yake, zabuni mbili (2) zilizofanikiwa kutangazwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea zilijumuisha aina mbili tu za mbolea aina ya DAP na UREA, na kuacha aina nyingine ambazo wakulima walitumia zaidi.

Vilevile, ukaguzi ulibaini kuwa, kuanzia mwaka 2020/21 hadi 2022/23, tani 48,530 kati ya tani 1,395,977 za mbolea ziliagizwa kutoka nje ya nchi kupitia Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja. Hii ina maana kwamba ni asilimia nne tu ya uagizaji wa mbolea kutoka nje ulifanywa kupitia Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja. Hii ilipunguza fursa ya kuimarisha uchumi kama manunuzi yangefanywa kwa pamoja. Pia uagizaji mdogo uliathiri upangaji wa bei elekezi.

#### 4.5 Athari katika kufikia malengo ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Mendeleo Endelevu

Sehemu hii, inatoa ufafanuzi kuhusu athari udhibiti usiyojitosheleza wa mazao ya biashara na udhibiti usiyojitosheleza wa usambazaji wa mbolea nchini kuelekea kufikia Malengo ya Maendeleo ya Endelevu na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Athari zinazoweza kupatikana ni kama zinavyooneshwa hapa chini:

Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano una nia ya kuhakikisha uzalishaji wa mazao ya biashara unaongezeka kutoka tani 794,000 mwaka 2019/20 hadi tani 1,583,200 ifikapo mwaka 2025/26. Pamoja na hitaji hilo, serikali kupitia bodi za udhibiti wa mazao, iko hatarini kutofikia malengo yaliyowekwa kwa sababu uzalishaji wa mazao ya biashara umekuwa ukipungua kwa miaka mingi. Kwa mfano, chai imeshuka kwa asilimia 26 kutoka 2018/19 hadi 2022/23, wakati korosho imeshuka kwa asilimia 33 katika mwaka huohuo. Mazao mengine ya biashara yalikosa ongezeko, na badala yake uzalishaji ulikuwa ukibadilika-badilika.

Zaidi ya hayo, katika ukaguzi wa udhibiti wa usambazaji wa mbolea, kuna matukio ya mara kwa mara ya mbolea zisizosajiliwa nchini na asilimia 14 ya mbolea haikupimwa ubora wake. Hii inadhoofisha uzalishaji wa mazao ya chakula na kuhatarisha kufikiwa kwa Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano.

Pamoja na hayo, kutotekelezwa ipasavyo udhibiti wa mazao ya biashara yanayouzwa nje ya nchi na udhibiti wa usambazaji wa mbolea kunaweza kuathiri ufikiwaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu. Ufikiaji duni wa thamani ya uzalishaji wa mazao ya biashara husababisha hatari ya kufikiwa kwa shabaha namba 8.2 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ambalo linalenga kuhakikisha kuongeza thamani na tija. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kupungua kwa uzalishaji kumesababisha kupungua kwa mapato yenye lengo la kuimarisha ukuaji wa uchumi.

Pia, kutotekelezwa ipasavyo udhibiti wa mazao ya biashara yanayouzwa nje ya nchi na udhibiti wa usambazaji wa mbolea kunaweza kusababisha athari ya kufikia lengo namba 2 la Malengo ya Maendeleo Endelevu ambalo lina lengo la kumaliza njaa. Kupitia shabaha namba 2.4 ya lengo hilo linalenga kuhakikisha kuwa kuna kuwapo na mifumo endelevu ya uzalishaji wa chakula na kutekeleza mbinu za kilimo zenye uthabiti kwa kuongeza tija na uzalishaji, zinazosaidia kudumisha mifumo ikolojia ambayo ingeweza kuboresha ardhi na ubora wa udongo. Kwa kuwa kuna udhaifu uliobainika katika usambazaji wa mbolea, na kwa kuwa kuna matukio ya uwapo wa mbolea isiyosajiliwa kuna athari ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara ambayo inaweza kusababisha njaa.

Zaidi ya hayo, usambazaji wa mbolea zisizosajiliwa kuna athari za moja kwa moja kwenye ufikiwaji wa shabaha namba 12.4 la lengo namba 12 la Mpango wa Maendeleo Endelevu kwani inakusudiwa kufikia udhibiti mzuri wa mazingira, kemikali, maji na udongo. Utumiaji wa mbolea zisizodhibitiwa zinaweza kuwa na athari kwa watumiaji kwani inaweza kuathiri mazingira ikiwa pamoja na udongo na maji.



## MAENDELEO YA RASILIMALI WATU

### 5.1 Utangulizi

Sura hii inatoa matokeo ya ukaguzi yanayotokana na ripoti za ukaguzi wa utendaji zinazohusiana na Elimu ya Ufundi, Utekelezaji wa Programu za Urekebu kwa Wafungwa pamoja na Uendelezaji, Ufuatiliaji na Tathmini ya Ujuzi wa Watumishi katika Sekta za Umma. Sura hii pia inaelezea eneo la ukaguzi, vyombo vya serikali vinavyohusika katika ukaguzi, uhusiano wa eneo la ukaguzi na Malengo ya Maendeleo Endelevu, Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Kaguzi hizi za Ufanisi ni pamoja na:

- (a) Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Udhhibiti wa Elimu ya Ufundi nchini;
- (b) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utekelezaji wa Programu za Urekebu kwa Wafungwa; na
- (c) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Uendelezaji, Ufuatiliaji na Tathmini ya Ujuzi wa Watumishi katika Sekta za Umma

#### 5.1.1 Usuli Kuhusu Maendeleo ya Rasilimali watu

Maendeleo ya Rasilimali watu ni jambo la msingi kwenye kila Mpango wa Maendeleo nchini Tanzania. Serikali kupitia udhibiti wa elimu ya ufundi imelenga kutathmini taratibu za usajili na uidhinishaji wa vibali kwa vyuo za ufundi, msaada wao katika kudhibiti ubora wa elimu, utoshelevu wa taratibu na utoaji wa taarifa za uthibiti wa elimu, na ufuatiliaji wa utoaji wa elimu ya ufundi ili kuwa na ujuzi wa kutosha kwa lengo la kukidhi mahitaji ya soko la ajira.

Aidha, Serikali kupitia Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR-MUUUB) imejikita katika kuhakikisha uwapo wa umahiri wa

watumishi wa umma ikiwa pamoja na orodha ya ujuzi na tabia ambazo ni mahususi na zimefafanuliwa vizuri, na zinatumiwa kuweka matarajio ya utendaji wa taasisi au utamaduni wa taasisi kwa ujumla. Shughuli za uendelezaji, ufuatiliaji, na tathmini ya umahiri wa watumishi katika sekta ya umma inatakiwa ionekane ni jambo zuri linalopaswa kuigwa.

Vilevile, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Jeshi la Magereza Tanzania, imejikita katika kutekeleza shughuli za urekebu wa wafungwa magerezani ambazo zinalenga kuwarekebisha wafungwa kupitia program za urekebu.

### 5.1.2 Uhusiano wa Uendelezaji wa Rasilimali watu na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Sehemu hii inaelezea uhusiano uliopo kati ya Maendeleo ya rasilimali watu na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano kupitia ukaguzi wa ufanisi kuhusu Udhhibiti wa Elimu ya Ufundi; Uendelezaji, Ufuatiliaji, na Tathmini ya Ujuzi wa Watumishi wa Umma; na Utekelezaji wa Programu za Urekebu kwa wafungwa kama inavyoelezewa hapa chini:

#### (a) *Uhusiano wa Maendeleo ya Rasilimali watu na Malengo ya Maendeleo Endelevu*

Tanzania kama mwanachama wa Umoja wa Mataifa, inalazimika kufuata Ajenda ya Umoja wa Mataifa ya mwaka 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu. Ili kukabiliana na changamoto za maendeleo ya rasilimali watu, ukaguzi wa ufanisi kuhusu udhibiti wa elimu ya ufundi ulifanyika. Ukaguzi huu unahusishwa na Lengo Na. 4 la Malengo ya Maendeleo Endelevu ambalo linaitaka Serikali kuhakikisha upatikanaji wa elimu jumuishi, yenye usawa na kukuza fursa za kujifunza kwa wote. Kupitia Shabaha 4.3, ifikapo mwaka 2030, serikali inapaswa kuhakikisha upatikanaji sawa wa elimu ya ufundi kwa wote (wanawake na wanaume), ikiwemo elimu ya juu pamoja na vyo vikiu.

Ukaguzi wa ufanisi kuhusu Uendelezaji, Ufuatiliaji na Tathmini ya Ujuzi wa Watumishi katika Sekta za Umma unahusiana na Lengo Na. 8 la Malengo ya Maendeleo Endelevu, ambalo linalenga kuimarisha ukuaji wa uchumi shirikishi na endelevu na ajira kwa wote. Kupitia shabaha 8.5 ifikapo mwaka 2030, serikali inapaswa kufanikisha ajira bora na yenye tija na nzuri kwa wanawake na wanaume wote, ikiwa pamoja na vijana na watu wenye ulemavu, na malipo sawa kulingana na thamani ya kazi.

**(b) Uhusiano kati ya Maendeleo ya Rasilimali watu na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano**

Usimamizi wa masuala ya rasilimali watu umebainishwa kupitia ukaguzi wa ufanisi katika udhibiti wa elimu ya ufundi ambayo unahusiana na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Aya ya 5.6 katika Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano inaelekeza upatikanaji wa zana za kujifunzia, warsha, waalimu wenye sifa, na uwekezaji wa kasi katika maendeleo ya ujuzi. Zifuatazo ni hatua muhimu katika kuboresha elimu ya ufundi:

- i) Kuwezesha upatikanaji wa vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote;
- ii) Kuboresha upatikanaji wa watumishi wa kitaaluma, wataalam wa maabara, wataalam wa karakana, na wataalam wa maktaba; na
- iii) Kupitia na kuhuisha mitaala inayoendana na soko la ajira.

Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26) unatambua umuhimu wa ukuaji katika eneo la utawala bora na utawala wa sheria ili kutambua maendeleo ya rasilimali watu. Kwa kuwa muhimu wa utawala bora katika kufikia malengo mapana ya mipango ya kitaifa, umethaminiwa katika Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Mpango-mkakati wake pia umejikita katika kukuza utawala bora katika utumishi wa umma.

Ukaguzi huu unahusishwa na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano katika maeneo yafuatayo:

- (i) Kuhimiza matumizi ya TEHAM ya kirafiki katika ngazi zote za mafunzo ya ujuzi na ujifunzaji;
- (ii) Kukuza uvumbuzi na uhamisho wa ujuzi na teknolojia; na
- (iii) Kukuza ujuzi wa ajira kwa makundi ya watu wenye mahitaji maalumu.

**(c) Uhusiano kati ya Utekelezaji wa Programu za Urekebu kwa Wafungwa na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu**

Ukaguzi wa ufanisi kuhusu Utekelezaji wa Programu za Urekebu kwa Wafungwa unahusiana na maeneo ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu kama ilivyoelezwa kwa ufupi katika **Jedwali Na. 5**.

**Jedwali Na. 5: Uhusiano kati ya Utekelezaji wa Programu za Urekebu wa Wafungwa na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu**

Mipango	Maeneo ya kipaumbele	Maeneo ya Mkakati
Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano	Kuimarisha usalama wa umma, sheria na utaratibu	Programu ya Kuendeleza Huduma za Magereza (Usajili wa Vyuo vitano vya Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini ifikapo Juni 2026)
Malengo ya Maendeleo Endelevu	Lengo Na. 16. Kukuza jamii zenye amani na umoja kwa maendeleo endelevu, kutoa upatikanaji wa haki kwa wote na kujenga taasisi zenye ufanisi, uwajibikaji na umoja katika ngazi zote	Shabaha Na. 16.1 Kupunguza kwa kiasi kikubwa aina zote za ukatili na vifo vinavyoambatana na ukatili kila mahali.

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu.*

**5.1.3 Mikakati na Jitihada za Serikali katika Maendeleo ya Rasilimali watu**

Jedwali Na. 6 hapa chini linaonesha muhtasari wa Mikakati na Jitihada za Serikali katika kuboresha maendeleo ya rasilimali watu:

**Jedwali Na. 6: Mikakati na juhudi zilizofanywa na Serikali katika kuboresha rasilimali watu**

S/N	Mikakati ya Serikali	Juhudi za Serikali
1.	<b>Udhibiti wa Elimu ya Ufundi</b>	
	Mpango mkakati wa Wizara ya Elimu (2016/17 - 2020/21)- Kuboresha ujuzi katika sekta za kiuchumi zilizochaguliwa, ambazo zimegawanywa katika uchumi wa msingi (biashara ya kilimo, utalii na ukarimu, na nishati) pamoja na kuwezesha sekta ya ujenzi, usafirishaji na vifaa, teknolojia ya habari na mawasiliano.	Kwa mujibu wa hotuba ya Waziri wa elimu wakati wa bunge la bajeti 2022/23, iliriporitiwa kuwa serikali imeanzisha ujenzi wa vyuo 16 vya Maendeleo ya Watu ili kuongeza upatikanaji wa elimu ya ufundi ambayo itasaidia kuongeza wahitimu nchini.
	Mpango-mkakati wa Baraza la Taifa la Elimu ya ufundi na Mafunzo ya ufundi stadi 3	Pia, Serikali imeweza kununua samani na vifaa vya kujifunzia katika vyuo vya Ufundi ikiwemo, Chuo cha Ufundi Kongwa, Chuo cha Ufundi Kasulu, Chuo cha Ufundi Nyasa, na Chuo cha Ufundi Ruangwa. Aidha, Serikali inaendelea kujenga vituo vya umahiri ikiwemo katika Chuo cha Ufundi

<sup>3</sup> Kwenye taarifa hii, Baraza la Taifa la Elimu ya ufundi na Mafunzo ya ufundi stadi itajulikana kama Baraza la Elimu ya Ufundi.



S/N	Mikakati ya Serikali	Juhudi za Serikali
	(2021/22- 2025/26), Serikali imepanga mikakati ya kuboresha ubora na utoaji wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi katika ngazi zote.	Arusha, vyuo ya Teknolojia Dar es Salaam na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji katika nyanja za Nishati, Usindikaji Ngozi, Uchukuzi na Tehama kwa ajili ya kuboresha wahitimu wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi nchini.
2.	<b>Ujuzi wa watumishi katika Taasisi za umma</b>	
	Katika Mpango-mkakati wa Miaka Mitano wa (OR-MUUUB) 2021/22 -2025/26, Serikali iliweka mkakati wa kuwa na utawala bora na kuliwezesha taifa katika muundo wa kijamii na kiuchumi, kuhakikisha utamaduni wa uwajibikaji, ili kutoa utendaji mzuri na kudhibiti rushwa na maadili mengine katika jamii. Lengo ni kuwezesha huduma ya umma kufanya kazi kwa ufanisi na kwa kuzingatia utofauti wa kijamii.	Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania imeweza kumhusisha mtumishi wao wa umma katika mafunzo katika nchi za nje kama India, China, Korea na Japan. Jumla ya Watumishi wa Umma 334 walipatiwa mafunzo ya kozi ndefu na jumla ya Watumishi wa Umma 914 walipatiwa mafunzo ya kozi fupi.
3.	<b>Urekebushaji wa wafungwa</b>	
	Katika Mpango-mkakati ya Huduma za Magereza Tanzania kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2020/21 na mwaka wa fedha 2021/22 hadi 2025/26, Serikali iliweka mikakati ya mipango iliyoivezesha Jeshi la Magereza Nchini kuzingatia mikakati iliyotengwa kwa ajili ya programu bora za marekebisho ya utoaji wa huduma kwa wafungwa.	Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilianzisha Kitengo cha Huduma za Urekebukwa Wafungwa chini ya Jeshi la Magereza Tanzania ili kuwarekebisha wafungwa. Pia, Jeshi la Magereza Tanzania lilianzisha Gereza la Shule ya Ufundi Ruanda-Mbeya na gereza la vijana (Wami Viijana) mkoani Morogoro. Aidha, Jeshi la Magereza Tanzania limeanzisha Stashahada ya kawaida ya Sayansi ya Urekebu kwa Maofisa Magereza katika Chuo cha Mafunzo ya Urekebu Tanzania

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi juu ya Mikakati na Juhudi zinazofanywa na Serikali, 2023.*

## 5.2 Malengo na Mawanda ya Ukaguzi

### 5.2.1 Malengo ya Ukaguzi

Lengo kuu la ukaguzi, lilikuwa kutathmini endapo Wizara husika kama zilisimamia ipasavyo maendeleo ya rasilimali watu kwa kuzingatia udhibiti wa Elimu ya Ufundi, umahiri wa watumishi katika huduma za umma na programu za urekebu wa wafungwa.

Malengo mahususi ya ukaguzi yalikuwa ni:

- (i) Kubaini endapo Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kupitia Baraza la Taifa la Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, imesimamia ipasavyo utoaji wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili kuhakikisha kuwa wahitimu kutoka vyuo vya Ufundi wana ubora wa hali ya juu na wanaitikia mabadiliko ya mahitaji pamoja na ubunifu wa kiteknolojia duniani.
- (ii) Kutathmini endapo Wizara zinazohusika zina ufanisi wa kusimamia maendeleo, ufuatiliaji na tathmini ya umahiri wa watumishi ili kuongeza ufanisi wa watumishi katika utoaji wa huduma kwa umma.
- (iii) Kutathmini endapo Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia Jeshi la Magereza Tanzania limetekeleza kwa ufanisi programu za urekebu kwa wafungwa ili kuwawezesha wafungwa kuunganishwa upya na jamii pindi wanapomaliza vifungo vyao.

### 5.2.2 Mawanda ya Ukaguzi

Ukaguzi wa Udhhibiti wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ulilenga katika kutathmini michakato katika usajili na utoaji wa Elimu na mafunzo ya ufundi kwa vyuo vya Ufundi, msaada unaotolewa kwa vyuo vya Ufundi ili kuhakikisha ubora wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi yanayotolewa. Ukaguzi ulitizama utoshelevu wa taratibu zinazotumika kuhakikisha uzingatiaji wa ubora wa elimu na mafunzo ya ufundi yanayotolewa, utoshelevu katika uratibu na utoaji taarifa juu ya udhibiti wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo, na utoshelevu katika kufuatilia utoaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo. Ukaguzi ulihusisha miaka minne ya fedha, kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2022/23.

Kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa uendelezaji, Ufuatiliaji na Tathmini ya Uwezo wa Watumishi katika Sekta ya Umma. Ukaguzi ulilenga kutathmini ufanisi wa OR-MUUUB katika kuhakikisha kuwa taasisi za umma zinatabua mapungufu katika umahiri wa watumishi, kuendeleza mipango ya kujenga umahiri, kutekeleza mipango ya kujenga umahiri na kupima utendaji wa watumishi wao. Ukaguzi ulihusisha kipindi cha Miaka Mitano ya Fedha kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2022/23.

Pia, katika utekelezaji wa programu za urekebu wa wafungwa Ukaguzi huu ulilenga kutathmini ufanisi wa mipango ya urekebu. Hasa, ulilenga katika kusanifu mipango ya urekebu, utekelezaji wake, mchakato wa kutekeleza, kuunganisha michakato, ufuatiliaji na kuratibu utekelezaji wake. Ukaguzi huu ulihusisha miaka minne ya kifedha kutoka 2019-20 hadi 2022-23.

### 5.3 Matokeo ya Ukaguzi kwenye Udhhibiti wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo

Sehemu hii inatoa muhtasari wa matokeo ya ukaguzi wa ufanisi kuhusu Udhhibiti wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo kama ilivyoelezewa hapa chini:

#### 5.3.1 Udhhibiti Usiotosheleza wa Utoaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo kwa Kuendana na Mahitaji ya Soko la Ajira

Ukaguzi ulibaini kuwa, Baraza la Elimu ya Ufundi halikusimamia ipasavyo utoaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo nchini. Hii ni kwa sababu ukaguzi ulibaini kuwa usambazaji wa mafundi mchundo ulikuwa mdogo kuliko mahitaji ya soko la ajira katika sekta za umma na binafsi kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 7.

**Jedwali Na. 7: Mgawanyo wa Soko la Ajira kwa Ngazi ya Mafundi Mchundo**

Sekta	Mahitaji ya Mafundi Mchundo <sup>4</sup>	Idadi ya Mafundi Mchundo waliopo	Asilimia ya Upungufu wa Mafundi Mchundo
TEHAMA	67,936	25,476	63
Nishati na Madini	8,254	5,505	33
Biashara ya kilimo	46,198	35,203	23
Utalii na Ukarimu	6,374	5,214	18
Ujenzi	22,216	18,506	17
Usafiri	6,316	5,867	7
<b>Jumla</b>	<b>157,294</b>	<b>95,771</b>	<b>39</b>

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi katika Jarida la Baraza la Elimu ya Ufundi (Januari - Februari, 2021)

Jedwali Na. 7 linaonesha upungufu wa jumla kwenye ujuzi kwa wastani wa asilimia 39, ambapo sekta ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ilikuwa na upungufu wa asilimia 63 wa Mafundi Mchundo, ikionesha bado kuna uhitaji mkubwa wa wataalamu wenye ujuzi ili kukukidhi mahitaji ya sekta. Vilevile, Sekta ya Nishati na Madini ilikuwa na upungufu wa asilimia 33, ikionesha kutolingana kwa kiasi kikubwa kati ya usambazaji na mahitaji. Aidha, sekta za utalii na ukarimu, na usafirishaji zilionesha mapungufu ya chini kwa asilimia 18 na asilimia 7.

Utoaji duni wa Elimu ya Ufundi na mafunzo uliosababisha kutokidhi kwa mahitaji ya soko la ajira ulichangiwa na mambo yafuatayo na:

Survey on mapping skills gap and Skills demand survey by Line Manager.

## Tathmini isiyoridhisha kuhusu Mahitaji ya Elimu ya Ufundi Inayokidhi Mahitaji ya Soko la Ajira

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini, Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi havikufanya utafiti wa kutosha wa soko la ajira kuhusu elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ili kuendana na mahitaji ya soko la ajira. Tafiti hizo zingeweza kuonesha eneo ambalo linahitaji uboreshaji ili kuchochea mabadiliko na uvumbuzi katika utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kupitia Mitaala iliyohuishwa.

### Jedwali Na. 8:Tafiti zilizofanywa na vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kuhusu Umuhimu wa Utafiti wa Soko la Ajira

Mwaka wa Fedha	Vyuo vya ufundi	Idadi ya vyuo vilozafanya tafiti	Asilimia ya vyuo vya ufundi vilivyofanya utafiti
2018/19	393	145	37
2019/20	447	148	33
2021/22	451	145	32
2022/23	474	180	38

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kuhusu Tafiti zilizofanywa na Baraza la Elimu ya Ufundi (2023).*

**Jedwali Na. 8** linaonesha kutoka mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2022/23, idadi ya Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi vilizofanya tafiti za kufuatilia umuhimu wa utafiti wa soko la ajira zilikuwa chini ya nusu ya vyuo vya ufundi vilivyopo katika kila mwaka wa fedha, sawa na kati ya asilimia 32 hadi asilimia 38 ya vyuo vya ufundi vya Umma.

Hali hii ilisababishwa na ratiba za kufanya tafiti na kukosekana kwa miongozo kutoka Baraza la Elimu ya Ufundi ya kufanya tafiti za soko la ajira ili kutambua ujuzi unaohitajika.

Kufanyika kwa tathmini isiyojitoshleza ya mahitaji ili kuakisi mahitaji ya soko la ajira kulisababisha matokeo yafuatayo:

#### *(i) Uwapo wa Idadi ndogo ya Mafundi Mchundo Wenye Sifa ili Kukidhi Mahitaji ya Soko la Ajira*

Ukaguzi ulibaini kuwa, kutokana na ukuaji wa sekta ya ujenzi, kulikuwa na mapungufu makubwa ya mafundi mchundo wenye ujuzi yaliyoasababishwa na kuongezeka kwa mahitaji ya mafundi wenye ujuzi ili kukidhi mahitaji ya sekta. Hali halisi iliendana na wazo kwamba teknolojia mpya ilikuwa ikiathiri viwango

vya ujuzi vinavyohitajika mahali pa kazi, ili hali vyuo vya Kiufundi hazikufundisha stadi zote zinazohitajika. **Jedwali Na. 9** linatoa muhtasari wa maelezo ya mahitaji ya soko la ajira kwa mafundi mchundo waliopo hadi mwaka 2021.

**Jedwali Na. 9: Mahitaji ya Soko la Ajira katika Ngazi ya Mafundi Mchundo hadi mwaka 2021**

Sekta	Mahitaji ya Mafundi Mchundo	Idadi ya Mafundi Mchundo waliopo	Asilimia ya Upungufu wa Mafundi Mchundo
TEHAMA	67,936	25,476	63
Nishati na Madini	8,254	5,505	33
Biashara ya kilimo	46,198	35,203	23
Utalii na Ukarimu	6,374	5,214	18
Ujenzi	22,216	18,506	17
Usafiri	6,316	5,867	7
<b>Jumla</b>	<b>157,294</b>	<b>95,771</b>	<b>39</b>

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi katika Jarida la Baraza la Elimu ya Ufundi (Januari - Februari, 2021)*

**Jedwali Na. 9** linaonesha upungufu wa jumla kwenye ujuzi kwa wastani wa asilimia 39, ambapo sekta ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ilikuwa na upungufu wa asilimia 63 wa Mafundi Mchundo, ikionesha bado kuna uhitaji mkubwa wa wataalamu wenye ujuzi ili kukidhi mahitaji ya sekta. Vilevile, Sekta ya Nishati na Madini ilikuwa na upungufu wa asilimia 33, ikionesha kutolingana kwa kiasi kikubwa kati ya usambazaji na mahitaji. Aidha, sekta za utalii na ukarimu, na usafirishaji zilionesha mapungufu ya chini kwa asilimia 18 na asilimia 7.

**(ii) Ukuaji mdogo wa Sekta za Kiuchumi**

Sekta za kiuchumi zinazokuwa kama vile; Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama), Nishati na Madini, na Biashara ya Kilimo zilibainika kuwa na asilimia kubwa ya upungufu wa ujuzi kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 7**. Hali hii ilichangiwa na uwapo wa mipango duni ya maendeleo kwa ajili ya kuhakikisha upatikanaji wa idadi ya kutosha ya Mafundi Mchundo wenye ubora unaohitajika wa kiufundi ili kuongeza tija katika sekta ya uchumi. Hivyo basi, hali hii inaweza kusababisha kuzorota kwa sekta za kiuchumi.

### 5.3.2 Udhhibiti duni wa vyuo vya Ufundi katika kukidhi Ubora na Viwango Vinavyohitajika

Ukaguzi ulibaini changamoto katika usimamizi wa udhibiti wa masharti ya usajili wa vyuo vya Elimu ya Ufundi, kama ilivyobainishwa katika mapungufu yafuatayo:

#### a) Upungufu wa Walimu katika vyuo vya Elimu ya Ufundi

Ukaguzi ulibaini, vyuo vya ufund 41 kati ya vyuo 252 vya Elimu ya Ufundi nchini ziliripoti upungufu wa walimu vyuoni. Aidha, upungufu wa walimu ulithibitishwa pia katika vyuo vya Ufundi vilivyotembelewa, ambapo vyuo vya ufundi 4 kati ya 6 vilibainika kuwa na upungufu wa walimu ikilinganishwa na mahitaji. Vyuo hivyo ni Chuo cha Taifa cha Usafirishaji, Chuo cha Urithi wa Utalii na Mafunzo ya Biashara, Chuo cha Tiba Mwanza, na Vyuo vya Teknolojia na Chuo cha Samail. Aidha, ukaguzi ulibaini idara mbili za Chuo cha Tiba Mwanza, ambazo ni Sayansi ya Madawa na Tiba ya Kliniki, zilikuwa na uwiano wa uhaba wa walimu wanaohitajika kufundisha kwa kila mwanafunzi ikilinganishwa na uwiano unaohitajika ambao ni 1:25.

Hali hii ilisababishwa na upungufu wa kifedha wa kuajiri walimu wa kiufundi ili kukidhi mahitaji ya viwango vinavyohitajika. Matokeo yake, uwiano wa walimu na wanafunzi katika ufundishaji uliathirika na kusababisha idara husika kuwa na uwezekano mdogo wa kupokea ujuzi na msaada wa mtu binafsi, ambapo inaweza kupunguza ubora wa elimu ya ufundi inayotolewa.

#### b) Uwapo wa Vifaa visivyotosheleza na vyenye ubora unaohitajika kwa ajili kujifunzia

Ukaguzi ulibaini uwapo wa upungufu wa vifaa vya kujifunzia ambao unaweza kuathiri ubora wa elimu inayotolewa, kama ilivyowasilishwa katika **Jedwali Na.10**. Ukosefu wa vifaa vya kujifunzia ulisababishwa na utoaji duni wa elimu inayozingatia umahiri na mtaala wa mafunzo ya umahiri.

**Jedwali Na. 10: Upungufu wa Vifaa vya Kujifunzia katika vyuo vya ufundi vilivyotembelewa**

Jina La chuo cha Ufundi	Upungufu wa vifaa vya kujifunzia
Chuo cha Taifa cha Usafirishaji	<ul style="list-style-type: none"> <li>Uhaba wa madarasa, maabara, karakana na maktaba kusaidia mafunzo kwa idadi kubwa ya wanafunzi.</li> </ul>
Chuo cha Urithi wa Utalii na Mafunzo ya Biashara	<ul style="list-style-type: none"> <li>Ukosefu wa maabara ya kompyuta au maktaba.</li> </ul>
Chuo cha Tiba Mwanza	<ul style="list-style-type: none"> <li>Uwapo wa maabara moja ya kompyuta yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 20 tu.</li> </ul>
Chuo cha Uhasibu Tanzania - Mbeya	<ul style="list-style-type: none"> <li>Maktaba ndogo</li> <li>Vyoo chakavu</li> </ul>
Shule ya Uguzi Tawi la Nzega	<ul style="list-style-type: none"> <li>Ukosefu wa ofisi zenye ubora na kamati za uhakikisho wa ubora.</li> </ul>
Samail - Vyuo vya Teknolojia	<ul style="list-style-type: none"> <li>Upatikanaji wa Maktaba mtandao katika eneo la chou tu.</li> </ul>

*Chanzo: Ziara ya wakaguzi na Andiko la Baraza Na. 78.03.03.01 (2021)*

**Jedwali Na. 10**, linaonesha upungufu wa vifaa vya kujifunzia kuliathiri utoaji wa ujuzi katika viwango vinavyohitajika katika vyuo vya Ufundi husika. Aidha, ziara ya ukaguzi ilibaini uwapo wa miundombinu chakavu ya kujifunzia kama inavyooneshwa katika **Picha Na. 1**.

**Picha Na. 1: Hali halisi ya mwonekano wa vifaa vya kujifunzia katika vyuo vilivyotembelewa**



*Chanzo: Ziara ya ukaguzi iliyofanyika tarehe 11 Septemba, 2023*

**Picha Na. 1**, inaonesha uwapo wa vyoo vilivyochakaa na nguzo ya mbao inayoshikilia paa la chumba ili kuzuia kudondoka.

Aidha, ukaguzi umebaini upungufu wa walimu na miundombinu ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi, kama ilivyowasilishwa katika Jedwali Na. 11.

**Jedwali Na. 11: Hali ya vyumba vya Mihadhara na idadi ya Walimu na Wanafunzi**

Vyuo vya Ufundi	Idadi ya Wanafunzi	Idadi ya vyumba vya Mihadhara
Chuo cha Taifa cha Usafirishaji	13,945	54
Chuo cha Urithi wa Utalii na Mafunzo ya Biashara	2	1
Chuo cha Tiba Mwanza	74	7
Chuo cha Uhasibu Tanzania	3188	11
Shule ya Uuguzi ya Nzega	158	4
Vyuo vya Teknolojia vya Samail	27	5

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka Vyuo vya Ufundi vilivyotembelewa, 2023*

**Jedwali Na. 11** linaonesha uwapo wa upungufu wa vyumba vya mihadhara, ambavyo havitoshelezi idadi ya wanafunzi kwa masaa 40 yanayohitajika kwa wiki. Hali hii ilichangiwa na upungufu wa fedha kwa vyuo vya kiufundi kuongeza vyumba vya madarasa ili kuchukua idadi ya wanafunzi kulingana na masaa yanayohitajika kwa wiki. Hata hivyo, chuo vya Teknolojia cha Samail kilikuwa na vyumba vya kutosha vya mihadhara na vifaa vya kutosha vya kujifunzia.

### 5.3.3 Utoaji wa Usajili na ithibati isiyoridhisha kwa vyuo vya Ufundi na Walimu wa Ufundi

Utoaji wa usajili na ithibati usioridhisha kwa vyuo vya ufundi na walimu wa ufundi kama ilivyoielezwa hapa chini:

#### (i) Mchakato wa Usajili usioridhisha wa Vyuo vya Ufundi

Ukaguzi ulibaini baada ya kupokea fomu ya maombi iliyojazwa kutoka kwa vyuo vya ufundi kwa ajili tathmini na maandalizi ya ziara na tathimini, ili kutolewa kwa hali sahihi ya usajili, Baraza la Elimu ya Ufundi halikuweka muda muafaka wa kukamilisha mchakato huo ambao unazuia kufanyika kwa tathimini ya ufanisi wa mchakato wa usajili katika utoaji huduma.

Aidha, Vyuo vya Ufundi vilivyosajiliwa, iliabainika kutofuata taratibu za usajili kama vile uandikishaji wa wanafunzi wasio na sifa, walimu wa kitaaluma na rasilimali za kufundisha zisizojitoshesheza. Kutozingatiwa kwa mchakato wa usajili wa Vyuo vya Ufundi vilihusishwa na mapungufu katika mambo yafuatayo:



### ***Hatari ya kuwapo kwa vigezo visivyo na uhalisia wakati wa ukaguzi wa Ufuatiliaji***

Licha ya kaguzi za ufuatiliaji zilizotekelezwa na Baraza la Elimu ya Ufundi, ukaguzi uligundua kwamba, mkaguliwa alipewa taarifa za ukaguzi mapema, ambapo hali hii inaweza pelekea chuo husika kuweka mazingira mazuri tofauti kwa ajili ya ukaguzi ambapo sio mazingira halisi ya siku zote. Aidha, mapitio ya Ripoti ya Ukaguzi wa Ndani kwenye Idara ya Ufuatiliaji na Tathimini (Andiko la baraza Na. 27.03), yalibaini kuwa Baraza la Elimu ya Ufundi halikuwa na ratiba ya ukaguzi wa kushitukiza ambayo inaweza kuonesha uhalisia wa mazingira ya vyuo ambapo ukaguzi wa kawaida hauwezi kuonesha mapungufu sababu mkaguliwa tayari anakuwa na taarifa hivyo ni rahisi kurekebisha makosa. Baraza la Elimu ya Ufundi wanategemea kupewa taarifa kuhusu uvunjaji wa taratibu kutoka jamii inayozunguka vyuo vya ufundi au kupokea taarifa kupitia kilio cha wananchi ili kufanya ziara za ufuatiliaji wa kushitukiza, ili kubainisha upungufu ambao tayari umetokea kwa vyuo vya ufundi.

### ***Kutokuwapo kwa Mfumo wa Taarifa kwa ajili ya Kufuatilia Hali ya Usajili wa Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi***

Ukaguzi uligundua kuwa Baraza la Elimu ya Ufundi halikuwa na mfumo wa kufuatilia usajili au hali ya kibali kwa Vyuo vya Ufundi zilizosajiliwa. Ilibainika kuwa zoezi hilo bado linafanyika kienyeji ambapo vyuo vya ufundi vilitakiwa kuliarifu Baraza kwa barua kuhusu kuhuisha usajili na vibali.

Pia, kutokana na mapitio ya kanzidata ya usajili na vibali vya Vyuo vya Ufundi kutoka Baraza la Elimu ya Ufundi hadi kufikia Mei 2023 ilionekana kuwa idadi ya Vyuo vya Ufundi vyenye usajili wa muda ziliongezeka kutoka 36 kwa mwaka wa fedha 2019/20 hadi 63 kwa mwaka wa Fedha 2022/23. **Jedwali Na. 12** linaonesha kuongezeka kwa usajili wa muda wa vyuo vya ufundi.

**Jedwali Na. 12: Usajili wa muda wa Vyuo vya Ufundi**

Mwaka wa Fedha	Idadi ya vyuo vilivyovilivyojiandikisha	Idadi ya vyuo vilivyo katika usajili wa muda	Asilimia ya vyuo viliyo katika usajili wa Muda
2019/20	386	36	9
2020/21	421	47	11
2021/22	469	59	13
2022/23	492	63	13

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwa Hifadhi kanzidata ya Baraza la Elimu ya Ufundi, 2023

**Jedwali Na. 12** linaonesha ongezeko la usajili wa muda. Asilimia ya Vyuu vya Ufundi vyenye hadhi ya usajili wa muda ilibaki kuwa sawa kwa asilimia 9 mwaka 2019/20, kisha kuongezeka hadi asilimia 11 mwaka 2020/21, na zaidi hadi asilimia 13 mwaka 2021/22 na 2022/23.

**(ii) Usajili usioridhisha wa Walimu wa Ufundi**

Ukaguzi umebaini kuwa usajili wa walimu ulikuwa kutoka asilimia 67 mwaka 2019/2020 hadi asilimia 56 mwaka 2022/23 kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 13**. Mwelekeo huu wa usajili ulionesha idadi kubwa ya usajili wa walimu, umekuwa na tofauti katika idadi ya jumla na asilimia inayolingana ya walimu wa kiufundi waliosajiliwa katika kipindi cha ukaguzi.

**Jedwali Na. 13: Usajili wa Walimu wa Ufundi nchini**

Mwaka wa Fedha	Jumla ya Walimu wa Ufundi	Walimu wa Ufundi waliosajiliwa	Asilimia ya usajili (%)
2019/20	10,195	6,784	67
2020/21	10,239	6,869	67
2021/22	11,704	6,932	59
2022/23	12,392	6,935	56

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Takwimu za Usajili wa Walimu, 2023

**Jedwali Na. 13** linaonesha muhtasari wa usajili wa walimu wa ufundi kuanzia mwaka wa fedha 2019/2020 hadi 2022/23.

Aidha, ukaguzi ulichambua kiwango cha usajili wa walimu wa kiufundi katika maeneo yaliyotembelewa. **Jedwali Na. 14** linaonesha kiwango cha usajili wa walimu wa kiufundi katika kanda zilizotembelewa na timu ya ukaguzi.

**Jedwali Na. 14: Usajili wa Walimu wa Ufundi katika Kanda Zilizotembelewa**

Kanda zllizo tembelewa	Makadirio ya Idadi ya Walimu wa Ufundi	Idadi ya Walimu wa Ufundi waliosajiliwa	Asilimia ya Walimu waliosajiliwa
Kanda ya Kaskazini	2,071	1,179	57
Kanda ya Mashariki	4,452	2,566	58
Kanda ya Ziwa	1,417	763	54
Kanda ya Kusini	299	139	46
Kanda ya Nyanda za Juu Kusini	1,635	902	55
Kanda ya Magharibi	668	347	52
Kanda ya Kati	1,120	624	56
Ofisi ya Zanzibar	730	416	57

Kanda zilizotebelewa	Makadirio ya Idadi ya Walimu wa Ufundi	Idadi ya Walimu wa Ufundi waliosajiliwa	Asilimia ya Walimu waliosajiliwa
Jumla	12,392	6,935	56

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Takwimu za Usajili wa Walimu, 2023*

**Jedwali Na. 14** linaeleza kuwa usajili wa walimu wa ufundi katika Kanda ya Kusini ulikuwa asilimia 46. Kwa upande mwingine, katika Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Mashariki, Kanda ya Ziwa, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Magharibi, Kanda ya Kati na Zanzibar, usajili wa walimu ulianza asilimia 58 hadi 52. Kwa hiyo, wastani wa asilimia ya walimu walioandikishwa katika Kanda zote nchini ilikuwa asilimia 56.

Zifuatazo ni sababu zilizochangia usajili usioridhisha wa Walimu wa Ufundi:

#### ***Malengo ya usajili wa walimu yalikuwa chini ya mahitaji halisi***

Ukaguzi umebaini hadi kufikia mwaka 2019/20 Baraza la Elimu ya Ufundi ilikuwa tayari imesajili walimu 6,784 wa elimu ya ufundi na idadi ya walimu imeongezeka kutoka 10,195 hadi 12,392 mwaka 2022/23. Ingawa Baraza la Elimu ya Ufundi ilipanga kusajili walimu wa ufundi 6,000 ifikapo Juni 2026 lengo hili lilikuwa nusu ya walimu wa ufundi waliokuwapo ambao walisajiliwa katika miaka ya fedha, kuanzia 2019/20 hadi 2022/23.

#### ***Ukosefu wa malengo ya kila mwaka ya usajili wa walimu wa kiufundi***

Ukaguzi huo ulibaini kupitia mapitio ya Mpango-mkakati wa Baraza la Elimu ya Ufundi wa mwaka 2021/22-2025/26 kuwa Baraza la Elimu ya Ufundi ililenga kusajili Walimu wa Ufundi 6,000 ifikapo Juni 2026. Hata hivyo, baada ya kuangalia mfumo wa matokeo ya mpango huo wa kimkakati, ilibainika kuwa hakukuwa na malengo mahususi wa kila mwaka na viashiria vyake. Bila malengo ya kila mwaka yaliyofafanuliwa, Baraza la Elimu ya Ufundi haliwezi kupima maendeleo ya kila mwaka ya kusajili Walimu wa Ufundi 6,000 ifikapo mwezi Juni 2026.

#### ***(iii) Mchakato wa kutoa Ithibati wa Vyuo vya Ufundi usio na ufanisi***


Kupitia mapitio ya ithibati za vibali za kila mwaka, ukaguzi uligundua kuwa utekelezaji wa ithibati kwa Vyuo vya Ufundi zimekuwa zikishuka kila mwaka. Hivyo, ukaguzi ulibaini mapungufu ya mchakato wa ithibati kwa Vyuo vya Ufundi kama inavyofafanuliwa hapa chini:

#### ***Kuchelewa kwa kuanza kwa Mchakato wa Kuomba Ithibati***

Mapitio ya kanzidata ya Vyuo vya Ufundi imebaini kuwa, pamoja na sharti kwamba Vyuo vya Ufundi vihakikishe vinatimiza masharti baada ya kukamilika kwa usajili kamili, Vyuo vya Ufundi 51 sawa na asilimia 10.8 vilirekodiwa kuwa na ucheleweshaji wa kutoka hatua ya kwanza kwenda hatua ya pili. Kati ya Vyuo vya Ufundi 51, Vyuo vya Ufundi 16 zilikuwa katika kitengo cha Bodi ya Biashara, Utalii na Mipango, 22 zilikuwa katika kitengo cha Bodi ya Sayansi ya Afya na Ushirika, na 13 zilikuwa katika kitengo cha Bodi ya Ufundi za Sayansi na Teknolojia ya Ushirika.

Aidha ukaguzi ulibaini uwapo wa mchakato usioridhisha wa kupata vibali kwa Vyuo vya Ufundi ambao ulisababishwa na kupungua kwa vyuo visivyo idhinshwa mfululizo kwa kipindi chote cha ukaguzi. **Kielelezo Na. 16** inalinganisha idadi ya Vyuo vya Ufundi vilizopata ithibati na visizo na ithibati.

**Kielelezo Na. 16: Ulinganifu Kati ya idadi ya Vyuo vya Ufundi vilivyopata ithibati na zisizo na ithibati**



*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwenye Kanzidata za Vyuo vya Ufundi, 2023.*

Kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 16** kwa mwaka 2019/20, idadi ya vyuo 77 kati ya 350 ya vyuo vya ufundi havikupatiwa ithibati. Katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya vyuo vya ufundi 106 kati ya 421 havikupatiwa ithibati; katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya Vyuo vya Ufundi 128 kati ya 469 havikupatiwa ithibati; na mnamo mwaka wa fedha 2022/23, jumla ya Vyuo vya Ufundi 220 kati ya 272 havikupatiwa ithibati.

Ukaguzi ulibaini, kulikuwa na ongezeko la ukuaji katika Vyuo vya Ufundi vilivyoidhinishwa kutoka 151 kwa mwaka wa fedha 2020/21 hadi kufikia 220 kwa mwaka wa fedha 2022/23. Hata hivyo, kulikuwa na tofauti katika idadi ya Vyuo vya Ufundi visivyokuwa na vibali, na ongezeko kwa mwaka wa fedha 2022/23. Matokeo yake, wahitimu hawawezi kuwa na ushindani katika soko la ajira.

### ***Kutohuishwa kwa Ithibati kwa wakati unaofaa***

Mapitio ya kanzidata ya Baraza la Elimu ya Ufundi (Mei 2023), yamebaini uwapo wa rekodi za usajili na ithibati kwa jumla ya Vyuo vya Ufundi 474, vikiwemo Vyuo vya Ufundi 163 za bodi ya iashara, Utalii na Mipango Vyuo vya Ufundi za Sayansi ya Afya na Ushirika 212, na Vyuo vya Ufundi 99 za Ufundi za Sayansi na Teknolojia ya Ushirika. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini uchelewashaji wa ithibati kwa Vyuo vya Ufundi katika Bodi za Masomo kama inavyoelezwa katika **Jedwali Na. 15**.

**Jedwali Na. 15: Hali ya uhuishaji wa ithibati kwa Vyuo vya Ufundi**

Bodi za masomo	Idadi ya Vyuo vya Ufundi	Mwaka kutoka chuo vya Ufundi kilipopewa usajili kamili mpaka kuidhinishwa
Vyuo za Ufundi za Sayansi na Teknolojia ya Ushirika	3	9 - 11
Vyuo vya Biashara, Utalii na Mipango	2	7 - 9
Vyuo za Ufundi za Sayansi ya Afya na Ushirika	0	-

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwa kanzidata mpaka mwezi Mei 2023*

**Jedwali Na. 15** ukaguzi ulibaini kuwa isipokuwa kwa Vyuo vya Ufundi ambazo vipo chini ya Bodi ya Masomo Vyuo vya Ufundi za Sayansi ya Afya na Ushirika, bodi zilizobaki za masomo Vyuo vya Ufundi na Sayansi na Teknolojia ya Ushirika na Biashara, Utalii na Mipango vilikuwa na Vyuo vya Ufundi vitano, ambavyo vilizidisha miaka mitano kuomba kuhuisha usajili wa ithibati.

Kuchelewa kuhuisha vibali vya Vyuo vya Ufundi kulitokana na kukosekana kwa mfumo wa taarifa kwa ajili ya kufuatilia hali ya usajili na vibali vya Vyuo vya

Ufundi, usimamiaji wa mchakato wa utoaji wa vibali vya Vyuo vya Ufundi na mapungufu katika ufuatiliaji wa Vyuo vya Ufundi.

### 5.3.4 Upungufu katika Kuhuisha na Kuidhinisha Mitaala ili kukidhi Mahitaji ya Soko la Ajira

Ukaguzi ulibaini yafuatayo kuhusu uhuishaji wa mitaala katika Vyuo vya Ufundi za Elimu ya Ufundi na Baraza la Elimu ya Ufundi:

#### ***Matumizi ya Mitaala iliyopitwa na wakati Katika Vyuo vya Ufundi***

Mapitio ya ripoti ya Baraza la Elimu ya Ufundi No. NCP 78.03.03.01 ya 2020/21 yalibaini kuwa Vyuo vya Ufundi 35 kati ya 252 sawa na asilimia 14 ya Vyuo vya Ufundi vilivyotembelewa na wakaguzi vilikuwa vikifanya kazi kwa kutumia mitaala iliyopitwa na wakati. Vivyo hivyo, mapitio ya Baraza la Ufundi Na. NCP 85 kwa mwaka wa fedha 2022/23 ilionyesha kuwa Vyuo vya Ufundi 24 kati ya 105 vilivyotembelewa viliendeshwa kwa kutumia mitaala iliyopitwa na wakati kama ilivyowasilishwa katika Jedwali Na. 16.

**Jedwali Na. 16: Matumizi ya mitaala iliyopitwa na wakati katika Vyuo vya Ufundi Vilivyotembelewa**

Majina ya Vyuo vya Ufundi	Jumla ya idadi ya mitaala	Idadi ya mitaala iliyokwisha muda wake
Chuo cha Taifa ya Usafirishaji	41	7
Chuo cha Urithi wa Utalii na Mafunzo ya Biashara	2	2
Chuo cha Tiba Mwanza	6	3
Chuo cha Uhasibu Tanzania - Tawi la Mbeya	20	0
Shule ya Uuguzi ya Nzega	3	3
Samail Vyuo vya Teknolojia na Viwanda	3	0

**Chanzo:** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Mitaala katika Vyuo vya Ufundi Vilivyotembelewa, 2023

**Jedwali Na. 16** linaonesha Chuo cha Usafiriji kilikuwa na mitaala 7 kati ya 41 iliyoisha muda wake. Hata hivyo, mitaala yote ya Chuo cha Urithi cha Utalii na Mafunzo ya Biashara na Shule ya Uuguzi ya Nzega ilikuwa imeisha muda wake.

Sababu zilizochangia ni Vyuo vya Ufundi kufanya kazi na mitaala uliyopitwa na wakati ni pamoja na; kukosekana kwa barua za ukumbusho zilizotumwa kwa Vyuo vya Ufundi zilizotembelewa, ukosefu wa mfumo maalumu wa kufuatilia

mitaala iliyokwisha muda wake au muda mfupi kabla ya kuisha muda wake, ufuatiliaji usioridhisha na kucheleweshwa kwa uthibitishaji wa mitaala Iliyowasilishwa na Vyuo vya Ufundi.

### 5.3.5 Ufuatiliaji Usioridhisha wa Vyuo vya Ufundi Vilivyosajiliwa ili kuhakikisha Vinatoa Elimu ya Ufundi na Mafunzo Bora

Ukaguzi ulibaini yafuatayo kuhusu utekelezaji wa ufuatiliaji katika Elimu ya Ufundi na Mafunzo:

#### (a) Ufuatiliaji usioridhisha katika kuhakikisha ubora wa elimu na mafunzo ya Ufundi ya kazi yanatolewa

Katika Mapitio ya ripoti za Utendaji wa Mwaka 2019/20 hadi Mwaka 2022/23, Ukaguzi ulibaini kuwa, Baraza la Elimu ya Ufundi halikufanya ufuatiliaji katika Vyuo vya Ufundi na elimu ya ufundi kama ilivyopangwa. Hata hivyo, kulikuwa na kupungua kwa idadi ya Vyuo vya Ufundi vilivyofuatiliwa kwa mwaka wa fedha 2021/22, na Vyuo vya Ufundi 50 tu asilimia 11 vilivyo ufuatiliwa kati ya Vyuo vya Ufundi 465. Katika mwaka wa fedha 2022/23, kulikuwa na ongezeko la shughuli za ufuatiliaji, ambapo Vyuo vya Ufundi 105 kati ya 474 vilifuatiliwa, vikionesha ufuatiliaji wa ufuatiliaji wa asilimia 22. **Jedwali Na. 17** linaonesha kiwango cha ufuatiliaji kwa mwaka mzima.

**Jedwali Na. 17: Asilimia za Ufuatiliaji wa Utekelezaji kwa kipindi cha (2019/20-2022/23)**

Mwaka wa Fedha	Idadi ya Vyuo vya Ufundi	Idadi ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji uliofanywa	Asilimia ya ufuatiliaji (%)
2019/20	407	119	29
2020/21	441	283	64
2021/22	465	50	11
2022/23	474	105	22


**Chanzo:** *Uchambuzi wa Wakaguzi kuhusu Ripoti ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji, 2023*

**Jedwali Na. 17** linaonesha, katika Mwaka wa Fedha 2019 /20, kati ya Vyuo vya Ufundi 407, Vyuo vya Ufundi 119 vilitembelewa katika zoezi la ufuatiliaji sawa na asilimia 29 ya vyuo vilivyotembelea. Pia, kumekuwa na ongezeko la ufuatiliaji kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21 ambapo Vyuo vya Ufundi 283 kati ya 441 vilifuatiliwa na kusababisha kuimarika kwa upatikanaji wa huduma kwa asilimia 64. Pia ilibainika kuwa kiwango cha ufuatiliaji kilitofautiana mwaka hadi mwaka. Asilimia 29 kwa mwaka wa fedha 2019/20, iliongezeka hadi asilimia 64 katika 2020/21, ilipungua hadi asilimia 11 kwa

mwaka wa fedha 2021/22, na kuongezeka hadi asilimia 22 kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Aidha, kwa upande wa Kanda za Baraza la Elimu ya Ufundi ilibainika kuwa idadi ya ziara kila mwaka ya ufuatiliaji ilibadilika na kushuka kwenye Kanda zote. **Kielelezo 17** kinaonesha ziara za ufuatiliaji wa Elimu ya Ufundi katika kanda zote.

**Kielelezo Na. 17: Kiwango cha Ufuatiliaji katika Kanda vilivyotembelewa (2019/20-2022/23)**



*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Ripoti za Ufuatiliaji wa Utekelezaji, 2023*

**Kielelezo Na. 17** kinaonesha muhtasari wa asilimia za ziara za ufuatiliaji kama vilivyofanyika kwa Kanda vilivyotembelewa (2019/20-2022/23). Hii ilisababishwa na uhaba wa fedha vilivyotolewa katika Idara ya ufuatiliaji wa Uboru. Pia, katika mwaka wa fedha 2021/22, Baraza la Elimu ya Ufundi haikupokea fedha, hivyo kusababisha kutembelea kwa Vyuo vya Ufundi vichache. Sababu nyingine ni uhaba wa Watumishi ambapo katika kipindi cha ukaguzi, Baraza la Elimu ya Ufundi lilibainika kuwa na upungufu wa Watumishi



74 kati ya 198 waliopo, kwa mujibu wa muundo mpya wa Baraza la Elimu ya Ufundi, 2023.

**(b) Baraza la Elimu ya Ufundi halijahuisha Miongozo, Kanuni, na Taratibu za kudumisha Viwango vya Ubora**

Ukaguzi ulibaini kuwa Kanuni za Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi zilizotungwa mwaka (2004), zilichelewa kuhuishwa kwa muda wa miaka 17, wakati Usajili wa Kanuni za Vyuo vya Ufundi kwa mwaka 2001, hazikuhuishwa kwa miaka 19. Nyaraka zingine, ikiwa pamoja na uhibitaji ubora na uhakiki wa ubora, tuzo za kitaifa za kiufundi, programu za shahada, mipango ya usimamizi wa ubora, tathmini ya kibinafsi, na tuzo za kigeni, iliyotengenezwa mwaka 2005, haikuhuishwa kwa miaka 18 hadi 19. Aidha, utengenezaji wa mitaala na mapitio, iliyoanzishwa mwezi Juni 2010, haikuhuishwa kwa miaka 13.

Baraza la Elimu ya Ufundi lilitokana na kutopewa kipaumbele kwa shughuli zinazohusu mchakato wa mapitio ya kanuni na miongozo, bila kujali kuwa na mipango ya shughuli hizo. Pia, hakukuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya kupitia upya kanuni na miongozo. Hivyo, inaweza kuathiri utoaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo nchini.

**(c) Uwapo wa Uvunjaji Sheria kwenye Vyuo vya Ufundi**

Katika mapitio ya Taarifa za Ufuatiliaji wa utekelezaji kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2022/23, ukaguzi ulibaini kulikuwa na ukosefu wa mafunzo ya Elimu na Mafunzo ya umahiri kwa Watumishi wengi wa kitaaluma, upungufu wa walimu wenye sifa husika na kutokuwapo kwa mifumo imara ya kuhakikisha ubora wa Vyuo vya Ufundi. Aidha, Vyuo vya Ufundi vilikuwa vinafanya kazi na mitaala iliyoisha muda wake na isiyoidhinishwa. Kukosekana kwa mfumo wa utawala ni miongoni mwa changamoto zilizobainishwa katika Taarifa ya ufuatiliaji iliyofanywa na Baraza la Elimu ya Ufundi **Jedwali Na. 18** linaonesha asilimia ya kiwango cha Vyuo vya Ufundi vilivyoonesha makosa haya.

**Jedwali Na. 18: Makosa yalionekana kwenye Vyuo vya Ufundi**

Makosa yaliojitokeza	Asilimia ya Vyuo vya Ufundi vilivyotembelewa ambavyo vilikutwa na makosa			
	2019/20	2020/21	2021/22	2022/23
Ukosefu / mifumo dhaifu ya uhakika ubora wa Vyuo vya Ufundi	35	77	6	15

Ukosefu wa mafunzo ya umahiri kwa Watumishi wengi wa kitaaluma	83	132	2	60
Upungufu wa Watumishi wa kitaaluma wenye sifa zinazofaa	87	27	2	61
Vyuo vya Ufundi vinazofanya kazi na mitaala iliyokwisha muda wake/isiyoidhinishwa	6	35	2	24
Kukosekana kwa mfumo wa utawala	-	17	-	49

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Ripoti za Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Baraza la Elimu ya Ufundi, 2023*

**Jedwali Na. 18** linaonesha makosa ya kutokuwapo kwa mifumo ya uhakiki wa uhibitaji ubora wa Vyuo vya Ufundi yaliongezeka hadi asilimia 77 mwaka 2020/21, kupungua hadi asilimia 6 mwaka 2021/22, na kisha kuongezeka hadi asilimia 15 mwaka 2022/23. Kwa upande mwingine, ukosefu wa elimu na Mafunzo ya umahiri kwa Watumishi wengi wa kitaaluma ulikuwa juu kwa asilimia 132 mwaka 2020/21, ulipungua hadi asilimia 2 mwaka 2021/22, na kuongezeka hadi asilimia 60 mwaka 2022/23.

Hii ina maana kwamba adhabu/hatua za utekelezaji zinazotolewa na Baraza la Elimu ya Ufundi kwa Vyuo vya Ufundi ni nyepesi na haziwezeshi vyuo vya Ufundi kujirekebisha kama sehemu ya kujifunza.

**(d) Kutofuatwa kwa Taratibu za udahili wa wanafunzi katika Mfumo**

Mapitio ya Ripoti za Ufuatiliaji kwa mwaka 2019/20 hadi 2022/23 yalibaini kuwa makosa yaliyobainika kufanywa mara kwa mara katika ripoti hiyo yalikuwa ni kutozingatia taratibu za udahili wa wanafunzi.

Ukaguzi ulibaini, kuanzia Mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2022/23 moja ya changamoto kubwa ilikuwa kutofuatwa kwa taratibu za udahili wa wanafunzi. Kati ya Vyuo vya Ufundi 119 vilivyotembelewa mwaka 2019, Vyuo vya Ufundi viwili vilikiuka taratibu za udahili. Mwaka 2020/21, jumla ya makosa 1,958 ya kutofuata taratibu za udahili wa wanafunzi yalifanyika katika Vyuo vya Ufundi 252 vya Ufundi, mwaka 2021/22 jumla ya makosa 581 ya kutofuata taratibu za udahili wa wanafunzi yalibainika kwa Vyuo vya Ufundi 105. Katika mwaka 2022/23, kesi 581 za utovu wa nidhamu kutokana na kutofuatwa taratibu za udahili wa wanafunzi zilirudiwa katika Vyuo vya Ufundi 105 vilivyokaguliwa.

### 5.3.6 Shughuli ya Uratibu usioridhisha wa utoaji wa Taarifa za Udhhibiti wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo

Katika kutathimini uratibu katika kuhakikisha usawa kwa sekta zote husika katika utoaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo, ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na masuala yanayozuia utekelezaji wa uratibu kwa usawa kwenye elimu ya ufundi na mafunzo yanayotolewa nchini, kama ilivyoelezwa hapa chini:

#### a) Upungufu wa idadi ya Watumishi kwa ajili ya kusimamia Elimu ya Ufundi na Mafunzo

Ukaguzi ulibaini kuwa Baraza la Elimu ya Ufundi lilikuwa na upungufu wa Watumishi. Kwa mujibu wa mpango wa uanzishwaji wa Baraza la Watumishi, watumishi 198 wanahitajika; Hata hivyo, kuna watumishi 124, wanaowakilisha asilimia 62.6, hivyo, kufanya upungufu wa Watumishi 74 (asilimia 37.4). Aidha, Baraza la Elimu ya Ufundi, katika udhibiti wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo, ilikabiliwa na changamoto ya uhaba wa Watumishi kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 19.

**Jedwali Na. 19: Upungufu wa Watumishi Katika Baraza la Elimu ya Ufundi**

Idara / Kitengo	Idadi ya Watumishi wanaohitajika	Idadi ya Watumishi waliopo	Tofa uti
Mwongozo wa Vyuho vya Ufundi na Msaada	34	35	-1
Maendeleo ya Mtaala na Tathmini	28	19	9
Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji	30	14	16
Uhakiki wa ubora	40	35	5
Utafiti wa Habari na Mipango	15	22	-7
Udahili, Mitihani na Utunuku	29	25	4
<b>Jumla</b>	<b>176</b>	<b>150</b>	<b>26</b>

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwenye Taarifa za Rasilimali watu (Baraza la Elimu ya Ufundi) 2023.*

**Jedwali Na. 19** linaonesha Baraza la Elimu ya Ufundi lina jumla ya Watumishi 150 kati ya 176 wanaohitajika kwa ajili ya udhibiti mzuri wa elimu ya kiufundi.

Upungufu wa Watumishi ulipelekea Baraza la Elimu ya Ufundi kukutana na changamoto mara kwa mara katika kutekeleza shughuli muhimu kama vile

ufuatiliaji wa tathmini, kuendeleza mtaala na tathmini, na shughuli za uhakiki ubora.

**b) Ukosefu wa fedha kwa ajili ya udhibiti wa Vyuo vya Ufundi**

Kupitia mapitio ya Taarifa za Utendaji za Baraza la Elimu ya Ufundi kwa miaka ya fedha 2019/20 hadi 2022/23, ukaguzi ulibaini bajeti iliyotegemea vyanzo vya serikali, haikutolewa kama ilivyopangwa katika miaka mitatu ya fedha (2020/21, 2022/22 na 2022/23) mfululizo, wakati fedha kutoka vyanzo vya ndani vya Baraza la Elimu ya Ufundi lilitolewa kwa asilimia 100 kama ilivyopangwa, kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 20**.

**Jedwali Na. 20: Makadirio na Bjeti halisi iliyo pokelewa na Baraza la Elimu ya Ufundi**

Chanzo cha fedha	Kipengele	Miaka ya Fedha			
		2019/20	2020/21	2021/22	2022/23
Kutoka Serikalini	Bajeti (Sh. bilioni)	2.00	2.00	2.00	2.00
	Fedha zilizopokelewa (Sh. bilioni)	0.73	0	0	0
	Asilimia ya fedha zilizopokelewa (%)	37%	0	0	0
Kutoka vyanzo vya ndani vya Baraza la Elimu ya Ufundi	Bajeti iliyopangwa (Sh. bilioni)	8.66	10.20	9.67	9.26
	Pesa zilizopokelewa (Sh. bilioni)	6.41	7.16	7.51	5.73
	Asilimia ya (%)	73.3	70.2	77.7	61.9

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka chanzo cha Baraza la Elimu ya Ufundi tarehe 31 Machi 2023, na Ripoti ya Utendaji wa Mwaka 2019/2020 hadi 2022/2023.*

**Jedwali Na. 20**, linaonesha fedha kutoka Serikalini hazikutolewa kama ilivyopangwa, kwani katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali ilitoa fedha kwa asilimia 37. Aidha kwa miaka mitatu mfululizo ya fedha kuanzia mwaka 2020/21, 2021/22 na 2022/23, Serikalini haikutoa fedha yoyote.

Kwa hiyo, kutokuwapo kwa fedha za kutosha kunaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa. Katika hali kama hiyo, shughuli zinaweza kutotekelezwa

kwa wakati, na kuifanya Baraza la Elimu ya Ufundi kutofanikisha mipango yake ya kila mwaka.

### 5.3.7 Ufuatiliaji wa usioridhisha wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo

Licha ya Mpango mkakati unaoelezea viashiria sita muhimu vya kufuatilia maendeleo ya elimu ya ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ikiwa pamoja na kuongezeka kwa Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, kuwezesha Vyuo vya Ufundi kupata vifaa vya kisasa, kuanzisha na kutumia miongozo na ramani za ujuzi, uanzishwaji wa mashirikiano kati ya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, kuimarisha uhusiano kati ya Vyuo vya Ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na viwanda, na uwezo wa Watumishi katika kuwajengea umahiri. ukaguzi ulikosa takwimu zilizokusanywa kwenye viashiria kutoka Wizara ya elimu.

Kushindwa huku kulitokana na ukosefu wa mfumo mzuri wa kukusanya taarifa. Mfumo wa Ufuatiliaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ulioandaliwa wenye lengo la kuona upungufu huu uitwao mfumo wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, ulikamilika kwa asilimia 66 mpaka wakati wa ukaguzi huu.

## 5.4 Matokeo ya Ukaguzi wa ufanisi Kuhusu ya Uendelezaji, Ufuatiliaji na Tathmini ya Umahiri wa Watumishi katika Sekta za Umma

### 5.4.1 Mapungufu katika Utambuzi na Uchambuzi wa madhaifu ya umahiri kwa Watumishi katika Taasisi za Umma

Ukaguzi umebaini, katika uhakiki wa mapungufu ya umahiri wa utambuzi na uchambuzi wa kukosekana kwa umahiri kwa watumishi katika taasisi za umma zilizotembelewa uliambatana na udhaifu ulioathiri ufanisi wa mipango ya kujenga umahiri ndani ya taasisi za serikali ili kukabiliana na mapungufu yaliyobainishwa. Yafuatayo ni mapungufu yaliyobainishwa wakati wa ukaguzi:

#### (a) Mapungufu katika mipango ya kutambua mapungufu katika Utambuzi wa Umahiri

Ukaguzi ulibaini, kumekuwa na mapungufu kwenye ujumuishaji wa tathmini ya mahitaji katika nyaraka muhimu za mipango ya taasisi kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 21.

**Jedwali Na. 21: Majumuisho ya Mahitaji ya Shughuli za Ujuzi katika Mipango ya Taasisi**

Aina ya Mipango	Wizara ya Fedha	Wizara ya Maji	Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania	Sekretarieti ya Aira	Mfuko wa hifadhi ya jamii kwa watumishi wa Umma	Mamlaka ya mapato	Mamlaka ya Bandari	Wilaya ya Pangani	Jiji Mwanza	Manispaa Mtwara
Mipango ya kimkakati	✓	×	×	×	×	✓	✓	×	×	✓
Mipango ya Mwaka	×	×	×	✓	×	✓	✓	×	×	×
Mipango mingine	×	×	✓	×	✓	✓	✓	×	×	×

*Chanzo: Uchambuzi wa Mkaguzi kutoka kwa Mkakati, Mwaka na Mipango Mingine 2018-2023*

**Muhimu**

- ✓ Inaonesha uwapo wa mpango
- × Inaashiria kutokuwapo kwa mpango

**Jedwali Na. 21**, linaonesha muhtasari wa taasisi zilizojumuisha tathmini ya mahitaji ya umahiri wa Watumishi katika mfumo wa tathmini ya mahitaji ya mafunzo katika mipango yao ya kimkakati. Kutokuingizwa kwenye mipango ya kujenga umahiri kulisababishwa na ukosefu wa mipango kamili ya kujenga umahiri, ambayo inaongoza lini na namna gani tathmini ya mahitaji ya umahiri itafanyika ili kusaidia mapungufu mengine ya umahiri kutambuliwa mapema.

**(b) Uchambuzi usioridhisha wa Upungufu wa Rasilimali watu**

Ukaguzi ulibaini, Taasisi zote 10 za umma zilizotembelewa hazikuwa na mpango kamili wa rasilimali watu, ambao ulipaswa kuwa mwongozo wa kuongoza uendeshaji wa mafunzo ya kujenga umahiri katika taasisi zao. Taasisi za umma zilizotembelewa zilibainika kuwa na Tathmini ya Mahitaji ya Mafunzo kama mwongozo wa uchambuzi wa kukosekana kwa mafunzo ya umahiri wa watumishi Zaidi ya hayo ilionekana kuwa Tathmini ya Mahitaji ya Mafunzo zilizowasilishwa, zilikosa tathmini ya taarifa muhimu kuhusu mapungufu mbalimbali katika taasisi kama vile mapungufu ya watumishi, mapungufu katika nyanja mbalimbali, na mapungufu ya ujuzi/umahiri kama ilivyowasilishwa katika **Jedwali Na. 22**.

**Jedwali Na. 22: Ujuzi Muhimu Uliojumuishwa katika Tathmini ya Mahitaji ya Umahiri wa Watumishi kwenye Taasisi za Umma**

Aina ya umahiri	Kiwango cha Tathmini (kulingana na Tathmini ya Mahitaji ya Mafunzo ya Mfumo wa Mapitio ya utendaji kazi kwa Watumishi wa Umma <sup>5</sup> kwa asilimia (%))										
	Wizara ya Fedha	Wizara ya Maji	Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania	Sekretarieti ya Aira	Mfuko wa hifadhi ya jamii kwa watumishi wa Umaa	Mamlaka ya mapato Tanzania	Mamlaka ya Bandari	Wilaya ya Pangani	Jiji Mwanza	Manispaa Mtwara	Wastani
Umahiri wa Msingi	5	0	27	25	13	8	1	0	0	0	7.9
Umahiri wa Uongozi	10	0	9	38	13	24	17	0	0	0	11.1
Umahiri umahiriwa kiufundi	85	100	64	37	74	68	82	100	100	100	81

*Chanzo: Tathimini ya uhitaji wa Mafunzo yanayohitajika na Mipango ya mafunzo ya kujengeana uwezo.*

Uchambuzi wa Jedwali Na. 22 linaonesha, kwa ujumla asilimia 81 ya mahitaji yote yaliyowasilishwa na tathmini ya mahitaji ya mafunzo yalikuwa juu ya uwezo wa kiufundi, wakati asilimia 11.1 ilishughulikia uwezo wa viongozi. Asilimia 7.9 ya mahitaji yalikuwa juu ya uwezo wa msingi. Pia ilioneka kwamba tathmini ya mahitaji ya umahiri ilifanyika hasa kwa uwezo wa kiufundi ambao una upungufu kwenye ujuzi mwingine. Sababu ya kutotathmini uwezo wa kiufundi ni uwapo mwongozo usiojitosheleza wa jinsi mahitaji ya umahiri yanavyopaswa kuchambuliwa.

Watumishi hawajui uwezo huo unachambuliwa vipi na iwapo kuna mfumo wowote wa kuchambua umahiri unaohitajika.

#### 5.4.2 Mapungufu katika Maandalizi ya Mipango ya Kukuza Ujuzi

Ukaguzi ulibaini, maendeleo ya mipango ya kujengeana uwezo hayakujitosheleza. Pia, hakukuwapo na ulinganifu kati ya mipango ya

<sup>5</sup> Mfumo wa Mapitio ya utendaji kazi kwa Watumishi wa Umma ilitumika kama zana ya tathmini ya mahitaji na Mfuko wa hifadhi ya jamii kwa watumishi wa umma.

kujengeana uwezo na mapungufu ya ujuzi uliotambuliwa na kutolingana kati ya programu za mafunzo na changamoto za utendaji zilizotambuliwa, kama inavyoelezwa hapa chini:

**(a) Mapungufu katika maaandalizi ya Mipango ya kujenga uwezo**

Ukaguzi ulibaini, taasisi za umma hazikuandaa mipango ya mafunzo ya kutosha kulingana na mahitaji ya Sera ya Mafunzo kwa Utumishi wa Umma Tanzania ya mwaka 2003 ambayo inaakisi mipango ya mafunzo ya mwaka.

Ukaguzi ulibaini kuwa taasisi za umma hazikuandaa mipango ya mafunzo ya kutosha na mipango ya mafunzo ya kila mwaka kulingana na matakwa ya Sera ya Mafunzo kwa Utumishi wa Umma Tanzania, 2003. Katika kipindi cha miaka mitano ni taasisi nne tu kati ya 10 zilizoandaa mipango ya mafunzo ya taasisi wakati taasisi sita zilizobaki hazikufanya hivyo. Aidha, ukaguzi ulitarajia kuwapo kwa mipango 50 ya mafunzo kwa mwaka kwenye Taasisi 10 za umma zilizotembelewa. Hata hivyo, ni mipango 18 tu kati ya 50 ya mafunzo ya kila mwaka ilitengenezwa katika taasisi kumi za umma ambazo zilitembelewa.

Hali hii ilisababishwa na uelewa mdogo kati ya watumishi wanaosimamia shughuli za mafunzo juu ya mahitaji ya kuendeleza mipango ya kujenga uwezo na mipango ya mafunzo ya kila mwaka katika taasisi za umma zilizotembelewa.

**(b) Utengenezaji wa Mipango usiyozingatia Changamoto zilizochambuliwa zinazohusiana na Kujenga Uwezo wa watumishi**

Ukaguzi ulibaini, mipango iliyoandaliwa ya kujenga uwezo haikuandaliwa kwa kuzingatia mapungufu ya umahiri yaliyobainika wakati wa tathmini ya mahitaji na kuchanganua changamoto.

Ilibainika kuwa mipango iliyobuniwa ya kuwajengea uwezo haikugusa kada zote wa Wakaguzi wa Ndani, Wahasibu na Maofisa wa Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi. Pia inaonesha ujumuishwaji usioridhisha wa kada za Rasilimali watu na Maofisa Utawala, Usimamizi wa Kumbukumbu na Maofisa wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

**(c) Kutoshirikishwa kwa wadau kikamilifu katika Uandaaji wa Mipango ya kujenga Uwezo**

Ukaguzi ulibaini, taasisi za umma zimekuwa zikiwashirikisha watumishi kwenye programu za mafunzo ya kuwajenga uwezo kwa mazoea. Uandaaji wa mipango



ulianza kwa kushirikisha watumishi na kukamilishwa na wakuu wa idara na timu zilizoteuliwa ndani ya taasisi. Hata hivyo, makundi mengine ya wadau, ikiwa pamoja na wateja, taasisi za mafunzo na bodi za kitaaluma hawakuhusishwa vya kutosha.

Kutoshirikishwa kwa wadau kulikuwa kwa asilimia 75 kwa taasisi zote isipokuwa Wizara ya Maji, ambayo ilikuwa na asilimia 50. Hii inaonesha kuwa kuna haja ya Taasisi za Umma kuweka uzito kwa kuwahusisha wadau kwenye uandaaji wa programu za kujenga uwezo ili kuwa na mipango madhubuti ambayo itaweza kusaidia kutatua changamoto za mapungufu ya umahiri yaliyobainishwa.

### 5.4.3 Utekelezaji usioridhisha wa Programu za kujenga uwezo ili kuongeza Umahiri wa Watumishi

Ukaguzi ulibaini mapungufu kwenye taasisi zilizotembelewa yaliyohusiana na utekelezaji usioridhisha wa programu za umahiri katika sekta za umma:


#### (a) Miongozo isiyotosheleza kuhusu Utekelezaji wa Programu ya Kujenga Uwezo

Ukaguzi ulibaini taasisi zote 10 zilizotembelewa zilionekana kupendelea kutumia mbinu ya mafunzo ya darasani katika kutekeleza mipango ya kujenga uwezo kuliko miongozo mingine kama vile kufanya kazi kwa mzunguko, vyeti vya kitaaluma kama vile Mhasibu wa umma aliyeidhinishwa, nafasi za kukaimu, mafunzo kwa vitendo, ushauri nasaha, ziara za kimasomo, mabaraza na kushirikishana uzoefu. Aidha, baadhi ya mifano ya utekelezaji wa uwezo haikuwa katika ripoti ya utekelezaji. Uongozi ulipendelea kutumia mbinu ya mafunzo ya darasani kwa sababu ya urahisi katika utekelezaji wake.

#### (b) Programu za Kujengeana Uwezo Zilizotekelezwa Hazikuzingatia Mahitaji ya Uwezo wa Taasisi husika

Ukaguzi ulibaini, kati ya taasisi kumi zilizotembelewa hakuna taasisi hata moja iliyoandaa mfumo wake wa umahiri. Mfumo pekee wa umahiri ulioandaliwa ulikuwa mfumo wa umahiri wa viongozi uliotengenezwa na OR-MUUUB mnamo mwaka 2008. Pia, licha ya kutokuwa na mfumo wa umahiri uliofafanuliwa katika taasisi za umma zilizotembelewa, mipango ya kujenga umahiri katika Taasisi za Umma ilikuwa pungufu kwa baadhi ya mambo machache, kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 18**.

**Kielelezo Na. 18: Mawanda ya Ujuzi wa Umahiri katika Programu Zinazotekelezwa za Kujenga Uwezo miongoni mwa Taasisi za Umma**



*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi (2023)*

**Kielelezo Na. 18** kinaonesha asilimia 71.83 ya juhudi za kujenga uwezo zilizotekelezwa katika Taasisi 10 za umma zilizotembelewa zilizingatia umahiri wa kiufundi<sup>6</sup>; wakati huohuo, asilimia 19.44 zilizingatia umahiri wa uongozi<sup>7</sup>. Asilimia 8.73 iliyobaki ya hatua zote za kujenga uwezo zilizotekelezwa katika taasisi za umma zilizingatia umahiri wa msingi<sup>8</sup>. Hali hii ilisababishwa na uwapo wa Mwongozo wa Umahiri wa Viongozi wa mwaka 2008 ambao umepitwa na wakati na kutumika bila kufanyiwa mapitio kwa zaidi ya miaka 14.

**(c) Utekelezaji usioridha wa Mfumo umahiri wa Uongozi**

Ukaguzi ulibaini, Taasisi 9 kati ya 10 zilizotembelewa hazikutumia Mfumo wa umahiri wa Uongozi kama inavyotakiwa na (OR-MUUUB). Ukaguzi ilitathmini kiwango cha utekelezaji wa Mwongozo kutoka kwa taasisi za umma zilizotembelewa kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 23**.

<sup>6</sup> Umahiri wa Kiufundi: Seti ya maarifa na ujuzi unaohitajika kufanya jukumu maalum, kazi, au utendaji ndani ya tasnia flani

<sup>7</sup> Umahiri wa uongozi: Ni seti ya ujuzi, mitazamo na tabia ambazo zinatumiwa kwa watumishi wenye majukumu ya usimamizi

<sup>8</sup> Umahiri wa msingi: Wao ni seti ya maarifa yanayohusiana, ujuzi, na uwezo ambao husababisha tabia muhimu zinazotarajiwa kutoka kwa wale wanaofanya kazi kwa shirika

**Jedwali Na. 23: Kiwango cha maarifa na utekelezaji wa Mwongozo wa umahiri wa Uongozi katika Utumishi wa Umma**

Jina la Taasisi	Ujuzi wa Mfumo wa umahiri wa viongozi	Matumizi ya Mfumo wa umahiri wa viongozi
Wizara ya Fedha		x
Wizara ya Maji	x	x
Mfuko wa Hifadhi ya jamii kwa watumishi wa Umma	x	x
Chuo cha utumishi wa Umma Tanzania	✓	x
Sekretariaeti ya Ajira	✓	✓
Mamlaka ya Mapato	x	x
Mamlaka ya Bandari	x	x
Mtwara Manispaa	x	x
Wilaya ya Pangani	x	x
Mwanza Jiji	x	x

*Chanzo:* Uchambuzi wa mihtasari ya Mahojiano (2023)

#### Ufunguo

- ✓ Inaashiria uwapo wa kipengele katika safu wima
- x Inaashiria kutokuwapo kwa kipengele katika safu wima

**Jedwali Na. 23** kwa ujumla linaonesha mfumo wa umahiri wa uongozi haukutumika katika Taasisi 9 kati ya 10 zilizotembelewa na Wakaguzi. Hata hivyo, taasisi za umma hazikufahamu kuhusu uwapo wa Mwongozo huo; katika Taasisi 10, ni Taasisi tatu tu waliokuwa na ujuzi wa Mwongozo wa umahiri.

Hali hii ilitokana na kutotekelezwa ipasavyo kwa Mwongozo wa umahiri wa uongozi kwenye ya taasisi zilizotembelewa.

#### (d) Mazingira yasiyoweza Kuimarisha Ujuzi wa Watumishi

Ukaguzi ulibaini, mazingira ya kazi katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mkoani Mtwara, Mkoa wa Mtwara, na Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, mkoani Tanga hayakuwa mazuri ili kutekeleza programu za kujenga uwezo na kuunga mkono juhudi za uimarishaji wa uwezo wa watumishi licha ya kupata mafunzo ya kuwajengea uwezo.

Kwa mfano, kulikuwa na majengo yaliyobomoka, maabara zisizopangwa kwa ajili ya karakana, vifaa vya Tehama na mikutano mubashara. Ilibainika sio Taasisi zote za umma zina mazingira mazuri ya kufanya kazi, bali zipo taasisi ambazo hazina vifaa vya Tehama, mtandao, umeme, maji, kompyuta, nk.

Picha Na. 2: Mazingira ya Ufanyaji Kazi



*Picha 2: Picha zinaonesha mazingira mawili Tofuti ya kazi: Picha ya kwanza upande wa kushoto inaonesha Mazingira mazuri ya kufanya kazi na Picha ya pili upande wa kulia inaonesha Mazingira yasio mazuri ya kufanya kazi. (Picha zilichukuliwa na wakaguzi tarehe 8 Desemba 2023)*

#### 5.4.4 Mapungufu katika Mfumo wa Usimamizi

Ukaguzi ulibaini mfumo wa sasa wa usimamizi wa utendaji kazi wa uongozi umekuwa na udhaifu unaoathiri malengo ya kuanzisha mifumo ya usimamizi wa utendaji kama ilivyofafanuliwa hapa chini.

##### (a) Utendaji wa Mpito usioridhisha kutoka Mfumo wa Mapitio ya utendaji kazi kwa Watumishi wa Umma kwenda Mfumo wa Taarifa ya Usimamizi wa Utendaji wa Watumishi wa Umma

Ukaguzi umebaini kuhama kwa kutoka mfumo wa utendaji kazi kwa Watumishi wa Umma kwenda Mfumo wa Taarifa ya Usimamizi wa Utendaji wa Watumishi wa Umma japokuwa haikupangwa wala kutekeleza vizuri. Mpango wa Mpito usiodhibitiwa ulisababisha mapungufu katika ufuatiliaji wa ufanisi/utendaji kazikatika Taasisi za Umma kama inavyoelezwa katika Jedwali Na. 24 kutoka robo ya pili ya mwaka wa fedha 2022/23.

Jedwali Na. 24: Utendaji kazi wa uongozi katika kipindi cha mpito

Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji	Taasisi za Umma	1 Julai 2022 - 30 Juni 2023	1 Julai 2023 - 30 Oktoba 2023
		Hali	Hali
Mfumo wa Mapitio ya	Wizara ya Fedha	Ulisitishwa isipokuwa kwa Upandishaji wa madaraja	Ulisitishwa

Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji	Taasisi za Umma	1 Julai 2022 - 30 Juni 2023	1 Julai 2023 - 30 Oktoba 2023
		Hali	Hali
utendaji kazi kwa Watumishi wa Umma	Wizara ya Maji	Ulisitishwa isipokuwa kwa Upandishaji wa madaraja	Ulisitishwa
	Mfuko wa Hifadhi ya jamii kwa watumishi wa Umma	Umetumia Mfumo wa Mapitio ya utendaji kazi kwa Watumishi wa Umma Iliyorekebisha	Ulisitishwa
	Chuo cha utumishi wa Umma Tanzania	ulisitishwa isipokuwa kwa Upandishaji wa madaraja	ulisitishwa
	Sekretariaeti ya Ajira	Ulisitishwa isipokuwa kwa Upandishaji wa madaraja	Ulisitishwa
	Mamlaka ya Mapato	Ulisitishwa	Ulisitishwa
	Mamlaka ya Bandari	Hautumiki	ulisitishwa
	Mtwara Manispaa	Ulisitishwa	Ulisitishwa
	Wilaya ya Pangani	Ulisitishwa	Ulisitishwa
	Mwanza Jiji	ulisitishwa	ulisitishwa
Mfumo Wa Taarifa Ya & Mfumo Wa Taarifa Ya Usimamizi Wa Utendaji Wa Watumishi Wa Umma	Wizara ya Fedha	Haipo	Hakuna mafunzo yaliyozinduliwa
	Wizara ya Maji	Haupo	Hakuna mafunzo yaliyozinduliwa
	Mfuko wa Hifadhi ya jamii kwa watumishi wa Umma	HaupoHaipo	Hakuna mafunzo yaliyozinduliwa
	Chuo cha utumishi wa Umma Tanzania	HaupoHaipo	Hakuna mafunzo yaliyozinduliwa
	Sekretariaeti ya Ajira	Haipo	Hakuna mafunzo yaliyozinduliwa
	Mamlaka ya Mapato	Haupo	Hakuna mafunzo yaliyozinduliwa
	Mamlaka ya Bandari	Haupo	Haitumiki <sup>9</sup>
	Mtwara Manispaa	Haupo	Hakuna mafunzo yaliyozinduliwa
	Wilaya ya Pangani	Haupo	Hakuna mafunzo yaliyozinduliwa
	Mwanza Jiji	Haupo	Hakuna mafunzo yaliyozinduliwa

*Chanzo: Uchambuzi muhtasari wa mahojiano kwa taasisi za umma zilizotembelewa (2023)*

<sup>9</sup> TRA inatumia Balanced Score Card (BSC) kama Mfumo wake wa Usimamizi wa Utendaji

**Jedwali Na. 24** linaonesha katika mwaka wa fedha 2022/23, Taasisi nne kati ya kumi zilizotembelewa zilitumia Mfumo wa Mapitio ya utendaji kazi kwa Watumishi wa Umma kwa madhumuni ya kupandishana vyeo lakini sio kama kipimo cha utendaji.

**(b) Utofauti katika Mifumo ya Usimamizi wa Utendaji ndani ya Taasisi za Umma**

Ukaguzi umebaini, kuna mifumo tofauti ya usimamizi wa utendaji katika Taasisi vilivyotembelewa ambavyo hutumiwa kutathmini utendaji wa watumishi wao. Ilibainika matumizi ya makundi makuu manne ya mifumo ya usimamizi wa utendaji serikali, na kila mfumo una hatua zake ambazo zinautofauti wa tathmini za utendaji.

Kutokana na utofauti huo unapelekea utofauti wa mifumo ya usimamizi wa utendaji katika sekta ya umma kupunguza ufanisi wa utendaji wa OR-MUUUB katika kusimamia utendaji wa watumishi katika sekta za umma.

**(c) Muunganisho usio na ufanisi wa Mifumo ya Usimamizi wa Utendaji na Vigezo vingine vya Rasilimali watu**

Ukaguzi ulibaini, mifumo haijaunganishwa na vigezo vingine vya rasilimali watu kati ya mashirika yaliyotembelewa. Tathmini ya utendaji ilifanyika tu kama shughuli nyingine yoyote ndani ya shirika, na matokeo ya tathmini ya utendaji yalitumika kwa njia ndogo sana katika maeneo mengine ya watumishi au masuala ya utawala.

**Jedwali Na. 25: Tathmini ya Ushawishi wa mifumo ya Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji katika Vigezo vingine vya Rasilimali watu**

Kigezo cha Rasilimali watu	Ushawishi	Matokeo
Zawadi za Utendaji	Ushawishi mdogo.	Vigezo vingine viliathiri sana tuzo za utendaji, pamoja na maamuzi yaliyofanywa na usimamizi wa juu wa Taasisi. (Kwa mujibu wa kanuni ya 27(7)(c) ya Kanuni za Utumishi wa Umma)
Programu za Mafunzo	Ushawishi mdogo	Ni Taasisi moja tu kati ya Taasisi tano zilizotembelewa zilikuwa na mfumo wa Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji ambao unaarifu programu za mafunzo. Katika vyombo vingine, programu za mafunzo zilitegemea hasa mahitaji ya mafunzo au fursa za mafunzo zinazopatikana. (Kwa mujibu wa kanuni ya 27(7)(a) ya Kanuni za Utumishi wa Umma)

Kigezo cha Rasilimali watu	Ushawishi	Matokeo
Kupandishwa madaraja	Ushawishi wa wastani	Iliungamanishwa wakatai wa kupandindwa madaraja lakini haikutoa taarifa ya utendaji wa ufanisi wa taasisi husika kwa wakati ndani ya taasisi ya umma. Kupandishwa madaraja kulizingatia muda fulani kwa kila mtu. Watumishi ambao hawakuwa na vigezo hawakustahili kupandishwa madaraja ya utendaji kwa mujibu wa Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji. (Kwa mujibu wa kanuni ya 27(7)(d) ya Kanuni za Utumishi wa Umma)
Vikwazo	Ushawishi mdogo	Hakukuwa na adhabu stahiki kwa watumishi kwa sababu ya utendaji usioridhisha katika Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji. (Kwa mujibu wa kanuni ya 27(7)(e) ya Kanuni za Utumishi wa Umma)
Uhamisho ndani na nje	Ushawishi mdogo	Uhamisho ndani na nje hakuzingatia tathmini ya utendaji kama njia ya kuboresha ufanisi. Uhamisho wa ndani na nje unategemea ushawishi wa mtu binafsi au masuala mengine ya nidhamu yasiyohusiana na Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji ili kuongeza ufanisi au kupunguza ufanisi katika nafasi yoyote. (Kwa mujibu wa kanuniya 106(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma)

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kuhusu muhtasari wa Mahojiano (2023)*

**Jedwali Na. 25** linaonesha jinsi mfumo wa usimamizi wa utendaji unavyoathiri vigezo muhimu vya rasilimali watu vinavyohusishwa na utendaji. Ukaguzi umegundua kuwa Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji ina ushawishi mdogo juu ya masuala muhimu ya usimamizi wa rasilimali watu. Aidha, Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji ilikuwa haijakamilika, isipokuwa kwa watumishi wachache katika nafasi za kitaaluma ambao wangepanya hivyo ikiwa inaweza kusababisha kupanda kwa madaraja. Kuna hatari ya kupata tathmini za utendaji zisizo za kweli au zisizo za haki zinazoweza kuathiri lengo la serikali la kuhakikisha utoaji wa huduma bora kwa umma.


### 5.5 Matokeo ya Ukaguzi katika Usimamizi wa Programu za Urekebu kwa Wafungwa Magerezani

Sehemu hii inatoa muhtasari wa matokeo ya Utekelezaji wa Programu za urekebu kwa Wafungwa, kama inavyooneshwa hapa chini:

### 5.5.1 Ongezeko la kiwango cha Wafungwa wanaorudia makosa kwa wastani wa asilimia 1.5 toka mwaka 2019 hadi 2023

Ukaguzi ulibaini kuwa licha ya programu za urekebu kutekelezwa, bado idadi ya wafungwa waliokuwa wanarudia makosa waliongezeka kwa asilimia 1.5 kutoka mwaka 2019 hadi 2023. (Rejea Kielelezo Na. 19).

**Kielelezo Na. 19: Ongezeko la wafungwa wanaorudia makosa kuanzia mwaka 2019 hadi 2023**




*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa taarifa za wafungwa wanaorudia makosa kutoka Jeshi la Magereza*

Kielelezo hapo juu kinabainisha kuwa, ongezeko la wafungwa wanaorudia makosa kunathibitisha kuwa kuna ongezeko la wafungwa waliotoka gerezeni lakini wanaendelea kurudia kufanya makosa yale yale.

Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa kiwango cha wafungwa waliokuwa wanarudia kufanya makosa yale yale baada ya kuachiwa huru ni wale waliofungwa vifungo vifupi. (Rejea **Kielelezo Na. 20**).



### Kielelezo Na. 20: Asilimia ya Wafungwa waliorudia Makosa yakihusianishwa na muda wao wa Kifungo



**Chanzo:** Uchambuzi wa Wakaguzi katika taarifa za wafungwa wanaorudia makosa kutoka Jeshi la Magereza

**Kielelezo Na. 20** kinaonesha, kuanzia mwaka 2019 hadi 2023, asilimia 59.22 ya wafungwa waliorudia makosa yao walikuwa na kifungo chini ya mwaka 1, asilimia 24.65 walikuwa na kifungo cha miaka 1-3, asilimia 10.1 walikuwa na kifungo cha miaka 3-5, asilimia 3.09 walikuwa na kifungo kati ya miaka 5-10, asilimia 0.37 walikuwa na kifungo cha miaka 10-15, asilimia 2.22 walikuwa na kifungo cha miaka 15-20, asilimia 0.32 walikuwa na kifungo cha miaka 20-30, na asilimia 0.01 walikuwa na kifungo zaidi ya miaka 30.

#### 5.5.2 Kutokuwapo kwa mitaala/miongozo rasmi iliyoandaliwa kwa madhumuni ya kutekeleza programu za urekebu kwa wafungwa

Ukaguzi ulibaini kutokuwapo kwa mtaala rasmi uliobuniwa au ulioandaliwa ili kuongoza utekelezaji wa programu za urekebu kwa wafungwa. Programu zilitekelezwa bila kuwa na miongozo rasmi.

Kwa hivyo, hakukuwa na miongozo ya wazi inayoeleza mpango fulani au muda uliowekwa wa wafungwa kushiriki katika programu za elimu; na kuifanya iwe vigumu kutathmini na kufikia matokeo yaliyokusudiwa ya programu za urekebuka wafungwa.

### 5.5.3 Uainishaji na Utenganishaji wa wafungwa ulijikita katika Kigezo cha jinsia na umri pekee

Lengo la uainishaji wafungwa ni kuhifadhi hadhi ya wafungwa kama binadamu na kubaini kama wana ujuzi maalumu ambao utawezesha kuwapanga wafungwa hao kwenye program za urekebu husika.

Mapitio ya fomu za uandikishaji wa wafungwa kutoka magereza saba yaliyotembelewa, ukaguzi ulibaini uainishaji wa wafungwa ulijikita kwenye jinsia na umri pekee, masuala mengine kama vile asili ya kosa, historia ya uhalifu na umuhimu wa urekebishaji hayakuzingatiwa. Pia, ukaguzi ulibaini wafungwa na mahabusu waliwekwa katika magereza ambayo yalipangwa na kujengwa kwa ajili ya mahabusu pekee.

Hali hii ilisababishwa na:

**(i) Miundombinu isiyotosheleza ya kusaidia uainishaji wa wafungwa**

Kupitia mahojiano na magereza yaliyotembelewa, ukaguzi ulibaini miundombinu mingi ya magereza ilijengwa wakati wa ukoloni. Kwa hiyo, baadhi ya majengo yalibainika kuwa ya zamani na mengine hayafai kutumika. Baada ya uhuru, Jeshi la Magereza lilianzisha falsafa ya urekebu, ambayo ilihitaji uainishaji wa wafungwa. Hata hivyo, miundombinu inayotumika tangu wakati huo ni kutoka enzi za ukoloni, ambayo haiungi mkono falsafa hiyo.

**(ii) Shughuli za msingi za magereza husika zinaamua uainishaji wa wafungwa**

Mapitio ya Fomu za Usajili na Udahili wa Magereza yalionesha kuwa wafungwa walitakiwa kuonesha utaalumu wao na aina ya urekebishaji waliotaka kuambatanishwa nao wakiwa gereza kulingana na ujuzi na uzoefu wao wa kazi. Hata hivyo, kutokana na fomu zilizopitiwa, ilibainika kuwa wafungwa walisajiliwa na kupewa kazi ya msingi iliyofanywa na gereza.

Licha ya uainishaji kuamuliwa na shughuli za msingi za magereza husika, hakukuwa na kuzingatia na kuweka kipaumbele kwa programu zingine wakati wa usajili wa awali wa wafungwa. Ukaguzi ulibaini shughuli nyingine za urekebu (tofauti na kilimo) hazikuweza kuwafikia wafungwa wote kwa sababu ya rasilimali, zana, na vifaa visivyotosheleza. Matokeo yake, sio wafungwa wote waliweza kufaidika na programu hizi.

Ukaguzi ulibaini hali hiyo ilisababishwa na magereza kujikita katika uzalishaji

badala ya kutoa huduma za urekebishaji kwa wafungwa. Hii ilitokana na mahitaji ya magereza kujiendesha yenyewe badala ya kutegemea fedha kutoka serikalini.

**(iii) Kutokuwapo kwa sera na miongozo ya uainishaji wa wafungwa**

Ukaguzi ulibaini hakukuwa na miongozo iliyopangwa kwa ajili ya uainishaji wa wafungwa. Matokeo yake, kulikuwa na tofauti kubwa jinsi mipango ya urekebishaji ilivyotekelezwa katika magereza yote, ambayo ilisababisha kushindwa kutathmini ufanisi wao.

Hii ilisababisha wafungwa kutazama programu kama adhabu na kushindwa kuunganika tena katika jamii, na hatimaye kuongeza kiwango cha wanaorudia kufanya makosa.

**5.5.4 Usambazaji Usiofaa wa Wafungwa katika Magereza Yaliyotembelewa**

Wakaguzi walitembelea magereza na kubaini magereza 6 kati ya 12 yalikuwa na wafungwa zaidi ya uwezo wa magereza hayo kutunza wafungwa. **Jedwali Na. 26** linaonesha uwezo wa magereza, idadi ya wafungwa, na asilimia ya msongamano wa wafungwa katika magereza yaliyotembelewa.

**Jedwali Na. 26: Uwezo wa Gereza na wafungwa waliopo**

Jina la Gereza	Kundi la Gereza	Uwezo wa Gereza	Wafungwa waliopo	Asilimia ya msongamano (wajuu/(chini))
Ruanda	Kuu	400	972	143.0
Mkuza	Wilaya	70	165	135.7
Kongwa	Wilaya	120	158	31.7
Mahenge	Wilaya	50	62	24.0
Ukonga	Wilaya	945	1157	22.4
Idete	Kilimo	200	231	15.5
Magu	Wilaya	134	140	4.5
Karanga	Kuu	841	737	(12.4)
Ubena Zomozi	Kilimo	200	156	(22.0)
Same	Wilaya	160	112	(30.0)
Gereza la wanawake-Morogoro	Kilimo	94	62	(34.0)
Kiberege	Kilimo	450	213	(52.7)
Wami Vijana	Kilimo	255	56	(78.0)

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka magereza yaliyotembelewa, 2023

**Jedwali Na. 26** hapo juu linaonesha msongamano katika magereza kadhaa kama ilivyoonekana wakati wa ukaguzi. Kati ya magereza yaliyotembelewa, gereza la Ruanda lilikuwa limejaa zaidi kwa asilimia 143 wakati gereza la Ubena lilikuwa chini ya asilimia 78. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini baadhi ya magereza kama Ubena zomozi, Gereza la Nyamagana, Kiberege na Wami vijana hayakufikia uwezo wake.

Pia, jedwali linaonesha kuwa magereza ya wilaya yalikuwa yamejaa zaidi ikilinganishwa na magereza ya kilimo ambayo yalitembelewa. Maofisa wa Magereza walieleza kuwa msongamano ulitokana na idadi ndogo ya vyumba vya malazi katika magereza, ambayo ilizuia uainishaji wa kutosha na kutenga wafungwa, ambayo iliathiri zaidi utoaji wa programu za urekebishaji kwa wafungwa.

Aidha, ukaguzi ulibaini Jeshi la Magereza halikuwa na mwongozo wa wazi wa usambazaji wa wafungwa katika magereza mbalimbali nchini.

### 5.5.5 Kukosekana kwa Mfumo Unaoruhusu elimu endelevu kwa wafungwa waliomaliza elimu ya msingi

Ukaguzi ulibaini hakukuwa na mazingira yanayoruhusu wafungwa (ambao ni wanafunzi) waliomaliza elimu ya msingi kuendelea na elimu zaidi katika Gereza la Wami-Vijana. Hali hii inawazuia wafungwa waliohitimu ngazi ya elimu msingi kuendelea na ngazi ya elimu inayofuata.

Hali hii ilitokana na kutokuwapo kwa utaratibu ulioandaliwa kuwaunganisha wafungwa waliohitimu shule ya msingi na taasisi zinazotoa elimu ya sekondari na vyo.

Ilibainika kuwa wafungwa waliomaliza elimu ya msingi bado waliainishwa kama wafungwa na kutakiwa kutumikia vifungo vyao, hivyo hawakuruhusiwa kuendelea na masomo ya sekondari nje ya gereza. Aidha, Gereza la Wami-Vijana halitoi elimu ya sekondari.

Pia, ukaguzi ulibaini Gereza la Wami-Vijana ndilo gereza pekee lililoundwa kutoa elimu rasmi ya msingi kwa wafungwa. Hata hivyo, gereza hilo lilianzishwa ili kuwahifadhi wafungwa wa kiume walio chini ya miaka 21, na hivyo kuwaacha wafungwa wa jinsia ya kike bila kuhudumiwa. Ilibainika zaidi kwamba wafungwa wa kike walikuwa wanafungwa katika magereza mengine yaliyopo ambapo hakuna elimu rasmi ya msingi inayotolewa.

### 5.5.6 Kutofanya kazi kwa Karakana ya Magereza ya Wami-Vijana

Ukaguzi ulibaini Gereza la Wami-Vijana lilikuwa na vifaa vya kutosha kutoa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi. Hata hivyo, kama inavyoonekana katika Picha Na. 3 (a na b) hapa chini, karakana zote hazifanyi kazi.

#### Picha Na.3(a) na (b): Karakana na Uwapo wa Vifaa katika Gereza la Wami-Vijana



Karakana ambazo hazikukamilika zilikuwa hazitumiki, hivyo kuzuia utoaji wa elimu ya ufundi licha ya kuwa na zana na vifaa vya kutosha. Aidha, hakukuwa na umeme wa kuwasha mashine, ambazo zilisababisha hathari kubwa ya kuharibika kwa sababu ya kutotumika kwa muda mrefu.

Kutotolewa ipasavyo kwa elimu rasmi na ya kiufundi kunachangia kuchakaa kwa zana na vifaa vinavyotumika katika utoaji wa elimu ya ufundi kwa wafungwa, na wafungwa kukosa haki yao ya kuijiendeleza kielimu. Hali hii inasababisha kuongezeka kwa kiwango cha kutojua kusoma na kuandika na utekelezaji duni wa mipango ya urekebu, ambayo husababisha wafungwa kushindwa kuunganika tena na jamii na kuongezeka kwa idadi ya wafungwa wanaorudia makosa.

### 5.5.7 Mtaala wa mafunzo ya Maofisa wapya wa magereza haujumuishi ipasavyo Programu za Urekebu

Mapitio ya Mtaala unaotumika kutoa mafunzo kwa Maofisa wa magereza, ulibaini kuwa Mtaala huo haukulenga utoaji wa programu za urekebu. Badala yake, unalenga kutoa maarifa muhimu kwa Maofisa, kama vile gwaride, afya, majukumu ya utawala, mwenendo wa maadili, na usalama gerezani, kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 27**.

#### **Jedwali Na. 27: Maudhui ya Mtaala wa Maofisa Magereza Wanaoanza Kazi**

Moduli	Masuala yaliyojumuishwa
Mafunzo ya Jumla	Katiba, demokrasia, utandawazi, uhalifu wa mtandao, vyombo vya serikali, nk
Uchimbaji	Uchimbaji wa Mkono, kuchimba miguu, mafunzo ya silaha, kujilinda, ufundi wa shamba, nk
Elimu ya Afya	Msaada wa kwanza, ajali, magonjwa, nk
Utawala wa Magereza	Ukaguzi wa magereza, kutoroka kwa wafungwa, usalama wa magereza, uainishaji wa wafungwa, na usafirishaji wa wafungwa
Huduma ya Jamii	Haki za Binadamu na Uhalifu

*Source: Uchambuzi wa wakaguzi wa Mitaala kwa Maofisa Wapya wa Magereza*

**Jedwali Na. 27** linaonesha maudhui ya Mtaala kwa Maofisa wapya wa Magereza. Ukaguzi ulibaini Mtaala uliobuniwa kwa ajili ya Maofisa wapya wa magereza ulijumuisha maudhui mbalimbali tofauti na mafunzo ya urekebu, ambalo ndio lengo kuu la huduma ya magereza. Maudhui hayo ni pamoja na masuala ya kisaikolojia, ushughulikiaji wa mahitaji maalumu na makundi yaliyo hatarini, mawasiliano, na ujuzi binafsi<sup>10</sup>.

Mahojiano na Maofisa Mafunzo wa Magereza yalibaini programu za urekebu wafungwa hazikujumuishwa katika Mtaala wa Maofisa wapya kutokana na ukosefu wa ukaguzi wa Mtaala wa mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa mtaala unajumuisha kazi ya msingi ya huduma za magereza.

Kukosekana kwa masuala ya urekebishaji wafungwa kwenye Mtaala kwa Maofisa wapya kulisababisha hathari ya kuajiri watumishi ambao wanaweza kuwahudumia wafungwa bila kuzingatia haki zao, na hivyo kupunguza uwezekano wa kutekeleza shughuli za urekebu kwa wafungwa kwa ufanisi. Hali hii inaweza kuwakatisha tamaa wafungwa kubadili tabia zao na kufanya marekebisho kutokana na uhalifu wao.


<sup>10</sup> [https://www.unodc.org/documents/centralasia/PrisonReform/training\\_curriculum-en.pdf](https://www.unodc.org/documents/centralasia/PrisonReform/training_curriculum-en.pdf)

### 5.5.8 Maofisa wachache wa Jeshi la Magereza walijiunga kusomea mafunzo ya astashahada na stashahada za Sayansi ya Urekebu katika Chuo cha Mafunzo ya Urekebu Tanzania

Jeshi la Magereza lilifanya jitihada ya kuanzisha Chuo cha Mafunzo ya Urekebu Tanzania mwaka 2015 kilichopo Ukonga, Dar es Salaam, kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa Maofisa wa Magereza, kwa ngazi ya astashahada na stashahada za Sayansi za urekebu.

Pamoja na jitihada zilizofanyika, idadi ya Maofisa Magereza waliopata mafunzo ya sayansi ya urekebu kutoka Chuo cha Mafunzo ya Urekebu Tanzania kwa mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2022/23 ilikuwa ndogo, kama inavyooneshwa katika Kielelezo Na. 21.

**Kielelezo Na. 21: Asilimia ya Maofisa Magereza waliopata mafunzo katika Chuo cha Mafunzo ya Urekebu Tanzania kwa mwaka wa fedha 2018/19 - 2022/23**



**Chanzo:** Uchambuzi wa wakaguzi kutoka kwa taarifa za Maofisa wa Magereza waliojiandikisha katika Chuo cha Mafunzo ya Urekebu Tanzania, 2023

**Kielelezo Na. 21** kinaonesha kuwa kwa kipindi cha miaka mitano, Maofisa wa Magereza waliopata mafunzo ya sayansi ya marekebisho hawakuzidi asilimia 50, isipokuwa kwa mwaka 2023, ambao walifika asilimia 77. Hii ina maana kuwa idadi kubwa ya Maofisa wa magereza hawakupata fursa ya programu za urekebishaji ili kuboresha uelewa na ujuzi wao wa kufanya mipango ya urekebishaji.

Matokeo yake, kulikuwa na idadi ndogo ya Maofisa Magereza waliopata mafunzo kuhusiana na mipango ya urekebishaji. Kwa mfano, katika magereza yaliyotembelewa, idadi ya Maofisa Magereza waliohudhuria elimu ya sayansi ya

urekebu ilikuwa ndogo ikilinganishwa na idadi ya Maofisa wa Magereza waliopo, kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 28.

**Jedwali Na. 28: Maofisa Magereza waliohudhuria mafunzo ya sayansi ya urekebu katika magereza yaliyotembelewa**

Gereza	Kundi la Gereza	Jumla ya Maofisa Waliopo	Maofisa waliohudhuria Mafunzo	Asimilia ya Maofisa waliopata Mafunzo
Mahenge	Wilaya	57	0	0
Ubena	Kilimo	92	0	0
Kongwa	Kilimo	82	0	0
Same	Wilaya	64	0	0
Karanga	Kuu	267	0	0
Kiberege	Kilimo	87	1	1
Gereza Wanawake - Morogoro	Kilimo	53	1	2
Wami-Vijana	Kilimo	87	2	2
Magu	Wilaya	62	1	2
Idete	Kilimo	63	2	3
Mkuza	Wilaya	149	5	3
Tukuyu	Wilaya	55	01	2
Ruanda	Wilaya	239	03	1
Kilosa	Wilaya	58	0	0
Ukonga	Wilaya	459	12	3

*Chanzo: Uchambuzi wa wakaguzi kwa taarifa za zilizokusanywa katika magereza, 2023.*

**Jedwali Na. 28** linaonesha kuwa chini ya asilimia 5 ya Maofisa wa magereza waliotembelea walipatiwa mafunzo ya urekebu kutoka Chuo cha Mafunzo ya Urekebu. Asilimia ya Maofisa Magereza waliopata mafunzo katika programu za urekebu ilikuwa hadi asilimia 3. Aidha, hakuna Afisa yeyote wa Magereza anayefanya kazi katika magereza ya Mahenge, Ubena na Kongwa aliyehudhuria mafunzo kuhusiana na programu ya urekebu.

Zifuatazo ni sababu zilizochangia Maofisa wachache wa Jeshi la Magereza kuhudhuria mafunzo ya urekebu.

- **Gharama za Mafunzo Kugharimiwa binafsi na Afisa husika:** Ilibainika kuwa kozi ya sayansi ya urekebu iliyotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Urekebu ilikuwa muhimu. Hata hivyo, Maofisa Magereza walitakiwa kujigharamia wenyewe. Hali hii ilipunguza idadi ya Maofisa Magereza waliohudhuria mafunzo hayo.
- **Ukosefu wa motisha ya Maofisa wa magereza kujiandikisha katika**



**mpango wa elimu ya urekebu:** Kupitia Mahojiano yaliyofanywa na Maofisa wa Magereza, ukaguzi ulibaini kuwa kukosekana na motisha kwa kuhusiana na mafunzo hayo ilichangia Maofisa kutokuwa na shauku ya kwenda kupata mafunzo hayo. Mtazamo wao ulitokana na imani kwamba maarifa yaliyopatikana wakati wa kozi ya ngazi ya kuingia katika Chuo cha Kiwira na kozi za uendelezaji zilizofuata ziliwapa ujuzi unaofaa ili kutimiza majukumu yao.

#### 5.5.9 Kukosekana kwa mipango rasmi ya kuunganisha wafungwa kwenye Jamii kwa wafungwa waliokaribia kumaliza vifungo vyao

Ukaguzi ulibaini kuwa licha ya ujuzi uliopatikana wakati wa kushiriki kwenye aina mbalimbali za programu za urekebu, hakukuwa na mipango rasmi ya kuandaa wafungwa waliokaribia kumaliza vifungo vyao ili kuunganisha katika jamii na kuondokana na changamoto ambazo wanaweza kukabiliana nazo baada ya kutoka gerezani.

Hali hii imetokana na ukosefu wa mpango wa kuunganisha rasmi wafungwa uliofafanua kwa kina mzunguko wa utoaji wa huduma za urekebu. Hali hii ilimaanisha kuwa hakukuwa na hatua ambazo mfungwa anatakiwa kupitia kuanzia wakati alipoingia gerezani hadi kuachiwa huru.

Matokeo yake, wafungwa walioachiwa hawakuandaliwa vyakutosha kujiunga tena na jamii. Ukosefu wa maandalizi ulipelekea kuwa vigumu kwao kupata huduma na misaada mbalimbali katika jamii. Jambo ambalo lilisababisha kungezeka kwa kiwango cha wafungwa wanaorudia kufanya makosa.

#### 5.5.10 Kukosekana kwa huduma za baada ya Kumaliza kifungo katika kuwezesha kuunganishwa tena katika jamii

Kupitia mahojiano na Maofisa Magereza waliotembelewa, ukaguzi ulibaini uhusiano kati ya wafungwa na Jeshi la Magereza unaishia wakati wafungwa wanapomaliza vifungo vyao. Aidha, walieleza kuwa hakuna huduma inayotolewa kwa wafungwa waliomaliza vifungo vyao ili kuwawezesha kuondokana na changamoto zilizojitokeza wakati wanaporejea katika jamii.

Mapitio ya Muundo wa Wizara ya Mambo ya Ndani yalionesha kuwa Wizara ina Kitengo cha Huduma za Baada ya Kumaliza Kifungo ili kuwezesha huduma ya kuunganisha tena wafungwa katika jamii. Sehemu hiyo ina mipango muhimu ya kushirikiana na jamii ili kuhakikisha utoaji wa huduma na usimamizi. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kitengo hicho kilianzishwa ili kuwezesha huduma za baada ya

kumaliza kifungo, kililenga wafungwa waliohukumiwa chini ya Mpango wa Huduma za Jamii na Programu ya Majaribio na sio kwa wafungwa waliomaliza vifungo vyao.

Ukosefu wa miongozo ya kutekeleza huduma za baada ya kifungo kulisababisha kukosekana kwa huduma za baada ya kifungo kwa wafungwa ambao walimaliza vifungo vyao. Hii ilileta hatari ya kurudia kufanya makosa wakati walipokutana na changamoto kutoka kwenye jamii katika harakati za kupata mahitaji yao ya msingi kama vile malazi na chakula.

#### 5.5.11 Kutokuwapo kwa viashiria muhimu vya kupima utendaji kuhusu programu za urekebu magerezani

Ukaguzi ulibaini Wizara ya Mambo ya Ndani ilikuwa na orodha ya ukaguzi ambayo Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini ilitumia kupima utendaji wa Taasisi zote zinazoripotiwa Wizarani.

Hata hivyo, mapitio ya orodha ya ukaguzi yalibaini orodha hiyo haikujumuisha viashiria ambavyo vitasaidia kupima utendaji wa Jeshi la Magereza katika kusimamia mpango wa urekebu. Kukosekana kwa vipengele vya urekebu katika viashiria muhimu vya kupima utendaji kulichangiwa na sababu kadhaa. Sababu hizi ni pamoja na kutoeleweka kwa malengo na matokeo ya kurugenzi husika, maendeleo hafifu ya utekelezaji wa mfumo madhubuti wa ufuatiliaji na tathmini ya mipango ya urekebu, na kutokuwapo kwa uratibu wa kutosha kati ya Jeshi la Magereza na Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi kuhusiana na mipango ya urekebishaji.

### 5.6 Athari katika kufikia malengo ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Mendeleo Endelevu

Yafuatazo ni maelezo kuhusu athari zilizojitokeza kama ilivyooneshwa hapa chini:

Katika ukaguzi wa udhibiti wa elimu ya Ufundi na mafunzo uligundua udhaifu ulijitokeza wa kutolingana kati ya aina ya waajiri wahitimu katika sekta zote za umma na binafsi kutokana na upungufu wa ujuzi mkubwa wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ili kuendana na soko la ajira. Pia, uhaba wa mafundi Mchundo katika kukidhi mahitaji ya soko la ajira uligundulika kuwapo, na upungufu wa ujuzi wa asilimia 39 katika sekta mbalimbali.

Aidha, ukaguzi ulibaini mapungufu katika kuhuisha na kuidhinisha mitaala ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira. Pia ukaguzi ulibainisha Baraza la Elimu la Ufundi kupitia Taasisi za Ufundi zinatumiya mitaala iliyopitwa na wakati ambayo

inaweza kuathiri wahitimu waliozalishwa kwa kutokidhi mahitaji ya soko la ajira. Sambamba na hilo, pia ukaguzi ulibaini kutofanyika vizuri kwa zoezi la uhalalishaji na uidhinishaji wa mitaala ambayo ni dalili ya elimu ya Ufundi inayotolewa na Baraza la Elimu ya Ufundi haukukidhi viwango vinavyohitajika ambavyo vitamwezesha mhitimu kushindana katika soko la ajira.

Aidha katika ukaguzi wa Maendeleo, Ufuatiliaji na Tathmini ya Uwezo wa Watumishi katika Sekta za Umma, ukaguzi ulibaini udhaifu ambao unaathiri mikakati ya Serikali katika kuboresha umahiri wa watumishi wa umma. OR-MUUUB ilikabiliwa na mapungufu ya utambuzi na uchambuzi wa mapungufu ya umahiri katika taasisi za umma. Ilibainika kuwa ni taasisi nne tu kati ya tisa zilizotembelewa ambazo zimejumuisa tathmini ya mahitaji kama tathmini ya mahitaji ya mafunzo katika Mpango mkakati wao, Wakati Taasisi tano bado hazikuwa zimefanya hivyo.

Pia, ilibainika kuwa mipango duni ya utekelezaji wa mipango ya kujenga uwezo wa kuongeza uwezo wa watumishi ambayo ilibainisha taasisi za umma ambazo hazikutekeleza mipango yote ya kujenga uwezo wakati wengine walitekeleza mipango ya kujenga uwezo kwa zaidi ya asilimia 100. Mwisho ukaguzi ulibaini, Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji kazi usiofaa ambao ni kutokana na mabadiliko yasiyo na ufanisi kutoka Mfumo wa Mapitio ya utendaji kazi kwa Watumishi wa Umma hadi Mfumo wa Taarifa y Usimamizi wa Utendaji wa Watumishi wa Umma. Ukaguzi ulibaini kuwa taasisi zote kumi (10) zilizotembelewa ziligundulika kuwa na mabadiliko kutoka Mfumo wa Mapitio ya utendaji kazi kwa Watumishi wa Umma kwenda Mfumo wa Taarifa ya Usimamizi wa Utendaji wa Watumishi wa Umma hayakupangwa vizuri na kutekelezwa hadi wakati wa ukaguzi. Hatimaye, Lengo la Mpango wa Maendeleo endelevu Na. 8 ambalo lililenga kukuza uchumi endelevu na jumuishi, na kuhakikisha uwapo wa ajira bora.

Aidha, athari za Utekelezaji wa shughuli za urekebu kwa Wafungwa katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu, ukaguzi ulibaini kuwa lengo lililopangwa la kuongeza Magereza yatakayotoa elimu ya mafunzo ya ufundi stadi yalikuwa kwa idadi ndogo ikilinganishwa na idadi ya magereza yanayopatikana nchini matokeo yake kulikuwa na ongezeko kwa wastani wa asilimia 1.5 la wafungwa wanaorudia makosa kutoka mwaka 2019 hadi 2023. Hii itapunguza kufikia lengo la 16 la maendeleo endelevu ya kwa kukuza jamii yenye amani na umoja kwa maendeleo endelevu, kwani matokeo yake kulikuwa na ongezeko la wafungwa wanaorudia kutenda makosa yale yale baada ya kuachiwa huru.



## USIMAMIZI WA MIPANGO MIJI

### 6.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa matokeo ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Mipango ya Miji. Vilevile, inaelezea eneo la ukaguzi, taasisi zilizokaguliwa, uhusiano uliopo wa shughuli za mipango miji na Mpango wa Maendeleo Endelevu na Mpango wa pili na tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, matokeo ya ukaguzi na athari katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa pili na tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

#### 6.1.1 Usuli Kuhusu Usimamizi wa Mipango Miji

Mipango Miji ni utaratibu wa upangaji wa matumizi ya ardhi katika miji ambayo inahusisha kuweka mifumo ya jumla ya matumizi ya ardhi, upangaji wa majengo kulingana na sifa zake, upangaji wa mitaa, mifumo ya usafirishaji na miundombinu mingine ambayo ni muhimu au inahitajika kwa ajili ya kukuza ustawi wa kiuchumi na ustawi wa jumla<sup>11</sup>. Mipango Miji, kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mipango Miji ya mwaka 2007 (4) (1), inalenga kuwezesha usimamizi endelevu, ufanisi na utaratibu wa matumizi ya ardhi. Husaidia kuhakikisha usalama na usawa katika upatikanaji wa rasilimali za ardhi huku ikiwezesha ushiriki wa wananchi katika kuandaa na kutekeleza sera na mipango ya matumizi ya ardhi<sup>12</sup>. Pia inatoa utaratibu wa kujumuisha kanuni husika zilizomo katika sera ya taifa na maendeleo ya kimuundo mara kwa mara kama itakavyofafanuliwa na Serikali<sup>13</sup>.

Nchini Tanzania, ukuaji wa miji kwa kiasi kikubwa sio rasmi na hauna mipango maalumu, kukiwa na sehemu kubwa ya wakazi wanaoishi katika maeneo ambayo hayana huduma za msingi kama vile huduma za maji safi na maji taka, barabara na umeme. Pia, hatari za kimazingira katika makazi ya mijini ni kubwa na athari

<sup>11</sup> Planning: The Town Planners' Perspective; Journal of Geography and Regional Planning, 2019

<sup>12</sup> Urban Planning Act 2007

<sup>13</sup> Town and Country Planning Act, 1956 (Revised 2002)

zinazotokana na mkusanyiko na hali mbaya ya mazingira zimetolewa taarifa kwa kina. Kwa mfano, mafuriko ya mwezi Aprili 2018 yaligharimu maisha ya watu 15 na kuzikosesha makazi familia zaidi ya 2,000 zilizokuwa zikiishi katika bonde la Mto Msimbazi jijini Dar es Salaam<sup>14</sup>.

### 6.1.2 Mipango Miji Ilivyoakisiwa kwenye Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa pili na tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano

#### *Mipango Miji Ilivyoakisiwa na Malengo ya Maendeleo Endelevu*

Mipango Miji inaingiliana sana na Malengo ya Maendeleo Endelevu, hasa Lengo la 11, ambalo linaangazia kuwa na miji na jamii endelevu. Shabaha ya tatu ya Lengo la 11 linalenga kuifanya miji kuwa jumuishi na endelevu, ikisisitiza kuimarisha usimamizi na mipango shirikishi na jumuishi ya upangaji wa makazi ifikapo mwaka 2030. Shabaha hii pia inasisitiza jukumu muhimu la mipango miji katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu. Kusimamia kwa ufanisi shughuli za mipango miji, itachangia kwa kiasi kikubwa kufikia shabaha ya tatu ya lengo la 11 la Malengo ya Maendeleo Endelevu, kuhakikisha kuwa miji na makazi ya watu ni jumuishi, stahimilivu na endelevu.

Zaidi ya hayo, mipango miji inaingiliana na Malengo ya Maendeleo Endelevu mengine, ikionesha athari zake za pande nyingi katika maendeleo endelevu. Kwa mfano, Lengo la tatu linaasisitiza afya na ustawi wa jamii, ambayo mipango miji inaweza kusaidia kwa kuhakikisha upatikanaji wa maji safi, usafi wa mazingira na vituo vya afya, maeneo ya kijani katika miji na hivyo kuboresha afya na ustawi wa wakazi wa mijini kwa ujumla. Zaidi ya hayo, Lengo la 7 linaasisitiza nishati ya bei nafuu na safi, ambapo mipango miji ina jukumu muhimu katika kukuza vyanzo vya nishati mbadala na miundombinu yenye ufanisi wa nishati, na kuchangia kutoa nishati endelevu kwa wakazi wa mijini.

Aidha, Lengo la 9 linaasisitiza juu ya viwanda, ubunifu, na miundombinu, likiangazia umuhimu wa maendeleo ya miundombinu thabiti na endelevu katika ukuaji wa miji. Upangaji miji hurahisisha ukuaji wa viwanda na uvumbuzi shirikishi na endelevu kwa kukuza uendelezaji wa miundombinu thabiti katika miji. Aidha, Lengo la 13 limejikita katika kukabiliana na tabia ya nchi, ambapo mipango miji inaweza kupunguza na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi kwa kuunganisha miundombinu inayostahimili hali ya hewa na mifumo endelevu ya usafirishaji katika mipango ya jiji.

<sup>14</sup> International Bank for Reconstruction and Development, 2019 Tanzania Country Environmental Analysis.

### ***Mipango miji kama ilivyoakisiwa kwenye Mpango wa pili na tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Tano***

Mwelekeo wa kimkakati wa Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2015/16 - 2020/21 ulikuwa ni kuhakikisha kuwa, Tanzania ina makazi yaliyopangwa na yenye huduma zote na yamefuata taratibu za upangaji, ikiwa pamoja na kuboresha usimamizi wa taka, kuwa na matumizi ya usafiri endelevu na nishati safi. Mpango pia unaangazia athari za ongezeko la watu mijini na kwenye makazi.

Mwelekeo wa kimkakati wa Mpango wa tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2021/22 - 2025/26, ni kuhakikisha usalama wa umiliki wa ardhi na kuhamasisha upangaji wa makazi kwa kufuata taratibu zote zinazotakiwa ikiwa pamoja na kuboresha usimamizi wa taka, matumizi ya usafiri endelevu na nishati safi. Hatua muhimu katika sehemu hii ni kukuza na kuwezesha upangaji, upimaji na utoaji wa hatimiliki ya vipande vya ardhi kwa ajili ya uwekezaji na makazi, kuandaa mpango kabambe wa maendeleo ya miji, visiwa na ukanda wa pwani, kuanzisha miradi ya makazi ya bei nafuu, kuboresha mifumo jumuishi ya utoaji taarifa za usimamizi wa ardhi, na kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika upimaji wa ardhi na utoaji wa hatimiliki.

#### **6.1.3 Mikakati na Jitihada za Serikali katika Usimamizi wa Mipango Miji**

Kwa mujibu wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 - 2020/21) Serikali iliweka mikakati ya kuongeza viwanja vilivyomilikishwa kutoka viwanja 952,516 mwaka 2015/16 hadi viwanja 2,952,516 ifikapo mwaka 2020/21. Pia, kwa mujibu wa Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26). Serikali iliweka mikakati ya kuongeza idadi ya Miji yenye mipango kapambe kutoka mipango kapambe 24 mwaka 2019/20 hadi mipango kapambe 54 ifikapo mwaka 2025/26 na kuongeza viwanja vilivyomilikishwa kutoka 1,551,716 mwaka 2019/20 hadi 4,051,716 (ikionesha ongezeko la viwanja 2,500,000) ifikapo mwaka 2025/26.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilipitia Sera yao ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995, Sera ya Taifa ya Makazi y amwaka 2000, Sheria ya Upimaji wa Ardhi ya mwaka 1959 na kuandaa Sera mpya ya Makazi. Vilevile, uendeshaji wa shughuli za sekta ya ardhi kupitia Mfumo jumuishi wa kielektroniki wa Taarifa za Usimamizi wa Ardhi (Integrated Land Management Information System). Aidha, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imefanikiwa kuandaa na kupitisha jumla ya michoro ya mipango miji 8,429 kati ya 8,000 iliyokuwa imepangwa kutekelezwa kutoka mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2022/23 ambayo inaonesha utendaji wa jumla kwa asilimia 105.

## 6.2 Malengo ya Ukaguzi na Mawanda ya Ukaguzi

### 6.2.1 Malengo ya Ukaguzi

Lengo kuu la ukaguzi lilikuwa kutathmini kama Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kupitia Mamlaka za Upangaji, zinasanifu ipasavyo, kuendeleza na kutekeleza mipango ya miji ili kuweka mazingira bora ya kiutendaji na ya kupendeza kwa ajili ya kuishi na kufanya kazi.

Hususan, ukaguzi ulijikita katika kutathmini kama;

- (a) Usanifu na uandaaji wa mipango ya jumla na ya kina ya mipango miji iliandaliwa kikamilifu;
- (b) Skimu za mipango miji zilizosanifiwa na kuidhinishwa zilitekelezwa kwa ufanisi;
- (c) Usimamizi wa utekelezaji wa miradi ya mipango miji iliyoandaliwa ulifanyika kwa ukamilifu; na
- (d) Tathmini ya utendaji wa mamlaka za upangaji juu ya mipango ya miji kama ulifanyika mara kwa mara.

### 6.2.2 Mawanda ya Ukaguzi

Wakaguliwa wakuu walikuwa ni Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ukaguzi huu ulilenga katika usanifu na uendelezaji wa mipango ya jumla na ya kina, utekelezaji mzuri wa ramani za mipango ya miji zilizosanifiwa na kuidhinishwa, usimamizi wa mipango miji iliyoendelezwa, na tathmini ya utendaji wa mamlaka za upangaji. Ukaguzi huu ulihusisha miaka minne ya fedha kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2022/23.

## 6.3 Matokeo ya Ukaguzi juu ya Usimamizi wa Mipango Miji

Sehemu hii inatoa matokeo ya ukaguzi kuhusu usimamizi wa Mipango Miji nchini Tanzania.

### 6.3.1 Usimamizi Usiojitosheleza wa Shughuli za Mipango Mmiji Nchini

Ukaguzi ulibaini kuwa usimamizi wa shughuli za mipango haukujitosheleza kwa sababu ya uwapo wa makazi yasiyopangwa. Hali hii ilitokana na kutokuwapo kwa maandalizi ya kutosha ya mipango kabambe na ya kina ambapo kuanzia mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2022/23, jumla ya mipango 76 ilipaswa kuandaliwa na kuidhinishwa. Ilibainika kuwa jumla ya mipango kabambe 40 ilitengenezwa, na mipango kabambe mitano pekee ndiyo iliyoidhinishwa hadi

kufikia mwaka wa fedha 2022/23, ambayo ni sawa na asilimia 6.58 ya malengo yaliyowekwa.

Ukaguzi huu ulibaini mapungufu makubwa katika usimamizi wa mipango miji, na kusababisha uwapo wa makazi yasiyopangwa katika halmashauri za manispaa, majiji, na miji nchini Tanzania. Licha ya maelekezo ya sera inayotaka upangaji, upimaji, na huduma za ardhi zitolewe kwa wakati lakini hazikutolewa kwa wakati, na kusababisha makazi yasiyopangwa kufikia asilimia 70 ya maeneo yote na ongezeko kubwa la maeneo yasiyopangwa.

Zaidi ya hayo, ukaguzi ulibaini mkoa wa Arusha ulikuwa na asilimia 95 ya ardhi yake yenye makazi yasiyopimwa, hii ilitokana na uwapo walowezi na wakulima katika maeneo yasiyopimwa. Ukosefu wa fedha na miongozo ya utekelezaji uliathiri ufanisi katika upangaji na uendelezaji wa miundombinu, na kuongeza changamoto katika kutekeleza kwa kufuata mpango kabambe na mifumo ya matumizi bora ya ardhi iliyoandaliwa.

Aidha, ukaguzi ulibaini kutofuatwa kwa mipango kabambe, hasa katika wilaya ambazo ni kitovu cha biashara, ambapo kulikuwa na ujenzi wa nyumba za kawaida badala ya ujenzi wa maghorofa wakati wa uendelezaji wa maeneo mapya. Usambazaji usiojitosheleza wa miongozo ya utekelezaji na ushiriki mdogo wa jamii katika mchakato wa kupanga uliongeza changamoto za utekelezaji. Hii inaonesha uhitaji wa haraka kuimarisha uratibu na kujengeana uwezo ili kushughulikia upungufu huu.

### 6.3.2 Usanifu na Uendelezaji wa Mipango Miji Usiojitosheleza

Ukaguzi huu ulibaini yafuatayo.

**(a) Wizara ya Ardhi, Nyumba na maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hawakuhakikisha kuwa Ramani za Mipango Miji zilizoandaliwa Zinakidhi Viwango**

Mapitio ya michoro ya Mipango Miji na michoro ya upimaji kwa miaka ya fedha kuanzia 2019/20 hadi 2022/23 katika mamlaka 5 kati ya 11 zilizochaguliwa za upangaji miji, ukaguzi ulibaini michoro ya mipango miji iliyoandaliwa haikujumuisha vipengele vyote vya mipango miji kama inavyotakiwa. Mambo ambayo yalikosekana ni pamoja na maeneo ya kupumzika, huduma za kijamii, maeneo ya maegesho ya magari, njia za usafirishaji, barabara na njia za watembea kwa miguu. Vipengele hivi vilikosekana kwa sababu skimu za mipango miji mingi huchukua maeneo madogo, kwa sababu michoro mingi ya mipango miji iliandaliwa kutokana na maombi wa wamiliki wa ardhi.

Kwa mujibu wa kiwango cha huduma, ukaguzi ulibaini kuwa, miji iliyoendelea kama Dar es Salaam, Mwanza, Tanga na Dodoma ilikosa njia za reli, barabara na



maeneo kwaajili ya matumizi ya umma katika Miji. Wakaguzi walipotembelea maeneo husika ilibainika kuwa, hakukuwa na barabara maalumu za huduma za usambazaji wa maji na hakukuwa na maeneo ya biashara na viwanda, huduma za elimu, eneo la kujenga majengo marefu na maeneo ya makazi. **Jedwali Na. 29** linaonesha hali ya mapungufu yaliyobainika kutoka katika kila mamlaka ya upangaji iliyotembelewa.

**Jedwali Na. 29: Ukubwa wa Maeneo ya Viwanja Usiyojitosheleza Yaliyotengwa kwaajili ya Huduma za Kijamii katika Michoro ya Mipango ya Miji Iliyoandaliwa**

Jina la Halmasha uri	Jina la Mchoro wa Mipango uliopitiwa na Namba ya Mchoro	Matu mizi ya ardhi	Ukubwa unaohita jika	Ukubwa kulingana na mchoro ulioidhinish wa	Asilimia ya Mapungu fu (%)
Manispaa ya Mtwara	Mjimwema "Mji wa Samia" D2157/117	Hospit ali ya Wilaya	Hekta 5-10	Hekta 2.2522	55
	Mjimwema Layout "Mji wa Samia" 03/MTW/162/082011-A	Soko	Hekta 4	Hekta 0.5844	85
Manispaa ya Kinondoni	Mabwepande DSM/KND/591/072022	Shule ya Msingi	Hekta 1.5-4.5	Hekta 1.057	30
		Kituo cha Petroli	Hekta 0.25-0.4	Hekta 0.2448	2
Manispaa ya Iringa	Mgongo-Nduli 07/IRA/313/112021	Soko	Hekta 4	Hekta 1.52	62
Halmasha uri ya Mji Mafinga	Luganga III 07/MAF/31/042019	Soko	Hekta 4	Hekta 0.75	81
		Eneo la Maduk a	Hekta 3.6	Hekta 3.06	15
Jiji la Dodoma	Ndachi I 08/NDCH/01/102019	Chuo	Hekta 5-10	Hekta 1.3	74
	Ndachi II 08/NDCH/02/102019	Eneo la Maduk a	Hekta 3.6	Hekta 0.8	78

*Chanzo: Uchambuzi wa Michoro ya Mipango miji iliyoidhinishwa kutoka Serikali za Mitaa zilizotembelewa, (2023)*

**Jedwali Na. 29** linaonesha michoro ya Mipango miji iliyoidhinishwa kutoka Serikali za Mitaa tano zilizotembelewa zilitoa maeneo na viwanja ambavyo

havikuzingatia ukubwa wa viwanja kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Mipango miji (Mipango na Viwango vya Nafasi), 2018. Kiwango cha chini kabisa cha upungufu kilibainika katika Manispaa ya Kinondoni, ambapo asilimia ya utofauti ilikuwa asilimia mbili, na ya juu kabisa ilikuwa katika Manispaa ya Mtwara, ambapo asilimia ya tofauti ilikuwa asilimia 85 ya michoro iliyo idhinishwa.

Hii ilitokana na ukosefu wa mapitio wakati wa kuandaa na kuidhinisha michoro ya mipango miji. Hii ilitokana na ukweli kwamba, Mipango ya kina ya michoro ya mipango miji iliandaliwa na kuidhinishwa na taasisi hiyo hiyo iliyoaanda michoro, yaani watumishi wa sekta ya ardhi wanaohusika na maandalizi ya michoro ya mipango ya kina katika Mamlaka ya Upangaji huripoti kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambayo ni Mamlaka ya uidhinishaji.

Hii ilisababisha miundombinu ya Serikali iliyojengwa kushindwa kutoa huduma stahiki kama ilivyopangwa. Kwa mfano, soko lililojengwa kwenye eneo la ukubwa wa hekta 0.5 badala ya eneo la ukubwa wa hekta 4 litakuwa na miundombinu michache ya kutolea huduma zilizokusudiwa. Kwa upande mwingine, chuo kilichojengwa kwenye eneo la ukubwa wa hekta 1.3 ambacho kilitakiwa kujengwa kwenye ukubwa wa hekta 5 hadi 10 hakitaweza kuweka vitu vyote muhimu vinavyohitajika kwa taasisi za elimu ya juu.

#### **(b) Mamlaka za Upangaji Hazikubaini Ipasavyo Maeneo yote kwa Ajili ya Kuingizwa katika Michoro ya Mipango miji**

Ukaguzi ulibaini kuwa, mamlaka za upangaji hazikubaini ipasavyo maeneo ya kuingizwa katika michoro ya mipango ya miji kutokana na kutopata ardhi kabla ya kuanza kwa shughuli za mipango miji. Hii imekuwa kikwazo kwa Mamlaka hizi kutambua maeneo ya upangaji na kuingizwa katika mpango wa upangaji kwani maeneo yaliyoendelezwa yatahitaji fidia kabla ya kuanza utekelezaji. Maeneo yanayotakiwa kuwemo katika mipango miji ni Mpangilio wa matumizi ya ardhi, nafasi za wazi, maeneo kwaajili shule, mifumo ya kisasa ya usafiri, vituo vya kijamii, na maeneo kwa ajili ya kupitisha huduma mbalimbali kama maji.

Mapitio ya michoro ya Mipango ya Kina katika mamlaka 7 za upangaji kati ya 11 zilizotembelewa ilibainika kuwa michoro ya mipango miji yote iliyopitiwa haikubainisha kisawasawa maeneo ya kuingizwa katika Mipango ya Miji. Ilibainika kuwa, Halmashauri moja ya Jiji la Dodoma iliweza kuweka mambo matatu yanayotakiwa ambayo ni mpangilio wa matumizi ya ardhi, eneo kwa ajili ya shule na michezo, na eneo kwa ajili ya mambo ya usafirishaji. Pia halmashauri moja ambayo ni Jiji la Dar es salaam iliweza kuweka vipengele viwili ambavyo ni kuweka mpangilio wa matumizi ya ardhi na maeneo ya wazi. Aidha, halmashauri zingine tano zilizosalia ziliweza kuweka kipengele kimoja tu

ambacho ni mpangilio wa matumizi ya ardhi lakini vipengele vingine kama vile maeneo ya wazi, maeneo ya shule na michezo, maeneo ya usafiri wa kisasa, maeneo ya kijamii, na maeneo kwa ajili ya kupitisha huduma mbalimbali hazikuwekwa kwenye michoro ya mipango miji.

Hii ilisababishwa na hali halisi ya maendeleo katika Mamlaka nyingi za upangaji ilikua mbele kushinda mipango ya serikali iliyopo. Pia, Halmashauri hazikuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya kulipa fidia na kupata ardhi kwa ajili ya upangaji. Ukaguzi ulibaini kuwa, ni Halmashauri tatu tu kati ya kumi na moja zilizotembelewa ambazo zilipanga na kupokea kiasi cha fedha zilizopangwa kwa ajili ya fidia. Halmashauri zilizobakia aidha hazikupanga fidia au zilipanga fidia, lakini hakuna fedha iliyotolewa kwa ajili ya fidia.

Kwa hiyo, wamiliki wa ardhi waliendeleza maeneo yao kulingana na mahitaji yao. Hii ilisababisha uwapo wa makazi yasiyopangwa, ambayo baadaye husababisha kufanyika kwa urasimishaji wa makazi yasiyopangwa ambapo hali hii siyo rafiki kwa maendeleo ya mji.

**(c) Baadhi ya Mamlaka za Upangaji Zilizotembelewa Hazikujumuisha Ipasavyo Maeneo ya Maendeleo ya Baadaye katika Mipango yake ya kina**

Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 11 zilizotembelewa kulikuwa na jumla ya Mipango ya Kina 79 iliyochaguliwa kwa ajili ya ukaguzi. Ambapo asilimia 61.54 tu zilijumuisha maeneo kwaajili ya maendeleo ya baadaye. Asilimia ya kuwa na maeneo ya maendeleo ya baadae ilikuwa kuanzia asilimia 22.58 hadi asilimia 100. Mamlaka tatu za upangaji ambazo ni Manispaa ya Kinondoni, Halmashauri ya Mji wa Mafinga na Manispaa ya Ilemela ziliweza kuingiza maendeleo ya baadaye katika Mipango ya Kina yao, ikifuatiwa na Manispaa ya Mtwara na Halmashauri ya Mji wa Masasi zilihusisha maendeleo ya baadae kwa zaidi ya asilimia 80. Pia mamlaka nne za upangaji ambazo ni Manispaa ya Iringa, Jiji la Mwanza, Jiji la Tanga na Halmshauri ya Mji wa Korogwe zilijumuisha maeneo ya maendeleo ya baadaye kwa asilimia 67. Jiji la Dodoma liliweza kuhusisha maeneo ya maendeleo ya baadae kwa asilimia 22.58 na jiji la Dar es Salaam halikuwa na taarifa za kujumuisha maendeleo ya baadaye kwa kuwa hakukuwa na mpango wa kina wa uendelezaji wa maeneo mapya; badala yake, lilikuwa na mipango ya urasimishaji tu, ambayo haina maeneo ya kuendelezwa baadae.

Hii ni kwasababu maeneo mengi ya upangaji hayakuwa yanamilikiwa na Mamlaka za Upangaji hivyo kuhitaji ulipaji wa fidia kwani maendeleo katika miji husika (Majiji, Halmashauri za Manispaa na Halmashauri za Miji) yalikuwa mbele ya mipango iliyoandaliwa.

Hali hii imesababisha kutokuwa na maeneo ya kutosha yaliyotengwa kwa ajili ya maendeleo muhimu ya baadaye, kama vile hospitali, shule na ofisi za

Serikali, ambayo yanahitaji mamlaka ya upangaji kutumia fedha zaidi kwa ajili ya fidia na kupata maeneo kwa ajili ya maendeleo ya baadae.

**(d) Mamlaka za Upangaji Hazikuhusisha Wadau vya Kutosha Katika Uandaaji na Usanifu wa Mipango miji**

Mapitio ya Muhtasari ya vikao vya mwaka 2023 kuhusu ushirikishwaji wa wadau wakati wa uandaaji wa mipango kabambe kutoka Mamlaka za Upangaji zilizotembelewa yalibaini kuwa, mara nyingi, Mamlaka za Upangaji zilihusisha Taasisi za Serikali pekee katika uandaaji wa ramani za mipango miji. Katika mamlaka za serikali za mitaa 11 zilizotembelewa jumla ya wadau 4,550 kati ya 117,951 waliokusudiwa walishirikishwa katika kipindi cha miaka minne ya ukaguzi ambayo ni sawa na asilimia 37 ya wadau wote waliokusudiwa.

Kwa namna hii, ushirikishwaji usiojitosheleza wa wadau wakati wa upangaji na usanifu unaweza kusababisha ukosefu wa maoni muhimu yanayohusu upangaji wa miji kutoka kwa wadau. Hii ilisababisha gharama kubwa ya kuhamishwa kwa miundombinu mbalimbali ya huduma kama vile miundombinu ya usambazaji maji na mifereji ya maji ya mvua, nguzo za umeme na barabara.

**6.3.3 Skimu za Mipango miji Zilizoandaliwa Hazikutekelezwa Kikamilifu**

Ukaguzi ulibaini kuwa, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mamlaka za Upangaji hazikutekeleza kikamilifu skimu za upangaji kama ilivyoelezwa hapa chini:

**(a) Miji Haikuendelezwa Kulingana na Ramani ya Mipango miji Iliyoidhinishwa**

Mapitio ya Mipango ya jumla, ramani za Mipango miji, na ramani za upimaji na utembeleaaji wa maeneo yaliyopangwa katika Mamlaka za Upangaji, ukaguzi ulibaini kuwa, Miji haikuendelezwa kulingana na mipango ya jumla na ya kina iliyoidhinishwa. Ukaguzi ulibaini kutokuzingatiwa kwa ramani za mipango miji iliyoidhinishwa katika maeneo yafuatayo, kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na. 30**.

**Jedwali Na. 30: Kiwango cha Utekelezaji wa Mpango Kabambe na Mipango ya Miji iliyoidhinishwa katika Mamlaka ya Mipango ya Ziara**

Mkoa	Jina la Halmashauri	Mpangilio wa Matumizi ya Ardhi	Maeneo ya Wazi yaliyovamiwa	Ukosefu wa Ramani ya Muonekane wa Mji	Ukosefu wa Maeneo ya miundombinu kama maji	Ukosefu wa Maeneo ya Michezo	Ukosefu wa mtandao wa barabara za kisasa	Kutozingatia Eneo la Ujenzi wa Majengo
Dodoma	Jiji la Dodoma	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓
Iringa	Manispaa ya Iringa	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓
	Halmashauri ya Mji wa Mafinga	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓
Dar es Salaam	Jiji la Dar es Salaam	✓	✓	✓	✓	✓	✓	x
	Manispaa ya Kinondoni	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓
Mtwara	Manispaa ya Mtwara	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓
	Halmashauri ya Mji wa Masasi	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi katika Mipango Kapambe (Master Plan kutoka Mamlaka ya Serikali za Mitaa zilizotembelewa, (2023)*

**Jedwali Na. 30** linaonesha kwamba, Mamlaka za Serikali za Mitaa zote zilizotembelewa hazikuwa na mpangilio wa matumizi ya ardhi, maeneo ya wazi yalikuwa yamevamiwa, na kutokufuata taratibu za ujenzi wa majengo ya ghorofa. Mambo mengine yaliyokosekana ni ukosefu wa ramani ya muonekano wa mji, ukosefu wa maeneo ya miundombinu kama maji, maeneo ya michezo, na ukosefu wa mtandao wa barabara za kisasa. Ilibainika kuwa, ni Halmashauri ya Jiji la Dar es Salam pekee ndiyo iliyo zingatia mahitaji ya maeneo yenye majengo ya ghorofa. Pia, Ukaguzi ulibaini kutofuata vya kutosha Skimu za

Mipango miji na Viwango vya uendelezaji wa miji kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 31.

**Jedwali Na. 31: Uzingatiaji wa Viwango vya Mipango ya Uendelezaji wa Miji katika Skimu za Mipango**

Jina la Halmashauri	Uzingatiaji wa Vipengele Juu ya Uchunguzi wa Jumla kutoka kwa Mamlaka za Mipango						
	Ukubwa wa viwanja katika Maeneo ya Mji	Uwiano wa kiwanja na umbali wa nyumba toka kwenye mpaka wa kiwanja	Upana wa Barabara na njia ya waenda kwa miguu	Maeneo ya wazi	Maeneo ya Maegesho ya Magari	Maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kupitisha Miundombinu	Ujumuishaji wa maeneo kwa ajili ya reli
Jiji la Dodoma	✓	x	x	x	x	x	x
Manispaa ya Iringa	✓	✓	x	x	x	x	x
Halmashauri ya Mji wa Mafinga	✓	✓	x	x	x	x	x
Jiji la Dar es Salaam	✓	x	x	x	x	x	x
Manispaa ya Kinondoni	✓	x	x	x	x	x	x
Manispaa ya Mtwara	✓	✓	x	x	x	x	x
Halmashauri ya Mji wa Masasi	✓	✓	x	x	x	x	x

**Chanzo:** Uchambuzi wa wakaguzi wa Mipango miji Iliyopitiwa (Mipango na Viwango vya Eneo) Mwaka 2018 ukilinganisha na Utekelezaji Mwaka (2023)

**Jedwali Na. 31** linaonesha kwamba, Mamlaka zote za Upangaji zilizotembelewa zilikidhi takwa la ukubwa wa viwanja katika maeneo ya miji. Mamlaka nne za Upangaji, sawa na asilimia 57, zilizingatia matumizi ya uwiano wa kiwanja na umbali wa nyumba toka kwenye mpaka wa kiwanja. Mamlaka zote za upangaji zilizotembelewa hazikukidhi matakwa ya mipango miji katika upana wa barabara na njia ya waenda kwa miguu, Maeneo ya wazi, Maeneo ya Maegesho ya Magari, Maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kupitisha miundombinu na ujumuishaji wa maeneo kwa ajili ya reli.

Mapungufu ya utendaji yaliyobainishwa yalitokana na usimamizi usiojitosheleza wa sheria za uendelezaji wa miji katika Mamlaka husika za upangaji na ucheleweshaji wa uidhinishaji wa Mipango Kabambe na Mipango ya Kina. Kwa mfano, Mipango Kabambe wa Mamlaka ya Mji wa Mafinga ulitakiwa kuidhinishwa

mwaka 2020; lakini kufikia Januari 2024 ulikuwa haujaidhinishwa. Mapungufu haya yalisababisha uwapo wa ujenzi holela ndani ya Mamlaka za Upangaji.


**(b) Mamlaka za Upangaji Hazikuhakikisha Upatikanaji wa Rasilimali kwa ajili kuwezesha Utekelezaji wa Shughuli za Mipango miji**

Ukaguzi ulibaini kuwa, kulikuwa na changamoto katika utengaji wa rasilimali, kama ilivyofafanuliwa zaidi hapa chini:

**(i) Utengaji wa Rasilimali Fedha Usiyojitosheleza**

Mapitio ya Ripoti za Maendeleo ya Mwaka na taarifa ya bajeti ya mwaka wa fedha kuanzia 2019/20 hadi 2022/23, yanaonesha kuwa, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilipanga rasilimali fedha kutekeleza shughuli za upangaji miji. Hata hivyo, ilibainika kuwa, kiasi cha bajeti kilichopangwa hakikutolewa chote kama inavyooneshwa katika Kielelezo Na. 22.

**Kielelezo Na. 22: Fedha zilizopangwa na zilizopokelewa kwa ajili ya shughuli za mipango miji**



**Chanzo:** Ripoti ya Utendaji wa Mwaka na taarifa za bajeti za Miaka ya Fedha, (2019/2020-2022/2023) kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:

**Kielelezo Na. 22** kinaonesha kuwa, katika miaka yote minne, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi haikupokea fedha kama ilivyopangwa. Pia, fedha zilizotolewa zilikuwa kati ya asilimia 61 hadi asilimia 89 ya bajeti. Aidha,

ilibainika kuwa, utoaji wa fedha uliongezeka kutoka shilingi 47 bilioni mwaka 2019/20 hadi shilingi 153 bilioni mwaka 2022/23.

Pia, utoaji usiojitosheleza wa fedha kulingana na bajeti ulibainika katika Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Fedha zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa mipango miji katika Idara ya Maendeleo ya Vijiji na Miji kwa kipindi cha miaka 3 ya fedha (2019/20 hadi 2021/22), idara ilipokea asilimia 5, 4 na 26 ya fedha zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2019/20, 2020/21 na 2021/22 mtawalia.

Kupitia mapitio ya Bajeti ya Mwaka na taarifa ya bajeti ya Miaka ya Fedha kuanzia mwaka 2019/20 hadi mwaka 2022/23 Mamlaka za Upangaji zilizotembelewa, ukaguzi ulibaini kuwa, asilimia ya fedha ambazo hazijatolewa ilikuwa kuanzia asilimia sifuri hadi asilimia 81.

Mamlaka za upangaji zilizotembelewa, na Ofisi ya Raisi - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilionesha kuwa, utoaji usiojitosheleza wa fedha ulihusishwa na muundo uliopo wa sasa ambao Maofisa wanaoshughulikia masuala ya ardhi, yaani, wapangaji miji, wapima, n.k katika mamlaka za upangaji hawapo chini ya mamlaka za upangaji. Maofisa hawa walikuwa wakiripoti kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Matokeo yake, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi haikutoa kipaumbele cha kutoa fedha kwa sekta ya ardhi katika mamlaka za upangaji.

#### (ii) Upangaji wa Rasilimali watu Usiojitosheleza

Mapitio ya Ripoti ya Mwaka ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa miaka ya fedha kuanzia mwaka 2019/20 hadi mwaka 2022/23 ilionesha kuwa, Wizara haikuwa na rasilimali watu wa kutosha kusimamia utekelezaji wa shughuli za mipango miji. Ripoti hiyo ilionesha kuwa, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021, Makao Makuu ya Wizara, Ofisi za Ardhi za Mikoa na Mamlaka za Upangaji kulikuwa na watumishi 2,139, ambapo idadi iliyotakiwa ilikuwa watumishi 5,234 na kuwa na upungufu wa watumishi 2,895<sup>15</sup> sawa na asilimia 55 ya watumishi wanaohitajika. Aidha, mgawanyo wa watumishi katika mamlaka Upangaji na Ofisi za Ardhi za Mikoa nchi nzima hadi Juni 2023 imeoneshwa katika **Jedwali Na. 32**.

<sup>15</sup> Ripoti ya Maendeleo ya Mwaka ya MLHSD kwa 2020/2021



**Jedwali Na. 32: Idadi ya Watumishi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Ofisi za Ardhi za Mkoa kwa nchi nzima**

Kada	Watumishi Wanaohitajika (a)	Watumishi Waliopo (b)	Upungufu wa Watumishi (c)=a-b	Asilimia ya Upungufu (%) (c/a) * 100
Wapangaji wa Miji	786	175	611	77.7
Wapima Ardhi	1,018	145	873	85.8
Maofisa Ardhi	1,206	605	601	49.8
<b>Jumla</b>	<b>3010</b>	<b>925</b>	<b>2085</b>	<b>69.3</b>

*Chanzo: Uchambuzi wa wakaguzi wa IKAMA ya Watumishi katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mwaka (2023)*

**Jedwali Na. 32** linaonesha kuwa, upungufu wa watumishi unaanzia asilimia 49.8 hadi asilimia 85.8. Kwa upande mwingine, upungufu mdogo ulibainika kwa Maofisa wa ardhi, na upungufu mkubwa ulibainika katika kada ya upimaji wa ardhi, ambayo ilikuwa na upungufu wa asilimia 85.8. Vilevile, upungufu mdogo ulibainika kwa Maofisa wa ardhi waliopungua kwa asilimia 49.8. Kwa ujumla, upungufu wote ni asilimia 69.3.

Ukaguzi pia ulibaini upungufu wa watumishi kutoka Mamlaka za upangaji zilizotembelewa. Upungufu wa watumishi unaanzia asimila 10 hadi asilimia 71, kama ilivyoelezwa katika Jedwali Na. 33.

**Jedwali Na. 33: Upungufu wa Watumishi kutoka Mamlaka za Upangaji zilizotembelewa mwaka 2022/23**

Mkoa	Halmashauri	Watumishi Wanaohitajika	Watumishi Waliopo	Upungufu	Asilimia ya Upungufu
Dodoma	Jiji la Dodoma	93	45	48	52
Iringa	Manispaa ya Iringa	38	16	22	58
	Halmashauri ya Mji wa Mafinga	20	9	11	55
Dar es Salaam	Jiji la Dar es Salaam	75	31	44	59
	Manispaa ya Kinondoni	58	22	36	62
Mtwara	Manispaa ya Mtwara MC1	24	8	16	67
	Halmashauri ya Mji wa Masasi	16	7	9	56

Mkoa	Halmashauri	Watumishi Wanaohitajika	Watumishi Waliopo	Upungufu	Asilimia ya Upungufu
Mwanza	Manispaa ya Ilemela	20	18	2	10
	Jiji la Mwanza	48	27	21	44
Tanga	Jiji la Tanga	48	14	34	71
	Halmashauri ya Mji wa Korogwe	20	9	11	55

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa IKAMA ya Watumishi kutoka Mamlaka za Upangaji zilizotembelea Mwaka (2023)*


**Jedwali Na. 33** linaonesha kuwa, upungufu wa watumishi ulianza asilimia 10 hadi 71, ambapo jiji la Tanga lilikuwa na mahitaji makubwa ya watumishi kwa asilimia 71. Upungufu huu ulisababisha mzigo mkubwa wa kazi kwa watumishi katika mamlaka za upangaji. Pia, ilisababisha utendaji usiojitosheleza katika usimamizi wa shughuli za mipango miji.

Matokeo yake, kulikuwa na udhibiti usiojitoleza wa uendelezaji wa miji. Upungufu wa watumishi wanaohusika na shughuli za mipango miji katika maeneo yaliyotembelewa ulisababisha ukosefu wa udhibiti wa uendelezaji wa miji. Hii ilithibitishwa na ukosefu wa wasimamizi wa ardhi katika ngazi ya chini ili kuhakikisha kuwa, ujenzi unaoendelea wa uendelezaji wa miji unafuatiliwa kwa ukaribu. Wasimamizi wa ardhi kwa ngazi za chini wangeweza kuchunguza na kufuatilia kwa karibu uendelezaji wa ardhi unaoendelea.

### (iii) Vipande vya Ardhi Vilivyopangwa Havikupimwa kwa Wakati

Ukaguzi ulibaini kuwa, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kupitia Ofisi za Ardhi za Mikoa na Serikali za Mitaa, haikupima viwanja vilivyopangwa kwa wakati. Mapitio ya Ripoti ya Mwaka ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ya Mwaka wa Fedha 2019/20 mpaka 2022/23, ilionesha viwanja vilivyopangwa kupimwa havikupimwa katika mwaka husika wa kifedha, kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 23**.

### Kielelezo Na. 23: Kiwango cha Upimaji wa Viwanja dhidi ya Malengo Yaliyowekwa



Chanzo: Ripoti za Utendaji wa Mwaka wa Fedha, (2019/20-2022/23)


**Kielelezo Na. 23** kinaonesha kuwa, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilifikia malengo yake kwa kupima viwanja kwa wakati uliopangwa katika miaka ya fedha 2019/20 na 2020/21. Asilimia ya viwanja vilivyopimwa kwa wakati ilikuwa asilimia 120 na asilimia 116 katika miaka ya fedha 2019/20 na 2020/21, mtawalia. Hata hivyo, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi haikufikia malengo yake yaliyojiwekea ya kupima viwanja kwa wakati kwani iliweza kupimwa kwa asilimia 94 na asilimia 63 katika miaka ya fedha 2021/22 na 2022/23, mtawalia. Hii ina maana kwamba, viwanja 24,166 havikupimwa katika mwaka wa fedha 2021/22, wakati viwanja 185,023 havikupimwa katika mwaka fedha 2022/23.

Hali hii ilisababisha utoaji usioridhisha wa hatimiliki ambapo kwa miaka ya fedha minne iliyopita, kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2022/23, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi haikuweza kutoa hatimiliki kwa asilimia 100 ya malengo iliyojipangia. Kwa wastani, utoaji wa hatimiliki ulikuwa asilimia 22.5. kwa kila mwaka, hatimiliki zilizotolewa zilikuwa asilimia 20 (sawa na hati 39,626) katika mwaka wa fedha 2019/20, asilimia 38 (sawa na hati 75,171) katika mwaka wa fedha 2020/21, wakati katika mwaka wa fedha 2021/22 ilikuwa asilimia 15 (sawa na hati 72,982) na asilimia 17 (sawa na hati 85,512) katika mwaka wa fedha 2022/23.

Utoaji usiojitosheleza wa hatimiliki ulichangiwa na kutokuwa na uwezo wa kupima viwanja kwa wakati, pia ulichangiwa na ufahamu mdogo wa wamiliki wa viwanja juu ya upatikaji wa hatimiliki na ukosefu wa mfumo mzuri utakao

weza kuharakisha mchakato wa utoaji hati. Matokeo yake, kulikuwa na ukusanyaji mdogo wa mapato kutoka vyanzo vya ardhi kama katika Kielelezo Na. 24.

**Kielelezo Na. 24: Mapato Yaliyokusanywa kutoka Vyanzo vya Ardhi**



**Chanzo:** Ripoti za Utendaji wa Mwaka wa Fedha, (2019/20 - 2022/23)

**Kielelezo Na. 24** kinaonesha ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vya ardhi ulikuwa kati ya asilimia 58 na asilimia 61, ambayo ni ya chini ikilinganishwa na na taarifa ya utendaji. Hii ilihusishwa na upimaji wa viwanja vilivyopangwa usiyojitosheleza.

**(iv) Mfumo wa Kieletronik Unaojiendesha wa Shughuli za Mipango Miji Usiyojitosheleza**

Ukaguzi ulibaini kuwa, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeweza kusanikisha (install) Mfumo Jumuishi wa Usimamizi na utoaji taarifa za Ardhi katika mikoa 2 kati ya 6 hadi kufikia mwezi Juni 2023. Mikoa hiyo ni Dodoma na Dar es Salaam sawa na asilimia 3.3 ya lengo lililokusudiwa. Hii ina maana kwamba, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilifanya kazi chini ya kiwango kwa asilimia 96.67% dhidi ya lengo la kuhakikisha mfumo unafanya kazi katika mikoa 6 mpaka mwezi Juni 2023.

Aidha, mapitio ya taarifa fupi ya Mkutano wa Watumishi wa Sekta ya Ardhi wa Mkoa wa Dar Es Salaam uliofanyika tarehe 03 Juni 2023 ulibainisha changamoto nyingine za mfumo. Changamoto hizo zilikuwa ujuzi mdogo katika utumiaji wa Mfumo unaopelekea taarifa kujirudiarudia katika mfumo, na ilionekana mfumo una uwezo mdogo wa kuhifadhi taarifa na hauwezi kupata taarifa zote

zinazohitajika. Kutokana na hili taarifa ya michoro ya upimaji na mipango ya miji haikuweza kubadilishwa na kuwekwa kwenye mfumo kwa kuwa ilikuwa na ukubwa na muundo unaokinzana na mfumo.

Hali hii imechangia kutofikiwa kwa lengo la kutekeleza mfumo uliolenga kurahisisha shughuli za mipango miji.

#### 6.3.4 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa, Hawakusimamia vya Kutosha Kutekeleza Skimu za Mipango Miji na Mipango Kabambe

Ukaguzi ulibaini kuwa, Mamlaka za Upangaji hazikuwa na mifumo madhubuti ya kudhibiti uendelezaji wa miji kwa sababu hakukuwa na taarifa yoyote juu ya Mwongozo wa mpangilio wa matumizi ya ardhi, kuhakikisha ushiriki wa wananchi katika masuala yanayohusiana na ardhi na matumizi ya walinzi wa Ardhi kwaajili ya kufanya doria wakati wa ujenzi. Katika mamlaka za upangaji 6 kati ya 11 ya mamlaka zilizotembelewa hutumia utoaji wa vibali vya ujenzi kama nyenzo ya kudhibiti uendelezaji wa miji.

Usimamizi usiojitosheleza wa udhibiti wa endelezaji ulisababisha waendelezaji kufanya uendelezaji bila kupata idhini kutoka kwa mamlaka ya upangaji. Aidha, kutokuwa na uwezo wa kutekeleza ipasavyo taratibu za uendelezaji wa miji kulisababisha changamoto, ikiwa pamoja na kujenga kwenye nafasi za wazi, kujenga bila mpangilio na uendelezaji kuendelea kufanyika kwenye maeneo ambayo hayajapimwa.

#### 6.3.5 Tathmini Isiyojitosheleza ya Utendaji ya Mamlaka za Upangaji katika Shughuli za Mipango Miji

Ukaguzi ulibaini tathmini ya utendaji kazi isiyojitosheleza ya Mamlaka za upangaji katika shughuli za upangaji miji kama ilivyofafanuliwa hapa chini.

##### (a) Ufuatiliaji usijitosheleza wa Utendaji wa Mamlaka za Upangaji

Kupitia Ripoti za Utendaji ya mwaka ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kutoka mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2022/23 ukaguzi ulibaini kuwa, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilitakiwa kutembelea na kutathmini utendaji wa Halmashauri kila robo mwaka. Hata hivyo, Wizara haikufuatilia utendaji wa Halmashauri kama inavyotakiwa, kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 34**.

**Jedwali Na. 34: Ufuatiliaji wa Shughuli za Mipango Miji katika Mamlaka za Upangaji**

Mwaka wa Fedha	Shughuli ya kufuatiliwa	Idadi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Zinzapaswa Kufuatiliwa	Idadi Halisi Mamlaka za Serikali za Mitaa Zilizofuatiliwa	Asilimia ya Ufuatiliaji
2019/20	Udhibiti wa Viwango vya Uendelezaji Miji	111	45	41
2020/21	Upangaji, Upimaji na Utoaji wa hati	Hakuna Takwimu	22	-
2021/22	Upangaji, Upimaji na Utoaji wa hati	Hakuna Takwimu	61	-
	Shughuli za jumla	184	46	25
2022/23	Uandaaji na utekelezaji wa mipango kina	184	98	53
	Uandaaji na Utekelezaji wa Mipango ya Urasimishaji	184	162	88
	Udhibiti wa Viwango vya Uendelezaji Miji	30	46	153

*Chanzo: Uchambuzi wa wakaguzi kutoka Ripoti za Utendaji wa Mwaka wa Fedha wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, (2019/20) na (2022/23)*

**Jedwali Na. 34** linaonesha kwamba, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi haikuweza kufuatilia Mamlaka zote za upangaji kama ilivyopanga. Hata hivyo, Wizara ilizidi lengo la ufuatiliaji wa Udhibiti wa Viwango vya Uendelezaji Miji kwa asilimia 153 katika mwaka wa fedha 2022/23. Kufanya zaidi ya lengo kulitokana na utekelezaji wa mpango mpya wa kupanga, kupima na kukamilikisha kuliko hitaji ufuatiliaji wa karibu. Kiwango cha ufuatiliaji wa shughuli zingine zilizopangwa kutekelezwa kilianzia asilimia 25 hadi asilimia 88.04.

Kwa mwendelezo huohuo, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa haikufuatilia na kutathmini utendaji wa Serikali za Mitaa juu ya shughuli za mipango miji. Hii ilitokana na kwamba, shughuli za upangaji wa miji zinatekelezwa na watumishi wa sekta ya ardhi waliopo halmashauri na taarifa zote za utekelezaji zinawasilishwa kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Hii ilitokana na mabadiliko ya muundo wa utawala wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Muundo huo umeondoa watumishi wote wa sekta ya Ardhi waliopo halmashauri na kuwapeleka wizara ya Ardhi.

Hali hii ilisababishwa na matumizi hafifu ya fedha na upungufu wa rasilimali watu ili kuwezesha ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za mipango miji katika Mamlaka za Upangaji. Matumizi ya bajeti iliyotolewa kwaajili ya ufuatiliaji kwa miaka yote minne ya ukaguzi yalikuwa kati ya asilimia 83.76 hadi asilimia 102.42. Rasilimali watu kwaajili ya ufuatiliaji na tathmini ilikuwa chini ya asilimia 55 ya mahitaji.

**(b) Ufuatiliaji Usiojitosheleza wa Utekelezaji wa Mambo Yaliyobainishwa Wakati wa Utekelezaji wa Shughuli za Ufuatiliaji na Tathmini kwenye Mamlaka za Upangaji**

Ukaguzi huu ulibaini kuwa Wizara hazikutoa taarifa kwa mamlaka za upangaji baada ya ufuatiliaji. Pia, wizara hazikufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa masuala yaliyobainishwa wakati wa ufuatiliaji. Kukosekana kwa ufuatiliaji wa masuala yaliyobainishwa wakati wa ufuatiliaji wa mamlaka za upangaji kulitokana na upungufu wa rasilimali kama vile rasilimali fedha na rasilimali watu. Hivyo kusababisha mambo yaliyobainishwa wakati wa ufuatiliaji kutotekelezwa.

**6.4 Athari katika kufikia malengo ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Mendeleo Endelevu**

Sehemu hii inaelezea athari za changamoto zilizoonekana katika usimamizi wa jumla wa mipango miji kuelekea kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Shabaha Na. 3 ya lengo la Maendeleo Endelevu Na.11 inalenga ukuaji wa miji kuwa jumuishi na endelevu yenye kujumuisha upangaji endelevu wa makazi na usimamizi katika nchi zote ifikapo mwaka 2030. Mipango ya maendeleo ya Miaka mitano yani mpango wa pili na watatu inalenga kuhakikisha kuwa na makazi ya mijini yaliyopangwa na yenye huduma zote za msingi.

Ripoti ya Tathmini ya Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano inaonesha fursa ambazo hazijafikiwa wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambapo kasi kubwa ya ongezeko la watu na ukuaji wa miji ulitoa fursa kwa wawekezaji na wadau wengine kuwekeza katika miradi ya nyumba, ikiwa pamoja na mikopo kwaajili ya ujenzi wa makazi. Kutokana na ongezeko la watu kwa mwaka kufikia asilimia 2.97, Tanzania kila mwaka idadi ya watu imekuwa ikiongezeka kwa milioni 1.5 kila mwaka tangu mwaka 2015, na wawekezaji wangetumia fursa hii kuongeza kipato.

Fursa nyingine ambayo ilikuwa haijafikiwa wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ni uboreshaji wa mtandao wa usafiri mijini kwa kuwa kulikuwa na ongezeko la watu kwa wastani wa asilimia 5.1 kwa mwaka, ambayo iko juu kwa asilimia 1.0 ya nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara na asilimia 3.0 juu kuliko wastani wa kimataifa kwenye maeneo ya mijini kama vile Dar es Salaam, Arusha, na Mwanza. Uboreshaji wa mitandao ya usafiri wa mijini utapunguza msongamano.


Mikakati katika Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano inalenga kukuza na kuwezesha upangaji, upimaji na utoaji wa hatimiliki kwa ajili ya uwekezaji na makazi, uandaji wa mipango kabambe ya miji, visiwa na ukanda wa pwani, kuanzisha mipango ya makazi ya bei nafuu, Kuboresha na kuongeza Mfumo wa utoaji taarifa ya usimamizi wa ardhi, na kukuza matumizi ya TEHAMA katika upimaji wa ardhi na utoaji wa hati.

Ukaguzi ulibaini kuwa, mfumo jumuishi wa utoaji wa taarifa za usimamizi wa ardhi, uliwekwa katika mikoa miwili kati ya mikoa sita iliyopangwa kufikiwa hadi Juni, 2023 ambayo ni sawa na asilimia 33 ya lengo lililopangwa. Aidha, Mpango wa tatu wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano, 2021/22 - 2025/26 uliweka mikakati ya kuongeza idadi ya Miji yenye mipango kabambe (Master Plans) kutoka 24 mwaka 2019/20 hadi 54 mwaka 2025/26 ikionesha jumla ya mipango kabambe 30 ilipaswa kupitishwa. Kwa miaka mitatu ya utekelezaji mipango kabambe mitano iliidhinishwa sawa na asilimia 16.67 na mipango kabambe 31 iliweza kuandaliwa.

Pia, mikakati ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ilikuwa kuongeza idadi ya viwanja vilivyopimwa na kumilikishwa kutoka viwanja 1,551,716 mwaka 2019/20 hadi viwanja 4,051,716 (ikionesha ongezeko la viwanja 2,500,000 vilivyomilikishwa) ifikapo mwaka 2025/26. Kwa miaka mitatu ya fedha kuanzia mwaka 2020/21 hadi 2022/23 jumla ya viwanja vipya vilivyomilikishwa vilikuwa viwanja 233,665 ambavyo ni sawa na asilimia 9 ya lengo la viwanja 2,500,000 vilivyopangwa kumilikishwa.

Hii inaonesha hatari ya kutofikia lengo lililowekwa la Mpango wa tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu ifikapo mwaka 2030.





## USIMAMIZI WA HUDUMA ZA BIMA NA UREJESHAJI WA MIKOPO YA WANAFUNZI WA ELIMU YA JUU

### 7.1 Utangulizi

Sura hii inatoa matokeo ya ukaguzi yanayotokana na ripoti za ukaguzi wa ufanisi zinazohusiana na usimamizi na ufuatiliaji wa watoa huduma za bima pamoja na usimamizi wa urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu nchini. Sura hii pia inaelezea eneo la ukaguzi, vyombo vya serikali vinavyohusika katika ukaguzi, uhusiano wa eneo la ukaguzi na Malengo ya Maendeleo Endelevu, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na matokeo ya ukaguzi kuhusiana na kaguzi hizi.

Kaguzi hizi za Ufanisi ni pamoja na:

- (a) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi na Ufuatiliaji wa Watoa huduma za Bima; na
- (b) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Urejeshaji wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

#### 7.1.1 Usuli kuhusu Ukaguzi wa Usimamizi na Ufuatiliaji wa watoa Huduma za Bima na Urejeshaji wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu

Sekta ya bima nchini Tanzania imekuwa kwa kiwango kikubwa tangu kuanzishwa kwa soko huria mwaka 1996, ambapo kumekuwa na ongezeko kubwa la watoa huduma za bima hapa nchini. Watoa huduma hawa hutoa bidhaa mbalimbali za bima, ikiwa pamoja na bima za maisha na za jumla zinazokidhi mahitaji mbalimbali ya watu binafsi na ya kibiashara. Sekta ya bima inapozidi kukua ni muhimu kuwa na udhibiti na usinamizi toshelevu ili za kudumisha - sekta hiyo. kwa sasa, sekta ya bima nchini Tanzania inasimamiwa na Sheria ya Bima Na.10 ya mwaka 2009, ambayo ilianzisha Mamlaka ya Udhibiti yenye jukumu la kusimamia sekta ya bima na kufuta iliyokuwa Sheria ya Bima ya mwaka 1996.

Aidha, tangu mwaka 1994/95, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imepewa mamlaka ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wasiojiweza kiuchumi ambao wamepata udahili katika vyuo vya elimu ya juu vyenye ithibati ndani na nje ya nchi. Bodi pia ina jukumu la kuhakikisha mikopo yote iliyotolewa kwa wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu na Vyuo vya Kati inarejeshwa kikamilifu. Kiasi kinachorejeshwa kinahudumia wanafunzi wengine wanaostahili ili kuhakikisha uendeleu wa mpango wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na kati hapa nchini.

Kuanzia mwaka 1994/95 hadi 2022/23, wanafunzi 759,722 wa Kitanzania wenye sifa na uhitaji walidahiliwa katika Vyuo vya Elimu ya Juu na hivyo kuwawezesha kuendelea na masomo. Hili liliwezekana kupitia mgao wa jumla wa shilingi 5.99 trilioni. Hata hivyo, Bodi imekabiliwa na changamoto nyingi tangu kuundwa kwake. Changamoto Hizo ni pamoja na ongezeko la waombaji wa mikopo, kutengewa fedha kidogo kutoka serikalini, ucheleweshaji wa utoaji wa mikopo, na urejeshaji hafifu wa mikopo.

### 7.1.2 Uhusiano kati ya Usimamizi wa Huduma za Bima na Mikopo ya Elimu ya Juu na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa pili na tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano

Ili kuzuia athari mbaya ambazo zinaweza kujitokeza dhidi ya hatari ya kuto kufikiwa mchango wa sekta ndogo ya bima katika uchumi, Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano umezingatia maeneo matatu ya kipaumbele na hatua muhimu kwa ajili ya sekta ndogo ya bima.

Kuhusu mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu nchini, chini ya Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Serikali ilikuwa na lengo la kuongeza idadi ya wanafunzi wa masomo ya sayansi na uhandisi katika elimu ya kati na ya juu wanaopata mikopo kwa asilimia 56 ifikapo mwaka 2020. Hatua muhimu ni pamoja na kuongeza upatikanaji wa mikopo ya wanafunzi katika ngazi ya elimu ya juu. Vilevile, chini ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Serikali ina mkakati wa kuongeza upatikanaji wa mikopo ya wanafunzi katika Elimu ya Juu hasa kwa wale wa Sayansi, Hisabati, kada maalumu na adimu.

**Jedwali Na. 35** linatoa muhtasari wa uhusiano ulioelezwa wa maeneo yaliyokaguliwa ambayo ni; huduma za bima na mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

**Jedwali Na. 35: Uhusiano wa maeneo yaliyokaguliwa na Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano**

Eneo lililokaguliwa	Maeneo muhimu ya Kipaumbele katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka mitano	Hatua muhimu
Huduma za bima	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kuandaa programu za uhamasishaji na uhamasishaji wa umma juu ya masuala ya bima;</li> <li>• Kuunda bidhaa za bima zinazotokana na mahitaji ya ndani; na</li> <li>• Kutengeneza mfumo kurahisisha mchakato wa madaai, kushughulikia malalamiko na suluhu za huduma za bima.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kuunda na kuendesha programu za uhamasishaji wa umma;</li> <li>• Kuendeleza na kukuza bidhaa za bima zinazotokana na mahitaji ya ndani; na</li> <li>• Kutengeneza mfumo thabiti wa kushughulikia malalamiko</li> </ul>
	Ufadhili wa Ndani kwa Taasisi binafsi	Ili kueneza na kutanua bidhaa za bima na kueneza sekta ya bima, Serikali itaharakisha tathmini ya kanuni za bima za Mfumo wa Kiislam (Takaful). Kuidhinishwa kwa kanuni za utoaji wa huduma za bima kwa kuzingatia mfumo wa kiislam (Takaful) utawezesha kuvutia uwekezaji nchini katika kutoa huduma hizi.
Mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu	Ubora na elimu stahiki	Kuongeza upatikanaji wa mikopo ya wanafunzi katika Elimu ya Juu hasa kwa wale wa Sayansi, Hisabati, kada maalumu na adimu.

*Chanzo: Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26*

Aidha, maeneo yaliyokaguliwa ya usimamizi wa huduma za bima na urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na elimu ya kati yanatekeleza ajenda ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ya mwaka 2030. Ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi na ufuatiliaji wa watoa huduma za bima unahusishwa na lengo namba 8 linahusu *"Kukuza ukuaji wa uchumi endelevu, shirikishi, ajira kamili*

na yenye tija na kazi zenye staha kwa wote". Ukuguzi huu ulilenga katika shabaha namba 8.10, inayoitaka Serikali kuimarisha uwezo wa taasisi za fedha za ndani ili kuhimiza na kupanua upatikanaji wa huduma za kibenki, bima na fedha kwa watu wote.

Kadhalika, ukuguzi wa ufanisi katika usimamizi wa urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu unahusishwa na lengo namba 4 linalohusu **"kuhakikisha elimu bora inayojumuisha na inayolingana na kukuza fursa za kujifunza maishani kwa wote"**. Ukuguzi huu ulilenga shabaha namba 4.3 ambayo inaitaka serikali kufikia mwaka 2030, kuhakikisha upatikanaji sawa kwa wanawake na wanaume kwa elimu ya ufundi, mafunzo ya ufundi na elimu ya juu ya bei nafuu na bora, ikijumuisha vyuo vikuu.

### 7.1.3 Mikakati na Juhudi za Serikali katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu

Serikali chini ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano sambamba na Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha wa mwaka 2020/21 hadi 2029/30 chini ya sekta ndogo ya bima, serikali ilipanga: kusambaza bidhaa za bima mbalimbali na kutanua ueneaji wa sekta ya bima; kukuza makampuni ya bima na mifumo ya hifadhi ya jamii ili kuhamasisha uwekaji akiba wa muda mrefu; na kuimarisha mfumo wa kisheria na udhibiti kwa mfumo madhubuti wa bima ya amana.

Mapitio ya Taarifa ya Mwaka ya Soko la Bima kwa Mwaka ulioishia mwaka 2022, yalibaini kuwa, serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania imetengeneza bidhaa mpya 16 za bima zinazokidhi mahitaji ya watu wa kipato cha chini. Bidhaa hizi ni pamoja na bima ndogo, bima ya mifugo, bima ya kilimo, bima ya afya, bima ya mazishi na bima ya vyombo vya baharini. Pia serikali ilisajili mawakala 13 wa bima kutoa bima kupitia majukwaa ya kidijitali yanasambazwa na waendeshaaji wa mitandao ya simu.

Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania pia imetengeneza Mfumo wa Usimamizi wa taarifa za bima, ili kuboresha usimamizi na ufuatiliaji wa tasnia ya bima.

Vilevile, chini ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Serikali imejiwekea malengo ya kuhakikisha wanafunzi wa Elimu ya Kati na Elimu ya Juu wanaopata mikopo wanaongezeka kutoka asilimia 60 mwaka 2019/20 hadi asilimia 90 mwaka 2025/26. Juhudi hizi ni pamoja na kuhakikisha wanafunzi wa Elimu ya Ufundi wanaopata mikopo inaongezeka kutoka asilimia 20 mwaka 2019/20 hadi asilimia 35 mwaka 2025/26.

## 7.2 Malengo na Mawanda ya ukaguzi

### 7.2.1 Malengo ya Ukaguzi

Lengo kuu la ukaguzi huu lilikuwa kutathmini endapo Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini wamesimamia ipasavyo usimamizi na ufuatiliaji wa watoa huduma za bima na urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kutoka kwa wanufaika.

Mahsusi, ukaguzi ulitathmini endapo:

- (i) Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania imesimamia na kufuatilia ipasavyo Watoa huduma za Bima ili kuhakikisha kuwa makampuni ya bima yanakidhi matakwa ya kisheria, kiufundi na kifedha; na
- (ii) Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imesimamia ukusanyaji wa marejesho ya mikopo kutoka kwa wanufaika ili kuhakikisha uendelevu.

### 7.2.2 Mawanda ya Ukaguzi

Ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi na ufuatiliaji wa watoa huduma za bima ulijikita zaidi katika kutathmini endapo Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania inasimamia na kufuatilia makampuni ya bima ipasavyo ili kuhakikisha kwamba yanafanya kazi zao kwa uthabiti wa kisheria, kiufundi na kifedha unaohitajika. Ukuguzi huu ulitathmini shughuli za ukaguzi kwa watoa huduma za bima, uthabiti wa kifedha wa makampuni ya bima, usimamizi wa madai ya bima kwa wakati, haki, na kwa uwazi na usimamizi wa uhamasishaji wa umma kuhusu huduma za bima. Taasisi kuu iliyokaguliwa ilikuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania kwa sababu ndiyo yenye jukumu la kusimamia sekta ya bima nchini na kuhakikisha kuwa kampuni za bima zinatengamaa na zinafanya kazi kwa haki na uwazi. Ukaguzi ulihusisha miaka minne ya fedha, kuanzia 2019/20 hadi 2022/23. Kipindi hiki kilichaguliwa kwa sababu tasnia ya huduma za kifedha, ikijumuisha bima, ilichangia shilingi 5,720.8 bilioni katika pato la taifa katika kipindi hiki, ikiwa ni asilimia 3.6 ya pato la taifa kwa mwaka 2021.

Aidha, ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi wa urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ulilenga kutathmini jinsi Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inavyokusanya mikopo inayodaiwa na iliyochelewa kutoka kwa wanufaika, mchakato wa makisio wa marejesho ya mikopo, tathmini ya ufanisi wa mchakato katika kufuatilia wanufaika katika makundi yote. Ufanisi wa mchakato wa madai katika kuimarisha urejeshaji wa mikopo, urejeshaji wa mikopo kutoka kwa waliokiuka kwa kuhakikisha kuwa kiasi kinachohitajika

kinakusanywa kwa ufanisi ndani ya muda uliotakiwa. Taasisi kuu iliyokaguliwa ilikuwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB). Hii ni kwa sababu Bodi imepewa dhamana ya kukusanya mikopo inayodaiwa kutoka kwa wanufaika wa mikopo na kuitumia kama fedha za mzunguko kuendeleza shughuli za Bodi.

Ukaguzi ulihusisha miaka minane (8) ya fedha kuanzia 2014/15 hadi 2022/23 kutokana na maboresho mbalimbali yaliyofanywa na na Bodi. Maboresho hayo ni pamoja na mabadiliko ya makato ya kila mwezi kutoka asilimia 8 hadi 15 na kuanzishwa kwa sera ya viwango vya sifuri kwa kuondolewa kwa ada ya kutunza thamani ya fedha na adhabu kwa mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

### 7.3 Matokeo ya Ukaguzi katika Usimamizi na Ufuatiliaji wa Watoa huduma za Bima


Ukaguzi huo unatambua juhudi zinazofanywa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania katika kuendelea kuwasimamia na kuwafuatilia watoa huduma za bima. Juhudi hizo ni pamoja na; usajili wa watoa huduma za bima 1,165, uanzishaji wa Mfumo wa Usajili kwa Njia ya Mtandao kwa ajili ya kusajili watoa huduma za bima, kuidhinisha bidhaa mpya za bima, na kutekeleza programu mbalimbali za uhamasishaji wa bima katika Kanda na Ofisi ya Zanzibar. Pamoja na jitihada hizo, ukaguzi umebainimapungufu mbalimbali kama ifuatavyo:

#### 7.3.1 Ongezeko la Madai ya Bima Yanayodaiwa kwa Makampuni ya Bima kwa asilimia 11

Wakaguzi walipitia Taarifa ya Utendaji wa Soko la Bima iliyotolewa mnamo Agosti 2022 yenye taarifa za kuanzia mwaka 2019 hadi 2021 na taarifa za mwaka kutoka Kampuni za Bima kwa Mwaka 2022. Ukaguzi ulibaini kuwapo kwa madai ambayo hayajalipwa mwishoni mwa kila mwaka katika aina mbalimbali za biashara zinazofanywa na kampuni za bima.

**Kielelezo Na. 25** Kinatoa uchambuzi kuhusu ongezeko la madai ambayo hayajalipwa kwa wanufaika na makampuni ya bima za jumla na maisha kila mwisho wa mwaka kuanzia 2019 hadi 2022.

**Kielelezo Na. 25: Madai Yanayodaiwa kwa Makampuni ya Bima za Jumla na na Bima za Maisha kwa Kipindi cha kuanzia Mwaka 2019 - 2022**



*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Ripoti ya Utendaji wa Soko la Bima ya 2019 - 2021 na Marejesho ya Kila Mwaka ya Hesabu za Bima kwa Mwaka wa Kalenda 2022.*

**Kielelezo Na. 25** kinaonesha kuwa madai ambayo hayakulipwa yaliongezeka kutoka shilingi 114.532 bilioni kutoka mwaka 2019 hadi shilingi 127.253 bilioni mwaka 2022, sawa na ongezeko la 11% kwa miaka minne iliyokaguliwa. Ukaguzi ulibaini kuwa mambo yafuatayo yalichangia zaidi uwapo kwa madai ambayo hayajalipwa na kampuni za bima kwa walengwa:

**(a) Uwapo wa Mlipuko wa UVIKO-19**


Ripoti ya Utendaji wa Soko la Bima iliripoti kwamba janga la UVIKO-19 lilisababisha ongezeko la madai ya bima ya maisha. Hii ni kwa sababu kutokana na athari za UVIKO-19 katika uchumi, madai ya biashara ya bima ya maisha yalibainika kuongezeka, huku uwiano wa manufaa ukifikia asilimia 67.6 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 58.6 mwaka 2020. Ingawa bima ya maisha ilipata ongezeko la asilimia 9 ya malipo ya fidia kwa wateja, bima ya jumla ilipata ongezeko la asilimia 3.3 tu la uwiano wa hasara hadi kufikia asilimia 47.4 mwaka 2021.

**(b) Kucheleweshwa kwa Ulipaji wa Madai Yaliyoidhinishwa na Makampuni ya Bima**

Baada ya mapitio ya Kumbukumbu za Madai ya makampuni ya bima na Ripoti za Ukaguzi wa makampuni hayo zilizofanywa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima

kwa mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2022/23. Ukaguzi ulibaini kuwa baadhi ya makampuni ya bima yalichelewesha ulipaji wa madai hayo kwa zaidi ya siku 45 baada ya kupokea madai hayo kikamilifu na kutoa hati za malipo kwa wadai kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 26**.

**Kielelezo Na. 26: Uchambuzi wa Ucheleweshaji wa Ulipaji wa Madai Yaliyoidhinishwa na Kampuni za Bima kuanzia 2019-2023**



**Chanzo:** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa za Ukaguzi za Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania za Mwaka 2019/20-2022/023

**Kielelezo Na.26** kinaonesha matukio ya ucheleweshaji wa malipo ya madai kutoka kwa makampuni ya bima na madai ambayo yalisalia bila kutatuliwa kwa zaidi ya siku 45 baada ya kutoa hati ya malipo kwa wadai husika. Wastani wa siku zilizochukuliwa kulipa madai zilianzia siku 59 hadi 216 zilizotumiwa na kampuni ya bima ya Meticulous na MGen Tanzania. Jumla ya asilimia 30 ya madai yaliyocheleweshwana makampuni ya bima yalikuwa shilingi milioni 439.15 kama ilivyobainika katika Ripoti za Ukaguzi za Mamlaka ya Bima kuanzia mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2022/23. Kwa hivyo, ucheleweshaji wa ulipaji wa madai uliathiri haki za wanufaika kulipwa madai yao kwa wakati.

Ucheleweshwa wa madai kwa malipo yaliyoidhinishwa na kampuni za bima kuna athari zifuatazo. Kwanza, wateja wa bima mara nyingi hukabiliwa na ugumu wa kifedha wanapopata ucheleweshaji wa kufikia malipo yao ya bima. Masuala ya kisheria, kama vile mizozo na adhabu za udhibiti, yanaweza pia kuongeza gharama za madai kwa bima na wateja wa bima. Mapungufu yaliyobainishwa



yanaangazia umuhimu wa ulipaji wa wa madai kwa ufanisi na kwa wakati ndani ya sekta ya bima.

Kucheleweshwa kwa malipo ya madai yaliyoidhinishwa na kampuni za bima kuna athari kadhaa. Kwanza, wateja wa bima mara nyingi hukabiliwa na ugumu wa kifedha wanapopata ucheleweshaji wa kupatiwa malipo yao ya bima. Masuala ya kisheria, kama vile mizozo na adhabu za kisheria, yanaweza pia kuongeza gharama za madai kwa kwa kampuni za bima na wamiliki wa sera. Matokeo haya yanaangazia umuhimu wa ulipaji wa madai ifaayo na kwa wakati unaofaa ndani ya tasnia ya bima.


### 7.3.2 Kutofanyika kwa Uchambuzi wa Viashiria vya hatari kwa Mawakala wa Huduma za Bima kulipelekea Mamlaka ya Usimamizi wa Bima kutokagua ipasavyo Mawakala wa Bima Nchini

Kulingana na uongozi wa Mamlaka ya Bima Tanzania, uchambuzi wa hatari kwa mawakala wa bima unahitajika kufanywa kwa kuzingatia wingi wa biashara na kufuata mwenendo wa soko kwenye biashara kwa mujibu wa leseni. Hii ni kwa sababu asili ya hatari kwa wakala wa bima inatofautiana na ile ya makampuni ya bima, ambao ni wabeba hatari za bima. Mamlaka iliongeza kuwa uteuzi wa mawakala wa bima huanza kwenye kanda ambapo Mameneja wa Kanda huchagua mawakala wakati wa uandaaji na ujumuishaji wa bajeti ya kila mwaka ili kufuatilia masuala ya tabia ya soko kwa watoa huduma za bima katika eneo lao.

Hata hivyo, ukaguzi haukupata msingi na ushahidi uliotumiwa na Mamlaka ya Bima katika kuchagua mawakala wa bima kwa ajili ya ukaguzi utakaofanywa kupitia makao makuu au Ofisi za Kanda za Mamlaka ya Bima. Kutofanyika kwa uchanganuzi wa hatari kwa mawakala wa bima kulichangiwa zaidi na mapungufu katika mipango ya ukaguzi wa vihatarishi na kauli kwamba mawakala wa bima hukaguliwa kupitia kwa makampuni ya bima. Jambo hili lilisababisha Mamlaka ya Bima kushindwa kubainisha misingi ya kuchagua mawakala wa bima kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi.

Hivyo basi, mawakala wa bima hawakukaguliwa ipasavyo na Mamlaka ya Bima Tanzania kwa kipindi kilichokaguliwa kuanzia 2019/20 hadi 2022/23, kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 27**.

**Kielelezo Na. 27: Utendaji wa Ukaguzi Uliofanywa na Mamlaka ya Bima Tanzania kwa Mawakala wa Bima 2019/20 - 2022/23**



*Chanzo: Uchambuzi wa Mipango Kazi na Taarifa za Ukaguzi za Mamlaka ya Usimamizi wa Bima kuanzia 2019/20 hadi 2022/23 (2023).*

Ukaguzi usiotosheleza kwa mawakala wa bima pia ulichangiwa na mipango ya ukaguzi ndani ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima kutozingatia hitaji la kupanga na kutenga rasilimali kwa ajili ya ukaguzi wa mawakala wa bima nchini.

Wakati wa ukaguzi huu Mamlaka ya Usimamizi wa Bima ilitaarifu kuwa, mawakala wa bima hukaguliwa kupitia Kampuni za Bima wakati wa ukaguzi wa kampuni hizo na kwamba mipango ya ukaguzi ipo kwa ajili ya ukaguzi wa madalali wa bima kulingana na masuala yaliyoainishwa. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa ni sharti la Mwongozo wa Taratibu za Ukaguzi kwamba Mamlaka ya Usimamizi wa Bima inapaswa pia kukagua mawakala wa bima kwa kutumia orodha ya maeneo na taratibu za ukaguzi wa mawakala wa bima iliyotolewa na na Mamlaka hiyo. Tathmini zaidi ya Mipango ya Utekelezaji ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima kwa miaka ya fedha 2021/22 na 2022/23, ilibaini kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima kupitia Ofisi zake za Kanda ilipanga kufanya kaguzi za uendeshaji wa soko kwa mawakala 55 na 190 ifikapo Juni 2022 na 2023 mtawalia.

Ukaguzi usiotosheleza kwa mawakala wa bima unaweza kusababisha kuongezeka kwa kutofuata mifumo ya kisheria iliyopo katika sekta ya bima na watoa huduma za bima.

**7.3.3 Ufuatiliaji Usiojitosheleza wa Utekelezaji wa Mapendekezo Yanayotolewa kwa Watoa Huduma za Bima Wakati wa Ukaguzi**


Ukaguzi ulibaini kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima haikufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa awali, wakati wa ukaguzi uliofuata ili kuthibitisha kiwango cha utekelezaji. Kwa mfano, katika miaka ya 2022 na

2023, Mamlaka ilitoa mapendekezo 140 kutoka kwa ukaguzi wa makampuni ya bima; hata hivyo, hakuna ufuatiliaji wowote uliofanywa na Mamlaka.

Wakati wa ukaguzi Mamlaka ilieleza kuwa, maagizo/mapendekezo yaliyotolewa katika Ripoti za Ukaguzi kuhusu kutofuata sheria, kanuni, miongozo au waraka yanajadiliwa katika Mikutano ya Kamati ya Utekelezaji wa Sheria, na mijadala/maamuzi yao yanajumuishwa katika Jedwali, ikionesha mambo yanayotokana na kila mkutano wa Kamati ya Utekelezaji wa Sheria. Baada ya hapo, ufuatiliaji wa maamuzi ya kamati hufanywa na Kitengo cha Sheria.

Ukaguzi ulibaini kuwa, jedwali linaloonesha masuala yaliyoibuliwa wakati wa mikutano ya Kamati ya utekelezaji wa sheria lilitayarishwa. Hata hivyo, mapitio ya Matoleo ya Masuala yanayotokana na mikutano iliyofanywa yalibaini kwamba si mapendekezo yote kuhusu kutofuata sheria, kanuni, au miongozo iliyotolewa kutoka kwa kila ripoti ya ukaguzi ilijadiliwa, kuamuliwa, na kujumuishwa katika majedwali hayo. **Kielelezo Na. 28** kinaonesha ni kwa kiasi gani mikutano ya kamati ya utekelezaji wa sheria ilijadili na kuamua maagizo/mapendekezo yaliyopendekezwa kutoka katika ripoti za ukaguzi.

**Kielelezo Na. 28: Ulinganisho wa idadi ya maagizo yaliyotolewa na ripoti za ukaguzi baada ya ukiukwaji wa sheria dhidi ya idadi ya maagizo yaliyoamuliwa na mikutano ya kamati ya utekelezaji wa Sheria**



*Chanzo: Ripoti za Ukaguzi, Mihutasari yaa vikao, na Majedwali kuhusu Mambo yatokanayo na Vikao vya Kamati ya Utekelezaji wa Sheria.*

**Kielelezo Na. 28** kinaonesha kuwa, kwa wastani, idadi ya maagizo kuhusu - kufuata sheria, kanuni, na miongozo au waraka iliyotolewa kutoka Ripoti za

Ukaguzi ilikuwa 34, na kuamuliwa na Kamati ya Ufuatiliaji wa Sheria ilikuwa 3, na hivyo kusababisha wastani wa ufaulu wa asilimia nane tu.

Ufuatiliaji usiotosheleza na utoaji wa taarifa juu ya hali ya utekelezaji wa maagizo/mapendekezo yaliyotolewa wakati wa ukaguzi kunaweza kusababisha tathmini isiyoridhisha ya matokeo ya mapendekezo kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Bima yaliyotolewa kwa makampuni ya bima. Kwa hivyo, hatari za kurudiwa kwa makosa yanayofanywa na kampuni za bima zinaweza kubaki juu.

### 7.3.4 Uwapo wa Kampuni za Bima Zinazojiendesha chini ya kiwango cha ukwasi kinachohitajika kutokana na kutofanyika kikamilifu kwa uchambuzi wa kiwango cha ukwasi

Muundo ulioidhinishwa wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania, unaeleza kwamba miongoni mwa kazi muhimu za Kurugenzi ya Usimamizi ni kufanya uchambuzi wa kifedha na Utengamo wa makampuni ya bima. Kurugenzi ya Usimamizi na Ukaguzi inatekeleza kazi hii kupitia Kitengo cha Uchanganuzi wa Taarifa na Takwimu. Tathmini ya uchanganuzi wa kifedha na ukwasi wa kampuni za bima unaofanywa na Kitengo cha Uchanganuzi na Takwimu, kwa ujumla hufanywa nje ya tovuti kulingana na taarifa za kila robo mwaka zinazowasilishwa kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania na makampuni ya bima kila robo mwaka.

Hata hivyo, mapitio ya Taarifa za Uchambuzi wa Kifedha na Ukwasi zilizoandaliwa na Mamlaka ya Bima Tanzania yamebaini kuwa Mamlaka iliweza kufanya tathmini ya mchanganuo wa hali ya kifedha na ukwasi kwa makampuni ya bima yenye leseni kuanzia mwaka 2019 hadi robo ya tatu ya 2022. Hata hivyo, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima haikufanya tathmini ya mchanganuo wa kifedha na ukwasi katika robo ya mwisho ya mwaka 2022 na mwaka mzima wa 2023. **Jedwali Na. 36** linatoa uchanganuzi wa kina kuhusu tathmini ya uchambuzi wa hali ya kifedha na ukwasi iliyofanywa na Mamlaka ya Bima Tanzania kwa kampuni za bima kwa kipindi kilichokaguliwa toka mwaka 2019 hadi 2023.

**Jedwali Na. 36: Kiwango cha Tathmini ya Uchambuzi wa Kifedha na Ukwasi wa Makampuni ya Bima yenye Leseni uliofanywa na Mamlaka ya Bima toka mwaka 2019 hadi 2023**

Mwaka wa Kalenda	Idadi ya Makampuni Yaliyosajiliwa	Idadi ya Makampuni Yaliyofanyiwa Tathmini				Asilimia ya Makampuni Yaliyofanyiwa Tathmini			
		Robo ya 1	Robo ya 2	Robo ya 3	Robo ya 4	Robo ya 1	Robo ya 2	Robo ya 3	Robo ya 4
2019	32	32	32	32	32	100	100	100	100
2020	34	34	31	33	30	100	91	97	88

Mwaka wa Kalenda	Idadi ya Makampuni Yaliyosajiliwa	Idadi ya Makampuni Yaliyofanyiwa Tathmini				Asilimia ya Makampuni Yaliyofanyiwa Tathmini			
		Robo ya 1	Robo ya 2	Robo ya 3	Robo ya 4	Robo ya 1	Robo ya 2	Robo ya 3	Robo ya 4
2021	33	33	33	32	33	100	100	97	100
2022	35	33	31	35	0	94	89	100	0
2023	36	0	0	0	0	0	0	0	0

**Chanzo:** Uchambuzi wa Taarifa za Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania kuhusu Hali ya kifedha na ukwasi kwa Makampuni ya Bima kuanzia mwaka 2019 hadi 2023

**Jedwali Na. 36** linaonesha kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ilifanya tathmini ya hali ya kifedha na ukwasi kwa makampuni ya bima kwa kiasi kikubwa kwa mwaka wa kalenda 2019 hadi 2022, ukiwakilisha utendaji wa zaidi ya asilimia 90. Hata hivyo, Mamlaka haikufanya uchambuzi katika robo ya 4 ya mwaka wa kalenda 2022 na mwaka mzima wa kalenda wa 2023.


Kutofanyika kikamilifu kwa tathmini ya hali ya kifedha na ukwasi kwa makampuni ya bima nchini umesababisha yafuatayo:

**(a) Asilimia 48 ya Kampuni za Bima za Jumla na asilimia 40 ya Kampuni za Bima za Maisha zilibainika kujiendesha chini ya kiwango cha ukwasi kinachokubalika kisheria**

Kanuni ya 21(1) ya Kanuni za Bima za mwaka 2009 inaelekeza mali za kampuni ya bima zinazohusika na biashara ya jumla ya bima kuzidi jumla ya madeni ya kampuni kwa asilimia 20 ya malipo halisi ya bima au kiwango cha chini zaidi kilichobainishwa katika Kanuni hiyo. Kwa hivyo, kampuni za bima zinatakiwa kudumisha kiwango cha ukwasi kwa zaidi ya asilimia 0, wakati mahitaji ya busara yanahitaji makampuni kufikia angalau asilimia 50 ya uwiano.

Hata hivyo, Ukaguzi ulibaini baadhi ya kampuni za bima zilikuwa zikifanya kazi kwa kiwango cha ukwasi kilicho chini ya kiwango cha kisheria cha asilimia 0 kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 29:**

**Kielelezo Na. 29: Kiwango cha Utiifu wa Viwango vya Kisheria vya Ukwasi Kampuni za Bima za Jumla na Bima ya Maisha kufikia tarehe 30 Juni 2022**




Chanzo: Uchambuzi wa Taarifa za Mamlaka ya Bima Tanzania juu ya Tathmini ya hali ya Ukwasi kwa Kampuni za Bima hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022

**Kielelezo Na. 29** kinaonesha kuwa asilimia 48 ya Kampuni za Bima za Jumla na asilimia 40 ya kampuni za Bima za Maisha zilikuwa zikijiendesha chini ya kiwango cha ukwasi cha asilimia 0 kinachohitajika kisheria. Kwa hiyo, makampuni hayo ya bima yalikuwa yakijiendesha kwa kiwango hasi cha ukwasi katika kipindi husika. Kutokana na hali hiyo, Kampuni za Bima zinafanya biashara ya bima za jumla zilitakiwa kuongeza mtaji wa Shilingi 56,773.03 milioni. Kinyume chake, Kampuni za biashara za bima za maisha zilitakiwa kuongeza mtaji wa Shilingi 6,209.07 milioni ili kufikia kiwango cha kisheria kulingana na matakwa ya Kifungu cha 20(1) cha Sheria ya Bima Na.10 ya mwaka 2009.

**(b) Asilimia 60 ya kampuni za Bima za Jumla na asilimia 67 ya Kampuni za Bima za Maisha zilikuwa zikijiendesha chini ya kiwango cha cha tahadhari (prudential level) cha asilimia 50**

Uchambuzi zaidi wa Taarifa za Ukwasi za Kampuni za Bima ulibaini kampuni za bima za jumla na bima za maisha zinazojiendesha kwa kiwango cha ukwasi kinachokubalika kisheria cha asilimia 0 (kiwango chanya cha ukwasi). Bado, zilikuwa hazijakidhi kiwango cha hadhari cha angalau asilimia 50 ya uwiano, kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 30:**

**Kielelezo Na. 30: Kampuni za Bima zilizo na Kiwango cha ukwasi kilicho juu ya Kiwango cha Kisheria lakini chini ya Kiwango cha Tahadhari**



**Chanzo:** Uchambuzi wa Taarifa za Mamlaka ya Bima Tanzania juu ya Tathmini ya hali ya Ukwasi kwa Kampuni za Bima hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022.

**Kielelezo Na. 30** kinaonesha kuwa 60 asilimia ya Kampuni za Bima za Jumla na asilimia 67 ya Kampuni za Bima za Maisha zilikuwa zikijiendesha chini ya kiwango cha tahadhari cha asilimia 50. Kutokana na hali hiyo, Kampuni za Bima za Jumla zilitakiwa kuingiza mtaji wa kiasi cha shilingi 12,265.07 milioni. Kwa upande mwingine, Kampuni za Bima za Maisha zilitakiwa kuongeza mtaji wa kiasi cha shilingi 3,375.12 milioni ili kufikia kiwango cha tahadhari cha asilimia 50.

Kufuatia uchambuzi zaidi, ukaguzi ulibaini uwapo wa kampuni za bima zinazofanya kazi chini ya kiwango kinachohitajika cha ukwasi ulisababishwa na:

**i) Uwapo wa Gharama za Uendeshaji na Kupungua kwa Malipo ya Jumla**

Mapitio ya Taarifa ya Ukaguzi wa mwezi Julai 2022 uliofanywa na Mamlaka ya Bima Tanzania kwenye kampuni ya bima ya MAXINSURE (TANZANIA) LIMITED, yalibaini kuwa gharama za uendeshaji wa Kampuni ikilinganishwa na asilimia ya malipo halisi yaliyopatikana yaliongezeka kutoka asilimia 79.1 mwaka 2020 hadi asilimia 110.1 mwaka 2021 juu ya kiwango cha juu cha tahadhari cha asilimia 25 na juu zaidi kuliko wastani wa sekta wa asilimia 44.3 kwa mwaka 2020. Taarifa hiyo pia iliripoti kuwa, katika kipindi cha mpito kilichoishia tarehe 31 Machi 2022, kampuni ilirekodi uwiano wa gharama za usimamizi wa asilimia 83.3. Hii ina maana kwamba kampuni ilikuwa ikipata hasara katika biashara.

Aidha, ukaguzi ulibaini pia malipo ya jumla ya kampuni hiyo yalipungua kwa asilimia 34.3 kutoka shilingi milioni 10,474 mwaka 2020 hadi shilingi Milioni 6,884 mwaka 2021. Aidha, katika kipindi cha mpito kilichoishia tarehe 30 Septemba 2022, kampuni hiyo ilipata hasara ya shilingi 1,925 milioni.

***ii) Uwapo wa Idadi ndogo ya Kampuni za Kitaalamu katika masuala ya Bima Nchini***

Mapitio ya Utafiti wa Bima Jumuishi na namna ya kugharimia fidia ya hasara kwa unafuu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2023), yalibaini uwapo wa makampuni sita tu ya wataalam wa bima yaliyokuwa yakifanya kazi nchini hadi kufikia Juni 2023. Hali hii inaashiria kwamba kulikuwa na uhaba wa wataalam wa bima waliohitimu na wenye uzoefu wa bima ambao hatimaye iliathiri ubora wa uandikishaji wa malipo (premium underwriting) katika makampuni ya bima, madalali au mawakala. Kwa hivyo, kulikuwa na hatari ya kutoza malipo yasiyo sahihi, ambayo hatimaye yangechangia katika ufilisi wa makampuni ya bima.

Tatizo la ukwasi kwenye kampuni za bima unaonesha kuwa hazina pesa za kutosha kukidhi madeni yao, na hivyo kuathiri hali ya kifedha ya kampuni.

Kutokana na usimamizi usioridhisha wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima katika kuhakikisha kwamba kampuni za bima zinakuwa na ukwasi unaohitajika. Makampuni ya bima hayafuatilii ipasavyo hali zao za kifedha kupitia udumishaji wa viwango vya ukwasi vinavyokubalika, na hayasimamii ipasavyo hali zao za kifedha. Ukwasi duni husababisha shida ya mtiririko mzuri wa fedha na kupungua kwa uwezo wa kifedha wa kusuluhisha madai ya bima yanapotokea.

Kwa upande mwingine, hali hii inaweza kusababisha moja kwa moja kuanguka kwa makampuni ya bima.

**7.3.5 Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania Haikuhakikisha kikamilifu Kampuni za Bima Zinawekeza Dhamana Inayotakiwa kisheria katika Benki Kuu ya Tanzania**

Mapitio ya Taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania kuhusu Dhamana zilizowekezwa na Makampuni ya Bima dhidi ya Kamishna wa Bima kufikia tarehe 07 Januari 2024 kwa mujibu wa Kanuni ya (20)(1) ya Kanuni za Bima ya mwaka 2009 inayataka makampuni ya bima kuweka na kudumisha amana ya dhamana (security deposit) ya angalau asilimia 50 ya kiwango cha chini cha mtaji uliopo katika Benki Kuu ya Tanzania. Ilibaini kuwa, asilimia 54 ya Makampuni ya Bima hayakufuata matakwa ya Kanuni ya 20 ya Kanuni za Bima za mwaka 2009. **Jedwali Na. 37** linatoa muhtasari wa hali ya uwekaji wa amana za dhamana katika Benki Kuu ya Tanzania kwa makampuni ya bima.



**Jedwali Na. 37: Hali ya Utunzaji wa Amana ya Chini ya Dhamana katika Benki Kuu ya Tanzania kwa Makampuni ya Bima**

Jumla ya Makampuni ya Bima (Idadi na asilimia)	Idadi ya Makampuni yenye Amana ya dhamana juu ya kiwango Kinachotakiwa	Idadi ya Makampuni yenye Amana ya dhamana chini ya Kiwango kinachotakiwa	Idadi ya makampuni yasiyokuwa na Amana ya dhamana
35	16	11	8
100%	46%	31%	23%

*Chanzo: Mapiitio ya Taarifa ta Amana zilizowekezwa na Makumpuni ya Bima Benki Kuu ya Tanzania ya tarehe 07 Januari 2024 na Taarifa ya Utendaji wa Soko la Bima ya Disemba 2022*

**Jedwali Na. 37** linaonesha kwamba mpaka kufikia tarehe 31 Desemba 2023, asilimia 46 ya makampuni ya bima yaliyosajiliwa yalikuwa yamewekeza amana ya dhamana katika Benki Kuu ya Tanzania juu ya kiwango kinachotakiwa, asilimia 31 walikuwa na amana ya dhamana chini ya kiwango kinachotakiwa sawa na pungufu ya jumla ya shilingi bilioni 4.26, na asilima 23 hawakuwa na amana ya dhamana katika benki ya sawa na jumla ya shilingi 8.26 bilioni.

Kulingana na uongozi wa Mamlaka ya Bima Tanzania, wakaguzi walipaswa kujumuisha salio katika taarifa za Benki Kuu na salio lililopo kwenye Akaunti ya uaminifu wakati wanachakata endapo makampuni ya bima yamekidhi matakwa ya kisheria ya kuwa na amana Benki Kuu ya Tanzania. Hii ni kwa sababu akaunti hiyo inashikilia fedha za makampuni ya bima zinazolenga kutimiza matakwa ya Kanuni ya 201(1) ya Kanuni za Bima za mwaka 2009, wakati kampuni hizo zinasubiri mnada kutangazwa na Benki Kuu ya Tanzania.

Hata hivyo, wakaguzi hawakuzingatia fedha za makampuni zilizowekwa na kampuni za bima katika akaunti ya uaminifu kama sehemu ya amana ya dhamana/uwekezaji uliowekezwa Benki Kuu ya Tanzania, kwa sababu salio lililokuwapo kwenye Akaunti ya Uaminifu halijakidhi matakwa ya Kanuni ya 20 (1) ya Kanuni za Bima za mwaka 2009, kama zilivyorekebisha mwaka 2021. Hii ni kwa sababu, salio la makampuni ya bima lililoshikiliwa katika Akaunti ya Uaminifu linapaswa kuwekezwa Benki Kuu ya Tanzania katika dhamana za serikali ili ziweze kutambuliwa kama uwekezaji kwa mujibu wa Kanuni ya 20(1) ya Kanuni za Bima za mwaka 2009.

Mapungufu na kutokuwekeza amana ya dhamana ya kima cha chini katika Benki Kuu ya Tanzania kwa makampuni ya bima, kulichangiwa zaidi na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima kutofuatilia ipasavyo utekelezaji wa matakwa ya Kanuni ya 20(1) ya Kanuni za Bima za mwaka 2009 inayozitaka Kampuni za Bima kuwekeza angalau asilimia 50 ya mtaji kama amana Benki Kuu ya Tanzania. Hii ina maana kwamba ikiwa kampuni yoyote kati ya hizo itashindwa kujiendesha au kufilisika,

wateja wa bima hawatapata fidia yoyote kwa madai yao na kutorejeshewa malipo yao ya ununuzi wa bima husika.


## 7.4 Matokeo ya Ukaguzi katika Usimamizi wa Urejeshaji wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu

### 7.4.1 Ongezeko la mikopo ambayo Haijalipwa hadi shilingi Trilioni 3.15

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imeagizwa na Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Sura Na. 178 ya mwaka 2008, kusimamia utoaji wa mikopo ya wanafunzi na urejeshaji wa mikopo hiyo. Kwa mujibu wa Mwongozo wa Urejeshaji na Marejesho ya Mikopo wa Bodi ya Mikopo wa 2019, marejesho ya mikopo lazima yafanywe kila mwezi. Wanufaika walioajiriwa wanapaswa kuchangia asilimia 15 ya mishahara yao ghafi, huku wanufaika walioajiri wakitakiwa kurejesha si chini ya shilingi 100,000/= au asilimia 10 ya mapato yanayopaswa kulipiwa kodi.

Uchambuzi wa takwimu zilizotolewa na hali ya urejeshaji wa mikopo ulibainisha kuwa mikopo ambayo haijalipwa inaongezeka kila mwaka, kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 31**. Mikopo ambayo haijalipwa ilibainika kuongezeka kutoka shilingi Trilioni 1.25 katika mwaka wa fedha 2015/16 hadi kufikia shilingi Trilioni 4.84 katika mwaka wa fedha 2021/22, ikiwakilisha ukuaji wa wastani wa asilimia 23.

**Kielelezo Na. 31: Hali ya Mikopo ya Wanafunzi Inayodaiwa**




**Chanzo:** Uchambuzi wa Wakaguzi katika kumbukumbu za wakopaji za mwaka 2022, 2023

**Kielelezo Na. 31** kinaonesha kuwa kiwango cha mikopo ambayo haijarejeshwa iliongezeka kutoka asilimia 59 katika mwaka wa fedha 2015/19 hadi kufikia asilimia 83 katika mwaka wa fedha 2021/22. Hali hii inaonesha kuwa serikali inafanya uchangiaji wa fedha za kufadhili mikopo kwa kiasi kikubwa kutokana na urejeshaji wa mikopo usioridhisha.

Kuongezeka kwa mikopo ambayo haijalipwa kulichangiwa zaidi na kupungua kwa urejeshaji wa mikopo kama inavyoonyeshwa katika **Kielelezo Na. 32**:

**Kielelezo Na. 32: Mwenendo wa Ukusanyaji wa Marejesho ya Mikopo ya Wanafunzi**



*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi katika Kanzidata ya Marejesho ya Mikopo, 2022*

**Kielelezo Na. 32** kinaonesha kuwa katika mwaka wa fedha 2019/20, Bodi ya Mikopo ilirekodi makusanyo ya juu zaidi ya ulipaji wa mikopo tangu kuanzishwa kwake, ambayo yalikuwa shilingi bilioni 191. Hata hivyo, mwenendo wa ukusanyaji ulianza kushuka hadi kufikia shilingi bilioni 170 katika mwaka wa fedha 2022/23. Hali hii ilisababishwa na mabadiliko ya sera, ikiwemo sera ya ukadiriaji sifuri mnamo Julai 2021, kubadilisha adhabu na ada za kuhifadhi thamani ya fedha kuwa sifuri.

Ongezeko la madai ambayo hayajalipwa ilisababisha serikali kutenga bajeti zaidi kwa ajili ya ufadhili wa wanafunzi kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 38.

**Jedwali Na. 38: Ruzuku ya Serikali katika utoaji wa mikopo ya wanafunzi**

Mwaka wa Fedha	Kiasi (Sh. bilionii)
2018/19	268.9
2019/20	219.4
2020/21	334.0
2021/22	393.8


Chanzo: Ripoti za utendaji za Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa mwaka 2019-2022

Jedwali Na. 38 linaonesha uchangiaji wa Serikali kwenye utoaji wa mikopo ya wanafunzi uliongezeka kutoka shilingi bilionii 268.9 katika mwaka wa fedha 2018/9 hadi kufikia shilingibilionii 393.8 katika mwaka wa fedha 2021/22 sawa na ongezeko la shilingi bilioni 124.9.

#### 7.4.2 Wanufaika Wachache Walirejesha Mikopo yao

Ukaguzi ulibainisha kuwa kiwango cha wanufaika wanaolipa mikopo yao kilipungua kwa miaka tofauti. Hali hii inaonesha kuwa sehemu ndogo ya wanufaika wanalipa mikopo yao kila mwaka. Idadi ya wanufaika wanaolipa mikopo yao ilipungua kutoka asilimia 39 mwaka 2017/16 hadi asilimia 23 mwaka 2022/23 kama inavyooneshwa katika Kielelezo Na. 33.

**Kielelezo Na. 33: Idadi ya wanufaika wenye Mikopo iliyofikia muda wa malipo dhidi ya Wanufaika waliolipa Mikopo yao kila mwaka**




Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa hifadhidata ya mikopo iliyoiva ya HESLB, 2023 na Marejesho Halisi

**Kielelezo Na. 33** kinaonesha kiwango cha wanufaika wanaolipa mikopo yao kilipungua kutoka mwaka 2017/16 hadi mwaka 2022/23, ikionesha kwamba sehemu ndogo ya wanufaika wanalipa mikopo yao kila mwaka. Kwa mfano, mwaka 2018/19, asilimia 35 ya wanufaika walilipa mikopo yao, wakati 2022/23, wanufaika asilimia 23 walilipa mikopo yao.

Hali hii ilichangiwa kutofuatilia kwa ufanisi kwa wanufaika wa mkopo; ambapo kati ya wanufaika 486,549 wenye mikopo iliyo tayari kulipwa wanufaika 197,232 tu ndio waliobainishwa na kuandikiwa hati za madai, sawa na asilimia 41 ya wanufaika wote wenye mikopo iliyotayari kulipwa.

Tathmini zaidi ya Taarifa za Mikopo na Kanzidata ya Mikopo iliyoiva, ilionesha kuwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu haikutambua na kutoza asilimia 61 ya wanufaika wenye mikopo iliyoiva hadi kufikia mwezi Septemba 2023, kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 34**.

**Kielelezo Na. 34:** Hali ya Utambuzi wa Wanufaika wa Mikopo ya Elimu ya Juu kuwezesha urejeshaji



*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kwa Kanzidata ya Mikopo iliyoiva, 2023*

**Kielelezo Na. 34** kinaonesha idadi ya walengwa ambao hawajatambuliwa kuongezeka kutoka 101,710 mwaka 2014 hadi 307,353 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 202 kwa kipindi cha miaka 8.

Ukaguzi ulibaini masuala mbalimbali yalichangia ongezeko hili. Masuala hayo ni pamoja na ukaguzi usiotosheleza kwa waajiri, kutounganishwa kwa mfumo ya

TEHAMA na wadau wakuu wenye hifadhi kubwa taarifa za wanufaika wa mikopo walioajiri, kampeni za uhamasishaji zisizo na tija, matangazo yasiyotosheleza katika kufuatilia wanufaika, na ukosefu wa uratibu miongoni mwa wadau.

Hivyo basi, uchambuzi wa Kanzidata ya Mikopo iliyoiva na Taarifa za Mikopo kwa mwaka 2023, ulibaini kulikuwa na ongezeko kubwa la mikopo iliyoiva kwa muda wa miaka kumi kutoka asilimia 0.42 mwaka 2014/15 hadi asilimia 2.52 katika mwaka wa fedha 2022/23. Hali hii ina maana kwamba mikopo hiyo ilikuwa hatarini zaidi kwani ilitarajiwa iwe imerejeshwa ndani ya kipindi cha miaka 10 hadi 15, hata hivyo Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu haikukusanya malipo yoyote kutoka kwenye mikopo hiyo.

### 7.4.3 Marejesho ya mikopo kutoka kwa wanufaika binafsi yalifanywa kwa wastani wa asilimia 11 ikilinganishwa na asilimia 38 kutoka kwa wanufaika walioajiriwa

Ukaguzi ulibaini kuwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ilikusanya sehemu ndogo ya marejesho ya mikopo kutoka kwa wanufaika binafsi kwa wastani wa shilingi bilioni 38 sawa na asilimia 11 kuanzia mwaka 2014/15 hadi 2022/23 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 39**. Hii inaonesha kuwa HESLB ilijikita zaidi katika kukusanya marejesho ya mikopo kutoka kwa wanufaika walioajiriwa.

**Jedwali Na. 39: Ulinganisho wa Ukusanyaji wa Mikopo kutoka kwa wanufaika walioajiriwa na wanufaika binafsi**

Miaka ya fedha	Makusanyo ya Jumla kutoka kwa wanufaika walioajiriwa (Sh. bilioni) (A)	Makusanyo ya Jumla kutoka kwa wanufaika walioajiriwa binafsi (Sh. bilioni) (B)	Jumla ya Makusanyo kwa mwaka (Sh. bilioni) C=(A+B)	Asilimia ya marejesho kutoka kwa wanufaika walioajiriwa binafsi B/C*100	Asilimia ya marejesho kutoka kwa wanufaika walioajiriwa A/C*100
2014/15	65.61	1.91	67.5	2.8	97.2
2015/16	94.98	3.48	98.5	3.5	96.5
2016/17	199.41	7.9	207.3	3.8	96.2
2017/18	369.89	14.11	384.0	3.7	96.3
2018/19	539.93	27.63	567.6	4.9	95.1
2019/20	713.84	42.63	756.5	5.6	94.4
2020/21	881.89	54.59	936.5	5.8	94.2
2021/22	1,032.51	84.54	1,117.1	7.6	92.4
2022/23	1,181.40	104.7	1,286.1	8.1	91.9

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi uliofanywa katika Kanzidata ya Mikopo iliyotayari kulipwa na Leja ya Mikopo, 2023.*

**Jedwali Na. 39** linaonesha kuwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ilikusanya kiasi kidogo cha marejesho ya mikopo kutoka kwa wanufaika binafsi, kati ya asilimia 2.8 mwaka 2014/15 hadi asilimia 8.1 mwaka 2022/23. Hadi kufikia mwaka wa fedha 2022/23 Bodi ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 1,181.40 kutoka kwa walengwa walioajiriwa na shilingi bilioni 104.70 kutoka kwa walengwa waliojijiri.

Kukosekana kwa ufanisi wa ukusanyaji wa mikopo iliyokomaa kulitokana na kukosa mikakati ya ufuatiliaji ikiwa pamoja na kukosekana kwa muunganisho wa mfumo wa TEHAMA na taasisi kama Mamlaka ya Mapato Tanzania, Shirika la Taifa la Uhifadhi ya Jamii, Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini, Tume ya Vyuo Vikuu, Mamlaka ya Vitambulisho na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni zenye kanzidata nyingi za wanufaika kama inavyooneshwa hapa chini:

***Uunganishaji usiojitosheleza wa Mifumo ya TEHAMA ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya juu na Wadau wengine Muhimu***

Mapitio ya mifumo mikuu (OLAMS na ILMS) inayosimamia utoaji na urejeshaji wa mikopo yalibaini kuwa mifumo hiyo haikuunganishwa kikamilifu na mifumo ya wadau muhimu, ikiwa pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania, Shirika la Taifa la Uhifadhi ya Jamii, Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini, Tume ya Vyuo Vikuu, Mamlaka ya Vitambulisho na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni. Hii ilizuia ushirikishanaji wa taarifa kwa ajili ya kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wanufaika na ukusanyaji wa marejesho kutoka kwa waajiri na walengwa binafsi kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 40**. Ukaguzi ulibaini kuwa Mfumo wa Bodi ya Mikopo umeunganishwa katika mfumo wa Serikali wa kushirikiana taarifa mtandao. Hata hivyo, ushirikiano huo ulilenga katia eneo la malipo tu.

**Jedwali Na. 40: Kiwango cha muunganisho wa Mfumo wa Bodi ya Mikopo na Mifumo ya Wadau Wengine**

Jina la mdau	Jina la mfumo	Hali ya muunganiko	Umuhimu wa mfumo husika kwa Bodi ya Mikopo
Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa	Mfumo wa IDENCRAFT	Haijaunganishwa	Kutambua walipo walengwa, majina na umri.
Mamlaka ya Mapato Tanzania	Mfumo wa utumaji taarifa kwa njia ya mtandao (E-Filling)	Haijaunganishwa	Kutambua majina ya wamiliki wa biashara.
Mfuko wa Huhifadhi wa Watumishi wa Umma	Mwanachama wa Mfuko wa Huhifadhi wa Watumishi wa Umma	Haijaunganishwa	Kutambua majina ya wanachama wenye kipato.

Jina la mdau	Jina la mfumo	Hali ya muunganiko	Umuhimu wa mfumo husika kwa Bodi ya Mikopo
Mfumo wa Bima ya Afya ya Taifa	Haijulikani	Haijaunganishwa	Kutambua majina ya wanachama wenye kipato.
Mfuko wa Taifa la Uhifadhi ya Jamii	haijulikani	Haijaunganishwa	Kutambua majina ya wanachama wenye kipato.
Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni	Mfumo wa Usajili kwa njia ya mtandao	Haijaunganishwa	Kutambua majina ya wamiliki wa biashara na eneo la biashara.
Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini,	e-RITA	Haijaunganishwa	Kujua usimamizi wa ufilisi, huduma za udhamini, uhakiki wa taarifa, na usaidizi wa kisheria muhimu katika kusaidia shughuli na malengo ya Bodi ya Mikopo katika kusimamia mikopo ya wanafunzi.
Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora	HCMIS	Umeunganishwa	Kutambua taarifa za ajira za watumishi wa umma.

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Mawasiliano kati ya Bodi ya Mikopo, wadau, na, Jukwaa la serikali la kushirikiana taarifa kwenye mtandao, 2023*

Ukosefu wa muunganisho wa mfumo wa Bodi ya Mikopo na Mifumo ya Wadau wengine ulisababishwa na kutokuwapo kwa tathmini ya kina ya utaratibu wa kuwatafuta walengwa, hasa baada ya kuhitimu. Zaidi ya hayo, tatizo hilo lilichangiwa na muundo usiotosheleza wa mfumo, ambao ulisababisha kutopatana zaidi na mifumo mingine.

Hivyo basi, hali hii inaifanya Bodi ya Mikopo kupata taarifa zenye makosa katika kuwatambua wanufaika wa mikopo katika mifumo, kwani baadhi ya wanufaika wa mikopo wanakosa taarifa muhimu kama vile mwaka wa kuhitimu, anuani, namba za simu, kada walizosoma n.k; na kukosekana kwa ufuatiliaji wa wanufaika wa mikopo. Hivyo, kusababisha kutokusanywa kwa marejesho ya mikopo, jambo ambalo linaweza kuathiri uendeleu wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.



#### 7.4.4 Shilingi bilioni 150.28 hazikutozwa na Bodi ya Mikopo kwa Waajiri wasiotimiza masharti

Ukaguzi ulibaini kuwa Bodi ya Mikopo haikuchukua hatua za utekelezaji kuhusu waajiri walioshindwa kuwasilisha majina ya watumishi waliokuwa wanufaika wa mikopo kutoka Bodi ya Mikopo Wanafunzi wa Elimu ya Juu, kinyume na Kifungu cha 21(2) cha Sheria ya Bodi ya Mikopo kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 41.

**Jedwali Na. 41: Idadi ya Faini ambazo hazikutozwa kwa Waajiri**

Mwaka wa fedha	Idadi ya waajiri walioyunja Sheria	Kiwango cha adhabu walichastahili kutozwa kwa mwajiri mmoja (Sh. Milioni)	Jumla ya Faini ambazo hazikutozwa (Sh. bilioni)
2022/23	220	7	1.54
2021/22	2111	7	14.78
2020/21		7	N/A
2019/20	3524	7	24.67
2018/19	2815	7	19.71
2017/16	3561	7	24.93
2016/17	5634	7	39.44
2015/16	3603	7	25.22
<b>Jumla kuu</b>			<b>150.28</b>

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Notisi za Kumbusho kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, 2023.*

**Jedwali Na. 41** linaonesha kuwa jumla ya faini ambazo hazikutozwa na Bodi ya Mikopo kwa waajiri ni Shilingi bilioni 150 kutoka mwaka wa fedha 2015/16 hadi 2022/23. Shilingi bilioni 1.54 hazikutozwa katika mwaka 2015/16 ambazo ziliongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 25.22 mwaka 2022/23. Ukaguzi ulibaini Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu haikutekeleza adhabu kwa waajiri wasiotimiza masharti kutokana na kukosekana kwa mikakati madhubuti ya kukusanya mapato ya ada na faini. Hii ni kwa sababu Bodi ya Mikopo haikutuma hati za madai kwa wanufaika wenye mikopo ambayo ilikuwa haijalipwa kwa zaidi ya miaka kumi, kinyume na aya ya 4.1 (a, b &c) ya Mwongozo wa Marejesho ya Mikopo, 2019.

Hii ilisababisha mikopo iliyo tayari kulipwa kupitisha muda wa malipo kwa zaidi ya miaka kumi kwani hakuna hatua zilizochukuliwa dhidi yake. Hivyo, malimbikizo ya mikopo ya muda wa miaka kumi yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 6.7 mwaka 2014/15 hadi shilingibilioni 110 kwa mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la shilingibilioni 103.3 katika kipindi cha miaka 8 kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 42.

**Jedwali Na. 42: Idadi ya Wanufaika walio na mikopo inayodaiwa kwa zaidi  
ya kipindi cha miaka kumi**

Mwaka wa fedha	Idadi ya Wanufaika	Kiasi kilichopitiliza miaka 10 (Sh. bilioni)
2014/15	10,259	6.74
2015/16	11,364	8.07
2016/17	12,811	9.87
2017/16	14,492	12.22
2018/19	20,167	19.78
2019/20	27,882	35.38
2020/21	33,282	59.60
2021/22	38,750	83.79
2022/23	42,969	109.91

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa leja ya Mkopo kufikia Juni 2023.*

**Jedwali Na. 42,** linaonesha kulikuwa na ongezeko kubwa la wanufaika walio na kiasi ambacho hakijarejeshwa kutoka 10,259 hadi 42,969. Hata hivyo, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu haikuchukua hatua zozote kurejeshwa kiasi ambacho hakikuwa kimerejeshwa.

## 7.5 Athari katika kufikia malengo ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Mendeleo Endelevu

### *Athari kutokana na Usimamizi na Ufuatiliaji wa Watoa Huduma za Bima*

Mapungufu katika usimamizi wa watoa huduma za bima umesababisha unufaikaji wa bima (insurance uptake) kwa watu wanaoripoti kuwa wamekata bima, kupungua kutoka asilimia 15 mwaka 2017 hadi asilimia 10 mwaka 2023, sawa na upungufu wa kawaida wa watu milioni 0.7, kama ilivyooneshwa katika Ripoti ya Finscope ya mwaka 2023. Hii inamaanisha kuwa usimamizi na ufuatiliaji wa huduma za bima nchini zinazohusisha maisha na zisizo za maisha zinahitaji juhudi zaidi kutekelezwa na serikali.

Hali hii imeathiri hatua muhimu za serikali katika kuimarisha huduma za bima ambayo zinalenga kuhakikisha asilimia 18 ya watu wazima wanatumia huduma za bima chini ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Aidha iliathiri lengo la serikali la kuhakikisha asilimia 50 ya watu wazima wanapata na kutumia bidhaa za bima ifikapo mwaka 2030 chini ya Mipango Kabambe ya Maendeleo ya Sekta ya Fedha kuanzia mwaka 2020/21 hadi 2029/30.

Kutokuwapo kwa Sera ya Bima ya Kitaifa ilikuwa sababu kuu ya ongezeko kidogo la ukataji wa bima mpya na wawekezaji wapya katika tasnia ya bima nchini. Hii ilisababisha kutofikiwa kwa malengo ya usajili wa watoa huduma wapya kutoa huduma za bima. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha 2020/21, 2021/22 na 2022/23, watoa huduma wapya waliosajiliwa walikuwa asilimia 68, asilimia 39 na asilimia 63 ya malengo yaliyowekwa, mtawalia. Hatimaye, Lengo Na. 8 la

Mpango wa Maendeleo Endelevu chini ya Shabaha Na, 8.10 ambalo linaitaka Serikali kuimarisha uwezo wa taasisi za fedha za ndani ili kuhimiza na kupanua upatikanaji wa huduma za benki, bima na fedha kwa wote halikuweza kufikiwa.

***Athari katika Usimamizi wa Urejeshaji wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu***

Mapungufu yaliyoonekana katika Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwenye eneo la usimamizi na ukusanyaji wa marejesho ya mikopo kutoka kwa wanufaika, yamesababisha ongezeko la mikopo iliyochelewa kwa muda wa zaidi ya miaka kumi kutoka shilingi bilioni 6.7 mwaka 2014/15 hadi shilingi bilioni 110 mwaka 2022/23. Hali hii ilichangiwa hasa na kutofuatilia kwa urejeshaji wa mikopo ilivyopaswa kufanywa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini.

Mapungufu katika urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu unaweza kudhoofisha lengo la serikali la kuhakikisha wanafunzi wa elimu ya juu na elimu ya kati wanaopata mikopo wanaongezeka kutoka asilimia 60 kwa mwaka 2019/20 hadi asilimia 90 kwa mwaka 2025/26 kama ilivyolengwa chini ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano.

## USIMAMIZI WA MALIASILI



### 8.1 Utangulizi

Sura hii inatoa matokeo ya ukaguzi yaliyotokana na ripoti za ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi wa fukwe, uwezesaji wa wachimbaji wadogo wa madini, na usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Vilevile, sura hii inatoa maelezo juu ya maeneo yaliyokaguliwa, taasisi za Serikali zilizohusika, uhusiano wa kaguzi hizi na athari za matokeo yake katika Malengo ya Maendeleo Endelevu pamoja na Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano:

Kaguzi hizi za ufanisi ni pamoja na:

- (a) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Fukwe;
- (b) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Uwezesaji wa Wachimbaji Wadogo wa Madini; na
- (c) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi.

#### 8.1.1 Usuli wa Usimamizi wa Maliasili

Tanzania imejaliwa rasilimali nyingi za asili ikiwemo fukwe za kuvutia, madini na rasilimali za uvuvi katika maziwa na Bahari ya Hindi.

Fukwe zina umuhimu mkubwa katika maisha ya binadamu, ikiwa pamoja na vivutio vya utalii na kutumika na wenyeji na wageni kama maeneo ya kupumzika na kupata burudani. Utalii kwa sasa ni miongoni mwa sekta zinazoongoza kwa uchumi nchini Tanzania, ikichangia asilimia 17 ya Pato la Taifa na asilimia 25 ya mapato ya kigeni. Pia, katika mwaka 2021 sekta hii ilichangia takribani asilimia 5.3 ya ajira zote nchini. Hata hivyo, sekta hii inakabiliwa na changamoto kama vile kukosekana kwa mpango endelevu wa maendeleo na uwekezaji katika

maeneo ya pwani pamoja na fukwe kutokutumika vya kutosha kwa ajili ya shughuli za utalii.

Uchimbaji wa madini unafanywa zaidi na wachimbaji wadogo nchini Tanzania, ambapo zaidi ya watu milioni 1.2, sawa na asilimia 90 ya nguvu kazi ya uchimbaji madini nchini wanajihusisha na uchimbaji mdogo. Hata hivyo, sekta hii ndogo inakumbwa na changamoto mbalimbali zikiwemo ujuzi mdogo na taarifa finyu za kijiolojia na uwapo wa mashapo; ukosefu wa teknolojia sahihi za uchimbaji na uchenjuaji wa madini; ukosefu wa mitaji; pamoja na ukosefu wa mafunzo sahihi kwa ajili ya kuendeleza sekta hii ndogo.

Zaidi ya hayo, sekta ya uvuvi nchini Tanzania imekuwa ikikua kwa wastani wa asilimia 1.5 kwa mwaka na ina jukumu muhimu la kijamii na kiuchumi katika usalama wa chakula na ustawi wa kijamii na kiuchumi. Matumizi ya sasa ya samaki kwa kila mtu ni kilo 8.5 na samaki wanachangia asilimia 30 ya ulaji wa protini ya wanyama kila siku. Pia sekta hii inachangia asilimia 1.7 ya Pato la Taifa na kutoa ajira za moja kwa moja kwa wavuvi 195,435 na wafugaji wa samaki 30,064. Hata hivyo, sekta hii inakabiliwa na changamoto kadhaa, ambazo ni huduma ndogo za ugani, upatikanaji mdogo wa fedha, upotevu wa mazao ya samaki baada ya mavuno, uongezaji mdogo wa thamani ya mazao ya samaki pamoja na upatikanaji mdogo wa teknolojia sahihi za uvuvi na ufugaji wa samaki.

### 8.1.2 Uhusiano kati ya Usimamizi wa Maliasili, Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

Sehemu hii inatoa maelezo juu ya usimamizi wa maliasili kama inavyohusiana na Malengo ya Maendeleo Endelevu pamoja na Mpango wa Pili na wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano kama inavyoelezwa hapa chini:

#### (a) Uhusiano kati ya Usimamizi wa Maliasili na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Ili kushughulikia masuala yanayohusiana na usimamizi wa maliasili nchini, kaguzi za ufanisi tatu zilifanyika katika masuala ya usimamizi wa fukwe, madini na rasilimali za uvuvi. Uhusiano wa kaguzi hizi na Malengo ya Maendeleo Endelevu umeelezwa hapa chini:

Ukaguzi wa Utendaji wa Usimamizi wa Fukwe unahusishwa moja kwa moja na Lengo namba 14 shabaha ya kwanza, pili na ya saba kati ya Malengo ya Maendeleo Ebdelevu 17 ya Umoja wa Mataifa. Shabaha ya 14.1 na 14.2 zinalenga kuzuia na kupunguza kwa kiasi kikubwa uchafuzi wa mazingira ya baharini,

hususa shughuli za ardhini na kuhifadhi angalau asilimia 10ya maeneo ya pwani na baharini, kwa kuzingatia sheria za kitaifa na kimataifa na kwa kuzingatia taarifa bora zaidi za kisayansi zinazopatikana katika nchi zote ifikapo mwaka 2030. -Shabaha14.7 inalenga kuongeza faida za kiuchumi kutokana na matumizi endelevu ya rasilimali za baharini, ikiwa pamoja na utalii. Kwa hivyo, kuwa na usimamizi wa fukwe mzuri kutaimarisha mipango ya serikali ya kufikia Lengo la 14.1, 14.2 na 14.7.

Ukaguzi wa Ufanisi katika Uwezeshaji wa Wachimbaji Wadogo wa Madini nchini unahusishwa na lengo la Maendeleo Endelevu Na. 8, ambayo linalenga kukuza uchumi jumuishi na endelevu pamoja na ajira nzuri na zenye tija kwa wanawake na wanaume wote ifikapo 2030. Pia lengo la Maendeleo Endelevu Na. 1 linalenga kutokomeza umaskini katika aina zake zote kila mahali.

Aidha, Ukaguzi wa Utendaji wa Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi unahusiana na lengo namba 14, shabaha ya 4 na 6 ya Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa, ambayo yanalenga uhifadhi na matumizi endelevu ya bahari, na rasilimali za baharini kwa maendeleo uendelevu. Hasa, lengo linasisitiza kudhibiti ipasavyo, uvunaji na kukomesha uvuvi wa kupita kiasi na makosa mengine ya uvuvi ili kurejesha akiba ya samaki na kupiga marufuku aina fulani za ruzuku za uvuvi zinazochangia kuzidisha uwezo na uvuvi wa kupita kiasi.

**(b) Uhusiano kati ya Usimamizi wa Maliasili na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano**

Uhusiano wa Ukaguzi wa Ufanisi katika usimamizi wa maliasili na Mpango wa Pili na Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano umeelezwa katika **Jedwali Na. 43** hapa chini:

**Jedwali Na. 43: Uhusiano wa Usimamizi wa Maliasili na Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano**

Jina la Ukaguzi	Development Plan	Eneo/Sekta	Hatua za Kuchukua
Usimamizi wa Fukwe	Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano	Utalii	Kuboresha mazingira wezeshi ya sekta ya utalii, kuwa na bidhaa mbalimbali za kitalii sambamba na utambuzi wa maeneo mapya ya kitalii
	Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano	Utalii	Kuwezesha uandaaji wa bidhaa mbalimbali za kitalii ili kuchochea maendeleo endelevu
		Uchumi wa Bluu	Kuimarisha uratibu wa miundombinu ya utafiti, uwekezaji, uzalishaji,

Jina la Ukaguzi	Development Plan	Eneo/Sekta	Hatua za Kuchukua
			uhifadhi, utalii, na huduma za usafiri wa baharini
Uwezeshaji wa Wachimbaji Wadogo wa Madini nchini	Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano	Madini	Uchenjuaji na uongezaji dhamani wa madini Mafunzo na uendelezaji wa ujuzi
		Uchimbaji wa Madini	Kuwajengea uwezo wachimbaji wadogo wakiwemo vijana na wanawake ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli za uchimbaji madini Kuwezesha uongezaji dhamani na uchenjuaji wa madini Kuimarisha Shirika la Madini la Taifa, Masoko ya Madini pamoja na Vituo vya vya Mfano Uchimbaji na Uchenjuaji wa Madini
	Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano	Kilimo	Uboreshaji wa shughuli za utafiti na mafunzo katika sekta ndogo ya uvuvi Kuimarisha udhibiti wa rasilimali za uvuvi na biashara za uvuvi baharini na nchi kavu kwa kuzingatia usimamizi bora wa mazingira
			Kuhifadhi maeneo tengefu ya uvuvi Kuhakikisha upatikanaji wa mitaji, utaalamu, ujuzi, maarifa na vifaa vya uvuvi kwa wavuvi Kuimarisha uwezo wa taasisi za uvuvi

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kwenye Mpango wa Pili na Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2024*

### 8.1.3 Mikakati na Jitihada za Serikali katika Usimamizi wa Maliasili

Ili kuhakikisha matumizi bora ya maliasili, Serikali kupitia Wizara husika imeweka mikakati ya kuhakikisha usimamizi mzuri wa maliasili. **Kielelezo Na. 35** kinaonesha maelezo zaidi.

**Kielelezo Na. 35: Hali ya Utambuzi wa Wanufaika wa Mikopo ya Elimu ya Juu ili Kuwezesha Urejeshaji**

Usimamizi wa Fukwe	Uwezesaji wa Wachimbaji Wadogo wa	Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi
<ul style="list-style-type: none"> <li>• Utambuzi wa maeneo yenye fukwe kwa mwaka 2016 na 2021</li> <li>• Uandaaji wa mikakati kama vile ushindi wa haraka kwa mwaka 2019</li> <li>• Uandaaji wa mkakati wa Masoko na Uendelezaji wa Kusini mwa Tanzania 2021-2026</li> <li>• Uandaaji wa Mpango Mkakati kwa Mwaka 2021/22- 2025/26</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Uandaaji wa Mkakati wa Uendelezaji na Uwezesaji wa Sekta Ndogo ya Madini mwaka 2019</li> <li>• Uanzishwaji wa Vituo vya Mfano vya Uchimbaji na Uchenjuaji wa Madini</li> <li>• Ununuzi wa Mashine ya Uchorongaji kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa madini</li> <li>• Uanzishwaji wa Masoko ya madini</li> <li>• Utoaji wa mafunzo mbalimbali kwa wachimbaji wa madini</li> <li>• Utoaji wa mafunzo katika taasisi za kifedha</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Uandaaji wa Mpango Mkakati wa Uvuvi (2020/21-2025/26)</li> <li>• Uandaji wa Miongozo ya vitengo vya usimamizi wa fukwe (2017)</li> <li>• Kuimarisha ukuaji wa sekta ya uvuvi</li> <li>• kuzuia ongezeko la matumizi ya vifaa haramu vya uvuvi na kuendeleza ufugaji wa samaki</li> </ul>

**8.2 Malengo na Mawanda ya Ukaguzi**

**8.2.1 Malengo ya Ukaguzi**

Lengo kuu la ukaguzi lilikuwa kutathmini kama Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Madini na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zimesimamia ipasavyo maliasili kama inavyohusiana na utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Malengo mahsusi yalikua ni kutathmini iwapo:

- (i) Wizara ya Maliasili na Utalii, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Kitengo cha Hifadhi na Maeneo Tengefu ya Bahari zimesimamia fukwe ipasavyo ili kutunza mazingira na kuongeza shughuli za kitalii kupitia fukwe hizo;



- (ii) Wizara ya Madini kupitia Shirika la Madini la Taifa pamoja na Tume ya Madini imewawezesha ipasavyo wachimbaji wadogo wa madini ili kuwezesha ukuaji wa sekta ndogo ya madini nchini; na
- (iii) Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) zimeteteleza kikamilifu njia mbalimbali za udhibiti ili kuwezesha uvuvi endelevu nchini.

### 8.2.2 Mawanda ya Ukaguzi

Ukaguzi katika usimamizi wa fukwe ulihusisha Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Maliasili na Utalii na Kitengo cha Hifadhi na Maeneo Tengefu ya Bahari. Ukaguzi huu ulijikita kwenye Ufanisi wa uendelezaji wa fukwe ili kuongeza shughuli za kitalii, utunzaji wa mazingira katika maeneo ya fukwe, ukuzaji na utafutaji wa soko la utalii kupitia fukwe na utendaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika ufuatiliaji wa fukwe. Ukaguzi huu uliangalia taarifa za kipindi cha miaka minne ya fedha kuanzia 2019/20 hadi 2022/23.

Ukaguzi katika uwezesaji wa wachimbaji wadogo wa madini nchini ulihusisha Wizara ya Madini, Shirika la la Madini la Taifa na Tume ya Madini. Lengo la ukaguzi lilikuwa kutathmini utoshelevu katika uwezesaji wa wachimbaji wadogo wa madini nchini kwa kuangalia, matumizi ya rasilimali, uratibu na ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa shughuli za wachimbaji wadogo wa madini. Tathmini ya vipengele hivi ilifanywa kwa miaka mitano ya fedha, kuanzia 2018/19 hadi 2022/23.

#### ***Mawanda ya Ukaguzi katika Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi***

Ukaguzi wa usimamizi wa rasilimali za uvuvi ulijumuisha Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Ukaguzi huo ulilenga katika kutathmini uandaaji na utekelezaji wa hatua za udhibiti na ufuatiliaji; ukamilifu, utoshelevu, na uhuishaji wa kanzidata; pamoja na mpango wa ukaguzi wa ubora wa samaki na namna ya kutoa adhabu mbalimbali; na utoshelevu wa uratibu wa wadau katika usimamizi wa shughuli za uvuvi. Tathmini hii ilifanyika kwa kulenga taarifa za miaka mitano ya fedha, kuanzia 2018/19 hadi 2022/23.

### 8.3 Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Usimamizi wa Fukwe

Tanzania inakadiliwa kuwa na kilomita 1424 za ukanda wa fukwe. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa hadi Oktoba 2023, fukwe 71 kati ya 79 (sawa na asilimia 89) ya maeneo ya fukwe yaliyotambuliwa nchini bado hayajaendelezwa na kutumika kwa ajili ya shughuli za kitalii. Badala yake, maeneo hayo yalitumika kwa madhumuni mengine, kama vile kilimo (wakulima wadogo wa korosho na nazi), ufugaji wa mifugo, shughuli za uvunaji wa chumvi, n.k.

Pamoja na kubaini maeneo ya fukwe kuwa na sifa nzuri kwa utalii wa fukwe, kama vile kuogelea, kupiga mbizi, michezo ya kwenye maji, na uoteaji wa jua. Hata hivyo, fukwe hizo zilikosa sifa za kusaidia shughuli muhimu kwa ajili ya kufanya fukwe eneo muhimu kwa ajili ya kupumzika na kustarehe kwa ajili ya utalii.

Matumizi madogo ya maeneo ya fukwe kwa ajili ya utalii kuliikosesha serikali kupata mapato yatokanayo na utalii wa fukwe. Uchambuzi wa mapato kutoka kwenye fukwe zilizotembelewa ulionesha ukusanyaji wa mapato kutoka kwenye fukwe haukuongezeka kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, fukwe 2 kati ya 5 zilizopo ya maeneo ya hifadhi za bahari, ambazo ni Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma na Hifadhi ya bahari ya Tanga Silikanti, mapato yaliyokusanywa yalibainika kupungua kutoka shilingi 7,165,204 na shilingi 30,964,023 mwaka 2019/20 hadi shilingi 5,765,810 na shilingi 24,506,556 kwa mwaka 2022/23 mtawalia. Wakati huohuo, fukwe ya Thanda katika ukusanyaji wa mapato ya Hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Mafia iliongezeka kutoka shilingi 801,148,614 mwaka 2029/20 hadi shilingi 1,182,593,303 mwaka 2022/23 baada ya kuendelezwa.

Ukaguzi ulibaini matumizi yasiyo na ufanisi wa fukwe zinazopatikana nchini ambao ulisababishwa na:

#### 8.3.1 Mikakati ya Wizara ya Maliasili na Utalii, Mamlaka za Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hazikuwezesha Maendeleo ya Fukwe kwa Utoshelevu

Ukaguzi ulibaini mapungufu kadhaa katika usimamizi na uendelezaji wa fukwe ndani ya Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii ilikuwa ikifanya kazi kwa kutumia mpango kabambe wa utalii uliopitwa na wakati kutoka mwaka 2002,

ambao uliandaliwa zaidi ya miongo miwili iliyopita. Mpango huu uliopitwa na wakati unashindwa kushughulikia mahitaji ya sasa, hasa maeneo yanayohitaji uwekezaji ili kusaidia mikakati ya kisasa na mipango ya usimamizi wa fukwe. Pia, licha ya kuwa na Mkakati wa Mafanikio wa Haraka wa mwaka 2019, Wizara ya Maliasili na Utalii haikujumuisha mapendekezo yake katika mpango wa mwaka wa utekelezaji. Kwa mfano, mapendekezo kama vile kuanzisha taasisi inayohusika na usimamizi wa fukwe na maendeleo hayakuwapo katika Mipango yote minne ya utekelezaji kutoka mwaka wa 2019/20 hadi mwaka 2022/23.

Vivyo hivyo, mikakati ya Wizara ya Maliasili na Utalii ya kuutangaza utalii wa fukwe haijitosheshezi. Wakati Bodi ya Utalii Tanzania inapaswa kuendana na mabadiliko ya teknolojia hasa mikakati ya masoko na uendelezaji wa rasilimali watu, ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya wateja na mapendeleo ya wateja, ukaguzi ulibaini kuwa mikakati ya Bodi ya Utalii Tanzania ya kutangaza utalii ulijikita zaidi kwa wanyama pori na utalii wa utamaduni na utalii wa fukwe ulipewa nafasi kidogo.

Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa haikuwa na mipango maalumu ya usimamizi wa fukwe nchini, hii inamaanisha kuwa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa haikuweka kipaumbele katika kuendeleza fukwe kama sehemu ya majukumu yake, licha ya kuwa fukwe nyingi ziko chini ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupitia Serikali za Mitaa ambayo ni Mamlaka ya Upangaji.

Kwa upande wa Mamlaka ya Uhifadhi wa Bahari, ukaguzi ulibaini kuwa pia kulikuwa na upungufu katika mikakati na mipango ya kuwezesha maendeleo ya fukwe. Kwa kipindi cha ukaguzi kuanzia mwaka 2019/20 - 2022/23, Ukaguzi ulibaini kuwa Kitengo cha Uhifadhi wa Bahari na Maeneo Tengefu kilikosa Mpango mkakati. Pia, kulikuwa na ukosefu wa mipango ya usimamizi ya jumla katika mamlaka za hifadhi za bahari mbili kati ya tano zilizotembelewa, wakati tatu kati ya tano zilikosa Mipango ya Usimamizi Mkuu iliyohuishwa.


Upungufu ulioonekana ulihusishwa na kutokuwapo kwa muda uliopangwa na bajeti ya kutekeleza mikakati. Kwa hiyo, haikuwa rahisi kupima utendaji wa utekelezaji wa mkakati uliowekwa.

### 8.3.2 Utekelezaji usioridhisha wa Mikakati na Mipango ili Kuwezesha Uendelezaji wa Fukwe

Ukaguzi ulibaini kuwa asilimia 80 ya mikakati iliyopangwa na Wizara ya Maliasili na Utalii katika Mkakati wa Mafanikio wa Haraka wa mwaka 2019

hazikutekelezwa, wakati asilimia 60 ya hatua katika Mpangomkakati wa Maliasili na Utalii wa 2021/22-2025/26 hazikutekelezwa (Rejea Kielelezo Na. 36).

**Kielelezo Na. 36: Utekelezaji wa Mikakati ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2022/23**



**Chazo:** Mipango Mikakati na Taarifa za Utekelezaji za Wizara ya Maliasili na Utalii kuanzia mwaka 2020/21 mpaka 2022/23

**Kielelezo Na. 36** kinaonesha kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii haikutekeleza kikamilifu mipango iliyopangwa. Asilimia 80 ya mikakati iliyopangwa katika Mkakati wa Mafanikio wa Haraka wa mwaka 2019 na asilimia 60 ya mikakati katika Mpango mkakati wa Wizara ya Maliasili na utalii haikutekelezwa. Mikakati iliyopangwa ambayo haikutekelezwa katika Mkakati wa Mafanikio wa Haraka wa mwaka 2019 ni pamoja na kuanzisha au kuteua taasisi itayohusika na usimamizi wa jumla wa fukwe na kuipa nguvu Mamlaka ya Maeneo Maalumu ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje kwa ajili ya kuendeleza ukanda wa pwani (fukwe). Pia, mikakati ambayo haijatekelezwa kwenye Mpango Mkakati wa Wizara ya Maliasili na Utalii ni pamoja na kuanzisha kituo cha Mikutano, Maonesho na vivutio kitakachojengwa maeneo ya fukwe na kuanzishwa kwa meli za utalii wa bahari ambavyo vilipangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2022/23.

Changamoto zilizobainishwa zilisababishwa na ukosefu wa fedha za kutekeleza shughuli hiyo. Matokeo yake mikakati iliyopangwa haikutekelezwa. Mfano kutotekelezwa kwa mikakati ya Wizara ya Maliasili na Utalii wa kuanzisha kwa kituo cha mikutano, maonyesho na vivutio kulisababishwa na kutokutolewa kwa fedha iliyotengwa kiasi cha shilingi milioni 658.

### 8.3.3 Kutozingatia Mahitaji Muhimu ya Usimamizi wa Mazingira

Ukaguzi ulibaini kuwa asilimia 82 ya fukwe zilizotembelewa katika Serikali za Mitaa hazikuzingatia masuala ya mazingira, asilimia 25 ya fukwe za kibinafsi zilizotembelewa hazikuzingatia masuala ya mazingira, na asilimis 100 ya fukwe zilizotembelewa zilizo chini ya serikali hazikuzingatia masuala ya mazingira. Maeneo ambayo hayakuzingatiwa yalikuwa katika vyoo na uondoshaji wa maji taka na kutodhibiti shughuli za kibinadamu na kutokufanya ukaguzi wa kimazingira. Sababu za kutozingatia masuala ya mazingira yameelezwa kwa kina katika **Jedwali Na. 44**.

**Jedwali Na. 44: Sababu za Kutozingatia Mahitaji ya Mazingira**

Sababu za Jumla za kutozingatia mahitaji ya mazingira	Idadi ya Fukwe zenye tatizo hili	Idadi ya Halmashauri zinazokabiliwa na tatizo hili
Usimamizi wa Sheria usiyojitoshereza	9	4
Ufuatiliaji usiyojitoshesheza	11	4
Kukosekana kwa uhamasishaji wa Jamii juu ya mazingira	2	2
Fukwe kutokupewa kipaumbele	1	1

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa kutoka Halmashauri zilizotembelewa, 2023*

**Jedwali Na. 44** linaonesha sababu mbalimbali za kutokufuata matakwa ya mazingira katika Halmashauri zilizotembelewa. Hizi ni pamoja na usimamizi wa Sheria usiyojitoshesheza na ufuatiliaji usiojitoshesheza na kukosekana kwa uhamasishaji wa mambo ya mazingira katika jamii.

Kutozingatiwa kwa masuala ya mahitaji ya ulinzi wa mazingira kulichangiwa na kutotekelezwa ipasavyo na vyombo vinavyohusika, ambavyo ni Kitengo cha Uhifadhi wa Bahari na Maeneo Tengefu, OR-TAMISEMI, na Wizara ya Maliasili na Utalii, jambo ambalo liliruhusu shughuli za kibinadamu zilizoathiri mazingira. Zaidi ya hayo, hakukuwa na ufuatiliaji wa kutosha wa vyombo vyote vitatu ili kuhakikisha utiifu wa masuala ya ulinzi wa mazingira. Aidha, usimamizi wa fukwe haukupewa kipaumbele kwa sababu Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo inahusika na utalii haikuwa na takwimu za wageni wa utalii wa fukwe na mchango wa utalii wa fukwe, jambo ambalo lilichangia kwa kiasi kikubwa kutokuwapo kwa ufanisi katika kusimamia fukwe.

Matokeo yake, shughuli zinazoendelea za binadamu ziliwezesha uharibifu wa mazingira, kama vile kukata miti ya mikoko na kuchimba mchanga wa matumbawe kando ya maeneo ya fukwe. Aidha, hatua kali za kudhibiti masuala ya mazingira hazikuwapo kutokana na kushindwa kufanya tathmini ya athari za

mazingira ya uendelezaji mbalimbali unaofanyika katika maeneo ya fukwe. Hii ilisababisha uharibifu wa makazi ya asili ya viumbe hai, ikiwa pamoja na maeneo ya kuzaliana viumbe hai katika maeneo ya fukwe/pwani.

### 8.3.4 Mikakati Isiyojitoshesheza ya Kutangaza Utalii wa Fukwe

Aidha, Mpango-mkakati Shirikishi wa 2017/18-2021/22 wa bodi ya Utalii Tanzania unaitaka bodi ya utalii kutekeleza Mkakati wa Kimataifa wa Masoko kwa kusisitiza matumizi ya mbinu za kisasa za masoko ya kidijitali, ikiwa pamoja na masoko ya mtandaoni.

Ukaguzi ulibaini kuwa Bodi ya Utalii Tanzania imetengeneza mikakati mitano ya kutangaza utalii. Lakini mikakati hiyo, haikulenga moja kwa moja katika kutangaza fukwe, kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 45.

**Jedwali Na. 45: Mikakati ya Bodi ya Utalii Tanzania ilivyo Husisha utangazaji wa Fukwe**

Jina la mikakati	Mambo yaliyohusihwa na Mkakati	Maoni ya Ukaguzi
Mkakati wa kuitangaza Tanzania Kusini wa mwaka 2021-2026	Ulihusisha kwa ujumla wake utangazaji wa bidhaa za utalii. Ulikuwa umejikita katika kutangaza utalii kwa njia ya kidijitali na mitandao ya kijamii kwa kutengeneza kipande cha video chenye mandhari mbalimbali zilizochukuliwa katika; Hifadhi ya Taifa ya Mikumi, Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa	Masuala ya fukwe hayakuingizwa sana kwa sababu Mkakati wa utangazaji na uendelezaji wa kusini mwa Tanzania 2021-2026 uliandaliwa chini ya mradi wa Usimamizi wa Maliasili na Ukuaji wa Utalii ujulikanao kama REGROW kama mkakati wa kuitangaza na kuiendeleza kusini. Mkakati huu una malengo ya muda mfupi na kati hadi mwaka 2026.
Mkakati wa Kimataifa wa Utangazaji na Kufanya Tanzania kuwa Kituo cha Utalii 2020 - 2025	Mkakati ulijika katika kutangaza utalii kwa ujumla wake bila kutaja bidhaa ya utalii inayokusudiwa kutangaza.	Mkakati huu hauna malengo ya muda mfupi wala ya kati. Malengo yote yanapaswa kufikiwa mwaka 2025, lakini sio maalumu kwaajili ya fukwe tu.
Mkakati wa kutangaza Utalii wa Ndani wa mwaka 2018 - 2023	Mkakati ulijikita katika kutangaza utalii wa jumla wa ndani, Fukwe zikiwa	Mkakati huo hauna malengo ya muda mfupi wala kati. Malengo yote yanapaswa

Jina la mikakati	Mambo yaliyohusihwa na Mkakati	Maoni ya Ukaguzi
	miongoni mwa bidha za kutangazwa.	kufikiwa ifikapo mwaka 2023.
Mkakati wa Kutangaza Utalii wa Utamaduni Tanzania, Mei 2021	Haikujikita katika masuala ya fukwe. Ilijikita zaidi katika kutangaza utamaduni.	Mkakati umejikita zaidi katika suala la utalii wa utamaduni. Mkakati hauna masuala yanayohusiana na fukwe.
Mkakati wa Kutumia Teknolojia ya “Bar Codes” kukiwa na vivutio mbalimbali vya utalii	Ulijikita katika kuanda video fupi zinazo oneshwa vivutio mbalimbali vya utalii nchini ikiwa pamoja na utalii wa fukwe.	Ulijikita katika vivutio mbalimbali vya utalii ikiwa pamoja na utalii wa fukwe.

*Chanzo: Mipango mikakatii ya Bodi ya Utalii Tanzania kuanzia mwaka 2020 hadi 2026..*

**Jedwali Na. 45** linaonesha mkakati mmoja kati ya mitano iliyosomwa na wakaguzi ilijikita katika kutangaza utalii wa fukwe kwa kutumia teknolojia ya “Bar Code”. Kwa kutumia teknolojia ya “Bar Code”, watumiaji au wateja wa utalii wapatapo hiyo “bar code” huunganishwa moja kwa moja na klipu fupi za video zenye bidhaa za utalii na fukwe ikiwa miongoni. Mikakati mingine minne haikulenga moja kwa moja kukuza utalii wa fukwe, kama ilivyoelezewa katika **Jedwali Na. 45**.

### 8.3.5 Utekelezaji Usiojitosheleza wa Mipango iliyopo ya Kutangaza Utalii wa Fukwe

Kwa kipindi cha mwaka 2020/21 na 2021/22, shughuli zote zilizopangwa kwenye maendeleo ya utalii wa fukwe na utalii wa meli na kuimarisha utangazaji wa bidhaa mpya za utalii hazikutekelezwa. Vilevile, kwa mwaka wa fedha 2020/21, fedha kwaajili ya kutekeleza shughuli za utalii wa fukwe hazikutolewa. Sababu ya kutotekelezwa kwa shughuli zilizopangwa ilikuwa mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19.

Utekelezaji usiojitosheleza wa mipango ya kutangaza utalii wa fukwe kumechangia kutofikia lengo la kuongeza idadi ya watalii nchini na lengo la kuwa na vivutio mbalimbali vya utalii.

### 8.3.6 Uratibu usiojitosheleza katika Kutangaza Utalii wa Fukwe

Ukaguzi huo kupitia mahojiano na Maofisa wa Bodi ya Utalii Tanzania umebaini kuwa uratibu unafanyika kati ya Kitengo cha Uhifadhi wa Bahari na maeneo Tengefu na Bodi ya Utalii pale wanapokuwa na tukio maalumu. Hata hivyo, hakukuwa na nyaraka zozote kuthibitisha kufanyika kwa uratibu huo. Pia,

hakukuwa na utaratibu na uratibu uliopangwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hii ni kwa sababu kila taasisi inafanya kazi kwa kujitegemea na haina ushirikiano wa wowote katika kutangaza utalii wa fukwe.

Uratibu usiyojitosheleza katika kukuza na kutangaza fukwe nchini ulisababishwa na mikakati na mipango isiyojitosheleza ya kutangaza utalii wa fukwe pamoja na kutokuwa na kipaumbele katika kutangaza utalii wa fukwe ikilinganishwa na bidhaa nyingine za utalii. Kwa hiyo, ongezeko la mapato kutokana na bidhaa za utalii wa fukwe haijaweza kufikiwa.

### 8.3.7 Ufuatiliaji na Uratibu wa Shughuli za Fukwe Nchini Usiojitosheleza

#### (i) *Ufuatiliaji Usiyojitosheleza wa Fukwe na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*

Ukaguzi ulibaini kuwa, licha ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) kuwa na jukumu la kufuatilia kazi inayofanywa na Serikali za Mitaa, ikiwa pamoja na usimamizi wa fukwe, Wizara haikutekeleza jukumu lake la kufuatilia utendaji wa Serikali za Mitaa kikamilifu. Hii ni kwa sababu OR - TAMISEMI haikuwa na viashiria vya kutumia kufuatilia uendelezaji wa fukwe nchini. Mapitio ya mipango ya mwaka ya Idara ya Maendeleo ya Vijijini na Mjini haikuwa na mipango au mifumo ya ufuatiliaji wa fukwe. Idara ilijikita katika mambo ya utawala na haikuweka kipaumbele katika usimamizi wa fukwe.

Vilevile, OR-TAMISEMI ilikosa takwimu na taarifa kwa ajili ya kupima utendaji wa Serikali za Mitaa. Kama mwangalizi wa Serikali za Mitaa, OR-TAMISEMI ilikosa takwimu ambazo zingeweza kutumika kufanyia maamuzi mbalimbali ili kuboresha usimamizi wa fukwe, ili kuimalisha utalii wa fukwe, na kulinda makazi ya asili. Hii ilisababishwa na Serikali za Mitaa kutowasilisha ripoti za utendaji kwa OR - TAMISEMI kuhusu usimamizi wa fukwe nchini. Matokeo yake, OR - TAMISEMI haina taarifa kuhusu utalii wa fukwe. Hivyo OR - TAMISEMI haikuweza kupima utendaji wa Serikali za Mitaa kuhusu usimamizi wa fukwe nchini.

#### (ii) *Mikutano ya Bodi ya Robo Mwaka kwaajili ya Tathmini ya Utendaji wa Kitengo cha Uhifadhi wa Bahari na Maeneo Tengefu Haikufanyika Ipasavyo*

Bodi ya Wadhamini ya Kitengo cha Uhifadhi wa Bahari na Maeneo Tengefu inatakiwa kufuatilia utendaji wa Kitengo cha Uhifadhi wa Bahari na Maeneo Tengefu kila robo mwaka. Ukaguzi ulibaini kuwa kwa kipindi cha miaka mitatu,



kuanzia Julai 2020 hadi Juni 2023, Bodi ya Wadhamini ilikutana kutathmini utendaji kazi wa Kitengo cha Uhifadhi wa Bahari na Maeneo Tengefu katika robo mwaka 7 kati ya 12 zinazotakiwa katika kipindi cha miaka mitatu. Mahojiano na Maofisa kutoka Kitengo cha Uhifadhi wa Bahari na Maeneo Tengefu hawakutoa sababu za mikutano ya bodi kutokufanyika kama ilivyopangwa.

Hii imesababisha tathmini isiyojitosheleza ya utendaji wa Kitengo cha Uhifadhi wa Bahari na Maeneo Tengefu, na hivyo, kukosa maelekezo/usauri kutoka kwa Bodi juu ya utendaji wao katika robo mwaka tano.

***(iii) Usimamizi na Uratibu usiyojitosheleza kati ya Wizara***

Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa mwaka 2021/22 hadi 2025/26 unasisitiza uendelezaji wa bidhaa mpya za utalii na unalenga kuongeza mchango wa sekta ya utalii katika Pato la Taifa kutoka asilimia 6 hadi 11. Hata hivyo, kufikia malengo haya kunahitaji kuimarisha mifumo ya kitaasisi na kuimarisha uratibu miongoni mwa wadau husika wanaohusika katika huduma za utalii.

Licha ya umuhimu wa usimamizi wa fukwe kwa ajili ya maendeleo ya utalii, ukaguzi uliangazia utawala na uratibu usiyojitosheleza miongoni mwa wizara zinazohusika na usimamizi wa fukwe nchini Tanzania. Wadau hao ni Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa, Kitengo cha Uhifadhi wa Bahari na Maeneo Tengefu, Mamlaka ya Maeneo Maalumu ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje na Wizara ya Maliasili na Utalii wanahusika moja kwa moja katika usimamizi wa fukwe. Hata hivyo, hakuna chombo chochote kinachohusika na kuratibu usimamizi wa fukwe. Kila mdau hufanya kazi chini ya sheria tofauti bila kuunganishwa na sheria za wadau wengine, na hivyo kusababisha usimamizi wa fukwe kugawanyika katika taasisi mbalimbali za serikali.

Kwa mujibu wa ripoti ya kuboresha usimamizi wa fukwe nchini Tanzania ya mwaka 2020, baadhi ya sheria ambazo zipo ni pamoja na Sheria ya Utalii (Sura ya 364) inayotumiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii; Sheria ya Hifadhi wa Bahari na Maeneo Tengefu (Sura ya 146) inayotumiwa na Kitengo cha Uhifadhi wa Bahari na Maeneo Tengefu; Sheria ya Mipango miji (Sura ya 113) inayotumiwa na Serikali za Mitaa; Sheria ya Kanda Maalumu ya Kiuchumi (Sura ya 420 Iliyorekebishwa Mwaka 2012) inayotumiwa na Mamlaka ya Maeneo Maalumu ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje, na Sheria ya Bodi ya Utali (Sura ya 364) inayotumiwa na Bodi ya Utalii Tanzania. Kila taasisi ina mamlaka katika eneo lake bila kuwa na taasisi moja ya kuratibu shughuli za utalii.

Ukosefu wa uratibu umedhihirishwa na kukosekana kwa kufanyika mikutano /vikao vya wadau wa utalii wa fukwe na kupeana taarifa taarifa. Wizara ya

Maliasili na Utalii, kama Wizara mama, inakosa takwimu kamili juu ya shughuli za utalii wa fukwe, na takwimu za watalii na mapato kutoka utalii wa fukwe hazipo kwenye Takwimu za Wizara ya Maliasili na Utalii. Uhaba huu wa takwimu za kuaminika na kukosekana kwa uratibu kunaathiri sana utangazaji wa fukwe zilizoendelezwa kunakofanywa na Bodi ya Utalii Tanzania, na upatikanaji wa takwimu za mapato kutokana na utalii wa fukwe ambazo zimekuwa hazitolewi na Wizara ya Maliasili na Utalii.

#### 8.4 Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Uwezesaji wa Wachimbaji Wadogo wa Madini Nchini

Sehemu hii inaonesha matokeo ya ukaguzi katika uwezesaji wa wachimbaji wadogo wa madini kama ilivyoelezewa hapa chini:

##### 8.4.1 Wachimbaji wadogo wa madini hawakuwezeswa ipasavyo

Ukaguzi ulibaini kuwa wachimbaji wadogo hawakuwezeswa kama ilivyokusudiwa. Hii ilitokana na upatikanaji mdogo wa taarifa mbalimbali za kijiolojia na uwapo wa mashapo, ukosefu wa vifaa na teknolojia sahihi ya uchimbaji na uchenjuaji wa madini pamoja na upatikanaji mdogo wa mtaji wa kuendeshea shughuli za uchimbaji kama ilivyofafanuliwa hapa chini.

##### (a) Idadi ya Ndogo ya Wachimbaji Wadogo wa Madini walipata Taarifa za Kijiolojia na Uwapo wa Mashapo

Mapitio ya Taarifa za Leseni za Uchimbaji mdogo, Mipango Mikakati ya Shirika la Madini la Taifa, na ripoti za utendaji wa mwaka kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2022/23 zilibainisha kuwa wachimbaji wadogo hawakupata taarifa za kutosha za kijiolojia na uwapo wa mashapo. Hii ilithibitishwa na uwapo wa idadi ndogo ya wachimbaji wadogo waliopewa taarifa hizi kupitia Shirika la Madini la Taifa pamoja na Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania.

**Jedwali Na. 46** linatoa maelezo juu ya kiwango ambacho taarifa za kijiolojia na uwapo wa mashapo zilizotolewa kwa wachimbaji wadogo kila mwaka.

**Jedwali Na. 46: Hali ya Utoaji wa Taarifa za Jiolojia na Uwapo wa Mashapo kwa Wachimbaji Wadogo Nchini**

Mwaka wa Fedha	Idadi ya Leseni Ndogo Hai za Wachimbaji Wadogo	Idadi ya Wachimbaji waliopata taarifa za kijiolojia na uwapo wa mashapo <sup>16</sup>	Asilimia ya Waliopata
2018/19	1,885	600	32
2019/20	3,491	600	17
2020/21	4,915	200	4
2021/22	6,153	Hakuna Taarifa	-
2022/23	6,437	Hakuna Taarifa	-

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa za Utendaji za Mwaka za Shirika la Madini la Taifa, 2018/29 - 2022/23*

**Jedwali Na. 46** linaonesha kuwa idadi kubwa ya wachimbaji wadogo waliopata taarifa hizi ilionekana katika mwaka wa fedha 2018/19, ambapo asilimia 32 ya wachimbaji wadogo waliweza kuzipata. Mwenendo wa upatikanaji wa taarifa ulipungua kutoka asilimia 32 mwaka 2018/19 hadi asilimia 4 kwa mwaka 2020/21, na upatikanaji wa taarifa hizi ulikuwa chini ya asilimia 35 katika miaka yote iliyokaguliwa.

Hali hii ilisababishwa na mambo mbalimbali yakiwemo:

**(i) Uchunguzi wa Kijiolojia Usiojitosheleza**

Mapitio ya Ripoti ya Utendaji wa Mwaka kutoka Shirika la Madini la Taifa yalibaini kuwa kati ya Leseni 6000 zilizotolewa kwa ajili ya wachimbaji wadogo, Shirika la Madini la Taifa liliweza kufanya utafiti wa kijiolojia kwa ajili ya wachimbaji 41 tu katika mwaka wa fedha 2021/22. Utafiti huo ulifanyika katika maeneo ya Songea-Ruvuma (Makaa ya Mawe), Katoro-Geita (Dhahabu), Ubenazomozi-Dodoma (Dhahabu), na Kilindi-Tanga (Dhahabu). Maelezo zaidi ya utafiti huu yameainishwa katika **Jedwali Na. 47** hapa chini.

<sup>16</sup> Taarifa kutoka Wizarani, Shirika la Madini la Taifa na Tume ya Madini zilionesha aina tofauti za taarifa za kijiolojia kama vile aina za madini na njia ya kuchukua sampuli.

**Jedwali Na. 47: Utafiti wa Kijiolojia kwa ajili ya Wachimbaji Wadogo**

Aina ya Madini	Idadi ya Tafiti	Idadi ya Leseni zilizofanyiwa Utafiti
Makaa ya Mawe	2	34
Dhahabu	4	7
Almasi	0	0
Madini ya Viwandani	0	0

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Ripoti za Utafiti wa Kijiolojia zinazoandaliwa na Shirika la Madini la Taifa, 2023*

**Jedwali Na. 47** linaonesha kuwa utafiti ulifanyika kwa aina mbili tu za madini, yaani dhahabu na makaa ya mawe. Hakukuwa na utafiti wa aina nyingine za madini, hasa almasi na madini ya viwandani. Vilevile, utafiti ulifanyika kwa leseni saba za dhahabu na 34 za makaa ya mawe kati ya zaidi ya leseni 6000 zilizotolewa kwa wachimbaji wadogo.

Ukaguzi ulibaini kuwa, mapungufu haya yalitokana na sababu mbalimbali zikiwemo:

**(i) Gharama kubwa za Uendeshaji wa Mashine za Uchongaji kwa ajili ya Kufanyia Utafiti wa kijiolojia**

Ukaguzi ulibaini kuwa wachimbaji wadogo hawakuweza kulipia rigi kwa ajili ya kufanyia utafiti wa kijiolojia, kwani gharama ya kupeleka rigi eneo la kazi (kabla ya kuanza kazi) na kuirudisha ilikuwa takribani sh. milioni 30. Kiasi hiki ni kikubwa sana kikilinganishwa na kipato cha wachimbaji wadogo. Matokeo yake, wachimbaji walilazimika kufanya shughuli zao bila kuwa na taarifa sahihi za kijiolojia na uwapo wa mashapo.

Vilevile, ukaguzi ulibaini kwamba gharama za uchongaji wa matundu ya utafiti wa kijiolojia hazikuwa rafiki kwa wachimbaji wadogo, kwani zilianzia sh. 250,000 hadi sh. 400,000 kwa mita moja ya tundu.

**(ii) Upungufu wa Wajiolojia katika Shirika la Madini la Taifa**

Mapitio ya Ikama ya Shirika la Madini la Taifa ya mwaka 2022/23 yamebainisha kuwa Shirika hilo lilikuwa na wajiolojia 7 kati ya 16, sawa na asilimia 44 ya mahitaji. Aidha, ukaguzi ulibaini kutokuwapo kwa wajiolojia waliopangiwa majukumu ya moja kwa moja ya kuwasaidia wachimbaji wadogo wa madini; badala yake, wajiolojia waliokuwapo walipangiwa majumu ya Shirika kama vile uchongaji na uchimbaji kwa ajili ya Shirika la Madini la Taifa.

**(iii) Upungufu wa Vijaa vya Utafiti wa Kijiolojia kwa Ajili ya Wachimbaji Wadogo**

Ukaguzi ulibaini kuwa hakukuwa na idadi inayotosha ya mashine hizo za kufanyia utafiti kwani Shirika lilinunua mashine 5 kati ya 10 zilizotakiwa, hii ni sawa na 50% ya malengo. Hata hivyo idadi ya mashine zilizopangwa kununuliwa na ambazo zimeshanunuliwa haikidhi idadi na mahitaji ya wachimbaji wadogo nchini.


Ukosefu wa taarifa sahihi za kijiolojia ulipelekea ufanyaji kazi kwa kubahatisha na kutokua na uhakika. Hali hii inasababisha matumizi ya teknolojia za uchimbaji wa madini ambayo hazikidhi viwango, hivyo kupeleka kupungua kwa uzalishaji wa madini pamoja na kupunguza mapato ya Serikali.

**(b) Upatikanaji Usiotosheleza wa Vifaa vya Uchimbaji na Uchenjuaji wa Madini kwa Wachimbaji Wadogo**

Aya ya 4.4 ya Mpango-mkakati wa Shirika la Madini la Taifa 2017/16 - 2020/21 inasisitiza juu ya uwezesaji wa wachimbaji wadogo wa madini kwa kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya uchimbaji na uchenjuaji. Aidha, Shirika lina wajibu wa kusaidia maendeleo ya vituo vya mfano kwa ajili ya wachimbaji wadogo kwa ajili ya kuwezesha mafunzo kwa vitendo.

Mapitio ya Ripoti ya Utendaji wa Vituo vya Mfano kwa ajili ya wachimbaji wadogo kuanzia Julai 2021 hadi Juni 2022 yalibainisha kuwa ni asilimia 5 tu ya wachimbaji wadogo walipata teknolojia bora za uchimbaji na uchenjuaji wa madini kupitia vituo hivyo. Maelezo zaidi yametolewa katika **Kielelezo Na. 37** hapa chini.

**Kielelezo Na. 37: Upatikanaji wa Teknolojia Bora ya Uchimbaji na Uchenjuaji wa Madini kwa wachimbaji wadogo kupitia Vituo vya Mfano**



*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Ripoti ya Utendaji wa Vituo vya kwa ajili ya wachimbaji wadogo, 2022*

**Kielelezo Na. 37** kinaonesha idadi ndogo ya wachimbaji wadogo wa madini walipata huduma ya vifaa vya uchimbaji na uchenjuaji wa madini kupitia vituo vya mfano. Ilibainika kuwa wachimbaji wadogo 48 tu, sawa na asilimia moja ya leseni zote zilizotolewa mwaka 2021/22, walipata huduma za uchenjuaji. Sanjari na hilo, ni wachimbaji 233 tu, sawa na asilimia nne ya leseni zote zilizotolewa mwaka 2021/22, walipata huduma ya uchimbaji wa madini kupitia vituo hivyo.

Changamoto katika upatikanaji wa teknolojia ya uchimbaji na uchenjuaji wa madini kwa wachimbaji wadogo zilisanabishwa na:

**(i) Kutotosheleza kwa Vifaa vya Uchimbaji na Uchenjuaji wa Madini kwa ajili ya wachimbaji Wadogo**

Taarifa ya Utendaji wa vituo vya mfano iliyoandaliwa na Shirika la Madini la Taifa katika mwaka wa fedha 2021/22, ilionesha kuwa ni kituo kimoja tu (Katente katika Mkoa wa Geita) kati ya vituo vitatu vya mfano vilikuwa na vifaa vya uchimbaji kwa ajili ya kuwakodishia wachimbaji wadogo. Kituo hiki kilikua na vifaa 233 vilivyokodishwa kwa wachimbaji wadogo wawili tu, ambao ni kutoka Mgodhi Choo (Vifaa 50) na Mgodhi wa Nyakafuru (Vifaa 183).

**(ii) Utayari Mdogo wa Wachimbaji Wadogo wa Madini**

Ukaguzi ulibaini kuwa wachimbaji wadogo wengi hawakuwa tayari kupata teknolojia bora za uchimbaji na uchenjuaji wa madini. Hii ilitokana na ukosefu wa fedha za kutosha za kununua vifaa hivyo, kwani bei ya kuvinunua ni ghali, hivyo kuhitaji uwekezaji mkubwa kinyume na kipato cha wachimbaji.

**(iii) Umbali Mrefu wa Vituo vya Mfano kwa Ajili ya Wachimbaji Wadogo**

Ukaguzi ulibaini kuwa vituo vya mfano vilikua vichache na vilikua mbali na maeneo mengi ya uchimbaji mdogo wa madini. Kwa mfano, kituo cha mfano cha Lwamgasa mkoani Geita, kilikua mbali kwani kilihudumia wachimbaji kutoka maeneo ya Kahama, Kagera, na Ushirombo yaliyo umbali wa kilomita zaidi ya 100 kutoka kituo hicho.

Ripoti ya Kitaalam juu ya Mbinu Rafiki za Mazingira za Kuimarisha Uzalishaji wa Dhahabu katika Maeneo ya Wachimbaji wa Wadogo wa Madini iliyoandaliwa mwaka 2020 na Shirika la Madini la Taifa, ilibainisha kuwa matumizi duni ya vifaa bora vya uchimbaji na uchenjuaji wa madini, hupunguza uzalishaji wa madini. Kwa mfano, matumizi ya zebaki wakati wa uchenjuaji huzalisha takribani asilimia 15 hadi asilimia 30 ya kiwango cha dhahabu zilizopo kwenye mwamba. Hii inamaanisha kuwa zaidi ya asilimia 70 ya dhahabu inaweza kuachwa bila kuzalishwa kwa matumizi ya teknolojia duni ya uchenjuaji kama matumizi ya zebaki, na hivyo kupunguza uzalishaji wa madini.

**(c) Hakukuwa na Wachimbaji Wadogo wa Madini waliopata Mkopo ama Fedha za Ruzuku kutoka Serikalini**

Ukaguzi huo ulibaini kupitia Ripoti za Utendaji wa Mwaka kutoka Wizara ya Madini kuwa hakukuwa na wachimbaji wadogo waliopata mikopo ama ruzuku kutoka taasisi za fedha kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2022/23.

Ukaguzi ulibaini kuwa mambo yafuatayo yalichangia changamoto hii:

**(i) Ukosefu wa Vigezo kwa Wachimbaji Wadogo**

Vigezo vilivyowekwa kwa ajili ya kupata mikopo na ruzuku ni pamoja na umiliki wa leseni halali ya uchimbaji wa madini, nakala za cheti cha usajili wa kampuni, nakala za risiti za kila mwaka za malipo ya tozo mbalimbali za Serikali, mrabaha, namba ya utambulisho wa mlipakodi (TIN Namba) na kodi zilizolipwa ndani ya miezi sita. Wachimbaji wadogo pia walitakiwa kuwasilisha mipango ya usimamizi wa mazingira na ripoti za robo mwaka za uzalishaji wa madini kwa

miezi sita. Kwa namna hiyo, wachimbaji wadogo wengi hawakuweza kukidhi vigezo hivyo.

**(ii) Mafunzo ya Taasisi za Fedha Yasiyojitosheleza**

Ukaguzi ulibaini kutokuwapo kwa mafunzo yanayojitosheleza juu ya utoaji wa mikopo kwa wachimbaji wadogo katika taasisi za fedha. Katika miaka mitano ya fedha ya ukaguzi huu (2018/19 - 2022/23), taasisi moja tu ya kifedha (*KCB Bank*) ilipatiwa mafunzo. Taasisi nyingine tatu za fedha (*NMB, CRDB, AZANIA*) zilishiriki katika kongamano la uhamasishaji wa sekta ndogo ya madini lililoandaliwa na Shirika la Madini la Taifa kabla ya kusainiwa kwa hati ya makubaliano.

Upatikanaji wa mikopo na ruzuku usioridhisha umeathiri upatikanaji wa mtaji wa kutosha kwa wachimbaji wadogo. Hili lilithibitishwa na idadi ndogo ya leseni za uchimbaji mdogo wa madini zilizotolewa kuanzia 2018/19 hadi 2022/23 katika Ofisi za Maofisa Madini Wakazi zilizotembelewa. **Jedwali Na. 48** linaonesha hali iliyobainika wakati wa ukaguzi:

**Jedwali Na. 48: Idadi ya Leseni za Uchimbaji Mdogo Zilizotolewa dhidi ya Zinazofanya Kazi kuanzia 2018/19 hadi 2022/23**

Jina la Ofisi ya Afisa Madini Mkazi	Leseni Zilizotolewa	Leseni Zinazofanya Kazi	Asilimia ya Zinazofanya Kazi
Ruvuma - Makaa ya Mawe	3004	190	6
Lindi - Chumvi	348	104	30
Geita - Dhahabu	790	116	15
Shinyanga - Almasi	241	115	48
<b>Jumla</b>	<b>4383</b>	<b>525</b>	<b>12</b>

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Leseni za Uchimbaji Mdogo wa Madini kutoka Ofisi za Maofisa Madini Wakazi zilizotembelewa, 2023*

**Jedwali Na. 48** linaonesha kuwa idadi ya leseni zilizokuwa zinafanya kazi ilikuwa asilimia 12 ya jumla ya idadi ya leseni zote zilizotolewa. Asilimia ya chini ya leseni hizi ilikuwa katika madini ya makaa ya mawe katika mkoa wa Ruvuma, wakati asilimia kubwa ilikuwa katika madini ya almasi katika mkoa wa Shinyanga.

**8.4.2 Utengaji na Matumizi ya Rasilimali yasiyojitosheleza kwa ajili ya Kuwawezesha Wachimbaji Wadogo wa madini**

Ukaguzi ulibaini changamoto katika kuhakikisha utengaji na matumizi ya kutosha ya rasilimali kwa ajili ya kuwasaidia wachimbaji wadogo. Hii ilioneshwa



na kutotambuliwa na kuingizwa kikamilifu kwa mahitaji yao katika mipango na bajeti ya Wizara na taasisi zake, utengaji wa rasilimali usijitosheleza na ukosefu wa mipango ya kutathmini matumizi sahihi ya rasilimali zilizotengwa. Maelezo zaidi yametolewa hapa chini:

**(a) Utambuzi na Uhusishwaji wa Mahitaji ya Wachimbaji Wadogo Usiojitosheleza wakati wa Utengaji wa Rasilimali**

Ukaguzi ulibaini kuwa mahitaji na vipaumbele vya wachimbaji wadogo havikuhusishwa kikamilifu wakati wa maandalizi ya mipango na bajeti. Ilibainika kuwa Mpango Mkakati wa Wizara ya Madini ulipendekeza kutoa zana za uchimbaji zenye gharama nafuu kwa wachimbaji wadogo. Hata hivyo, hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza mpango huo. Ukaguzi pia ulibaini kuwa mpango huu haukuonekana katika Mipango ya Wizara ya Utekelezaji ya Mwaka, na haukuonekana kuwa moja ya vipaumbele vya Wizara.

Changamoto katika eneo hili ilichangiwa na mambo yafuatayo:

**(i) *Ukosefu wa Taarifa za Kutosha juu ya Wachimbaji Wadogo wa Madini***

Ukaguzi ulibaini ukosefu wa taarifa za kutosha za wachimbaji wadogo ambazo zingetumika wakati wa uandaaji wa mipango na bajeti. Hii ilithibitishwa na ukosefu wa kanzidata ya wachimbaji wadogo, hali hii ilisababisha ugumu katika kuainisha kwa ukamilifu mahitaji na changamoto za wachimbaji wadogo wakati wa utengaji wa rasilimali.

**(ii) *Mipango ya Kuwawezesha Wachimbaji Wadogo Haikushirikishwa Ipasavyo kwa Wadau***

Ukaguzi huo ulibaini kuwa kulikuwa na ushirikishwaji mdogo wa mipango ya kuhakikisha maendeleo ya wachimbaji wadogo. Kwa mfano, Mkakati wa Kuendeleza na Kusaidia Sekta Ndogo ya Madini ulioandaliwa na Shirika la Madini la Taifa haukushirikishwa kwa wadau muhimu kama Wizara ya Madini na Tume ya Madini. Hali hii inaweza kusababisha mgongano katika upangiliaji wa mahitaji na vipaumbele vya wachimbaji wadogo.

Utambuzi na uhusishwaji wa mahitaji na vipaumbele vya wachimbaji wadogo usiojitosheleza ulipelekea mapungufu katika mgawo wa fedha kwa ajili ya kuwawezesha wachimbaji wadogo. Hii kwa upande mwingine ilisababisha utekelezaji usijitosheleza wa mipango mbalimbali juu ya wachimbaji hawa.

### **(b) Utengaji Usiojitosheleza wa Rasilimali kwa ajili ya kuwasaidia Wachimbaji Wadogo**

Ukaguzi ulibaini kuwa hakukuwa na utengaji wa rasilimali uliojitosheleza. Hii ilithibitishwa na ukosefu wa uwezesaji wa kifedha pamoja na ukosefu wa wataalam wa kutosha kwa ajili ya kuwasaidia wachimbaji wadogo.

Athari kubwa na suala hili ni mapungufu katika kutimiza wajibu wa kuwawezesha wachimbaji wadogo wa madini. Vilevile suala hili linachangia ukosefu wa mtaji wa kununua vifaa bora vya uchimbaji hivyo kupunguza kasi ya maendeleo ya sekta ndogo ya madini nchini.

### **(c) Ukosefu wa Njia za kuhakikisha Matumizi Sahihi ya Rasilimali zilizotengwa kusaidia Wachimbaji Wadogo wa Madini**

Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Madini kupitia Tume ya Madini na Shirika la Madini la Taifa, haikuweka mikakati ya kutosha ya kuwezesha matumizi sahihi ya rasilimali zilizotengwa kwa ajili ya kuwawezesha wachimbaji wadogo wa madini.

Hii ilidhihirishwa na changamoto katika matumizi ya fedha kiasi cha sh. 7.29 bilioni zilizotengwa kama ruzuku kwa ajili ya wachimbaji wadogo kati ya 2015/16 na 2017/16 kupitia mradi wa SMMRP uliofadhiliwa na Benki ya Dunia. Barua yenye Kumb. Na. TIB/ORG/55/6/VOL. XXIV/23 iliyotolewa na Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) kuhusu hali ya utekelezaji wa mradi wa SMMRP ilibainisha kuwa kulikuwa na matumizi yasiyo sahihi ya pesa ya ruzuku, hii ilisababishwa na ukosefu wa utaratibu wa kuwezesha matumizi sahihi ya pesa hizo.

Changamoto hii inasababisha utambuzi na ugawaji wa rasilimali usiojitosheleza, hasa fedha, vifaa na wataalam kwa ajili ya kuwasaidia wachimbaji wadogo.

### **8.4.3 Uratibu Usiojitosheleza wakati wa Uwezesaji wa Wachimbaji Wadogo wa Madini**

Ukaguzi huu ulibaini uwapo wa mifumo ya mawasiliano isiojitosheleza, usambazaji wa taarifa kati ya watendaji muhimu usiojitosheleza na mapungu katika mfumo wa utoaji wa taarifa wakati wa uratibu wa uwezesaji wa wachimbaji wadogo. Maelezo zaidi juu ya suala hili yametolewa hapa chini:

#### **(a) Uratibu na Mifumo ya Mawasiliano Isiojitosheleza katika Uwezesaji wa Wachimbaji Wadogo**

Ukaguzi ulibaini kuwa vikao kati ya Wizara ya Madini na wadau wengine, hasa taasisi zake havikufanyika ipasavyo. Hali hii ilioneshwa na upungufu wa vikao vya thathmini ya kuangazia mambo yahasuyo uwezeshaji wa wachimbaji wadogo. Katika eneo hili, Wizara iliweza kufanya vikao vitano kati ya ishirini sawa na asilimia 20 ya malengo.

Hali hii ilisababishwa na ukosefu wa kipaumbele cha kutosha katika kushughulikia masuala ya wachimbaji wadogo ikidhihirishwa na upungufu wa fedha iliyotengwa kwa ajili hiyo. Athari ya changamoto hii ni ufikiaji mdogo wa malengo ya kuwasaidia wachimbaji wadogo.

#### **(b) Mikakati ya Kusambaza Taarifa kati ya Wahusika Wakuu haikutekelezwa**

Ukaguzi ulibaini utekelezaji usiojitosheleza wa mikakati ya usambazaji wa taarifa mbalimbali. Hii ilioneshwa na ukosefu wa utekelezaji wa mipango iliyopangwa.

Vilevile, ukaguzi ulibaini kuwa hali hii ilichangiwa na ukosefu wa Mkakati wa Mawasiliano wa Wizara kwa miaka mitatu ya fedha kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2020/21. Ukosefu wa mkakati wa mawasiliano katika Wizara ya Madini uliathiri usambazaji wa taarifa miongoni mwa wadau wa sekta ya madini na kusababisha changamoto katika utekelezaji wa mkakati wa kusaidia wachimbaji wadogo nchini.

#### **(c) Ukosefu wa Masuala yahasuyo Wachimbaji Wadogo katika Utoaji wa Taarifa Mbalimbali**

Kifungu cha 4.1 cha Mpango-mkakati wa Wizara ya Madini (2019/20 - 2023/24) kinatoa mpango wa utoaji taarifa za utendaji kazi. Mpango huo unaelezea taratibu na aina za ripoti ambazo zinapaswa kutolewa kwa ajili ufuatiliaji. Hii inajumuisha mipango ya utoaji wa taarifa nje na ndani ya Wizara kwa miaka mitano ya utekelezaji.

Hata hivyo, ukaguzi huu ulibaini kutokuwapo kwa masuala yanayohusiana na uwezeshaji wa wachimbaji wadogo wa madini katika Ripoti za Utendaji wa Mwaka za Wizara ya Madini katika baadhi mwaka wa fedha 2020/21, 2021/22, na 2022/23.

Ripoti za Utendaji wa Mwaka kwa miaka miwili tu ya fedha ya mwaka 2018/19 na 2019/20, zilitoa taarifa kuhusu uwezeshaji wa wachimbaji wadogo. Miaka

iliyobaki haikutoa taarifa ya hali ya utekelezaji ya uwezeshaji wa wachimbaji wadogo nchini.

Ukosefu wa taarifa za hali ya uwezeshaji wa wachimbaji wadogo katika mipango wa kila mwaka uliathiri utekelezaji wa programu mbalimbali zilizokusudiwa kuwezesha maendeleo ya wachimbaji wadogo kama inavyohimizwa katika Mpango Mkakati wa Wizara na sera ya madini.

#### 8.4.4 Ufuatiliaji na Tathmini Zisizojitosheleza katika Utendaji wa Shughuli za Wachimbaji Wadogo

Ukaguzi ulibaini ufuatiliaji usiojitosheleza katika uwezeshaji wa wachimbaji wadogo kutokana na mipango isiyojitosheleza katika ufuatiliaji na tathmini ya shughuli uchimbaji mdogo wa madini, mapungufu katika kufuatilia utekelezaji wa mipango ya kuwasaidia wachimbaji wadogo pamoja na changamoto katika ufuatiliaji wa mchango wa uwezeshaji wa wachimbaji wadogo. Maelezo ya ziada yametolewa hapa chini:

##### (a) Ufuatiliaji wa Uwezeshaji wa Wachimbaji Wadogo Usiojitosheleza

Ukaguzi ulibaini kuwa Shirika la Madini la Taifa halikutekeleza ipasavyo ufuatiliaji na tathmini ya uwezeshaji wa wachimbaji wadogo, kama inavyothibitishwa na kutokuwapo kwa Mfumo wa Utoaji wa Taarifa za Usimamizi (Pamoja na tafiti zisizojitosheleza.

Mapungufu hayo yalitokana na kutokuwapo kwa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini katika Wizara ya Madini, Tume ya Madini na Shirika la Madini la Taifa.

##### (b) Ukosefu wa Vigezo na Malengo katika Mipango ya kila Mwaka ya Ufuatiliaji na Tathmini ya shughuli ndogo za uchimbaji madini

Miongozo ya Wizara ya Fedha na Mipango ya Maandalizi ya Mipango na Bajeti, 2018/19 - 2022/23, inawataka Maofisa Masuuli kuhakikisha miradi ya maendeleo, mipango na shughuli zilizopangwa kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini zinazoendana na viashiria, vigezo na malengo yaliyo wazi ambayo yatazingatiwa wakati wa utekelezaji na ufuatiliaji wa mradi.

Ukaguzi ulibaini kupitia Mpango-mkakati wa Shirika la Madini la Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/22 - 2025/26 kuwa Shirika liliweka viashiria vitatu muhimu vya utendaji ili kufuatilia na kutathmini shughuli za wachimbaji wadogo nchini. Hata hivyo, hakuna kiashiria kilichokuwa na vigezo maalumu kwa ajili ya kupima utekelezaji wake kila mwaka.

Aidha, hakukuwa na malengo ya kila mwaka ya kufuatilia na kutathmini hali ya uwezeshaji wa wachimbaji wadogo. Ukosefu wa vigezo na malengo katika viashiria vya utendaji kutasababisha changamoto katika kupima utekelezaji wa malengo mbalimbali yaliyowekwa. Hivyo, kuleta ugumu katika kung'amua maeneo yanayohitaji juhudi na maboresho zaidi.

#### **(c) Ukosefu wa Mapitio ya Hali ya Utendaji wa Uwezeshaji wa Wachimbaji Wadogo Nchini**

Ripoti za Utendaji za Kila mwaka kuanzia Mwaka (2018/19 - 2022/23) kutoka Wizara ya Madini zilionyesha kuwa, Wizara haikufanya mapitio ya utendaji ya kutosha ili kutathmini maendeleo ya utekelezaji wa mipango ya kusaidia wachimbaji wadogo. Ilibainika kuwa Wizara haikujumuisha hatua yoyote ya mapitio ya utendaji katika mipango yake ya mwaka kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2020/21.

Hali hii imesababisha ukusanyaji usioridhisha wa taarifa za kiutendaji wa taasisi za Wizara katika uwezeshaji wa wachimbaji wadogo nchini

#### **(d) Ukosefu wa Ufuatiliaji wa Mara kwa Mara wa Mchango wa Uwezeshaji wa Wachimbaji Wadogo**

Kifungu cha 2 (ii) cha Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 - 2020/21) kinahitaji Wizara kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara na ukaguzi wa miradi inayotekelezwa na kuthibitisha matokeo yaliyoripotiwa.

Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara haikufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kutathmini ufanisi wa uwezeshaji wa wachimbaji wadogo. Badala yake, Wizara ilitegemea taarifa kutoka katika ripoti za utendaji kutoka kwa taasisi zake. Hata hivyo, ripoti hizi hazikujumuisha masuala ya uwezeshaji wa wachimbaji wadogo. Hii ilitokana na ukosefu wa rasilimali za kifedha kwa ajili ya kuhudumia shughuli hizo.

Hali hii inatokana na Wizara kutokuwa na mpango mathubuti wa ufuatiliaji na tathmini kwa ajili ya kuongoza shughuli za ufuatiliaji na tathmini. Madhara ya hali hii ni kuwapo kwa hatari ya kutofikia malengo yaliyowekwa ili kuhakikisha uwezeshaji wa shughuli za uchimbaji mdogo wa madini nchini.

## 8.5 Matokeo ya Ukaguzi katika Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi

Sehemu hii inatoa matokeo ukaguzi katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi kama ilivyoelezwa hapa chini:

### 8.5.1 Uwapo wa Uvuvi Haramu Nchini

Ukaguzi huo ulibaini kuendelea kwa shughuli za uvuvi haramu na zisizodhibitiwa, kama ilivyoelezwa hapa chini:

#### (a) Uwapo wa Zana na Njia Haramu za Uvuvi Nchini

Mapitio ya ripoti za uchunguzi kwa mwaka wa fedha 2020, ukaguzi ulibaini kuwa zana haramu za uvuvi ziliendelea kutumika katika shughuli za uvuvi, kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na. 49**.

**Jedwali Na. 49: Idadi ya Zana za Uvuvi Haramu katika Maeneo yaliyotembelewa wakati wa Ukaguzi**

Jina la Ziwa/Bahari	Idadi ya Mialo	Aina ya Zana Haramu za Uvuvi			
		Makokoro ya Kina Kirefu	Nyavu za Nailoni	Makokoro ya Kina Kifupi (>6")	Mikuki
Ziwa Tanganyika	107	12	9	1	0
Ziwa Victoria	580	1	25	60	0
Bahari ya Hindi	274	2	1	1	11

*Chanzo: Ripoti ya Utafiti wa Ziwa Tanganyika 2022, Ziwa Victoria kwa 2020 na Uvuvi wa Bahari kwa 2018*

**Jedwali Na. 49** linaonesha uwapo wa zana haramu za uvuvi katika Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria na Bahari ya Hindi. Idadi ya bidhaa hizi unatofautiana kutoka mwalo mmoja hadi mwingine, kulingana na kiwango cha uendeshaji wa zozi la doria.

Matumizi ya zana hizi haramu yalisababishwa mambo mbalimbali yakiwemo udhibiti usiojitoshelesha, ukosefu wa ufahamu wa athari za uvuvi haramu miongoni mwa wavuvi, udhibiti duni wa uingizaji wa zana za uvuvi haramu nchini, tamaa ya wavuvi kupata samaki wengi kwa mkupuo, na bei ndogo ya zana haramu za uvuvi ikilinganishwa na zile halali.

**(b) Ukosefu wa Taarifa za Kutosha Kuhusu Shughuli za Uvuvi nchini**

**Jedwali Na. 50** linaonesha uchambuzi wa utoaji wa taarifa au utunzaji wa kumbukumbu za takwimu za uvuvi katika Serikali za Mitaa, ikiambatana na masuala muhimu ambayo yanahitaji kuwekwa kwenye kumbukumbu. Jedwali limetoa mnyumbuliko wa idadi ya Serikali za Mitaa katika kutoa taarifa maalumu, inayoainishwa kama "mara nyingi zaidi," "mara chache," na "haijatolewa."

**Jedwali Na. 50: Utoaji wa Taarifa za Uvuvi katika Serikali za mitaa Zilizotembelewa**

Na.	Masuala Muhimu Yanayohitajika	Idadi ya Serikali za Mitaa Zilizotoa Taarifa		
		Mara Nyingi	Mara Chache	Haijatolewa Taarifa
1	Takwimu za Samaki	0	4	5
2	Idadi ya Wavuvi	0	2	7
3	Zana za Uvuvi	4	2	3
4	Mapato Yaliyokusanywa	0	2	7

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Takwimu kutoka katika Serikali za Mitaa Tisa zilizotembelewa, 2023*

**Jedwali Na. 50** linaonesha jinsi Serikali za Mitaa zilivyotoa taarifa mbalimbali za uvuvi. Kwa mfano, takwimu za samaki zilionekana kutoripotiwa katika Serikali nne za Mitaa kati ya tisa. Aidha, idadi ya wavuvi haikutolewa taarifa ipasavyo katika Serikali za Mitaa mbili na Serikali za Mitaa saba hazikutoa taarifa kabisa. Vivyo hivyo, taarifa juu ya zana za uvuvi zilitolewa mara nyingi katika Serikali za Mitaa nne lakini zilitolewa mara chache katika Serikali za Mitaa mbili. Taarifa juu ya mapato yaliyokusanywa zilitolewa kwa nadra katika Serikali za Mitaa mbili na hazikutolewa kabisa katika Serikali za Mitaa saba.

Mbali na hayo, asilimia 85 ya Serikali za Mitaa zilizotembelewa hazikuwasilisha taarifa za utekelezaji wa robo mwaka, nusu mwaka, na mwaka kwa Mkurugenzi, kinyume na kifungu cha 3 (a) (2) cha Kanuni za Uvuvi za mwaka 2020 pamoja na marekebisho yake. Kwa upande mwingine, kulikuwa na utoaji wa taarifa usiojitosheleza katika masuala muhimu ambayo yaliyohitaji kuripotiwa.

Utekelezaji usioridhisha katika eneo hili ulichangia ukosefu wa taarifa za kuaminika juu ya shughuli za uvuvi na rasilimali za uvuvi ndani ya nchi, ambayo ni muhimu katika kusimamia shughuli za uvuvi na kutengeneza matumizi bora za rasilimali za uvuvi.

## (c) Wavuvi na Zana za Uvuvi havikudhibitiwa kikamilifu

Ukaguzi ulibaini baadhi ya shughuli za uvuvi ambazo hazikusimamiwa vizuri kama ilivyoenezwa hapa chini:

**Utoaji wa Leseni na Kibali**

Ukaguzi umebaini uwapo wa zana za uvuvi ambazo hazijasajiliwa na shughuli nyingine za kibiashara ambazo hazikuzingatia kanuni za uvuvi. **Jedwali Na. 51** linaonesha kiwango cha vyombo vya uvuvi ambavyo havijasajiliwa.

**Jedwali Na. 51: Utendaji wa Usajili wa Vyombo vya Uvuvi**

Utafiti Uliofanyika	Jumla ya Vyombo vya Uvuvi	Vyombo Vilivyosajiliwa	Vyombo ambavyo Havijasajiliwa	Asilimia ya Vyombo ambavyo Havijasajiliwa
Utafiti katika Ziwa Tanganyika 2021	11,963	4,609	7,354	61
Utafiti katika Ziwa Victoria 2020	30,646	10,220	20,426	67
Utafiti katika Bahari 2018	9,242	5,343	3,899	42
Wastani wa Asilimia ya Vyombo ambavyo Havijasajiliwa				57

*Chanzo: Ripoti za Utafiti 2018/19, 2019/20 na 2021/22*

**Jedwali Na 51** linaonesha kuwa, kwa wastani, asilimia 57 ya vyombo vya uvuvi vinavyohusika katika shughuli za uvuvi havikusajiliwa kwa mujibu wa kanuni. Ziwa Victoria linaongoza kwa kuwa na asilimia 67 ya vyombo vya uvuvi visivyo na leseni. Aidha, asilimia 61 ya vyombo wa uvuvi katika Ziwa Tanganyika havikuwa na leseni. Matokeo haya yanaonesha kuwa rasilimali za uvuvi nchini hazikudhibitiwa kikamilifu.

**Uwapo wa Mialo Isiyoidhinishwa**

Ripoti ya utafiti, 2018 pamoja na Ripoti ya Takwimu za Uvuvi ya Mwaka (Januari-Desemba) 2020, zilionyesha uwapo wa mialo ambayo hayakusajiliwa pia haikua chini ya usimamizi wa Kitengo cha Usimamizi wa Fukwe. Uwapo wa mialo ambayo haikuwa chini ya usimamizi Kitengo cha Usimamizi wa Fukwe ulichangia uwapo wa shughuli za uvuvi zisizo endelevu. **Jedwali Na. 52** linagusia uwapo wa mialo hiyo.



**Jedwali Na. 52: Utendaji wa Usajili wa Kitengo cha Usimamizi wa Fukwe pamoja na Mialo**

Utafiti Uliofanyika	Idadi ya Mialo	Idadi ya Mialo yenye Kitengo cha Usimamizi wa Fukwe	Idadi ya Mialo isiyo na Kitengo cha Usimamizi wa Fukwe	Asilimia ya mialo isiyo na Kitengo cha Usimamizi wa Fukwe	Vyombo vya Uvuvi/Mialo isiyosajiliwa kwa Mwaka
Utafiti katika Ziwa Tanganyika 2021	107	59	48	45	69
Utafiti katika Ziwa Victoria 2020	580	573	7	1	35
Utafiti katika Bahari 2018	274	174	100	36	14

*Chanzo: Ripoti za Utafiti 2018/19, 2019/20 na 2021/22*

**Jedwali Na. 52** linaonesha kuwa Ziwa Tanganyika lilikuwa na asilimia 45 ya mialo isiyo na Kitengo cha Usimamizi wa Fukwe, jambo linaloonesha uwezekano wa kuwapo wa changamoto katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Hali hii imesababisha uwapo wa wastani wa vyombo vya uvuvi 69 visivyosajiliwa katika kila mwalo.

Ziwa Victoria lilionekana kuwa na asilimia ndogo sana asimilia 1 ya mialo isiyo na Kitengo cha Usimamizi wa Fukwe, na hivyo kuwa na vyombo vichache vya uvuvi ambavyo havijasajiliwa kuliko Ziwa Tanganyika. Uvuvi wa baharini ulikabiliwa na changamoto kubwa katika mwaka 2018 ambapo asilimia 36 ya mialo haikuwa na Kitengo cha Usimamizi wa Fukwe, ingawa kuna vyombo vichache vya uvuvi ambavyo havijasajiliwa. Hii ilitokana na ufuatiliaji wa mara kwa mara kwani vituo vingi vya uvuvi vilikuwa na vifaa vya doria pamoja na miundombinu mizuri ya kuwezesha zoezi hili.

Uwapo wa maeneo ya mialo isiyo na Kitengo cha Usimamizi wa Fukwe, ambacho kina jukumu la kusimamia mchakato wa usajili na leseni, umesababisha ongezeko la idadi ya wavuvi pamoja na vyombo vya uvuvi visivyosajiliwa na visivyo na leseni, ambayo huongeza athari ya uwapo wa shughuli za uvuvi haramu.

### 8.5.2 Utekelezaji Usioridhisha wa Usimamizi wa Shughuli za Uvuvi

Ukaguzi huo ulibaini utendaji usioridhisha katika kutekeleza shughuli za uvuvi bora nchini, kama vile utoaji wa leseni na usajili usioridhisha, usimamizi usiojitosheleza katika uvuvi wa samaki unaoruhusiwa kuvuliwa na usimamizi wa misimu ya kufunga shughuli za uvuvi usiojitosheleza. Maelezo zaidi yamebainishwa hapa chini:


Ukaguzi huo ulibaini kuwa vyombo 20,885 kati ya 28,615 sawa na asilimia 73 ya vyombo vyote vya uvuvi vilivyokuwa vinafanya kazi havikusajiliwa. Pia, ukaguzi wa vitabu vya usajili ulibaini kuwa asilimia 70 ya makosa yaliyojumuishwa yalitokana na kutosajiliwa na kutotoa leseni kwa wavuvi na vyombo vya uvuvi.

Ukaguzi ulibaini kuwa ingawa mchakato wa usajili uliratibiwa kuanzia ngazi ya chini ukihusisha Vitengo vya Usimamizi wa Fukwe kama waanzishaji wa mchakato wa usajili wa wavuvi, maeneo mengi ya mialo hayakuwa chini ya usimamizi wa vitengo hivi. Jumla ya maeneo 155 kati ya 961 ya mialo hayakuwa chini ya usimamizi wa Vitengo vya Usimamizi wa Fukwe, na kusababisha kuwapo kwa idadi kubwa ya vyombo vya uvuvi na wavuvi ambao hawajasajiliwa na wasio na leseni.

Ukaguzi ulibaini kuwa changamoto hii ilitokana na wavuvi wengi kuishi karibu na maeneo yao ya uvuvi na maeneo hayo yako mbali na ofisi za halmashauri zinazohusika na usajili na leseni. Kwa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Rorya iko zaidi ya kilomita 50 kutoka Kijiji cha Sota ambapo kuna shughuli nyingi za uvuvi. Kutokana na hali hii, Serikali za Mitaa ziliamua kufanya usajili wa mojawoja katika maeneo ya wavuvi kwa kuwahusisha Maofisa wa Kitengo cha Usimamizi wa Fukwe. Hata hivyo, kwa upande wa maeneo ya mialo ambayo hayakufikika kirahisi, wavuvi walikua wanafanya shughuli zao bila usajili wala leseni.

Uwapo wa vyombo vya uvuvi na wavuvi wasiosajiliwa na wasio na leseni umesababisha kuendelea kwa shughuli za uvuvi haramu, zisizotolewa taarifa ipasavyo pamoja na kutodhibitiwa kikamilifu, hivyo kushindwa kukusanya takwimu za uvuvi za kuaminika kutoka katika maziwa na bahari. Hali hii pia ilisababisha hasara ya jumla ya sh. 15,162,640,000, ambazo zingepatikana kupitia mapato ya leseni pamoja na ada ya Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania na kodi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania. **Kielelezo Na. 38** kinatoa takwimu juu ya uwezekano wa kupoteza mapato katika mikoa iliyotembelewa.

**Kielelezo Na. 38: Upotevu wa Mapato kutokana na Leseni ya Wavuvi, Kodi, na Ada za Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania katika Mikoa Iliyotembelewa**



*Chanzo: Ripoti za Utafiti 2018/19, 2019/20 na 2021/22*

Takwimu za **Kielelezo Na. 38** zinaonesha kuwa mikoa ya Dar es Salaam na Lindi ilikuwa na hasara ya chini ya shilingi milioni 500, huku asilimia ya vyombo ambavyo havijasajiliwa ikiwa chini ya asilimia 30. Miundombinu na jiografia nzuri vilichangia katika utendaji mzuri wa mikoa hii; shughuli za uvuvi katika mikoa hii zimepangiliwa, na kwa hivyo, zinaweza kudhibitiwa kwa urahisi.

Kwa upande mwingine, Mwanza, Mara, Kigoma na Pwani zilionekana kuwa na maeneo mengi ya mialo, jambo linaloleta ugumu katika kugawa rasilimali watu na fedha kwa ajili ya usajili. Aidha, mikoa hii haikufanya vizuri katika ufuatiliaji na udhibiti wa shughuli za uvuvi. Matokeo yake, hasara yao imekuwa juu ya sh. milioni 500, na asilimia ya vyombo visivyosajiliwa ilikua juu ya asilimia 60.


Changamoto zilizotatwa hapo juu zilitokana na mambo yafuatayo:

**(i) Udhibiti Usiojitosheleza wa Samaki wa Kuvua**

Kupitia uchambuzi wa takwimu zilizotolewa na Maofisa wa uvuvi kutoka vituo vya Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi na Mamalaka ya Serikali za Mitaa, ukaguzi ulibaini udhibiti usiojitosheleza juu ya uvuvi wa samaki wasiofikia ukubwa, hii

ilithibitishwa na uwapo wa samaki wadogo katika masoko. Hali ya uvuvi wa samaki wasiofikia ukubwa imeoneshwa katika **Kielelezo Na. 39**.

**Kielelezo Na. 39: Hali ya Uvuvi wa Samaki Wasiofikia Ukubwa**



**Vyanzo:** Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka Ripoti za Ufuatiliaji (2018/19-2022/23)

Kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 39**, uvuvi wa samaki walio chini ya ukubwa umepungua katika Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika, lakini uliendelea kuongezeka katika maeneno ya baharini. Ukaguzi huu ulibaini kuwa doria zilifanyika kwa nadra siku za wikiendi pamoja na usiku. Kwa hivyo, matokeo ya kupungua kwa uvuvi wa samaki walio chini ya ukubwa yanaweza yasiwe na uhalisia kulingana na ukosefu wa tawimu za kutosha.

Baada ya kukagua taarifa za utendaji za kila mwaka za kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa, ukaguzi ulibaini kuwa upungufu huu ulisababishwa na ukosefu wa maelekezo mahsusi ya samaki wanaoruhusiwa kuvuliwa ili kudhibiti shughuli ya uvuvi katika maeneo yao.

Aidha, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi ilitakiwa kufanya tafiti za tathmini na takwimu za samaki ili kupima juhudi za uvuvi katika maziwa na bahari. Hata hivyo, ilibainika kuwa TAFIRI haikufanya tafiti hizo mara kwa mara, kwa kuwa utafiti wa mwisho ulifanyika mwaka 2020.

Mapungufu haya yanahatarisha uendelevu wa uvuvi pamoja na usalama wa chakula. Hii inaweza kusababisha hasara ya kiuchumi ya muda mrefu mfano upungufu wa Samaki katika maziwa na bahari.

**(ii) Msisitizo mdogo juu ya Usimamizi wa Msimu wa Ufungaji wa Shughuli za Uvuvi**

Mapitio ya ripoti za utendaji (2018/19-2022/23) kutoka katika vituo vya ulinzi wa rasilimali za samaki vya Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa, ukaguzi ulibaini kuwa kuwa misimu ya ufungaji wa shughuli za uvuvi ilizingatiwa kwa kiasi fulani, kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na. 53**.

**Jedwali Na. 53: Hali ya Utekelezaji wa Msimu wa Ufungaji wa Shughuli za Uvuvi katika Halmashauri Zilizotembelewa**

Jina la Halmashauri	Utendaji katika Utekelezaji wa Msimu wa Ufungaji wa Shughuli za Uvuvi
Manispaa ya Kigamboni	Msimu wa ufungaji hufanywa kwa samaki aina ya Kamba tu kwa miezi saba (7), kutoka Septemba hadi Machi
Jiji la Dar es Salaam	Msimu wa ufungaji hufanywa kwa samaki aina ya kamba tu kwa miezi saba (7), kutoka Septemba hadi Machi
Wilaya ya Kilwa	Msimu wa ufungaji hufanywa kwa miezi mitatu kwa samaki aina ya pweza na kamba tu
Wilaya ya Mafia	Msimu wa ufungaji hufanywa kwa miezi mitatu kwa samaki aina ya pweza na kamba tu
Wilaya ya Rorya	Msimu wa hufanywa kwa siku 14 kwa mwezi kwa aina zote za samaki. Hufungwa kwa kila wiki ikifuatiwa na ufunguzi wa shughuli za uvuvi wa samaki kila mwezi mwaka mzima
Jiji la Mwanza (Nyamagana)	Msimu hufungwa kwa ajili ya daga tu na hufanywa kwa siku kumi kila mwezi
Manispaa ya Kigoma-Ujiji	Hakuna msimu ufungaji wa uvuvi wa samaki uliotekelzwa
Manispaa ya Ilemela	Msimu wa ufungaji ni kwa daga tu na hufanywa kwa siku kumi kila mwezi
Wilaya ya Ukerewe	Msimu wa ufungaji ni kwa daga tu na hufanywa kwa siku kumi kila mwezi

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa za Msimu wa Ufungaji wa Uvuvi kutoka Halmashauri Zilizotembelewa, 2023*

Takwimu katika **Jedwali Na. 53** zinaonesha kuwa kati ya halmashauri tisa zilizotembelewa, Halmashauri ya Wilaya ya Rorya pekee ndiyo ilitekeleza ipasavyo ufungaji wa msimu wa uvuvi kwa aina zote za samaki kwa siku 14. Halmashauri sita zilizobaki (sawa na Asilimia 75) zilitekeleza msimu wa

ufungaji, lakini kwa aina moja tu ya samaki (*dagaa*) katika kanda ya ziwa na samaki aina ya kamba na pweza katika bahari. Manispaa ya Kigoma-Ujiji haikutekeleza ufungaji wa msimu wa uvuvi wa aina yoyote ya samaki.

Changamoto tajwa hapo juu zilisababishwa na mambo yafuatayo:

- (i) Halmashauri hazikusimamia utekelezaji wa ufungaji wa msimu wa uvuvi ili kuepuka kupoteza mapato yanayokusanywa kutokana na ada ya leseni, ushuru wa samaki, nk. Hata hivyo, hakuna halmashauri hata moja iliyofanya uchambuzi wa faida na hasara ya utekelezaji wa ufungaji wa misimu hii; na
- (ii) Hakukuwa na mipaka ya kutenganisha maeneo ya mazalia ya samaki. Hii ni tofauti na mazingira ya baharini, ambapo maeneo ya hifadhi za samaki yametengwa na hufanyiwa doria za mara kwa mara, na hakuna shughuli za uvuvi zinazoruhusiwa.

### 8.5.3 Mapungufu katika Usimamizi wa Kanzidata ya Uvuvi

Katika eneo hili, ukaguzi uligundua mambo yafuatayo:

#### (a) Utunzaji wa Kumbukumbu katika Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi Usijitosheleza

Kanuni ya 69 ya Kanuni za Uvuvi, 2009, inahitaji Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Serikali za Mitaa kuwa na takwimu za kuaminika juu vyombo vyote vya uvuvi. Shughuli zote za uvuvi, kama vile leseni, upatikanaji wa samaki, maelezo ya chombo cha uvuvi na ukusanyaji wa mapato, lazima ziwekewe kumbukumbu na zihifadhiwe.

Wizara inatumia mfumo wa eCAS na mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za mapato ya uvuvi (FiRCIS) kukusanya taarifa za uvuvi kwenye mnyororo wa thamani wa soko la samaki. Mifumo hii inatosha kukusanya taarifa kuhusu usimamizi wa uvuvi, ikiwa pamoja na kuimarisha mifumo iliyopo ya kuchakata, kuhifadhi, na kuchambua takwimu kwa ufanisi kwa utendaji bora wa usimamizi.

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa njia za utunzaji wa kumbukumbu zilizotumika katika halmashauri zote zilizotembelewa hazikuruhusu upatikanaji wa taarifa za uvuvi kwa urahisi. Takwimu za uvuvi ziliandikwa kwenye madaftari, na zilikosa maelezo ya kutosha kama taarifa za leseni, maelezo ya chombo cha uvuvi, na ukusanyaji wa mapato. Mbali na hilo, katika halmashauri zote tisa zilizotembelewa, baadhi ya madaftari yenye taarifa za uvuvi kwa miaka kadhaa

yalikosekana. Hii ilileta mazingira magumu kwa wakaguzi na Maofisa wa uvuvi wakati kutafuta na kuangalia taarifa za mwenendo wa shughuli za uvuvi katika halmashauri hizo.

Ilibainishwa kuwa halmashauri zilibadili madaftari yenye takwimu za uvuvi pindi yanapojaa. Ubadilishaji huu wa mara kwa mara ulizuia mpangilio mzuri wa taarifa kutoka katika mialo kwenda halmashauri. Pia, haikuwa rahisi kupata habari kwani baadhi ya madaftari yalikuwa yamechakaa.

Ukaguzi huu ulibaini kuwa baadhi ya halmashauri zilizotembelewa ikiwemo Kilwa Mafia, Mwanza, Rorya na Ukerewe hazikuwa na mfumo jumuishi wa kusimamia taarifa za shughuli za uvuvi. Mahojiano na Maofisa wa uvuvi yalibaini kuwa halmashauri hazikuwa na kompyuta kwa ajili ya kazi hiyo. Aidha, baadhi ya Maofisa wa uvuvi wa kata na Maofisa wa Vitengo vya Usimamizi wa Fukwe hawakuwa na uwezo wa kutumia mifumo mbalimbali.

#### **(b) Utendaji Usiotosheleza katika Kukusanya na Kudumisha Takwimu za kila siku za uvuvi**


Ukaguzi ulibaini kuwa ukusanyaji na utunzaji wa takwimu za uvuvi za kila siku haukujitosheleza. Upungufu huo ulitokana na Wizara kutokuwa na takwimu za kutosha kuhusu shughuli za uvuvi. Kwa mfano, takwimu za kila siku za uvuvi wa samaki zilipatikana katika mialo 59 kati ya 595, sawa na chini ya asilimia 10 ya jumla ya idadi ya mialo iliyopo Ziwa Victoria.

Aidha, katika miaka ya fedha 2018/19 - 2022/23, ilibainika kuwa ni tafiti 1 kati ya tafiti 5 (sawa na asilimia 20) zinazohitajika kwa ajili ya kutathmini upatikanaji wa Samaki zilifanyika.

Kwa mujibu wa Maofisa wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, tathmini ya samaki wa nchi nzima haikufanyika kila mwaka kutokana na ukosefu wa fedha. Kwa ujumla Wizara hutenga bajeti ya shughuli hizi kila mwaka, lakini Serikali haitoi fedha hizo. Tangu utafiti wa mwisho ufanyike, Wizara imetenga kiasi cha sh. 38,200,000 kwa ajili ya shughuli hii, lakini fedha hizo hazijawahi kutolewa.

Kwa hivyo, upungufu wa takwimu za uvuvi kutoka katika tafiti za mara kwa mara na utegemezi wa takwimu za kukadiria unaweza kuathiri mchakato wa kufanya mipango mbalimbali juu ya usimamizi wa shughuli za uvuvi nchini. Hali kama hiyo ilibainishwa na ukaguzi ambapo halmashauri hazikukusanya takwimu za kila siku za uvuvi kwa mfumo wa kieletroniki wa (e-CAS) kama ilivyooneshwa katika **Kielelezo Na. 40** hapa chini:

### Kielelezo Na. 40: Utendaji wa Halmashauri katika Ukusanyaji wa Takwimu za Uvuvi za Kila Siku



*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kulingana na mapitio ya nyaraka na mahojiano, 2023*

**Kielelezo Na. 40** kinaonesha kuwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ilikuwa na eneo moja la mwalo ambalo lilikuwa likitumia mfumo wa e-CAS, sawa na asilimia 100, wakati Manispaa ya Kigoma ilikuwa na maeneo ya mialo 3 kati ya 4 yaliyokuwa yanatumia mfumo huu, sawa na asilimia 75. Halmashauri ya Wilaya ya Rorya alikuwa na mialo 3 kati ya 33 iliyokua inatumia mfumo wa e-CAS, sawa na asilimia 9 na Halmashauri ya Wilaya Ukerewe ilikuwa na mialo 6 kati ya 56 iliyokuwa inatumia mfumo huu, sawa na asilimia 11.

#### (c) Upungufu wa Kanzidata na Usimamizi wa Ubora wa Takwimu katika Mfumo wa Taarifa ya Ukusanyaji wa Mapato ya Uvuvi wa FiRCIS

Kupitia Mpango Mkuu wa Sekta ya Uvuvi, 2021/22 - 2036/37, ukaguzi ulibaini kuwa kanzidata katika Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato ya Uvuvi Tanzania Bara hazikutunzwa na kuhuishwa mara kwa mara. Baadhi ya taarifa muhimu, kama vile takwimu za tafiti mbalimbali hazikuhusihwa katika mfumo huo.

Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa makisio ya uvuvi wa samaki kila mwaka yaliyofanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi hayakutokana na takwimu zilizokusanywa kutoka katika maeneo yote ya mialo ya samaki nchini. Makisio haya yalitokana na baadhi ya mialo ambayo idadi yake ilikuwa chini ya asilimia kumi ya jumla ya maeneo yote ya mialo nchini. Hii inafanya mfumo wa takwimu



uliopo kutokuwa na uhalisia wa taarifa kwani haufanyi kazi vizuri tangu mwaka 2021 ulipotengenezwa.

Kwa kuongezea, mfumo huu haukuunganishwa kwenye kanzidata za Wizara, kama vile kanzidata ya Mfumo wa Kieletroniki wa Taarifa za Uvuvi (FIS).

Mapungufu yaliyobanika yalitokana Serikali, kupitia Wizara zake kutoweka msukumo na kipaumbele juu ya suala hili. Hii ilithibitishwa na utengaji mdogo wa fedha kwa ajili ya utunzaji na uhuishaji wa kanzidata za uvuvi.

#### 8.5.4 Uratibu Usiojitosheleza katika Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi

Ukaguzi ulibaini uratibu usiriodhisha miongoni mwa wadau katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi, kama ilivyobainishwa hapa chini:

##### (a) Ushauri na Mawasiliano kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Serikali za Mitaa na Taasisi ya Utafiti ya TAFIRI Hayakujitosheleza

Ukaguzi ulibaini uwapo wa uratibu usiojitosheleza katika kubadilishana taarifa kuhusu usimamizi wa uvuvi miongoni mwa wadau kama Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Serikali za Mitaa na Taasisi ya Utafiti wa wa Uvuvi. Maelezo zaidi yametolewa katika **Jedwali Na. 54**:

**Jedwali Na. 54: Majukumu ya Uratibu inayotakiwa kutolewa na Wadau**

Jina la Mdau	Majukumu ya Mdau	Maoni ya Wakaguzi
Serikali za Mitaa	Ukusanyaji na usambazaji wa takwimu na taarifa za uvuvi	Mamlaka za Serikali za Mitaa hazikuwasilisha taarifa za shughuli za uvuvi katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mujibu wa kanuni za Uvuvi za mwaka 2020. Timu ya ukaguzi ilitembelea ofisi za Mikoa ya Mwanza, Mara, Pwani, na Dar es Salaam lakini haikupata taarifa zozote za uvuvi zilizowasilishwa kwa Wizarani
Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Serikali za Mitaa na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi	kama moja ya mkakati ya usimamizi mzuri wa rasilimali za uvuvi; Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na wadau wengine, wanatakiwa kufanya tathmini ya uwapo wa samaki na	Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Serikali za Mitaa, na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (Tanzania) hazijaratibu jitihada za kufanya utafiti, ikiwa pamoja na tathmini ya uwapo wa samaki, tafiti za bioanuai, na utafiti juu ya masuala ya mazingira, kijamii na kiuchumi. Ukosefu wa ushirikiano miongoni mwa wadau hawa unaadhiri moja kwa moja usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwa ufanisi.

Jina la Mdau	Majukumu ya Mdau	Maoni ya Wakaguzi
	bioanuai, na utafiti juu ya masuala mazingira, kijamii na kiuchumi.	

*Vyanzo: Sera ya Taifa ya Uvuvi ya 2015 na Kanuni za Uvuvi, 2009*

**Jedwali Na. 55** linaonesha uratibu usiyojitosheleza katika usimamizi wa uvuvi kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mamlaka za Serikali za Mitaa, na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania

Hali hii ilitokana na mambo yafuatayo:

**Mapungufu katika mawasiliano:** Njia za mawasiliano na uratibu kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Serikali za Mitaa, na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) zisizoridhisha vimesababisha kutokuelewana, ucheleweshaji katika utoaji wa taarifa, na kutokuwapo kwa juhudi sawia miongoni mwao. Mawasiliano yalikuwa hayana ufanisi kwani Wizara haiwezi kuwasiliana moja kwa moja na Serikali za Mitaa. Badala yake, Wizara inapaswa kuwasiliana na OR-TAMISEMI kwa kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zipo chini ya OR-TAMISEMI na siyo Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Pia, Wizara ya Mifugo na Uvuvi haiwezi kuzielekeza moja kwa moja Serikali za Mitaa kufanya wajibu fulani kuhusu shughuli za uvuvi.

**Changamoto za Ushirikishwaji wa Takwimu:** Ugumu katika kushirikishana takwimu za uvuvi kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Serikali za Mitaa, na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania umezuia maendeleo ya usimamizi wa uvuvi. Kwa mfano, ilibainika kuwa takwimu zinazohusiana na uvuvi kutoka Halmashauri zilipekwa mikoani na hazikujumuishwa katika mfumo na kanzidata za Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

**Changamoto za Miundo ya Kitaasisi:** Miundo ya taasisi iliyopo na mahusiano ya kazi ndani ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania ilileta changamoto katika ushirikiano. Changamoto kubwa ni kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaripoti OR-TAMISEMI, na siyo katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Pia, wakati Wizara inahitaji taarifa za uvuvi, lazima ipitie OR-TAMISEMI.

**(b) Ushirikishwaji wa Taarifa Usiojitosheleza baina ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Serikali za Mitaa**

Ukaguzi ulibaini uwapo wa ushirikiano mdogo kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Mamlaka za Serikali za Mitaa juu ya ushirikishwaji wa taarifa za shughuli za

uvuvi. Ukaguzi haukupata makubaliano wala taratibu za wa utoaji wa taarifa kati ya Wizara na Serikali za Mitaa.

Ukaguzi ulibaini kuwa asilimia 98 ya Vitengo vya Usimamizi wa Fukwe vilivyotembelewa havikukusanya takwimu zozote za uvuvi zinazopasawa kupelekwa Wizarani na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kutokana na mahojiano yaliyofanyika na Maofisa wa Vitengo vya Usimamizi wa Fukwe katika maeneo ya Minazi, Mikindani, na Mjimwema yaliyopo Kigamboni Jijini Dar es Salaam, ilibainika kuwa shughuli ya kupata takwimu za samaki waliovuliwa na kuuuzwa katika maeneno ya mialo hazikufanyika kabisa.

### **(c) Ushirikiano Usioridhisha kati ya Watendaji muhimu katika Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi**

Kifungu cha 53(1) cha Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 kinaitaka Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuainisha maeneo ya utafiti kwa kushirikiana na TAFIRI na Serikali za Mitaa.

Ukaguzi ulibaini changamoto katika kushirikiana kama ilivyoonyeshwa na baadhi ya mapungufu katika kuwasiliana na kupanga shughuli za utafiti kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Serikali za Mitaa, na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) kwa miaka ya fedha 2018/19 hadi 2022/23. Hali hii ilithiirishwa na ukosefu wa maeneo yaliyoainishwa kwa ajili ya utafiti na ukosefu wa mawasiliano mazuri kuhusu usimamizi wa rasilimali za uvuvi.

Urekebishaji wa hali hii ni muhimu kwa ajili ya uelewa zaidi juu ya usimamizi bora wa shughuli za uvuvi. Ukaguzi unapendekeza kuwa ni muhimu kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania kuingiza shughuli za utafiti katika mipango yao ili kuhakikisha ufanyikaji wa tafiti za kina katika usimamizi wa uvuvi nchini.

### **8.5.5 Mipango, Ukaguzi na Adhabu kwa Wavunja Sheria Isiojitosheleza**

Ukaguzi ulibaini baadhi ya changamoto katika upangaji, ukaguzi na utoaji wa adhabu kwa wanaovunja sheria ikihusishwa na usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Maelezo zaidi yametolewa hapa chini:

#### **(a) Mpango wa Shughuli za Ukaguzi na Doria Usiojitosheleza**

Ukaguzi ulibaini kwa ujumla kuwa upangaji wa ukaguzi na doria haukuandaliwa ipasavyo. Hii ilionekana katika watendaji wote muhimu katika sekta ya uvuvi, ikiwa pamoja na Wizara mama, Vituo vya Ulinzi wa Uvuvi, na Serikali za Mitaa.

Haikubainika wazi jinsi rasilimali kwa ajili ya udhibiti wa shughuli za uvuvi zilivyotengwa wakati wa kuandaa mipango mbalimbali. Hakukuwa na vigezo, mbinu au njia zilizotumiwa kwa ajili kugawa rasilimali fedha, watu na vifaa katika maeneo na vituo


Ukosefu wa mipango unaweza kusababisha usimamizi duni wa rasilimali za uvuvi, na hivyo kuongeza shughuli haramu katika sekta ya uvuvi.

**(b) Ukaguzi Usiojitosheleza wa Zana za Uvuvi katika Mipaka**

Ripoti za ukaguzi (2018-2021/23) kutoka maeneo ya mipakani yaliyotembelewa zilibaini kuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi haikukagua uingizwaji wa zana za uvuvi kupitia mipaka mbalimbali ya nchi. Aidha, mapitio ya ripoti za utekelezaji wa Wizara za mwaka 2021/22 na 2022/23 yalionesha ongezeko la utaifishaji zana haramu za uvuvi aina ya wavu wa nailoni kutoka 223,324 hadi 362,509, mtawaliwa, sawa na ongezo la asilimia 38.

**Kielelezo Na. 41** kinaonesha idadi ya zana haramu za uvuvi ambazo bado zinatumika katika sekta ya uvuvi nchini Tanzania

**Kielelezo Na. 41: Hali ya Matumizi ya Zana Haramu Katika Tasnia ya Uvuvi Nchin**



*Chanzo: Ukaguzi wa Shughuli za Uvuvi<sup>17</sup>*

<sup>17</sup> Ripoti ya Utafiti wa Uvuvi wa Ziwa Tanganyika 2022, Ripoti ya Matokeo ya Utafiti wa wa Ziwa Victoria 2020 na Utafiti wa Uvuvi wa Bahari 2018

**Kielelezo Na. 41** kinaonesha kuna uwapo mkubwa wa zana haramu za uvuvi aina ya nyavu za nailoni katika Ziwa Victoria na makokoro ya kina kirefu katika maeneo ya bahari.

Mambo yaliyosababisha ukaguzi wa vifaa vya uvuvi visiyoridhisha katika maeneo ya mipaka ya nchi yamefafanuliwa hapa chini:

### ***Ukosefu wa Wakaguzi wa Kutosha Mipakani***

Timu ya Ukaguzi ilitembelea mipaka na kugundua kuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi haikuwa na Maofisa wa kutosha mipakani. Kwa mfano, katika mpaka wa Sirari, kulikuwa na afisa mmoja tu aliyekuwa anafanya kazi usiku na mchana. Kwa mujibu wa mahojiano na watumishi hawa, ukaguzi wa usiku haukufanyika ipasavyo kutokana na ukosefu wa watumishi wa kutosha, tofauti na Bandari ya Dar es Salaam, ambapo kulikuwa na watumishi wawili walioweza kufanya kazi kwa zamuya mchana na usiku. Hata hivyo, Wizara ya Mifugo na uvuvi haikuchukua hatua yoyote kuhakikisha uwapo wa watumishi kwenye mipaka.

### ***Vifaa vya Ukaguzi Visivyojitosheleza katika Mipaka***

Timu ya Ukaguzi ilibaini kuwa Maofisa katika eneo la mpaka wa Sirari, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere na bandari ya Dar es Salaam hawakuwa na vifaa vya kutosha kufanya shughuli za ukaguzi. Ingawa mizigo yote inayopita mpaka ilichunguzwa, wakaguzi wamegundua kuwa hakukuwa na uchunguzi wa uingizaji wa zana haramu za uvuvi. Hii ilithibitishwa na skana iliyokuwapo kutokuwa na uwezo wa kuchunguza zana haramu za uvuvi.

Ukosefu wa ukaguzi wa karibu wa zana za uvuvi ulisababisha kuongezeka kwa matumizi ya zana haramu katika shughuli za uvuvi. Zana hizi zina madhara makubwa, kwa mfano nyavu za nailoni zinaweza kusababisha uchafuzi wa mazingira katika maziwa na bahari.

### **(c) Utoaji wa Adhabu usiokuwa na Tija**

Ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatayo kutokana na ufanisi wa adhabu zilizotolewa kwa ukiukwaji wa sheria:

(i) **Utoaji wa Adhabu Haukusimamiwa Ipasavyo**


Ukaguzi ulibaini kuwa matukio ya uvuvi haramu yamekuwa yakijirudia, na mamlaka husika hazikufuata hatua za kisheria za kutokomeza matukio yao, badala yake, walikuwa na nia ya kupata mapato kutokana na matukio hayo kupitia faini na tozo mbalimbali.

Tatizo hili la uvuvi haramu husababisha kupungua kwa uwapo wa samaki nchini kupitia matumizi ya zana haramu za uvuvi. Uvuvi haramu hupelekea uvuaji wa samaki wachanga na wasiofikia vigezo vya kuvuliwa. Pia, wavuvi haramu hushughulikiwa katika mazingira ya nchi kavu wakati tayari kuna uharibifu ambao umekwisha fanyika majini.

(ii) **Mashtaka ya kesi za uvuvi hayakushughulikiwa kwa usahihi**

Mapitio ya mafaili ya utekelezaji kutoka katika Serikali za Mitaa zilizokaguliwa hayakuonesha kesi yoyote iliyopelekwa mahakamani. Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilikuwa na kesi mbalimbali zilizopatikana katika ukaguzi wa mafaili ya utekelezaji kutoka vituo vya udhibiti. **Kielelezo Na. 42** kinatoa maelezo ya ziada.

**Kielelezo Na. 42: Makosa ya Uvuvi Haramu Yaliyofanyika kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2022/23**



**Vyanzo:** Ripoti ya Hali ya Kesi ya kutoka katika Vituo vya Kanda vya Udhibiti (2018/19 hadi 2022/23)

**Kielelezo Na. 42** kinaonesha kuwa Ziwa Victoria lilipata jumla ya idadi wahalifu kesi 68. Kati ya kesi hizi 68 zilizowasilishwa mahakamani, ni kesi 22 tu ndizo zilizoamuliwa kwa kuwapendelea watuhumiwa, zikiwakilisha kiwango cha asilimia 32.

Aidha, ripoti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya mwaka 2021/22 imeonesha kuwa ni kesi thelathini tu zilizofunguliwa dhidi ya watuhumiwa 1687, na ni kesi saba tu kati ya 1,070 zilizosajiliwa mahakamani katika mwaka 2022/23.

Hali hii ilitokana na mambo yafuatayo:

### ***Utunzaji wa Nyaraka Usiojitosheleza***

Ukaguzi ulibaini kutolingana katika nyaraka za utekelezaji. Hakuna Halmashauri hata moja iliyokuwa na faili maalumu la kuwekea kumbukumbu kwa matumizi mbalimbali. Mbali na hilo, Halmashauri hazikuwa na faili maalumu la kwa ajili ya kutunza nyaraka za hali za kesi za wahalifu waliokamatwa na Polisi. Maofisa wa Halmashauri walieleza kuwa huwa wanapata taarifa kutoka katika mafaili yanayoshughulikiwa na polisi.

### ***Ukosefu wa Mafunzo ya kutosha kwa watumishi***

Mapitio ya mpango wa mafunzo na ripoti za utekelezaji kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi zilionyesha kuwa Wizara na Mamlaka za Serikali za Mitaa haikufanya mafunzo juu ya sheria ya uvuvi na ukiukwaji ili kusaidia upatikanaji wa ushahidi wa kutosha kwa polisi wakati wa kuandaa mashtaka. Hii imesababisha uandishi wa mashtaka usiojitosheleza. Kwa hiyo, ushahidi wa kesi haukuwasilishwa kwa usahihi, na uliishia kutoa hukumu inayopendelea mkosaji.

### ***Kuingiliana kati ya Malengo ya Kukusanya Mapato na Uhifadhi***

Kulingana na mahojiano na Maofisa wa uvuvi kutoka katika Halmashauri zilizotembelewa pamoja na vituo vya udhibiti, ilibainika kuwa halmashauri ziliandaa doria mbalimbali kwa ajili ya kukusanya mapato. Vilevile, vituo vya udhibiti vilipewa majukumu mawili, moja kukusanya mapato na lingine kufanya doria kwa ajili ya ufuatiliaji na uzuiaji wa uvuvi haramu.

## 8.6 Athari katika kufikia malengo ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Mendeleo Endelevu

Sehemu hii inatoa maelezo ya athari za kaguzi za ufanisi katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Maelezo zaidi katika eneo hili yametolewa hapa chini:

Serikali imehakikisha matumizi endelevu ya maliasili kwa kuandaa mikakati na jitihada mbalimbali. Hata hivyo, kwa kulingana na ukaguzi huu, ilibainika kuwa kulikuwa na upungufu katika kutekeleza mikakati na juhudi hizi. Hii, ilileta changamoto katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, kama ilivyoelezwa hapa chini:

Kuhusu ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi wa fukwe, ilibainika kuwa fukwe hizo hazikusimamiwa kikamilifu ili kuhifadhi makazi ya asili na kukuza utalii. Hii ilidhihirishwa na utekelezaji mdogo wa mikakati na mipango ya kusimamia fukwe na meneno ya pwani kwa ujumla.

Mapungufu haya ni kinyume na matakwa ya Mpango wa Pili na Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambayo inasisitiza kuwezesha mazingira rafiki ya sekta ya utalii. Hii inahatarisha ufikiaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu hususani lengo na. 14 ambalo, linatoa wito kwa nchi kubuni na kutekeleza sera za kuhifadhi na kutumia kifasaha rasilimali za baharini kwa maendeleo endelevu.

Vilevile, ukaguzi katika uwezeshaji wa wachimbaji wadogo wa madini ulibaini mapungufu katika kuwasaidia wachimbaji hawa, hii ilitokana na upatikanaji usioridhisha wa taarifa za kijiolojia pamoja na teknolojia ya uchimbaji na uchenjuaaji wa madini. Hii inahatarisha ufikiaji wa malengo katika Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, ambao unalenga kuwawezesha wachimbaji wadogo katika kufanya shughuli za uchimbaji wa madini. Vilevile, hali hii inahatarisha ufikiaji wa Lengo Na. 8 la Malengo ya Maendeleo Endelevu ambalo linalenga kukuza uchumi jumuishi na endelevu, ajira kamili na yenye tija kwa wachimbaji wadogo.

Aidha, ukaguzi katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi ulibainisha usimamizi usiojitosheleza wa rasilimali hizi kama inavyohibitishwa na mapungufu katika kutekeleza, kufuatilia na kudhibiti sekta hii. Hii haiendi sambamba na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambayo inasisitiza kuimarisha udhibiti wa rasilimali za uvuvi, biashara ya bidhaa za uvuvi na kuhifadhi maeneo ya uvuvi wa samaki. Sambamba na hili, mapungufu haya yanahatarisha ufikaji wa Lengo Na. 14 la Malengo ya Maendeleo Endelevu ambalo linalenga uhifadhi na matumizi endelevu ya bahari na rasilimali zake kwa maendeleo endelevu.





## USIMAMIZI WA UINGIZAJI WA MAFUTA

### 9.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa matokeo na hitimisho yatokanayo na Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Usimamizi wa Uingizaji wa Mafuta nchini. Sura hii pia inaelezea uhusiano kati ya eneo lililokaguliwa na Mpango wa Pili na wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu. Pia inaelezea mikakati na jitihada zilizochukuliwa na Serikali pamoja na ushabiliano wa athari za usimamizi wa uingizaji wa mafuta katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano.

#### 9.1.1 Usuli Kuhusu Usimamizi wa Uingizaji wa Mafuta

Uingizaji wa Mafuta nchini kupitia Mfumo wa Ununuzi wa Mafuta wa Pamoja umeongezeka kwa kiasi kikubwa kwa miaka ya hivi karibuni kutokana na ukuaji wa mahitaji ya bidhaa za ndani na za kusafirisha nje za nchi. Kwa mfano, kuanzia mwaka 2019 hadi 2022, uingizaji wa mafuta aina ya petroli umeongezeka kwa asilimia 31 na diseli kwa asilimia 37.

Vilevile, nchi ina mtandao wa vituo 23 vya kupokea mafuta bandarini na vituo 29 mikoani vyenye uwezo wa kuhifadhi mafuta kwa kiasi cha mita za ujazo 1,484,869.

Kwa mujibu wa Sheria ya Petroli ya mwaka 2015 [Sura ya 392], mnyororo wa usambazaji mafuta nchini Tanzania unasimamiwa kuanzia kwenye makadirio ya mafuta yanayohitajika hadi kuwafikia walaji wa mwisho. Vivyo hivyo, kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta, 2015 (Sura ya 392), mnyororo wa usambazaji wa mafuta unasimamiwa na Wizara ya Nishati kama mwangalizi mkuu wa sekta ya mafuta nchini.

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji hudhibiti na kusimamia taasisi kama Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja ambao ndio wenye dhamana ya uendeshaji wa mfumo wa Uagizaji wa Mafuta. Wakati huohuo, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania linajukumu la kuanzisha na kuendesha hifadhi ya Taifa ya Mafuta kwa mujibu wa kanuni ya 7 ya kanuni za Taifa za Uhifadhi wa Mafuta Kimkakati za Mwaka 2014.

### 9.1.2 Uhusiano wa Ukaguzi kuhusu Usimamizi wa Uagizaji wa Mafuta na Mpango wa Pili na wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Uingizaji wa Mafuta unahusiana na Mpango wa pili na wa tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 55**.

**Jedwali Na. 55: Uhusiano wa Uagizaji wa Mafuta na Mpango wa Pili na wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu**

Mpango	Eneo la Kipaumbele	Eneo la Kimkakati
Mpango wa pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano	Uhimilifu wa Uchumu	Utayari katika kukabiliiana na ongezeko la bei ya mafuta
Mpango wa tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano	Kukuza Uhimilifu wa Kiuchumi	Kuweka mazingira mazuri ya uendeshaji wa viwanda vya ndani
Malengo ya Maendeleo Endelevu	Lengo la 8. kukuza ukuaji endelevu na jumishi wa uchumi, ajira ya kudumu na yenye tija na kazi staha kwa wote	Shabaha 8.1: Kuendeleza ukuaji wa uchumi wa kila mtu kulingana na hali ya kitaifa na, angalau asilimia 7 ya ukuaji wa pato la taifa kwa mwaka katika nchi zilizoendelea

*Source: Uchambuzi wa Wakuguzi wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu*

**Jedwali Na. 55** linaonesha kuwa Mpango wa Pili na wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano; na Malengo ya Maendeleo Endelevu inasisitiza upatikanaji wa vitu muhimu vinavyokuza maendeleo ya kiuchumi nchini. Upatikanaji wa mafuta unawezesha maendeleo ya sekta zote kama vile sekta ya viwanda, usafirishaji, kilimo nk.

### 9.1.3 Mikakati na Jitihada za Serikali katika Usimamizi wa Uingizaji wa Mafuta

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanya jitihada mbalimbali kupitia Wizara ya Nishati, Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, na Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja katika kusimamia uagizaji wa mafuta ili kuhakikisha uwapo wa usalama wa usambazaji wa mafuta nchini, kama ifuatavyo:

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wakala Uagizaji Mafuta kwa Pamoja imeweka Mfumo wa Ufuatiliaji wa mafuta na Upakiaji ambao uliundwa kufuatilia kikamilifu taarifa za papo kwa papo za ushushaji wa mafuta katika vituo 22 vya Dar-Es-Salam, Tanga, na Morogoro. Kwa kipindi cha Januari 2024, mfumo huo ulikuwa katika hatua ya majaribio na ulitarajiwa kukabidhiwa Machi 2024. Uwapo wa mfumo huu utapunguza upotevu wa mafuta wakati wa ushushaji.

Pia, Serikali kupitia Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji imeweka Mfumo wa Taifa wa Taarifa za Petroli na Gesi ambao umetengenezwa kwa ajili ya kufuatilia na kutunza taarifa za mafuta ya petroli na gesi asilia zitokanazo na shughuli za mkondo wa kati na wa chini wa petroli Tanzania Bara. Mfumo huu umeundwa kuisaidia Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji kubaini kiasi cha mafuta katika vituo vya kupokelea na vituo vya uuzaji rejareja wa mafuta.

Aidha, Serikali kwa kupitia Mamlaka ya Bandari Tanzania imetoa tuzo ya mkataba wa ujenzi wa kituo kimoja cha kupokea mafuta kwa kipindi cha miezi 24 ili kutatua tatizo la ucheleweshaji wa ushushaji wa mafuta.

Sambamba na hilo, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania imepanga kukarabati tanki la mafuta Na. 8, lililopo ndani ya majengo ya TIPER, na kujenga matenki mapya karibu na TIPER ili kutengeneza ghala la kuhifadha.

## 9.2 Malengo na Mawanda ya Ukaguzi

### 9.2.1 Lengo kuu la Ukaguzi

Lengo kuu la ukaguzi lilikuwa kutathmini kama Wizara ya Nishati kupitia Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, na Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja, imesimamia ipasavyo uingizaji wa mafuta ili kuhakikisha kuna mafuta yanayotosha nchini Malengo mahsusi ya ukaguzi huu yalikuwa ni kutathmini kama Wizara ya Nishati kupitia Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji, Shirika la Maendeleo

ya Petroli Tanzania, na Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja imehakikisha kuwa:

- (a) Ukadiriaji wa mahitaji ya mafuta unafanyika ipasavyo;
- (b) Uagizaji na Upokeaji wa mafuta unafanyika ufanisi;
- (c) Miundombinu ya uhifadhi wa mafuta inatosheleza kwa ajili ya hifadhi za kawaida na za kimkakati;
- (d) Ufuatiliaji wa mara kwa mara wa kiwango cha mafuta kilichopo unafanyika kwa ufanisi; na
- (e) Uratibu na Upimaji wa utendaji kazi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, na Wakala wa Uagizaji Mafuta kuhusu uagizaji wa mafuta kama unafanyika kwa ufanisi.

### 9.2.2 Mawanda ya Ukaguzi

Taasisi kuu iliyokaguliwa ilikuwa Wizara ya Nishati kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, na Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja. Hii ni kwa sababu Wizara ya Nishati ndiyo muandaaji na msimamizi wa sera kwenye sekta ya mafuta inayojumuisha usimamizi wa uagizaji wa mafuta nchini. Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, ilikaguliwa kwa sababu ni chombo cha udhibiti chenye jukumu la kudhibiti mafuta yanayoingizwa nchini.

Kwa upande mwingine, Wakala wa Uagizaji Mafuta unahusika na uagizaji wa mafuta kupitia mfumo wa ununuzi wa mafuta kwa pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, ina jukumu la kuanzisha na kuendesha hifadhi ya Kimkakati ya mafuta nchini.

Ukaguzi huu ulijikita zaidi kwenye kungalia namna usimamizi wa uagizaji wa mafuta unavofanywa na Wizara ya Nishati kutipia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Wakala wa Uingizaji Mafuta kwa Pamoja na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania ili kuhakikisha uwapo wa mafuta ya kutosha kwenye mnyororo wa usambazaji wa mafuta nchini.

Hususan, ukaguzi uliangalia kama makadirio wakati wa kuainisha mahitaji yalifanyika ipasavyo, ufanisi wa mchakato wa kuagiza na kupokea mafuta, uwapo wa mafuta ya kutosha kwa ajili ya matumizi ya kawaida na yale ya kimkakati.

Ukaguzi pia uliangazia ufanisi wa mifumo iliyowekwa ya ufuatiliaji wa kiwango cha mafuta kilichopo. Vilevile, ukaguzi uliangalia masuala ya uratibu na ufanisi

wa Wizara ya Nishati kwenye kupima utendaji wa Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, na Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja.

Ukaguzi huu ulijikita katika kipindi cha miaka mitatu ya fedha, kuanzia mwaka 2020/2021 hadi 2022/2023.

### 9.3 Matokeo ya Ukaguzi katika Usimamizi wa Uingizaji wa Mafuta nchini

Sehemu hii inatoa muhtasari wa matokeo katika usimamizi wa uingizaji wa mafuta nchini. Maelezo ya ziada yametolewa hapa chini:

#### 9.3.1 Makisio, Uagizaji na Upokeaji wa Mafuta

Sehemu hii inatoa matokeo ya ukaguzi katika makisio, uagizaji na upokeaji wa mafuta unaofanywa na Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja ili kuhakikisha upatikanaji wa mafuta ya kutosha nchini, kama ifuatavyo:


##### (a) Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja Haukuchambua na Kuainisha Mwenendo wa Mauzo ya Mafuta wakati wa Kukisia Mahitaji ya Mafuta

Ukaguzi ulibaini kuwa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja hakuchambua taarifa ya mauzo ya mafuta ili kuainisha mwenendo wa mauzo ya mafuta nchini kutoka kwa kila Kampuni inayoagiza mafuta. Badala yake, Wakala alikuwa anapokea taarifa zilizochambuliwa kutoka Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji na kuainisha kiwango cha kuagiza kwa mwezi husika. Hii inamaanisha kuwa Wakala hakufanya kikamilifu uchambuzi wa historia ya mauzo ili kuainishwa mwenendo wa mafuta nchini.

Hali hii ilitokana na Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja kutegemea taarifa zilizochambuliwa na Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji.

Hali hii inatengeneza mazingira ya kuagiza kiasi kidogo kuliko mafuta yanayohitajika kwa matumizi ya ndani (rejea *kielelezo Na. 42 na 43*) na kusababisha Kampuni za Uagizaji wa Mafuta kutumia mafuta yaliyoagizwa kwa ajili ya kusafirisha nje za nchi kwa ajili ya mahitaji ya ndani ilikuepuka kuwa na upungufu wa mafuta kwenye soko (rejea *Kielelezo Na. 43*).


**Kielelezo Na. 43: Mwenendo wa Uagizaji na Utumiaji wa Mafuta ya Dizeli kuanzia mwaka 2019 hadi 2022**



*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kwa Taarifa za Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Mafuta kuanzia mwaka 2019 hadi 2022*

Kielelezo Na. 43 kinaonesha kuwa ni kwa mwaka 2019 pekee, ambapo kiasi cha mafuta yaliyoagizwa kilikuwa juu kuliko kiasi cha mafuta yaliyohitajika. Pia, hali hiyo ilishuhudiwa katika uagizaji na utumiaji wa mafuta aina ya petroli kama ilivyowasilishwa katika Kielelezo Na. 44.

**Kielelezo Na. 44: Mwenendo wa Uagizaji na Utumiaji wa Mafuta ya Petroli kuanzia mwaka 2019 hadi 2022**




*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kwa Taarifa za Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Mafuta kuanzia mwaka 2019 hadi 2022*

**Kielelezo Na. 44** kinaonesha kuwa, kwa mwaka 2019 na 2022, kiasi cha mafuta ya petroli yaliyoagizwa kilikuwa chini ya kiasi cha mafuta yaliyotumika.

Mapungufu yaliyobainishwa katika **Kielelezo Na. 42** na **43** yalitokana na changamoto katika kukisia mafuta ya kuagizwa kwa ajili ya matumizi ya ndani hali iliyopelekea kutumia mafuta yaliyoagizwa kwa ajili ya kusafirisha nje za nchi kwa ajili ya mahitaji ya ndani (rejea **Kielelezo Na. 45**).

**Kielelezo Na. 45: Hali ya Matumizi ya Ndani ya Mafuta yaliyoagizwa kwa ajili ya Kusafirisha Nje za Nchi kuanzia mwaka 2019 hadi 2022**



*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kwa Taarifa za Mamlaka ya Udhhibiti wa Maji na Mafuta kuanzia mwaka 2019 hadi 2022*

**Kielelezo Na. 45** kinaonesha kuwa, kuanzia mwaka 2019 hadi 2020, kulikuwa na ongezeko la matumizi ya ndani ya mafuta yaliyoagizwa kwa ajili ya nchi za nje. Pia ilionyesha kuwa kuanzia mwaka 2020 hadi 2022, kiasi hicho cha mafuta kilionekana kutoongeza kwa upande wa mafuta ya petroli na dizeli.


**(b) Makampuni 10 kati ya 33 (sawa na asilimia 30) ya Uagizaji wa Mafuta hayakukidhi Masharti ya Kuagiza Kiasi cha Mafuta Kilichotarajiwa**

Aya ya 10.2 (a) ya Mwongozo wa Utekelezaji wa Mfumo wa Ununuzi wa Mafuta kwa Pamoja wa mwaka 2020, inaitaka Wakala kupokea na kutathmini kiwango cha mafuta kilichoagizwa na Makampuni ya Uagizaji wa Mafuta, kilingana na dhamana ya benki/fedha taslimu ya asilimia 5, malipo ya tozo kwa Wakala na Taasisi zingine za serikali, na malipo ambayo hayakufanyika kwa kipindi cha nyuma.

Mapitio ya kiasi cha mafuta kilichoagizwa na Makampuni ya Uingizaji wa Mafuta kwa ajili ya matumizi ya mwezi septemba, 2023, na dhamana zilizowasilishwa kwa ajili ya uagizwaji wa mafuta, yalionesha kuwa ni kampuni 10 kati ya 33

(sawa na asilimia 30) hazikukidhi vigezo vya kuagiza mafuta kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 46**.

**Kielelezo Na. 46: Asilimia ya Makampuni ya Mafuta yaliyokidhi Vigezo**



**Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa kiwango kilichoagizwa na dhamana iliyowekwa, 2023**

**Kielelezo Na. 46** kinaonesha kuwa asilimia 30 ya Makampuni ya Uagizaji wa Mafuta hayakidhi vigezo vya kuagiza kiasi hicho cha mafuta.

Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja iliainisha kuwa kutokana na Mgogoro wa Kidiplomasia kati ya Urusi na Ukraini, na mabadiliko katika sera za fedha za Marekani yalisababisha Wakala kupuuza baadhi ya masharti ya kuhakikisha upatikanaji wa mafuta nchini.

Hali hii inahatarisha ufanisi wa Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja hasa pale Makampuni ya Uagizaji wa Mafuta yatakaposhindwa kukamilisha malipo na kuacha nafasi ya kuhusu ushushaji wa mafuta kutoka kwenye tenki.

**(c) Mwenendo wa Ucheleweshaji wa Kuanza Kupakua Mafuta uliongezeka kutoka asilimia 66 hadi 68 kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 na 2022/23 mtawalia**

Maupitio ya mikataba kati ya Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja na waingizaji wa mafutana pamoja na ya kumbukumbu za utoaji wa mafuta, ukaguzi ulibaini uwapo wa ucheleweshaji wa kuanza kupakua mafuta



uliongezeka kutoka asilimia 66 hadi 68 kwa 2020/21 na 2022/23 mtawalia kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 56**.

**Jedwali Na. 56: Asilimia ya Meli Kuchelewa Kuanza Kupakua**

Mwaka wa Fedha	Idadi ya Meli	Jumla ya Meli zilizopakua Mafuta kwa Wakati	Jumla ya Meli zilizochelewa kupakua Mafuta	% ya kuchelewa kuanza kupakua
2020/21	107	36	71	66
2021/22	110	36	74	67
2022/23	104	33	71	68

*Chanzo: Uchambuzi wa wakaguzi wa Mkataba na Taarifa za Ushushaji, 2023*

Kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 56**, kwa miaka yote ya fedha ucheleweshaji ulikuwa juu ya asilimia 50 na mwenendo wake uliendelea kuongezeka kutoka asilimia 66 mwaka 2020/2021 hadi asilimia 68 mwaka 2022/2023.

Uchambuzi zaidi wa kiwango cha ucheleweshaji unaoneshwa katika **Jedwali Na. 57**.

**Jedwali Na. 57: Kiwango cha Ucheleweshaji**

Mwaka wa Fedha	Jumla ya Meli zilizochelewa kupakua Mafuta	Hali ya Ucheleweshaji		
		Siku 0 hadi 7	Siku 7 hadi 14	Zaidi ya siku 14
2020/21	71	44	20	7
2021/22	74	57	15	2
2022/23	71	35	21	15

*Chanzo: Uchambuzi wa wakaguzi wa Mkataba na Taarifa za Upakuaji wa Mafuta, 2023*

**Jedwali Na. 57** linaonesha kuwa idadi ya Meli zilizochelewa kuanza kupakua mafuta kuanzia siku 7 hadi 14 na zaidi ya siku 14 ilikuwa kubwa katika mwaka wa fedha 2022/23 kuliko miaka iliyopita.

Aidha, mapitio ya ripoti ulionesha kuwa meli mbili zilichelewa kuanza kupakua kwa zaidi ya siku 30 kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Uwapo wa changamoto ya miundombinu na kutofuata tarehe iliyopangiwa meli ya kuanza kupakua mafuta, kulisababisha Meli kuchelewa kuanza kushusha kwa wakati. Kwa hiyo, kwa kipindi kilichokaguliwa, jumla ya dola za Marekani 26,934,426.35 kama gharama ya meli kuchelewa kuanza kupakua mafuta (Rejea **Jedwali Na. 58**), na mwenendo wa Meli kuchelewa kupakua uliongezeka kutoka asilimia 27 hadi 35.

**Jedwali Na. 58: Tozo kwa Kuchelewa kuanza kupakua Mafuta**

Mwaka wa Fedha	Idadi ya Meli zilizochelewa	Jumla ya Siku zilizochelewa	Jumla ya Tozo
2020/21	71	453	8,241,890.75
2021/22	74	329	6,322,120.00
2022/23	71	636	12,370,415.60
<b>Jumla</b>	<b>216</b>	<b>1,418</b>	<b>26,934,426.35</b>

*Chanzo: Uchambuzi wa wakaguzi wa Mkatoba na Taarifa za Upakuaji wa Mafuta, 2023*

**Jedwali Na. 58** linaonesha kuwa takribani Dola za Marekani 26,934,426.35 zilitozwa kwa kuchelewa kuanza kupakua mafuta.

Kupitia barua yenye Kumb. Na. MB. 108/431/12/106 ya tarehe 29 Novemba, 2023 kutoka Mamlaka ya Bandari Tanzania kwenda kwa mkandarasi, ilionesha kuwa Serikali kupitia Mamlaka ya Bandari Tanzania imetoa tuzo kwa mjumuiiko wa kampuni ya China Railway Major Bridge Engineering na kampuni ya WUHUAN Engineering kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya upokeaji wa mafuta kwa pamoja. Mradi huu unapaswa kutekelezwa ndani ya kipindi cha miezi 24 ili kutatua changamoto ya uchelewaji wa kupakua mafuta.

**(d) Kampuni za Uagizaji wa Mafuta hazikulipa Gharama za Ucheleweshaji kwa Wauzaji wa Mafuta kwa Wakati**

Mapitio ya taarifa zilionesha uwapo kwa madai ambayo hayajalipwa, kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 59**.

**Jedwali Na. 59: Hali ya Tozo za Kuchelewa Kupakua Mafuta kama ilivyokuwa tarehe 22 Septemba 2023**

Wauzaji	Salio la jumla katika Dola za Marekani hadi kufikia Juni 2023	Tozo katika Dola za Marekani kama ilivyokuwa tarehe 22 Septemba 2023
Muuzaji 1	983,108	2,627,858
Muuzaji 2	90,275	0.00
Muuzaji 3	6,294	590,452
Muuzaji 4	241,154	1,720,810
Muuzaji 5	1,012,182	0.00
Muuzaji 6	0.00	42,917
Muuzaji 7	0.00	351,123
Muuzaji 8	470,469	1,216,761
Muuzaji 9	0.00	270,224
Muuzaji 10	43,880	288,763
<b>Jumla</b>	<b>2,847,365</b>	<b>7,108,913</b>

*Chanzo: Uchambuzi wa wakaguzi wa Mkatoba na Taarifa za Upakuaji wa Mafuta, 2023*

**Jedwali Na. 59** linaonesha hadi kufikia Juni 2023, jumla ya Dola za Marekani 2,847,365.86 zilikuwa hazijalipwa. Pia, ilionesha kuwa hadi 22 Septemba 2023, kiwango cha tozo ambazo zilikuwa hazijalipwa ziliongeza hadi jumla ya Dola za Marekani 7,108,913.

Hata hivyo ilibainika kuwa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja umefanya maboresho kwenye Mwongozo wa Utekelezaji wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja ili kuhakikisha Kampuni za Uagizaji wa Mafuta zinalipa tozo za uchelewesahaji wa kupakua mafuta kwa wakati, Mwongozo huu unakusudia kujumuisha vifungu ambavyo vitaupa wakala, mamlaka za kukusanya tozo kwa wadaiwa kwa niaba ya wauzaji.

### 9.3.2 Ufuatiliaji wa Uwapo wa Mafuta na Usimamizi wa Sekta ya Mafuta

Sehemu hii inaonesha matokeo ya Ukaguzi katika mfumo wa kuhakikisha uwapo wa mafuta ili kukidhi mahitaji pamoja na mfumo wa utoaji wa taarifa ya uwapo wa mafuta kama ilivyoelezewa hapa chini:

**(a) Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji haikuweza kubaini Makampuni ya Uagizaji Mafuta ambayo yalikuwa na Mafuta ya kuweza kutumia chini ya siku 15**

Kupitia uchambuzi wa taarifa ya mafuta ya wiki ya 1 na ya 3 ya kila mwezi kutoka mwaka 2020 hadi 2023, ukaguzi ulibaini kuwa kati ya asilimia 12 hadi 62 (kwa petroli) na asilimia 14 hadi 65 (kwa dizeli) ya kampuni za uagizaji wa mafuta hazikuhifadhi mafuta yanayotosheleza kutumika kwa siku 15.

Hii ilitokana na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kutathmini upatikanaji wa mafuta kwa jumla badala ya mafuta yaliyopo katika kila Kampuni ya Uagizaji wa Mafuta. Hali hiyo inapunguza uwezekano wa kubaini Makampuni ya Uagizaji wa Mafuta yanayoshindwa kufikia vigezo.

Pia, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji haikutoa taarifa ya soko la hisa kwa kila bidhaa ya mafuta, hali hii ilipunguza uwezo wa Mamlaka wa kufuatilia na kubaini ufuataji wa taratibu zilizopo na vihatarishi katika mnyororo wa usambazaji wa mafuta nchini.

Hali hiyo, iliathiri usahihi katika kutathmini kiwango cha mafuta kilichohifadhiwa na Makampuni ya Uagizaji wa Mafuta, hali ambayp inaweza kuhatarisha mnyororo mzima wa upatikanaji na usambazaji wa mafuta nchini.

**(b) Mfumo wa Taifa wa Taarifa za Mafuta na Gesi haufanyi kazi Ipasavyo**

Kifungu cha 124(1) cha Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015 kinaeleza kuwa kutakuwa na Mfumo wa Taifa wa Taarifa za Mafuta na Gesi ambao utajengwa na kuendeshwa na Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji. Ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatayo:

- (i) Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji haujafanikiwa kuunganisha Mfumo wa Taifa wa Taarifa za Mafuta na Gesi ili kupata taarifa ya kiwango cha mafuta na gesi kwa njia ya kielektroniki na moja kwa moja***

Katika kupitia Mfumo wa Taifa wa Taarifa za Petroli na Gesi, ukaguzi ulibaini kuwa, ingawa mfumo huo ulikuwa ukifanya kazi mbashara na ulianza kutumika katika Kituo cha Taifa cha Taarifa za Petroli na Gesi tangu Novemba, 2021, lakini haujafanikiwa kupata taarifa ya uwapo wa mafuta kwa njia ya kielektroniki na moja kwa moja.

Mapitio ya taarifa ya ukaguzi wa shughuli za mafuta kwa mwaka wa fedha 2022-23 yalionesha kuwa hali hii ilitokana na kuchelewa kwa utambuzi wa waendeshaji wa mfumo wanaofaa ili kuwezesha uunganishaji wa taarifa wa moja kwa moja.

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ilichukua miaka miwili kuanzisha juhudi za kuunganisha Mfumo wa Kitaifa wa Mafuta na Gesi na mifumo ya waendeshaji ili kuwezesha kubadilishana taarifa kupitia mtandao moja kwa moja. Sababu nyingine iliyochangia ilikuwa kutegemea kupokea taarifa kwa njia ambayo sio ya kimtandao.

Hali hiyo, ilisababisha mfumo huo kutokuwa na taarifa za papo kwa papo za utendaji wa taasisi mbalimbali zinazosimamiwa na Wakala.

- (ii) Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji haikuchukua hatua kuhakikisha Makampuni ya Uagizaji wa Mafuta na zinazouza rejareja zinawasilisha kila taarifa za kiwango cha mafuta kilichopo kupitia Mfumo***

Kanuni ya 30 ya Mafuta (Wauzaji wa Jumla, Uhifadhi, wauzaji wa rejareja, na Watumiaji) ya 2022 inaelekeza wote wenye vibali vya kufanya biashara za mafuta kutoa taarifa kwa Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji. Mamlaka ilianzisha Mfumo wa Taarifa wa Mafuta na Gesi ambayo inazitaka

Kampuni za Uagizaji wa mafuta kutoa taarifa kwa Mamlaka kila siku kwa njia ya mtandao au ujumbe mfupi.

Katika kupitia Mfumo wa Taarifa wa Mafuta na Gesi ukaguzi ulibani kuwa wafanyabiashara hawa hawakuwasilisha taarifa kikamilifu kwenye Mfumo wa Taifa wa Mafuta na Gesi kuhusiana na kiwango cha mafuta walionayo. Na wale waliofanikiwa kuwasilisha hawakufanya hivyo kila siku kama kanuni inavyowataka.

Ukaguzi ulibaini kuwa kati ya makampuni 26 kati ya 65 yaliyopewa kibali kuuza mafuta kwa jumla (sawa na asilimia 40) ziliwasilisha zenye mapungufu.

***(iii) Mfumo wa Taifa wa Taarifa za Mafuta na Gesi haujaunganishwa na Taasisi nyingine za Serikali***

Mapitio ya Mfumo wa Taifa wa Taarifa za Mafuta na Gesi ukaguzi ulibaini kuwa, mfumo huo haukuunganishwa na mifumo mwingine au Taasisi zingine. Mapungufu haya yaliathiri upatikanaji wa taarifa kwa ajili ya ufuatiliaji, upangaji na kufanya maamuzi mbalimbali.

**9.3.3 Miundombinu ya Kupokea na Kuhifadhi Mafuta**

Sehemu hii inaonesha matokeo ya ukaguzi katika miundombinu ya upokeaji na uhifadhi wa mafuta kwa matumizi ya kawaida au ya kimkakati ilikuhakikisha usalama wa usambazaji wa mafuta nchini kama ifuatavyo:

**(a) Kukosekana kwa kituo cha Pamoja cha kupokea Mafuta**

Mapitio ya taarifa ya utendaji wa sekta ya mafuta kwa mwaka 2020 na 2021, yalionesha kuwa, hakuna kituo cha kupokea mafuta ya petroli cha pamoja. Kituo hicho kingehakikisha mafuta yanapokelewa kwa wakati na kingepunguza tozo zinazohusiana na ucheleweshaji wa utoaji wa mafuta.

Kwa kipindi cha mpito, Serikali aliamua kutumika miundombinu inayomilikiwa na Kampuni ya TIPER kama kituo cha kupokea mafuta kwa Pamoja. Hata hivyo, kutokana na ukosefu kwa miundombinu inayotosheleza, kituo hiki hakikuwa na uwezo wa kutunza mafuta ya diseli ya kutosha.

Kupitia barua yenye Kumb. Na. MB. 108/431/12/106 ya tarehe 29 Novemba, 2023 kutoka Mamlaka ya Bandari Tanzania kwenda kwa mkandarasi, ilionesha kuwa Serikali kupitia Mamlaka ya Bandari Tanzania imetoa tuzo kwa mjumuiko wa kampuni ya China Railway Major Bridge Engineering na kampuni ya WUHUAN

Engineering kwa ajili ya ujenzi wa ujenzi wa mradi miundombinu ya upokeaji wa mafuta kwa Pamoja. Mradi huo utakatekwa kwa kipindi cha miezi 24 ili kupunguza tatizo la uchelewashaji wa upakuaji wa mafuta.

### 9.3.4 Uratibu na Ufanisi kwenye Upimaji wa Utendaji


Sehemu inaonesha matokeo ya ukaguzi kuhusu uratibu na upimaji wa utendaji ili kuhakikisha upatikanaji wa mafuta ya kutosha nchini kama ifuatavyo:

#### (a) Wizara ya Nishati haikuandaa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Miundombinu ya Mafuta

Katika mapitio ya taarifa za utendaji wa Wizara ya Nishati kwa mwaka 2018/19-2022/23, ukaguzi ulibaini kuwa kwa miaka mitano wizara haikuweza kuandaa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Miundombinu ya Mafuta. Hata hivyo, katika mapitio ya Taarifa ya Utendaji wa Mwaka wa Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/22, iligundulika kuwa Wizara imeanza kuandaa andiko la awali la utekelezaji shughuli ya Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Miundombinu ya Mafuta (*Rejea Kielelezo Na. 9.5*).

Mwenendo wa Utekelezaji wa malengo ya Wizara ya Nishati Maendeleo ya PIDMP unaonyeshwa kwa mpangilio katika **Kielelezo Na. 46:**

#### Kielelezo Na. 47: Mtiririko wa Jitihada kwenye Uandaaji wa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Miundombinu ya Mafuta



**Chanzo:** *Uchambuzi wa Wakaguzi wa Mpango na Hali halisi ya Utekelezaji, 2023*

**Kielelezo Na. 47** kinaonesha kuwa katika mwaka 2020/21 Wizara ya Nishati ilifanikiwa kufanya uchambuzi wa hali, pia, katika mwaka wa fedha 2021/22 wizara iliweza kuandaa andiko la awali, ili kuongeza uendelevu kwenye mnyororo wa usambazaji na matumizi ya mafuta.

Wizara kwa sasa inatafuta mfadhili wa kufadhili maandalizi ya Mpango Mkuu wa Miundombinu ya Petroli. Kwa upande mwingine, ukaguzi uligundua kuwa kutopewa kipaumbele kwa maandalizi ya mpango huu kulisababishwa na kutoandaliwa kwa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Miundombinu ya Petroli hadi Septemba 2023.

Ukosefu wa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Miundombinu ya Petroli unaweza kuzuia uratibu wa Wizara ya Nishati wa maendeleo ya miundombinu ya petroli, na kusababisha kurudia kwa jitihada za serikali na kujenga mazingira ya kutokuwa na uhakika kwa wawekezaji, wadau wa sekta, na washirika wa biashara kutokana na majukumu yasiyoeleweka kati ya watendaji muhimu wa serikali.

**(b) Wizara ya Nishati haikupima Utendaji kazi wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, na Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja kuhusiana na Usimamizi wa Uingizaji wa Mafuta**

Wizara ya Nishati haikufanya ya kutosha katika kusimamia usalama wa upatikanaji wa mafuta. Hii ilichangiwa zaidi na mapungufu katika utendaji wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, na Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja katika kusimamia uingizaji wa mafuta. Ukaguzi huo ulibaini mapungufu yafuatayo.

***(i) Wizara ya Nishati haikupanga kupima ufanisi wa Taasisi Zake (Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, na Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja) kuhusiana na Usimamizi wa Uingizaji wa Mafuta***

Mapitio ya jalada la mawasiliano kati ya Wizara na Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, na Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja, ukaguzi haukuweza kuona taarifa inayoonesha utendaji taasisi zake kuhusiana na uagizaji wa mafuta nchini.

Hii ilitokana na ukosefu wa mpango wa kupima utendaji wa taasisi hizi. Kwa mujibu wa mapitio ya mipango mikakati ya Wizara ya Nishati kwa mwaka 2021/22-2025/26, ukaguzi ulibaini kuwa Wizara haikupanga kufanya upimaji wa utendaji wa shughuli zinazotekelezwa na taasisi zake.

**(ii) Wizara ya Nishati ilichambua Ripoti 3 kati ya 156 za kila wiki za kiwango cha mafuta kutoka Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kuanzia 2020/21 hadi 2022/23**

Kwa mujibu wa mapitio ya ripoti ya wiki ya mafuta kutoka Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kwenda Wizara ya Nishati, ukaguzi ulibaini kuwa, asilimia 2 tu ya taarifa hizo za wiki zilichambuliwa na Wizara. Maofisa wa Wizara walionesha kuwa ripoti hizo zilikuwa hazichambuliwi pale inapoonesha kuwa mafuta yaliyopo yanatosheleza. Ripoti hizo zikuwa zinaonesha jumla ya mafuta yanayopatikana nchini, sio mafuta yanayohifadhiwa na kila Kampuni ya Uagizaji wa Mafuta kwa kuzingatia ukubwa wa soko lake lamafuta nchini.

Ukosefu huu wa taarifa unaweza kusababisha Wizara kutochukua hatua stahiki. Taarifa za kiwango cha mafuta zinazotolewa kwa jumla zinaleta hatari ya uhaba wa mafuta na kupunguza uwezo wa Wizara kufanya maamuzi sahihi kuhusu sera za nishati na usambazaji wa mafuta.

**9.4 Athari katika kufikia malengo ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu**

Sehemu hii inaonesha Ushabiliano wa Athari za kufanya Ukaguzi wa ufanisi kwenye Usimamizi wa Uingizaji wa Mafuta na Mpango wa pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu kama inavyooneshwa hapa chini:

Wizara ya Nishati na Taasisi zake (Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, na Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja) ilikuwa na jukumu la kuhakikisha wa usalama wa ugavi wa mafuta nchini ili kuhamasisha maendeleo. Hata hivyo, kutokana na Ukaguzi uliofanyika, ilibainika kuwa mikakati na jitihada zilizowekwa hazikufanyika kwa tija na kwa ufanisi ipasavyo kama inavyooneshwa hapo chini.

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania halikuanzisha hifadhi ya kimkakati ya mafuta ambayo ingewezesha utulivu wa bei wa mafuta wakati wa dharula kama vile mgogoro wa kidiplomasia kati ya Urusi na Ukraine na mabadiliko ya sera ya fedha ya Marekani.

Pia, Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja ulikadiria kiwango kidogo cha mafuta kwa ajili ya matumizi ya ndani ukilinganisha na mafuta yaliyokuwa yakihitajika. Hali hiyo, ilisababisha kutumia mafuta ya kusafirisha kwenda nje kwa ajili ya matumizi ya ndani.



Aidha, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, haikubaini Kampuni ya Uagizaji wa Mafuta ambazo hazikuhifadhi mafuta ya kuweza kutumika kwa siku 15 kwa wakati wote. Hii inahatarisha upatikanaji wa mafuta nchini na kuadhiri ufikiaji wa Mpango wa Mendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano katika kukuza utulivu wa uchumi na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya kukuza ukuaji wa uchumi endelevu.



## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 10.1 Utangulizi

Sura hii inatoa hitimisho kwa kuzingatia mapitio na uchambuzi wa matokeo kutoka kwenye ripoti 14 za ukaguzi wa ufanisi zilizofanyika na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/24. Pia inaonesha mapendekezo yaliyotolewa kwa taasisi zilizokaguliwa.

### 10.2 Hitimisho la Ujumla

Ukaguzi huo unatambua juhudi zilizofanyika na taasisi zilizokaguliwa katika kuboresha utendaji wao ili kufikia malengo ya Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Mpango wa Maendeleo Endelevu ambao lengo lake kuu lilikuwa kuboresha uchumi na maendeleo ya binadamu. Jitiada hizo zilizochukuliwa zilibainika wakati wa kutekeleza maeneo mbalimbali ya kipaumbele katika eneo la huduma za afya, shughuli za kilimo, maendeleo ya rasilimali watu, mipango miji, bima na mikopo, maliasili na uingizaji mafuta.

Licha ya jitihada zilizochukuliwa na taasisi zilizokaguliwa kwenye kaguzi hizo 14 katika kuhakikisha kuwa malengo ya Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Mpango wa Maendeleo Endelevu yanatimizwa, ukaguzi ulibaini uwapo cha changamoto ambazo zinazuia kufikia malengo yaliyohitajika.

Mapungufu yaliyobainishwa katika maeneo yaliyotajwa yanahitaji kuchukua hatua kwa haraka ili kuhakikisha kuwa malengo ya Serikali yenye lengo la kukuza uchumi na maendeleo ya watu kama yalivyoainishwa katika Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Mpango wa Maendeleo Endelevu yanafikiwa.

### 10.3 Hitimisho Mahsusi

#### (i) *Usimamizi wa Huduma za Afya*

Ukaguzi unahitimisha kuwa Wizara ya Afya, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hazijahakikisha ipasavyo upatikanaji wa Huduma za Afya ya Akili unaochangiwa na upungufu katika kuwatambua watu wenye changamoto za kiakili, utoaji wa huduma za kisaikolojia katika jamii. ngazi ya jamii, kutoa rasilimali, kutoa huduma kamili za ukarabati, na kuhakikisha utoaji wa programu za uhamasishaji. Matokeo yake, kuna ongezeko la idadi ya watu wenye changamoto za afya ya akili ambao wamekuwa hawapati huduma za afya ya akili ipasavyo.

Pia, Ukaguzi unahitimisha kuwa Wizara ya Afya na Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania imedhibiti ipasavyo vifaatiba katika ufanisi, ubora na usalama kutokana na kutokuwapo kwa usajili, matengenezo na ubora wa vifaa vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi na kutathmini utendaji wa vifaatiba katika afya. Hii ni kwa sababu Wizara ya Afya na Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania hawajahakikisha ipasavyo usajili wa kutosha wa vifaatiba, matengenezo ya vifaatiba, ubora wa vifaatiba vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi, na utendaji wa vifaatiba katika vituo vya afya. Kutokana na hali hiyo, hakukuwa na utoaji wa kutosha wa huduma za uchunguzi hali iliyosababisha huduma za afya zinazotolewa na Vituo vya Afya ya Umma nchini kuwa duni.

#### (ii) *Usimamizi wa Shughuli za Kilimo*

Ukaguzi huu unatambua jitihada zilizooneshwa na Wizara ya Kilimo kupitia Bodi zake za Udhibiti wa Mazao na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania. Hata hivyo, mapungufu kadhaa yalibainika, na kuna wito wa hatua za kuboresha zaidi. Hakuna njia za wazi za kuainisha kiasi cha mazao ya biashara yatakayovunwa kwa msimu husika, na hii ni kwa sababu hakuna mipango ya uzalishaji ambayo imewekwa kama sehemu ya mipango ya mwaka ya taasisi. Sababu nyingine iliyobainishwa ni kutopatikana kwa Maofisa ugani kwa ajili ya kusimamia uzalishaji. Aidha, hakuna mfumo uliowekwa wa kuainisha gharama za uzalishaji wa mazao, ambao unaweza kutumika kama msingi wa kuweka bei elekezi. Mbali na hilo, bodi za mazao zilizotembelewa zina idadi ndogo ya masoko kutokana na ukosefu wa mikakati imara ya soko na utaftaji wa masoko mapya. Udhibiti duni wa mazao ya biashara umesababisha kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya biashara na hali hii imepelekea kupungua kwa mchango wa mapato kwenye Pato la Taifa.

Kwa upande mwingine, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea pamoja na Wizara ya Kilimo hazidhibiti kwa ufanisi usambazaji wa mbolea ili kuhakikisha upatikanaji

wa mbolea kwa wakulima. Kazi za udhibiti zinazofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea hazitoshi kuhakikisha upatikanaji wa mbolea bora zinazosambazwa sokoni. Pia, kuna vituo vichache vya usambazaji wa mbolea, na hali hii inaathiri upatikanaji wa mbolea kwa wakulima. Aidha, mpango wa ruzuku haufanyi kazi kwa ufanisi kwani uendeshaji wake umekuwa na udhaifu kama vile ukosefu wa vifurushi vya mbolea, na zaidi ya hayo asilimia 59 ya wauzaji wa mbolea si hai. Udhibiti usioridhisha wa mbolea unasababishwa na uwapo wa makisio ya mahitaji ya mbolea yasiyo na ufanisi kwani kuna Maofisa ugani wachache. Kuchelewa kwa upatikanaji wa mbolea kwa wakulima kumechangia matumizi duni ya mbolea. Hii imepelekea makisio ya mbolea kuwa juu kuliko matumizi halisi katika maeneo husika kwa asilimia 14 hadi 48.

### ***(iii) Usimamizi wa Maendeleo ya Raslimali Watu***

Ukaguzi unahitimisha kuwa, pamoja na jitihada kubwa za kuhakikisha udhibiti wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ya Elimu kupitia Baraza la Elimu la Ufundi halijahakikisha vya kutosha udhibiti na utoaji wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi nchini. Kwa ujumla, Ukaguzi ulibaini upungufu wa tathmini juu ya Elimu ya Ufundi inayotolewa kwenye vyuo vya ufundi inayoakisi mahitaji ya soko la ajira kutokana na upungufu wa tafiti za programu zilitolewa na Vyuo vya Ufundi, Upungufu katika mchakato wa utoaji wa usajili na lthibati za vyuo vya Ufundi na upungufu katika uidhinishaji wa Mitaala inayoendana na soko la ajira. Hii ilichangiwa na upungufu wa tathmini za Mahitaji yanayoakisi soko la Kazi ajira, Kukosekana kwa Mfumo wa utoaji taarifa ya kuhusu hali ya Usajili na idhini za Vyuo vya Ufundi, Hakukuwa na barua za ukumbusho zilizotumwa kwenye Vyuo vya Ufundi vilivyotembelewa juu ya hali ya Mitaala iliyoisha muda wake. Hivyo, kuna hatari ya Taasisi za Ufundi kutozingatia viwango vya usajili na uidhinishaji wa Vyuo vya Ufundi ambao unaweza kusababisha Elimu ya Ufundi na Mafunzo yanayotolewa kutokidhi viwango vya ubora unaohitajika, hivyo, wahitimu wanaweza kushindwa kwenye kushindana kwenye soko la ajira.

Aidha, pamoja na juhudi zilizofanywa na OR-MUUUB kuhusu kuendeleza taasisi za umma kwenye umahiri wa watumishi, hatua ambazo zimepitishwa hazikufanikiwa katika kushughulikia mapungufu ya umahiri yaliyopo kwa watumishi wa umma. Kumekuwa na idadi ndogo ya zana za kutathmini umahiri wa watumishi kabla au baada ya hatua za kujenga umahiri ndani ya Taasisi za Umma. Taasisi za umma zinahitaji mbinu za ubunifu na tofauti katika kutekeleza shughuli za umahiri na mipango ya kujenga uwezo ambayo itaongeza umahiri wa watumishi na kuwezesha utoaji bora wa huduma za umma. Hii ilisababishwa na kutokuwapo kwa zana maalumu ya usimamizi au mfumo wa kutathmini umahiri ulioendelezwa na kutokuwapo kwa mipango ya kujenga uwezo kwa Watumishi wa Umma. Kwa hivyo, ufuatiliaji wa umahiri wa watumishi

hautapatikana vya kutosha, kwani hali ya awali ya kuwezesha ufuatiliaji wa wafanyakazi haijafikiwa ili kuwezesha usimamizi wa kutosha wa watumishi. Lakini pia kumekuwa na idadi ndogo ya zana za kutathmini uwezo wa watumishi kabla au baada ya hatua za kujenga uwezo ndani ya taasisi za umma

Japokuwa kuna jitihada zinazofanywa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Jeshi la Magereza Tanzania katika kusimamia na kutoa programu bora za urekebishaji wafungwa. Ukaguzi unahitimisha kuwa programu za marekebisho kwa wafungwa hazikutekelezwa kwa ufanisi. Hii inasababishwa na ukosefu wa mitaala na miongozo ya magereza kwa ajili ya uendelezaji rasmi wa mipango ya urekebu, uainishaji na utengano wa wafungwa ulijikita kwenye jinsia na umri pekee, miundombinu isiyotosheleza ya uainishaji, shughuli za msingi za gereza zinaamua uainishaji, na ukosefu wa sera na miongozo ya uainishaji wa wafungwa; na Kukosekana kwa mipango rasmi ya kuunganisha wafungwa wanaotarajia kukamilisha kifungo chao. Matokeo yake, kunaongezeko la wafungwa asilimia 1.5 kwa wastani kutoka mwaka 2019/20 hadi 2023/24.

**(iv) Usimamizi wa Mipango miji**

Ukaguzi unahitimisha kuwa, licha ya juhudi kubwa za kuboresha usimamizi wa mipango miji, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hazijasimamia ipasavyo usanifu, upangaji, na utekelezaji wa shughuli za upangaji miji ili kutengeneza mazingira bora na ya kupendeza ya kuishi na kufanya kazi. Hii ni kwa sababu ya Usanifu na uendelezaji wa Mipango miji usiyojitoshesheleza, Skimu za Mipango miji zilizoandaliwa hazikutekelezwa kwa ufanisi, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais -Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kupitia Serikali za Mitaa hazikusimamia ipasavyo utekelezaji wa skimu za mipango miji na Mipango kabambe na hazikufuatilia na kutathmini utendaji wa Halmashauri katika shughuli za mipango miji.

Sababu ya kutofanya vizuri ilihusishwa na kutofuata viwango vinavyohitajika vya mipango miji, upungufu wa rasilimali watu na rasili mali fedha kuwezesha shughuli za upangaji miji na maendeleo ya miji zilibainika kuwa mbele ya Mipango ya kina iliyoandaliwa. Matokeo yake, usanifu na uendelezaji wa skimu za mipango miji haikufanyika kwa wakati na kuchelewesha umilikishaji wa viwanja kwa wananchi. Hivyo basi mazingira yaliyokusudiwa ya kupendeza ya miji kwaajili ya kuishi, kufanya kazi, na burudani hayakufikiwa kwa wakati.

**(v) Usimamizi wa Bima na Mikopo ya Elimu Juu**

Ukaguzi unahitimisha kuwa, pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania katika kuwasimamia Watoa huduma za Bima Nchini, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania haiwasimamii ipasavyo Watoa huduma za Bima ili kuhakikisha kuwa wanafanya kazi zao katika uthabiti

kisheria, kiufundi na kifedha unaohitajika. Kwa ujumla, ukaguzi ulibaini kuna usimamizi usioridhisha wa madai ya bima; ukaguzi usioridhisha unaofanywa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania kwa Makampuni ya Bima; ufuatiliaji usiotosheleza wa hali ya kifedha kwa Makampuni ya Bima Nchini; kutolipwa kwa madai ya bima kwa wakati, haki, na kwa uwazi na Makampuni ya Bima; na tathmini duni ya kiwango cha uelewa na kuridhika kwa Wateja wa Bima juu ya huduma za bima.

Usimamizi na ufuatiliaji usioridhisha wa Watoa huduma za Bima Nchini unachangiwa zaidi na; kucheleweshwa kwa ulipaji wa madai yaliyoidhinishwa na Makampuni ya Bima, kuwapo kwa janga la UVIKO-19 ambalo lilisababisha ongezeko la madai ya bima za maisha, kutotosheleza kwa mipango ya ukaguzi inayozingatia athari, uwapo wa gharama kubwa za usimamizi wa kampuni za bima na kupungua kwa malipo ya jumla, ufuatiliaji usioridhisha katika kuhakikisha Makampuni ya Bima yanawekeza angalau asilimia 50 ya mtaji wa hisa zilizolipwa kama amana ya dhamana katika Benki Kuu ya Tanzania. Hali hii ilisababisha; wamiliki wa sera kukabiliwa na ugumu wa kifedha kutokana na ucheleweshaji wa kupata malipo yao ya bima; athari za kisheria, kama vile migogoro na adhabu za kisheria; uwezekano wa kurudiwa kwa makosa yanayofanywa na makampuni ya bima, na wamiliki wa Sera za Bima wanaweza kubaki bila kulipwa fidia endapo Kampuni za Bima zisizo na amana Benki Kuu ya Tanzania zitafilisika.

Pia, ukaguzi unatambua jitihada zinazofanywa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu katika kusimamia urejeshaji wa mikopo kutoka kwa wanufaika ili kuhakikisha mfuko unakua endelevu. Hata hivyo, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, haikusanyi ipasavyo marejesho ya mikopo ya wanafunzi kwa sababu bado inategemea ruzuku kutoka serikalini kuwezesha ufadhili mzuri wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Kwa ujumla, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu haihakikishi kuwa mikopo ya wanufaika iliyoiva inakusanywa ipasavyo; utabiri wa malengo ya urejeshaji mikopo ni sahihi na wa kuaminika; Ufuatiliaji wa wanufaika wa mikopo unafanywa vya kutosha ili kuimarisha urejeshaji wa mikopo; Usimamizi wa madeni unafanywa vya kutosha ili kuimarisha ulipaji wa mkopo; na urejeshaji wa mikopo unafanyika kwa wakati na ipasavyo.

Utendaji usioridhisha wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Nchini katika ukusanyaji wa urejeshaji wa mikopo ulichangiwa na; uanzishaji wa sera ya ukadiriaji ya asilimia sifuri, utabiri usiotosheleza wa malengo ya urejeshaji wa mikopo, ufuatiliaji, utoaji ankara, na urejeshaji wa mikopo usioridhisha. Hivyo basi, ustahimilivu wa Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu unakabiliwa na tishio kubwa kutokana na kutokuwapo kwa ufanisi katika michakato ya urejeshaji wa mikopo. Aidha, kuongezeka kwa kiwango cha

mikopo ambayo haijarejeshwa kunaweza kuhatarisha uwezo wa Bodi wa kusaidia wanafunzi katika siku zijazo.

**(vi) Usimamizi wa Maliasili**

Hitimisho la ukaguzi huu ni kuwa, pamoja na jitihada za kuboresha utendaji ili kuhakikisha matumizi endelevu ya fukwe, Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hazijahakikisha usimamizi wa kutosha wa fukwe nchini. Hii ilidhihirishwa na uendelezaji wa fukwe usiojitosheleza kuwezesha ufanyikaji wa shughuli za kitalii. Pia ilibainika kuwa muuundo wa utendaji wa Wizara hizi hauwezi kuhamasisha ipasavyo masuala ya uendelezaji, uhamasishaji na utangazaji wa fukwe zilizopo nchini. Hali hii ilisababishwa na ukosefu wa fedha za kutosha kushugulikia masuala yahasuyo uendelezaji, uhamasishaji na utafutaji wa masoko kwa ajili ya fukwe. Kwa namna hiyo kuna hatari ya kupunguza uchangiaji wa sekta ya fukwe katika uchumi wa taifa kutokana na ukosefu wa utaratibu mzuri wa uratibu baina ya wadau na watendaji wakuu katika sekta hii.

Aidha, ukaguzi huu unatambua jitihada za Serikali katika kuboresha hali ya shughuli za uchimbaji mdogo wa madini nchini. Hata hivyo, Wizara ya Madini haijahakikisha uwezesaji wa kutosha kwa wachimbaji wadogo. Hii ilioneshwa na upatikanaji usiojitosheleza wa taarifa za kijiolojia, uwapo wa mashapo na taarifa za masoko ya madini; ukosefu wa mtaji kwa ajili ya uwekezaji pamoja na ukosefu wa teknolojia bora ya uchimbaji madini na uchenjuaji wa madini kwa wachimbaji wadogo. Hali hii ilitokana na Wizara kutohakikisha upatikanaji, uratibu na ufuatiliaji wa rasilimali unajitosheleza kwa ajili ya kuwawezesha wachimbaji wadogo. Changamoto hizi zinarudisha nyuma juhudi za kukuza sekta ndogo ya madinin nchini.

Vilevile, ukaguzi unatambua juhudi za Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi nchini. Hata hivyo, Wizara hizi hazikuhakikisha usimamizi mzuri wa rasilimali hizo. Kwa ujumla, ukaguzi ulibaini uwapo wa shughuli za uvuvi haramu; utekelezaji usiojitosheleza wa mbinu za usimamizi wa rasilimali za uvuvi; mapungufu katika kupanga, ukaguzi na utoaji wa adhabu kwa wavunjaji wa sheria na taratibu, pamoja na mapungufu katika usimamizi wa kanzidata ya uvuvi nchini. Mambo haya yalitokana na ukosefu wa rasilimali za kuwezesha utekelezaji wa mipango mbalimbali pamoja na uratabu usiojitosheleza baina ya wadau wa sekta hii ya uvuvi. Mdahara ya changamoto hizo ni uwapo wa uthibiti mdogo wa sekta hii na hivyo kuhatarisha uendeleu wa shughuliz uvuvi nchini.

**(vii) Usimamizi wa Uingizaji wa Mafuta**

Pamoja na jitihada zilizochukuliwa na Wizara ya Nishati Pamoja na Taasisi zake, ukaguzi unahitimisha kuwa Wizara na Taasisi zake ambazo ni Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania, na Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja hazisimamii ipasavyo mchakato wa Uingizaji wa Mafuta ilikuhakikisha usalama wa ugavi wa mafuta nchini. Ukisiaji wa mafuta, uagizaji na upokeaji haufanyiki ipasavyo, na miundombinu ya kupokea na kuhifadhi mafuta ya kimkakati haitoshelezi, hali hii inaleta hatari za ugavi na kusababisha kuongezeka kwa gharama ya mafuta. Hali hiyo imetokana na Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kutopima utendaji kazi wa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja na kutotathmini mafuta yaliyokuwa yanahifadhiwa na Kampuni ya Uagizaji wa Mafuta na vituo vya uuzaji wa mafuta ipasavyo. Pia, Wizara ya Nishati haikufuatulia ipasavyo utendaji wa taasisi zake kwenye uingizaji wa mafuta nchini. Hali hiyo inahatarisha ugavi wa mafuta Pamoja na kuongezeka kwa bei ya bidhaa hiyo.

**10.4 Mapendekezo ya Ukaguzi**

Sehemu hii inawasilisha mapendekezo yaliyotokana na uchambuzi wa changamoto zilizobainishwa kwenye ripoti hii. Ili kufanyia kazi mapungufu yaliyobainishwa kwenye usimamizi wa rasilimali watu, huduma za afya, shughuli za kilimo, maendeleo ya rasilimali watu, mipango miji, bima na mikopo na uingizaji wa mafuta, taasisi zilizokaguliwa zinashauriwa kutekeleza mapendekezo ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama inavyofafanuliwa hapa chini:

- (i) Wizara ya Afya inatakiwa kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya ya akili katika ngazi zote za vituo vya afya ili kuhakikisha kuwa wananchi wenye uhitaji wanapata huduma sahihi ya afya ya akili kwa wakati, na kuhakikisha vifaatiba vinasimamiwa ipasavyo ili kuhakikisha kunakuwa na usalama na ubora kwenye huduma za afya zinazotolewa na vituo vya afya nchini;
- (ii) Wizara ya Kilimo inatakiwa kuteua wakaguzi wa mazao ya biashara sambamba na kuhakikisha wanakuwa na vitendea kazi, ambao watawajibika moja kwa moja kwenye bodi zao za mazao ili kurahisisha ufuatiliaji wao na kuwafanya wawajibike kwenye Menejiment ya Bodi ya Usimamizi wa Mazao;
- (iii) Wizara ya Kilimo inatakiwa kutathmini ufanisi wa mifumo ya ununuzi ya mbolea kama vile mfumo wa pamoja wa manunuzi wa mbolea na mifumo mingine iliyopo, na kutumia matokeo yake katika kutatua



mapungufu yote yaliyoainishwa ili kuwezesha ununuzi na usambazaji wa mbolea kwa wakati ili kukidhi mahitaji ya mbolea;

- (iv) Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi wanatakiwa kufanya tathmini ya kina na endelevu ya uhitaji wa soko la ajira ili kuainisha mahitaji mapya ya ujuzi na kuhakikisha kuwa mitaala inayoandaliwa inazingatia soko la ajira;
- (v) Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inapaswa kuchukua hatua ya kuhakikisha kila Taasisi ya Umma ina mipango ya kutosha ya kutambua mapengo ya umahiri ili kuyaziba na kuwa na nguvu kazi yenye ujuzi, uelewa, mwenendo na tabia zinazohitajika ili kukabiliana na changamoto za sasa na za baadaye kwenye Taasisi za Umma;
- (vi) Wizara ya Mambo ya Ndani na Jeshi la Magereza wanatakiwa kuandaa na kutekeleza mitaala ya mafunzo ya urekebu kwa wafungwa ili kurahisisha utekelezaji wa programu za urekebu;
- (vii) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zinahimizwa: Kuandaa mikakati madhubuti ya kuwezesha usimamizi mzuri wa utekelezaji wa shughuli za Mipango miji nchini. Mikakati hiyo inapaswa kuwezesha kuwa na ufanisi katika usanifu, Upangaji, na utekelezaji wa shughuli za mipango miji ili kuwezesha kufikia kwa wakati malengo yaliyokusudiwa;
- (viii) Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania inapaswa kuimarisha mifumo ya kuhakikisha Kampuni za Bima zinawekeza mtaji wa kutosha ili kukidhi viwango vya vya ukwasi vinavyohitajika kisheria. Mifumo hiyo inapaswa kuhakikisha Kampuni za Bima zinaandikisha bima kwa faida huku zikipunguza gharama zao za usimamizi kulingana na malipo halisi ya bima;
- (ix) Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Nchini inatakiwa kuainisha wanufaika wa mikopo wanaodaiwa kwa siku au miezi kadhaa na kuweka mipaka ya wazi kati ya urejeshaji na urejeshwaji wa mikopo ili kuimarisha ufanisi katika ukusanyaji wa mikopo kutoka kwa wanufaika wenye changamoto za urejeshaji;
- (x) Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara Maliasili na Utalii na Kitengo cha Uhifadhi wa Bahari na Maeneo Tengefu wanatakiwa kuboresha uratibu na ufuatiliaji wa ufanisi wa fukwe ili kuhamasisha uendelevu, na kutangaza utalii wa fukwe;

- (xi) Wizara ya Madini inatakiwa kuhakikisha inawasaidia wachimbaji wadogo kwa kuwezesha upatikanaji wa taarifa za kijiolojia, teknolojia ya uchimbaji uchenjuaaji wa madini pamoja na utengaji na matumizi ya rasilimali za kutosha kuwasaidia wachimbaji hao;
- (xii) Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zinatakiwa kuhakikisha ufuatiliaji, udhibiti na shughuli za uchunguzi ili kukabiliana na uvuvi haramu nchini; na
- (xiii) Wizara ya Nishati inatakiwa kuweka mkazo uanzishaji wa mpango wa maendeleo ya miundombinu ya mafuta na kuratibu uendelezaji wa miundombinu ya kupokelea mafuta kwa Pamoja.

## VIAMBATANISHO

## **Kiambatisho 1: Uhusiano wa Kaguzi za Ufanisi zilizotekelezwa na Maeneo ya Kipaumbele ya Mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu**

Kiambatisho hiki kinaelezea uhusiano uliyopo kati ya kaguzi za Ufanisi zilizotekelezwa na Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu.

### **(a) Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Upatikanaji wa Huduma za Afya ya Akili Nchini**

Ukaguzi unahusishwa na uendelezaji wa rasilimali watu ikiwa ni sehemu ya maeneno mahususi ya Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Shughuli zinazohusishwa na ukaguzi huu ni shughuli za afya ambapo zinalenga kuimarisha utoaji wa huduma maalumu za kitaalamu katika ngazi za hospital za Taifa na rufaa, ikiwemo ujenzi n ukarabati wa vituo vya afya jumuishi. Hivyo basi, ukaguzi huu unalenga kuimarisha mifumo ya usimamizi wa shughuli za afya, kuboresha upatikanaji na utoaji wa huduma na kutatua changamoto za ubora wa huduma za afya.

Upatikanaji wa huduma za afya ya akili ni jambo la msingi nchini hasa kwenye kuimarisha maendeleo ya rasilimali watu. Hii ni kama ambavyo imeanishwa kwenye Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambao unalenga kuimarisha huduma za afya ikiwemo afya ya akili.

Ukaguzi huu pia unachangia utekelezaji wa lengo namba 3 lengo dogo 3.4 la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ambalo linalenga kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa watu wa rika zote ikiwemo afya ya akili.

Zaidi, ukaguzi unachangia lengo namba 10 kwa kuweka mkazo kwenye usawa wa upatikanaji wa huduma za afya ya akili. Pia, lengo namba 4 linalolenga kuimarisha upatikanaji wa elimu na mafunzo ya huduma za elimu ya afya ya akili. Vilevile, Lengo namba 11 na 17 ambayo yanalenga katika kuimarisha ushirikishwaji wa huduma za afya ya akili na kuhakikisha kuwa kwenye uendelezaji wa jamii kwenye miji na vijiji inahusisha upatikanaji wa afya ya akili.

## **(b) Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Udhhibiti wa Vifaatiba katika Hospitali na Vituo vya Afya vya Umma**

Ukaguzi unachangia katika utekelezaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambao unalenga kuimarisha maendeleo ya rasilimali watu. Eneo hili linalenga kuimarisha utekelezaji wa shughuli za afya ambazo zinalenga kuweka mkazo kwenye shughuli za chanjo na viwanda vya madawa na vifaatiba. Vilevile, inahimiza uwapo wa madawa, usambazaji wa madawa, chanjo na vitendanishi.

Kadhalika, inahimiza na kuwezesha uwekezaji wa sekta binafsi katika mnyororo wa madawa na vifaatiba; pia kuandaa na kuanzisha taratibu sahihi za utunzaji wa madawa na vifaatiba. Hivyo basi, ukaguzi huu utaimarisha usimamizi wa shughuli za afya na upatikanaji wa huduma za afya.

Vilevile, ukaguzi huu unachangia utekelezaji wa lengo namba 3 lengo dogo 3.4 la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ambalo linalenga kuhakikisha uwapo wa jamii yenye afya bora kwa rika zote. Kupitia kaguzi huu utachangia uwapo wa chanjo na madawa kwa magonjwa ambukizi na yasiyo ambukizi.

Hivyo basi, kupitia ukaguzi huu, mkazo umewekwa katika kupunguza vifo visivyotarajiwa kutoka kwenye magonjwa yasiyo ambukizi kwa theluthi moja kwa kutumia njia za kujikinga, kupata matibabu na kuhamasisha afya ya akili.

## **(c) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Udhhibiti wa Mazao**

Ukaguzi huu unahusishwa na eneo la kipaumbele kinachohusu kuchochea uchumi shirikishi na shindani na utoaji wa huduma.

Hususani, ukaguzi huu umejikita kwenye shughuli za kilimo zinazolenga kuimarisha muunganiko baina ya sekta za kilimo na sekta zingine za kiuchumi. Shughuli hizo zinalenga kuweka mazingira mazuri kwa sekta binafsi, ili kuwezesha upatikanaji wa faida kwenye uzalishaji na uuzaji wa mazao ghafi na mazao yaliyochakatwa nje ya nchi.

Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unalenga kuimarisha ufanisi na uzalishaji katika sekta ya kilimo kwa kuzingatia uzalishaji wa mazao ya kimkakati na kuimarisha ushindani wa mnyororo wa thamani ya mazao ya kilimo na biashara.

Vilevile, ukaguzi huu unachangia ufikiaji wa lengo namba 8 la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa, hususani lengo dogo 8.2 ambalo linahimiza ongezeko la uzalishaji kwa kutumia teknolojia ya juu, ubunifu huku ikiweka mkazo kwenye sekta ambazo zipo juu kwenye mnyororo wa thamani.

Zaidi, ukaguzi huu unachangia ufikiaji wa lengo namba 2 la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa, lengo dogo 2.3 ambalo linalenga kuondoa njaa, na kuhakikisha usalama wa chakula, kuimarisha lishe na kuhakikisha uwapo wa kilimo endelevu. Lengo dogo 2.3 linalenga kuzingatia ongezeko mara mbili la uzalishaji na kipato kwa wakulima wadogo wadogo. Pia, kujihusisha na malengo mapana ya maendeleo endelevu na ukuaji wa kiuchumi.

#### **(d) Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Usimamizi wa Usambazaji wa Mbolea kwa Wakulima**

Ukaguzi kuhusu usimamizi wa fukwe unahusishwa na shuguli za utekelezaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambao unalenga kuchochea uchumi shirikishi na shindani na utoaji wa huduma. Katika eneo hili la kipaumbele, ukaguzi unahusishwa na utekelezaji wa shughuli za kilimo ambapo inaweka mkazo kwenye kuongeza uzalishaji wa mazao ya kimkakati kwa kutumia mbolea.

Hivyo basi, ukaguzi huu unahimiza usimamizi mzuri wa mbolea kwa lengo la kuongeza mavuno ili kusaidia kupunguza ongezeko la bei za mazao. Hii itawezesha kuongeza upatikanaji wa faida kwa lengo la kunufaisha wananchi kupitia mfumo wa kilimo jumuiishi.

Vilevile, ukaguzi unachangia utekelezaji wa lengo namba 2 malengo madogo 2.3 na 2.4 la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ambalo linalenga kuzuia njaa ili kuwa na usalama wa chakula na kuimarisha lishe na kuwa na kilimo endelevu.

Ukaguzi huu utachangia kuimarisha utekelezaji wa shughuli za kilimo kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo na kipato kwa wakulima wadogo wadogo. Hii itasaidia kuwa na mfumo wa uzalishaji ambao ni endelevu, na kutumia njia za kilimo madhubuti ambazo zinaongeza uzalishaji.

#### **(e) Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Udhhibiti wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo Nchini**

Ukaguzi unachangia katika utekelezaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambao unalenga kuimarisha maendeleo ya rasilimali watu. Hususani, inalenga kuimarisha utekelezaji wa shughuli za elimu na uendelezaji wa ujuzi.

Kwa upande wa elimu bora, ukaguzi utachangia kuweka mkazo kwenye mapitio ya mitaala kwa kuyahusisha na soko la ajira na kuwezesha upatikanaji wa nyenzo za kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu. Kadhalika, ukaguzi utasaidia kuhamasisha ubunifu na tekinolojia ya kupeana habari.

Vilevile, ukaguzi unachangia utekelezaji wa lengo namba 4 lengo dogo 4.3 la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ambalo linalenga kuhakikisha uwapo wa elimu bora, jumuishi na yenye usawa kwa wote. Vilevile, ukaguzi unachangia uwapo wa elimu bora (ya ufundi na vyuo) yenye gharama nafuu kwa wanawake na wanaume.

**(f) Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Maendeleo, Ufuatiliaji na Tathmini ya Uwezo wa Watumishi katika Sekta za Umma**

Ukaguzi huu unachangia utekelezaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa katika eneo la uendelezaji wa rasilimali watu, ambapo mkazo umewekwa kwenye uendelezaji wa ujuzi.

Zaidi ukaguzi unachangia kwenye utekelezaji wa lengo namba 8 lengo dogo 8.5 la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ambalo linalenga kwenye uwapo wa ukuaji wa uchumi jumuishi na endelevu, uwapo wa ajira na kazi bora. Lengo hili linalenga katika kuimarisha utekelezaji wa sera zinaweka mkazo kwenye shughuli za uzalishaji, uwapo wa ajira bora zinazolenga kukuza uchumi na kuimarisha nguvu kazi.

Vilevile, ukaguzi huu unahusishwa na lengo number 4 la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa. Lengo hili linalenga kuangalia namna ambavyo sekta ya umma imeandaa mikakati ya elimu bora ikiwemo tathmini ya matumizi ya tekinolojia kwenye programu za mafunzo ili kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa yanazingatia uhitaji wa soko la ajira.

Ukaguzi pia unaweka mkazo kwenye utekelezaji wa lengo namba 10 la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ambalo linaangalia jukumu la sekta ya umma katika kupunguza matabaka, kuangalia namna ambavyo programu za mafunzo ya watumishi yanazingatia ujumuishi wa makundi yanayokandamizwa. Lengo hili pia linalenga kuhakikisha uwapo wa ushirikishwaji na upatikanaji wa jitihada za kuendeleza ujuzi kwa watumishi wote.

Vilevile, ukaguzi huu unalenga kutathmini ushirikishanaji baina ya sekta za umma, taasisi za elimu, sekta binafsi na mashirika yasiyo ya serikali kwenye kuendeleza ujuzi wa watumishi. Kadhalika, kupitia lengo hili kutachangia kuimarisha utoaji wa huduma za umma.

**(g) Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Utekelezaji wa Programu za Urekebu kwa Wafungwa**

Ukaguzi huu unahusishwa na eneo mahususi moja la Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa unaohusu uendeleu wa rasilimali watu. Hususani, lengo hili linatekeleza shughuli zinazohusu uongozi bora na utawala wa sheria kwa kuhimiza amani, ulinzi na utulivu wa kisiasa. Uongozi bora na utawala wa sheria

ni nguzo muhimu za Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa ambao ni msingi muhimu kwenye kuchangia utekelezaji wa Dira ya Taifa ya mwaka 2025.

Kupitia utekelezaji wa shughuli za urekebu kwa wafungwa, inategemewa itachangia kwenye maboresho ya tabia, ikiwa ni kitu muhimu katika kuimarisha amani, usalama na utulivu wa kisiasa nchini.

Vilevile, ukaguzi huu unachangia utekelezaji wa lengo namba 16 lengo dogo 16.1 la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa. Lengo hili linalenga kuimarisha amani na kuwa na jamii shirikishi yenye maendeleo endelevu; upatikanaji wa haki kwa wote, na kuwa na taasisi imara katika ngazi zote.

Lengo kuu ni kupunguza aina zote za uvunjifu wa amani na kushirikiana na Serikali na jamii katika kuondoa migongano na kukosekana kwa amani. Hivyo basi, kuimarisha utawala wa kisheria.

#### **(h) Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Mipango miji**

Ukaguzi kuhusu Usimamizi wa Mipango miji unachangia utekelezaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kwa kuzingatia uendelezaji wa shughuli za mipango miji, nyumba na maendeleo ya makazi.

Mkakati wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano katika eneo hili ni kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa na miji iliyopangika ikijumuisha kuwapo na usimamizi mzuri wa taka, usafiri bora na ulioimarika na matumizi ya nishati safi. Pia mipango miji inalenga kuhakikisha inakabiliana na changamoto za ongezeko la watu mijini.

Shughuli mahususi katika eneo hili la mipango miji ni kuchochea upangaji wa miji, upimaji na utoaji wa hati za ardhi na makazi; kuandaa mipango kabambe ya mji; kuwa na miradi ya nyumba ya bei rahisi; kuimarisha mfumo jumuishi wa usimamizi wa ardhi; kuunganisha mfumo wa upangaji na usimamizi wa ardhi na mipango ya sekta nyingine; na kuhimiza matumizi ya TEHAMA kwenye shughuli za upimaji na utoaji wa hatimiliki.

Zaidi, shughuli hizi za mipango miji zinachangia utekelezaji wa lengo namba 11 lengo dogo namba 11.3 la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ambalo linalenga kuifanya miji na makazi ya watu kuwa jumuishi, bora na salama. Lengo hili linaweka mkazo kuhusu ukuaji wa miji ambayo ni jumuishi shirikishi na endelevu. Kadhalika inalenga kuwa na upangaji wa makazi endelevu.



Hivyo basi, kwa kutekeleza lengo hili la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa itaimarisha usimamizi wa utekelezaji wa shughuli za mipango miji.

**(i) Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Usimamizi na Ufuatiliaji wa Watoa huduma za Bima Nchini**

Ukaguzi huu unahusishwa na shughuli za utekelezaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Inaweka mkazo kwenye utekelezaji wa shughuli zinazolenga kuulinda jamii kwa kuwaimarisha kiuchumi kwa lengo la kuifanya jamii iweze kukabiliana na uendeshaji wa maisha.

Ukaguzi huu unasaidia kuboresha ulinzi wa jamii katika sekta rasmi na zisizo rasmi, pia, kuhimiza uwekezaji toka sekta binafsi kwenye utoaji wa huduma za kijamii.

Zaidi, ukaguzi huu unalenga kuchangia utekelezaji wa lengo namba 8 lengo dogo 8.10 la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa. Lengo hili linahimiza uwapo wa ukuaji wa uchumi ambao ni shirikishi na endelevu, uwapo wa ajira na kazi za heshima. Utekelezaji wa shughuli za ulinzi wa jamii kwa kuzingatia ulinzi wa kifedha na kukabiliana na athari mbalimbali kunachangia uwapo wa jamii bora na endelevu.

**(j) Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Usimamizi wa Ulipaji wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

Ukaguzi unachangia katika utekelezaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambao unalenga kuimarisha maendeleo ya rasilimali watu. Hasa ukaguzi unaweka mkazo kwenye utekelezaji wa shughuli zinazolenga kuwa na elimu bora kwa kuhakikisha kunakuwa na ongezeko la utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu hasa wale wanaosoma masomo ya sayansi, hesabu na kozi maalumu.

Ukaguzi utasaidia kuongeza idadi ya wanafunzi wanaopata mikopo ya elimu ya juu, hivyo kuongeza idadi ya wahitimu kwa ngazi ya shahada.

Kadhalika, ukaguzi huu unachangia utekelezaji wa lengo namba 4 lengo dogo 4 (b) la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa; ambalo linalenga kuhakikisha uwapo wa elimu bora na kutoa fursa za elimu kwa wote. Hivyo basi, ukaguzi huu unalenga kupanua idadi ya nafasi za ufadhili kwenye elimu ya juu.

### **(k) Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Usimamizi wa Fukwe**

Ukaguzi kuhusu usimamizi wa fukwe unahusishwa na shughuli za utekelezaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambao unalenga kuchochea uchumi shirikishi na shindani na utoaji wa huduma.

Katika eneo hili la kipaumbele, ukaguzi unahusishwa na shughuli za utalii ambazo zinalenga kuweka umuhimu katika sekta ya utalii kwa lengo la kukuza uchumi na kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni. Utekelezaji wa shughuli hizi unachochea ukuaji wa utalii na uendelezaji wa maeneo mapya ya utalii ikiwemo fukwe kwa lengo la kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta.

Zaidi, ukaguzi unahimiza utekelezaji wa shughuli zinazolenga kukuza uchumi wa bluu ambazo zinafanyika kwenye fukwe mbalimbali. Jitihada hizi ziliwekwa ili kukuza shughuli za uwekezaji, uzalishaji, utunzaji wa fukwe na utalii ili kuhakikisha ukuaji endelevu wa fukwe.

Vilevile, ukaguzi huu unachangia utekelezaji wa lengo namba 14 malengo madogo 14.1, 14.2 na 14.7 la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa. Lengo hili linahimiza utunzaji na matumizi endelevu ya bahari na rasilimali za bahari. Hususani, lengo hili linalenga kuzuia uharibifu wa bahari na rasilimali zake zote kwa kuwa na usimamizi endelevu wa bahari na rasilimali zake. Zaidi, inalenga kuhakikisha unufaikaji wa nchi kupitia rasilimali za bahari ikiwemo utalii wa fukwe.

Vilevile, ukaguzi huu unahusishwa na malengo mengine endelevu ikiwemo lengo namba 8 ambalo linalenga kuhakikisha uwapo wa ajira bora na kukuza uchumi, hasa kwa kuimarisha ukuaji wa uchumi ambao ni endelevu kupitia shughuli za utalii wa fukwe na uchumi wa bluu. Lengo namba 13 linalohusu uwapo wa mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya Tabia nchi; na lengo namba 15 linaloweka mkazo kwenye umuhimu wa usimamizi endelevu wa maeneo ya bahari na maeneo ya fukwe.

### **(l) Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Uwezeshaji wa Wachimbaji Wadogo wa Madini**

Ukaguzi kuhusu usimamizi wa fukwe unahusishwa na shughuli za utekelezaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambao unalenga kuchochea uchumi shirikishi na shindani na utoaji wa huduma. Utekelezaji wa shughuli katika eneo hili la kimkakati unalenga kuwajengea uwezo wachimbaji wadogo wa madini ikijumuisha vijana na wanawake kushiriki kwenye shughuli za madini. Kadhalika, inalenga kuimarisha ongezeko la thamani kwenye madini.

Vilevile, ukaguzi huu unachangia utekelezaji wa lengo namba 8 lengo dogo 8.3 la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa, ambalo linalenga kuimarisha ukuaji wa uchumi jumuishi na ajira bora. Kadhalika, lengo hili linalenga kuhimiza uwapo wa sera zenye mrengo wa maendeleo ambazo

zitachangia katika shughuli za uzalishaji, ajira bora, ujasiriamali, ubunifu na kuhamasisha ukuaji wa wachimbaji wadogo na wa kati kupitia taasisi za fedha.

Hivyo basi, ukaguzi huu utaimarisha utekelezaji wa shughuli za uwezeshaji wa wachimbaji wadogo wa madini.

#### **(m) Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi Nchini**

Ukaguzi kuhusu usimamizi wa rasilimali za uvuvi unahusishwa na shughuli za utekelezaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambao unalenga kuchochea uchumi shirikishi na shindani na utoaji wa huduma. Katika eneo hili, inachangia utekelezaji wa shughuli za uvuvi, ambazo zinaweka mkazo kuimarisha sekta ya uvuvi, kulinda maeneo ya uvuvi ya baharini na kwenye maziwa. kulinda rasilimali za baharini na kwenye maziwa ambazo zipo hatarini kutoweka, kuwezesha uwekezaji katika shughuli za uvuvi na kuzipa ubora bidhaa zitokanazo na uvuvi.

Maeneo muhimu katika sekta hii ni pamoja na uvuvi wa baharini na kwenye maziwa. Hivyo basi, kupitia ukaguzi huu utaimarisha shughuli za uvuvi hasa kwa kuunganisha na jitihada zinazoendelea za uchumi wa bluu kwenye maeneo yote baharini na maziwa.

Ukaguzi pia unachangia utekelezaji wa lengo namba 14 lengo dogo 14.4 na 14.6 la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ambalo linaweka mkazo kwenye utunzaji na matumizi endelevu ya bahari na rasilimali za bahari kwa maendeleo ya bahari. Lengo hili linalenga kudhibiti shughuli za uvuvi na kutumia tekinolojia ya sayansi kutunza malighafi ya samaki.

Lengo hili linalenga kuzuia aina za uvuvi haramu na kuvua samaki juu ya kiwango kilichopangwa.

#### **(n) Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Usimamizi wa Uingizaji wa Mafuta Nchini**

Ukaguzi unachangia utekelezaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambao unalenga kuimarisha uchumi shirikishi na shindani. Shughuli zinazotekelezwa katika eneo hili zinalenga kuimarisha uchumi mdogo kwa lengo la kuchochea uchumi shindani ambao utaweza kutoa mwongozo wa kisera na ufanyaji wa maamuzi.

Hivyo basi, ukaguzi huu utasaidia uwapo wa mazingira mazuri ya kuendesha viwanda vya ndani ambavyo ni muhimu sana katika kuwezesha usimamizi mzuri wa uagizaji wa mafuta nchini.

Vilevile, ukaguzi huu unachangia utekelezaji wa lengo namba 8 lengo dogo 8.1 la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa; ambalo linalenga kuimarisha ukuaji wa uchumi shirikishi na endelevu. Lengo hili linalenga

kuimarisha ukuaji wa uchumi kwa mtu mmoja mmoja, hasa angalau kufikia asilimia saba ya ukuaji wa uchumi wa ndani kwa mwaka katika nchi zinazoendelea

PERFORMANCE AUDIT  
AUDIT PERFORMANCE A  
PERFORMANC

PERFORMANCE AUD  
AUDIT PERFORMANCE

PERFORMANCE AUDIT

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,  
A4 Barabara ya Ukaguzi,  
S.L.P 950, Tambukareli, 41104 Dodoma.

 +255(026)2161200,

 [ocag@nao.go.tz](mailto:ocag@nao.go.tz),

 [www.nao.go.tz](http://www.nao.go.tz)



PERFORMANCE AUDIT